

4 JUNI, 2013

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Arobaini na Mbili - Tarehe 4 Juni, 2013

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

### D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge salaam zenu kutoka Uganda, nilikokuwa nimekwenda huko. Wale wenzetu kule wameanzisha *Nyerere Day*, tarehe 1 Juni kila mwaka na wanaunganisha na mashahidi wa Uganda ambao siku yao inasherehekewa tarehe 3 Juni, kila mwaka.

Sasa hivi ni *Nyerere Day* mwaka wa Saba wanaadhimisha na mara nyingi kiongozi mmoja kutoka hapa nchini huwa anakwenda kule. Huwa kuna watu wengi sana. Watanzania na watu wa mataifa mengine. Wanafanya kazi ya kumwombea Mwalimu Nyerere kwa imani ya dini ya Kikatoliki awe mionganoni mwa Watakatifu Watakaotambulika katika nchi yetu.

Kwa hiyo, tulikwenda huko, mwombeeni Mwenyezi Mungu asaidie. Tunaendelea.

4 JUNI, 2013

## **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:-**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/2014.

### **MHE. JUMA S. JUMA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA ZA JAMII):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

### **MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI):-**

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

4 JUNI, 2013

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 133

### **Kituo cha Afya Kibiti Kupandishwa Hadhi**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA (K.n.y. MHE. ABDUL J. MAROMBWA)** aliuliza:-

Kituo cha Afya cha Kibiti kiliishaahidiwa kupandishwa hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya:-

Je, ni lini utekelezaji wa ahadi hiyo iliyotolewa na Rais utaanza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa viwango vya utoaji huduma za afya kila Halmashauri inapaswa kuwa na hospitali moja ya wilaya ili kutoa huduma za rufaa kwa wagonjwa katika vituo vya afya katika halmashauri hiyo. Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti inayo hospitali ya Wilaya ambayo ni hospitali ya Utete.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo wananchi waliomba kupitia risala iliyosomwa mbele yake, Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ilitembelea kituo hicho na kukagua miundombinu iliyopo ili kuona kama inakidhi vigezo. Timu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, iliridhia kituo hicho kupandishwa hadhi na kuwa kituo cha afya kilichopandishwa hadhi yaani *upgraded Health Center*.

4 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma ya kukifanya kituo hicho kutoa huduma za dharura, halmashauri kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo tayari imekamilisha ujenzi wa jengo la upasuaji, maabara, wodi ya watoto, nyumba za watumishi, jengo kwa ajili ya huduma za ushauri na matibabu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (*CTC*) kufanya ukarabati wa huduma ya wagonjwa wa nje (*OPD*) na wodi ya wazazi. Upanuzi huu hadi sasa umegharimu shilingi milioni 442 ambapo Serikali ilitoa shilingi milioni 181 na nyingine zilitoka kwa wadau wa maendeleo.

Aidha, Serikali ilipeleka watumishi tisa (9) na kufanya kituo hicho kuwa na watumishi 37 ili kiweze kutoa huduma hizo za dharura.

Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2010 kituo hicho kilanza kutoa huduma za dharura ambazo ni upasuaji wa wajawazito, huduma za wagonjwa wa nje na wa ndani, huduma za maabara, huduma za uzazi (*RCH services*), kuongeza damu na kutoa ushauri na matibabu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (*CTC Services*) na kadhalika.

Aidha, Serikali inaendelea na ujenzi wa jengo la watoto ambalo liko katika hatua ya kupauliwa na nyumba moja ya watumishi ambayo iko katika hatua ya *lenter*.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Kwa sababu huduma zinatakiwa ziendelee kutolewa, na inaonekana kuna matatizo ya upatikanaji wa dawa na watumishi.

Je, huu utaratibu wa kupeleka dawa utaanza lini?

Swali la pili, kwa kuwa tatizo hili la upanuaji wa Kituo cha Afya Utete linafanana na lile la Matai wilaya ya Kalambo. Je, ni lini Wilaya ya Kalambo ambayo ni mpya itapata hospitali mpya ya wilaya?

Kama bado mchakato unaendelea, ni lini kituo cha afya cha Matai kitakuwa upgraded ili kiweze kutoa huduma kwa ajili ya wananchi wa wilaya ya Kalambo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mwulize maswali kwa kifupi ili tuweze kuuliza na kujibiwa maswali mengi sana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu na wewe kwa kifupi pia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza huu utaratibu wa kupatikana kwa dawa ni wa *MSD* ambapo sasa hivi tumeanzisha *MSD* katika kanda mbalimbali. Najua Mbunge anayeuliza swali hili ni mtaalam na amebobea katika haya maeneo, kwa hiyo, *I have to be very careful.*

Kwa hiyo, hatuendi tena Dar es Salaam kama ilivyokuwa zamani, lakini tunaanzisha utaratibu unaitwa *integrated logistics systems* ambao unatusaidia kubaini aina ya magonjwa yaliyopo katika eneo ili kuweza kujua ni aina gani za dawa zitapelekwa katika eneo hilo. Hii ni pamoja na kwamba, kama dawa hizo hazipatikani katika eneo hilo kuna utaratibu maalum ambao anaweza akaenda katika private institutions na kupata hizo dawa lakini kwa utaratibu ambao umekbalika kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hii halmashauri ya Kalambo anayozungumza hapa Mheshimiwa Mbunge, ni wilaya mpya. Sasa hivi tunachofanya kwa utaratibu wetu wa kiserikali ni kwamba, kama kuna wilaya mpya imefunguliwa pale wananchi wanaendelea kuhudumiwa na ile Halmashauri mama kwa maana ya hospitali ile ya zamani mpaka tutakapokuja kuwa na utaratibu wa kwao.

4 JUNI, 2013

Katika kipindi cha mpito wanachofanya ni kuhakikisha wanateua eneo lingine ambalo wanafikiri linaweza likatoa huduma kwa maana ya kusaidia mpaka hapo hospitali ya wilaya itakapokuwa imejengwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nikiri mbele yako kwamba hii ni halmashauri ya wilaya mpya, kwa hiyo, utaratibu wake utakwenda kufuatana na mapendekezo ambayo yataletwa na wilaya.

**MHE. JENISTA J. MGAHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ilikuwa ni azma nzuri ya Serikali kuhakikisha kila kata inakuwa na kituo cha afya na hivyo ndivyo sera yetu ya afya inavyosema, kwa kuwa, kila halmashauri illishaandaa mpango huo lakini Serikali mpaka sasa imeshindwa kusimamia na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika yakiwemo maandalizi yaliyofanyika katika kata zangu za Magagula na kwingineko.

Je, Serikali sasa inasema nini kuhusu sera hiyo ili iweze kutimia na watanzania wengi hasa wa vijijini waweze kupata huduma za afya katika vituo vinavyoeleweka. (*Makofî*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOÀ NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hii sera anayoeleza Mheshimiwa Mbunge ni kweli ndivyo inavyofanyika na utaratibu wetu tulisema kwenye vijiji tuwe na zahanati na katika kata tuwe na vituo nya afya.

Kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kumekuwa na hali ya kusuasua, lakini nataka niseme jambo moja hapo. Kwa upande wa Serikali tunachofanya ni kungoja kwanza halmashauri yenye we inapokuwa imebadilisha hicho kituo kimejengwa labda mpaka kwenye hatua ya *lenter*, sisi ndipo tutaingia pale na kusaidia.

Najua kwamba, tukienda katika halmashauri nyingi tutakuta kwanza katika hizo kata hawajafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhagama amesaidia katika kuhamasisha wananchi wajenge hivi vituo vya afya. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakwenda kuangalia tuone jinsi ambavyo jithada hizo zinajitokeza ili tuone na sisi kama Serikali tunaweza tukasaidia.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Longido ni mionganoni mwa wilaya zilizoanzishwa mwaka 2005 na haina hospitali ya wilaya pamoja na kwamba, zile wilaya zingine saba zimepata hospitali za wilaya.

Je, ni lini sasa wilaya ya Longido itapewa hospitali ya wilaya kama zile halmashauri zingine Sita zilizopata hospitali za wilaya ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

**SPIKA:** Aah, kwa sababu ya Siha labda, lakini ni swali jipya. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Swali jipya kabisa, labda kwa sababu Siha inafanana fanana na huko basi. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama alivyosema kaka yangu pale, mimi ni jirani yake wa karibu sana na wagonjwa wa kwake wengine wanakwenda Kibong'oto hospitali pale, wanakuja katika eneo la kwetu na wengine wanakwenda mpaka Mawenzi.

Kwa kweli wana tatizo kubwa pale, lakini azma ya Serikali ni kwamba, tuwe na hospitali ya wilaya katika wilaya zote mpya kama nilivyoeleza hapa na ndiyo sera yenye we inavyokwenda. Mheshimiwa Lekule Laizer ni mtu ambaye amesimama mstari wa mbele sana kupigania kuwa na hospitali ya Wilaya. Nataka nimwambie nitakwenda, tutakaa

4 JUNI, 2013

wote kwa pamoja. Hii si mara ya kwanza kwa Mheshimiwa Mbunge anauliza swali hili. Tutasaidia ili tuweze kuona tunaondoaje tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pale Longido ukiwaacha hivi hivi watu watakuwa, kwa hiyo, tunachofanya sasa hivi ni kutumia ile hospitali ya wilaya mama kwa maana ya Monduli. Hata hivyo, pana tatizo pale na hivyo tutasaidiana naye kuona tunaondoa tatizo hili. (*Makofi*)

Na. 334

### **Hospitali ya Wilaya ya Babati Kuongezwa Ruzuku**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Babati inakabiliwa na upungufu mkubwa wa raslimali fedha na watu na inapata ruzuku ndogo sana ikilinganishwa na huduma inazotoa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza ruzuku ya hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uwepo wa upungufu wa raslimali watu na fedha katika hospitali zake za rufaa katika ngazi ya Wilaya. Hata hivyo, kila mwaka Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji huduma katika hospitali hizi. Katika hospitali ya wilaya ya Babati, Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kuajiri watumishi wa kada ya afya wapatao 28 na hii itapunguza tatizo la upungufu wastani wa asilimia 41 kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi kufikia asilimia 30 kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya afya katika hospitali ya wilaya ya Babati kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikuwa ni shilingi 1,504, 659,272 ambapo matumizi mengineyo yalikuwa ni shilingi milioni 196 na fedha za *basket fund* ni shilingi milioni 160. Hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2013 Halmashauri ilikuwa imepokea jumla ya shilingi milioni 312.

Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 fedha za matumizi ya kawaida zimeongezeka hadi kufikia shilingi 1,720,340, 232/= ambayo ni ongezeko la wastani wa asilimia 13. Maeneo ya kipaumbele katika Bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014 ni pamoja na kuongeza uwezo wa kukabiliana na tatizo la raslimali watu, uboreshaji wa vifaa tiba na dawa na kuboresha miundombinu ya afya iliyopo wilayani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya kuongeza ruzuku ya hospitali naomba niweke wazi kwamba, Bajeti zote za halmashauri huandaliwa na Halmashauri husika kwa kuzingatia vipaumbele vyake. Kwa mantiki hiyo, maamuzi ya kuongeza ruzuku ya hospitali ya wilaya ya Babati ni ya Halmashauri husika.

Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na uongozi wa Halmashauri hiyo ili kuangalia upya vipaumbele viliwyopo ikiwa ni pamoja na kutumia mapato ya ndani ili kuongeza ruzuku ya hospitali ya wilaya ya Babati.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa hospitali ya wilaya ya Babati, Mrara tangu mwaka jana mwezi wa pili, hususan madaktari na manesi hawakupokea *on call allowance* na *post mortem allowance*, tangu Serikali ilivyotangaza mwaka jana mwezi wa *February*. Naomba nifahamu ni lini watumishi hawa watalipwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Katika majibu ya Waziri amesema kwamba, bajeti ya mwaka jana hospitali ya Mlara ilipangiwa 1. 5 billioni lakini hadi Mei, ni shilingi milioni 312 tu ndiyo zimepokelewa na hii inaonesha ni jinsi gani ambavyo wanashindwa kufanya kazi kwa sababu Serikali haipeleki fedha.

Naomba nifahamu hizi fedha zinapelekwa lini ili hospitali hiyo iweze kufanya kazi zake kama ilivyojipangia?

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuhusu hili suala la *on call allowance* wala tatizo halikuwa hapo tu, mkoa mzima ule wa Manyara umekuwa na hili tatizo na lilikuwa ni la ki- *administration*. Tumezungumza na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, tunaliona hili tatizo na kama linajitokeza pale siwezi ku- *dispute* hiki anachokisema Mheshimiwa Mbunge.

Nitakachofanya baada ya kutoka hapa, nitamwomba Mheshimiwa Gekul, wale watumishi anaowasema pale kama unao kwa majina yao anipatie kuhusu hii *on call allowance* inayozungumzwa hapa ili kama ninakwenda kushuka na mtu nishuke naye sawasawa. Nijue ni akina nani hawa ambao wanasababisha. Hilo la kwanza kwa sababu nalifahamu hilo tatizo na liko mkoa mzima wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu fedha hizi ambazo zimekwenda pale, ninachosema hapa ninaripoti kile ambacho ninakijua, najua Mheshimiwa Gekul tena ni mtaalam sana wa mambo ya bajeti, ni kweli wamepewa 1.5 billion lakini nilipochekei tumekuta fedha ambazo *so far* zimekwenda ni hizo.

Mwaka huu haujaisha, nataka nimuahidi Mheshimiwa Mbunge, hapa ana- *address* kitu muhimu sana, sera tunayozungumzia Serikali hapa inahusu huduma zinazotolewa katika hospitali zetu na kama zimekwenda kiasi hiki tu ni suala la mimi kuzungumza na Wizara ya Fedha ili tuweze kujua tumekwama wapi, lakini nina hakika *currently* unaweza ukakuta *figure* hii ninayoitoa hapa imepanda kufuatana na fedha zitakazokuwa zimekwenda pale.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, haya yote mawili ninayachukua na tutayafanyiakazi kama Ofisi ya Waziri Mkuu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilikuwa naomba kuuliza swali la nyongeza.

Je, Serikali itakuwa tayari kuiangalia hiyo hospitali ya Mrara katika suala nzima la bajeti yake kwa sababu haihudumii Halmashauri ya Mji tu inahudumia Halmashauri mbili, Halmashauri ya Mjini na Vijijini na asilimia kubwa ya Tarafa mbili Mbugwe na Tarafa ya Babati zote zinahudumiwa hapo, Bajeti inayoletwa ni kwa ajili ya Halmashauri ya Mji kutokana na idadi ya watu?

Idadi kubwa ya watu wa vijijini pia ambao hawana hospitali pia wanahudumiwa hapo hapo katika hospitali hiyo?

**SPIKA:** Naibu Waziri majibu na yawe mafupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, sawasawa.

Mheshimiwa Spika, huyu anayezungumza ni Mbunge wa Babati Vijijini ambapo wao pale tuna *Designated Hospital* ambazo zinaitwa Hospitali Teule inaitwa *Doretha*. Lakini hii ni hospitali ya Kanisa la Pentekosite ndiyo wanahudumiwa pale.

**MBUNGE FULANI:** Kanisa Katoliki!

4 JUNI, 2013

*Okay kama ni Katoliki ndiyo hivyo hivyo, sasa nimebanwa hapa jamani kama mnavyoona. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba pale ndipo ambapo tumepeleka nguvu pale kwa sababu zipo karibu kilomita 80 kutoka pale wapo mbali kidogo. Kwa hiyo, pale tunapaimarisha kwa kushirikiana na lile Shirika kama nilivyosema.

Lakini pia anachosema ni kweli kwamba watu wengi wa Babati wanahudumiwa pale, na sivyo hivyo tu hiyo hospitali ndiyo inayotumika kama hospitali ya Mkoa hiyo hiyo kwa sababu ule ni Mkoa mpya pale.

Kwa hiyo, tunaiona point ya Mheshimiwa Mbunge tutashirikiana ili tuweze kusaidiana vizuri ili tuone jinsi ya kuongeza nguvu katika ile hospitali ya Babati Mjini pale.

Na. 335

### **Scholarship Zinazotolewa na Nchi za Nje**

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Baadhi ya nchi za nje zimekuwa zikitoa *Scholarship* kwa Tanzania kuitia Balozi zetu lakini baadhi ya *Scholarship* hizo hurudishwa bila kujazwa baada ya kukosa watu wanaokidhi vigezo vilivywerekwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia sehemu ya *Scholarship* hizo Watanzania wanaosoma nje ya nchi ambavyo wanajilipia ada ya kuzileta zote nchini na matokeo yake zikarudishwa?

(b) Je, Serikali imewahi kurudisha *Scholarship* ngapi kati ya mwaka 2005 - 2011 na zilitoka nchi gani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMII) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ninaomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kuratibu mafunzo kwa watumishi wa Umma, ikiwa ni pamoja na kuandaa sera, kutoa miongozo na maagizo mbalimbali kuihusiana na mafunzo na kufuatilia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili na kwa kuzingatia ushirikiano wa kiufundi uliopo kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali za nchi wahisani, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imekuwa ikipokea na kuratibu fursa mbalimbali za mafunzo ya muda mfupi na mrefu (Shahada za Uzamili na Shahada za Uzamivu) kutoka kwa Wahisani.

Wahisani ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuisaidia Serikali ya Tanzania kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma ni pamoja na Australia, Jamhuri ya Watu wa China, India, Jamhuri ya Korea, Japan, Ubelgiji, Uhlanzi, Malaysia, Misri, Singapore, Thailand, Israel, Sweden, Italy, Ujeruman, Jumuiya ya Madola na Mfuko wa Afrika wa Kujenga uwezo (*African Capacity Building Fund*).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa noamba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, fursa za mafunzo zinazotolewa na wahisani kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni kwa ajili ya Watumishi wa Umma wanaofanya kazi katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali pamoja na Taasisi zingine za Umma.

Kuhusu Watanania wanaosoma nje ya nchi kama ni miongoni mwa Watumishi walio chini ya Wizara, Wakala au Taasisi zingine za Umma wanastahili fursa hizo na Wizara inatoa fursa kwa wahitaji wanaostahili bila ubaguzi iwapo maombi hayo yatakuwa yamepitia katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka 2005 hadi 2011 Tanzania ilipokea nafasi za masomo 3,589 kutoka kwa Wabia wa Maendeleo wa nchi nilizositaja hapo awali na zote zilitumika ipasavyo kwa Watanzania bila ubaguzi wowote na hakuna nafasi ambazo zilirudishwa kwa sababu yoyote ile.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi ninaitwa Leticia Mageni Nyerere na siyo Leticia Mgeni Nyerere. Baada ya kusema hayo. Kutokana majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, inaonekana kwamba *scholarship* zinazoletwa nchini ni kwa ajili ya Watumishi wa Umma na Serikali.

Swali la kwanza, ni jinsi gani sasa wanafunzi wanaomaliza Kidato cha Sita kwenye shule za Kata wanufaika na *Scholarships* hizi ikiwa ni haki yao?

Swali la pili, je, ni utaratibu gani sasa unatumika kuwapatia *scholarship* watumishi waliopo Wilayani wakiwemo wale watumishi waliopo katika Wilaya ya Kwimba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMII) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, kwanza namwomba aniwie radhi sana, anisamehe sana.

Mheshimiwa Spika, tumekaa, tumekesha tumehangai na hili swali la Mheshimiwa la Leticia kwa sababu tulijua kwamba haya yote yataulizwa hapa atayaauliza. Ni hivi ukiruhusu hizi scholarship zikaenda tu kiholela kila mwanafunzi anayekwenda pale lazima ulipe thirty percent ya hiyo *scholarship* kwa maana ya gharama zote zile. Kwa hiyo, tunaelewa umuhimu wa *Private Sector* katika kuendeleza nchi yetu.

Hapa swali linasema hivi, kwa ajili ya Watumishi wa Umma, hawa Watumishi wa Umma ndiyo wanaopelekwa kule, hawa *private* tunaozungumza hapa hawapatiwi, Wamerekani wanapitia kwenye kitu kinaitwa *on line* wanaomba moja kwa moja na wanakwenda moja kwa moja kwa vigezo ambavyo watakuwa wamewawekea na vitu vingine vya namna hiyo.

Hawa tunaowasema ni wale ambao wanapitia katika mfumo wa kiserikali kwa maana ya Mawakala, kwa maana ya Taasisi, kwa maana ya *Organization* zote ndiyo wanaopita hapo.

Mheshimiwa Spika, sasa hawa anaowasema waliomaliza katika shule za kata hawa kama wanaingia katika mfumo huo lazima wapitie kwenye hili tundu kwa maana ya Bajeti kwa maana kwamba Serikali inapo Bajeti ili iweze kuwa-*consider* na hawa wanaozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachozungumza ni kwamba *sponsorship* hizi zote zinaratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Vinginevyo ukienda nje ya hapo itakuwa ni matatizo na wale walioko kule Marekani ambao wamekwenda kule hata kama wapo kule na anataka hizi fedha zikija zibakie kule kule haiwezekani lazima kwanza wapitie kwenye Ofisi hii hapa na Ofisi iseme barabara ipige mhuri halafu ndiyo waendelee kuhudumiwa. Huo ndiyo utaratibu lakini mimi ninaiona *concern* yake tunaweza tukashirikiana kumshauri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ili tuweze kusaidiana katika Jambo hili.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, Nashukuru sana kwa kuniona. Ningependa nimuulize swalilifuatalo. Swalil la Mheshimiwa Leticia Nyerere ni kwamba mara nydingine nafasi hizi zinapelekwa kupitia katika Balozi zetu zilizokuwepo huko nje. Lakini Balozi zimekuwa hazikubali kutoa ushirikiano na Watanzania ambao wamekuwa wakiishi kule au wakifanya masomo yao wakitaka kuendelea. Sasa kauli ya Serikali kuziagiza Balozi hizi ni nini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kama tulivyojibu hapa tumejaribu kucheki orodha zote, tume-cross cheki mpaka na Wizara ya Elimu ili kuweza kuona kama kuna matatizo hayo.

Sasa Mheshimiwa Mangungu anaongeza jambo lingine hapa anasema kwamba wakati mwingine kunakuwa na matatizo. Kwa kipindi hiki cha Mheshimiwa Leticia alichokiuliza hapa tumecheki zile zinazopita kwenye Ofisi ya Rais na zile zote zinazopita katika Wizara na nikawaita wale wahusika wote wakaja pale nikawarudisha mara mbili nikawaambia nenda mkaangalie vizuri isije ikawa kuna wengine wana-sleep mle ndani.

Lakini sasa sisi tunatumia Ubalozi katika kuratibu na kupitisha. Tunatoa kauli gani, sisi kauli ambayo tunaweza kutoa hapa ni kwamba ofisi zetu za Ubalozi zitoe ushirikiano kuhusu hao wanafunzi wanaoomba nafasi za kwenda kule na kwa maana hiyo basi tutamshauri Waziri mwenye

dhamana ili aweze kuratibu vizuri kupitia ofisi za Ubalozi ili sasa kusiwe na watu wengine ambao nafasi hizi zinazopatikana, lakini zikawa hazikuwa *utilize*. Lakini nataka nimthibitishie nafasi zote tulizopewa ambazo nimezitaja hapa zote zimetumika kama zilivyokuwa zimeonyeshwa katika wale ambao wanatuhsiani.

Na. 336

### **Vitabu vya Hisabati Visivyokuwa na Ubora**

**MHE. JAMES F. MBATIA** aliuliza:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha *South Carolina (USA)* chini ya ufadhilli wa *USAID* iliandika vitabu vya hisabati kwa shule za sekondari, vitabu ambavyo havikuandikwa kwa ubora unaokubalika; hili ikiwa ni sababu moja wapo kubwa inayosababisha wanafunzi wengi kufeli somo la hisabati.

(a) Je, vitabu hivyo vilihaririwa na wataalam wa somo husika?

(b) Je Wataalamu hao hawakuweza kubaini udhaifu huo na kama waliuona ni hatua gani zimechukuliwa?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Kuteuliwa lenye sehemu (a) na(b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2009 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliomba msaada wa vitabu vya Sayansi na Hisabati kutoka Serikali ya Marekani.

Aidha, Serikali ya Marekani kupitia Shirika lake la *USAID* ilitoa msaada huo chini ya usimamizi wa Chuo Kikuu

cha Jimbo la Carolina ya Kusini (*South Carolina State University (SCSU)*) ambacho kilisimamia na kuratibu msaada huo. Wakati huo huo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilikuwa imekwishapata msaada huo mwaka 2009 kwa masomo hayo ya Sayansi na Hisabati hususan katika uandishi wa vitabu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundzi ilikubaliana na Chuo Kikuu cha Jimbo la Carolina na Shirika la *USAID* kutumia vitabu viliivoandikwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar. Vitabu hivyo ni *Mathematics for Secondary School, Book 1, 2,3* na 4. Aidha, Wizara yangu iliteua wataalamu 6 wa Somo la Hisabati ambaao walifanya kazi ya kuvihariri vitabu hivyo mwaka 2010.

Baada ya vitabu hivyo kuhaririwa, jukumu la kuvihakiki na kuvitathmini lilitekelezwa na watathmini ambaao ni walimu watatu wa somo la Hisabati kutoka shule za Sekondari, mtaalamu mmoja kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania na mshauri mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Jimbo la *South Carolina*. Kazi ya uhakiki ilipomalizika Wizara yangu kuititia *EMAC* ilivipitisha vitabu hivyo na kuvipa hati ya ithibati kuwa vitabu vya kiada katika shule za Sekondari mwezi Mei, mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na wataalam iligundua kasoro kadhaa za kimaudhi ambazo hata hivyo, zisingesababisha wanafunzi kushindwa kuelewa mada husika. Aidha, Wizara yangu imeunda Kikosi kazi ambacho pamoja na mambo mengine, kimefanya uchunguzi wa kina kuhusu utendaji wa *EMAC*. Taarifa ya Kikosi Kazi hicho imekamilisha kazi yake na kuwasilisha mapendekezo ambayo yanafanyiwa kazi kabla ya kuchukua hatua stahiki.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa, vitabu hivi ni sumu kwa Taifa letu, kwa kuwa; maudhui yake, miongozi yake haifai kabisa kwa Taifa ni sumu.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo, kwa sababu jibu la swali hapa linaonekana vitabu vipewe ithibati mwaka 2011 mwezi Mei. Vitabu ninavyo hapa vimepewa ithibati tarehe 10 Juni, 2010 wanasma uhariri ulifanyika mwaka 2010 wakati vitabu vilishapewa ithibati na huu ni uhujumu wa uchumi zaidi ya bilioni 20,400,000,000. Swali la kwanza, je, kwa kuwa, yote haya yamefanyika na yanazidi kuua Taifa letu, Wizara itakubaliana nami kwamba viondolewe vyote kwa sababu tunaendelea kuliangamiza Taifa letu kwa kuwa Elimu ndiyo uhai wa Taifa hili?

La pili, kwa kuwa, Watendaji wa Wizara hii wanaonyesha udhaifu mkubwa sana wa kuangamiza elimu ya Taifa hili, waliojibu swali hili hapa waliomwandikia Waziri anaweza kuhakikisha na atoe ripoti hapa ya kuwawajibisha kwa sababu wanaudanganya Umma wa Tanzania na kuivunja *EMAC?* (*Makof*)

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbatia, kama ifuatavyo:-

Moja, ni kwamba vitabu vimeandikwa na wataalam wa kutoka Tanzania na kwa kushirikiana na watalaam kutoka Marekani kwa nia thabit ya kusaidia Tanzania kielimu, kazi hii imefanyika kimakini na kiutalaam, na kwa kutumia wataalam wa nchi hizi mbili, kazi hii imehakikiwa na baada ya kuona kuna matatizo kule ilitathminiwa kwamba matatizo yale ambayo yameonekana kwenye vitabu ni yale ambayo yanaweza kuathiri maudhui ya kitabu ama hapana, na yamehakikishwa na wataalam wetu kwamba siyo yatakayoweza kuathiri maudhui ya vitabu, na kwa hiyo, Serikali imeruhusu vitabu hivi viendelee kutumika, lakini vitafanyiwa uhakiki ili chapisho la pili lisiwe na matatizo yale ambayo yameonekana katika chapisho la kwanza.

Syo kweli kabisa kwamba ni sumu inaharibu elimu na kwamba hesabu haisomeki kabisa kwa sababu ya vitabu hivi. Hili jambo ni kutia sumu katika elimu yetu ambayo si kweli hata kidogo.

4 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili ambalo linasema kuhusu kukinzana kwa tarehe za ithibati hilo tutalifanya kazi na kuweza kulishughulikia ipasavyo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mimi ningependa kama Mheshimiwa James Mbatia, hiyo sumu anayosema angekuandikiani ili kusudi muione hiyo sumu inafanana namna gani inawezekana mkajibishana hapa tusijue hasa kinachozungumzwa ni nini?

Kwa hiyo, namuagiza Mheshimiwa James Mbatia hayo maandishi ya namna hiyo naomba uyapeleke kwenye Wizara na sisi tupewe taarifa. Kwa sababu maneno aliyyoatoa ni mazito. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Jenista Mhagama.

Na. 337

### **Kigezo cha Uwiano katika Kugawa Walimu**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa muda mrefu kupitia Bunge nimekuwa nikiombwa Serikali kutazama upya kigezo cha uwiano wa 1:41 katika kugawa walimu, ambacho kinabagua walimu wa vijijini na kuwanyima wanafunzi wa maeneo hayo kupata walimu wa kutosha na hivyo kukosa elimu bora ambayo ni haki yao:-

Je, ni lini Serikali itasikiliza rai hii ili kubadili kigezo hiki na kuwapa watoto wa wakulima vijijini haki ya kupata elimu bora kwa kupewa walimu wa kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
aliyibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua tatizo la uhaba wa walimu hasa katika maeneo ya vijijini. Upangaji wa walimu wa shule za msingi huzingatia uwiano uliopo kati ya walimu na wanafunzi katika shule zilizopo katika Halmashauri. Uwiano uliokubalika kwa nchi zilizo Kusini mwa Afrika ni wa mwalimu moja kwa wanafunzi 40 yaani *ratio* 1:40. Hata hivyo, upangaji wa walimu kwa kutumia uwiano wa 1:40 ulikuwa na mapungufu kwa vile zipo shule zenyе idadi ya wanafunzi wachache na zina wanafunzi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba kama hali ilivyo katika shule za msingi, Mkenda, Magwamila, Nambendo na Ifinga na zingine zilizopo katika Jimbo a Peramiho na kwa Tanzania nzima. Kwa msingi huo, shule hizo zinahitaji walimu kwa kila darasa/mkondo. Kwa kuzingatia changamoto hii kuanzia mwaka 2012/2013 Wizara imebadili kigezo hiki cha kutumia uwiano wa mwalimu kwa mwanafunzi na kupanga walimu kwa kuzingatia upungufu wa Walimu ikilinganishwa na mikondo iliyopo katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia kigezo cha upungufu na mikondo iliyopo, katika mwaka wa masomo 2012/2013, Halmashauri ya Songea Vijijini imepangiwa jumla ya walimu 96 wa ngazi ya Cheti watakaofundisha katika shule za msingi na waliokwisha ripoti tayari ni walimu 88 kati ya 96. Kutokana na kuripoti kwa walimu hawa, upungufu wa walimu katika Halmashauri ya Songea Vijijini kwa sasa ni walimu 199 tu, upungufu ambao unatarajiwa kumalizwa ndani ya miaka miwili ijayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inapenda kuwakumbusha tena Wakurugenzi na Maafisa Elimu wa Halmashauri kuwapanga walimu katika shule zenyе upungufu mkubwa wa walimu hususan shule za pembezoni.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kukubaliana na hoja yangu ya msingi niliyokuwa ninaitoa miaka yote humu Bungeni na kubadilisha hicho kigezo kwa manufaa ya wananchi wa Tanzania na watoto wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, lakini nina maswali mawili mafupi sana madogo.

La kwanza, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri hapa pamoja na kutuletea hao walimu alioswasema, amesema kwamba bado tuna upungufu walimu 199 na yeze amesema tu, mimi ninasema bado ni wengi sana. Je, katika mwaka huu wa Fedha ametupangia walimu wangapi kuja kuondoa kero ya tatizo la walimu katika Jimbo la Peramiho na Wilaya ya Songea kwa ujumla?

Swali la pili kwa kuwa mara nyingine viongozi wanaosimamia ugawaji wa walimu katika maeneo ya vijiji ndio wanaosababisha mgawanyo hafifu usiokuwa na tija kwa wanafunzi walalahoi vijiji. Je, Wizara inatoa tamko gani kukemea suala hilo na kuhakikisha uwiano unakuwa sawia watoto wote wapate elimu sawa? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa sababu ni mwalimu. Mwaka jana aliuliza swali kama hili na akasema sikulijibu vizuri na kweli na mimi nikakiri kwamba nilikuwa nina mapungufu katika kujibu hili swali mwaka jana.

Lakini baada ya yeze mwenyewe kunifuata tukakaa pamoja na kwa sababu sisi wote ni walimu tukakubaliana kabisa hoja hii tuipeleke Wizarani tukapange vigezo upya vya namna ya kuchagua hawa walimu. Mheshimiwa Mhagama na mimi nashukuru sana kama umekubaliana na hilo na kweli mwaka huu tumefuata vigezo hivyo vya kupanga walimu kutokana na uwiano wa mikondo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhagama anasema ana upungufu wa walimu 199 na sisi tumesema kwamba baada ya miaka miwili tatizo hili litakwisha kule Peramiho na mimi nimuahidi kwamba mwaka jana tumempa walimu 96 na mwaka huu kwenye ajira mpya tutampa walimu 110 iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kuhusu Ma-*DED* na Ma-*DOWANAOPANGA* walimu sehemu za mijini. Suala hili kwa kweli nilikuwa nikilipigia kelele. Mheshimiwa Waziri wa Elimu anafanya ziara huko tunapiga kelele. Lakini kwa kweli Waheshimiwa Wabunge na ninyi ni Wajumbe kwenye Halmashauri kule hebu tupigane kwa pamoja tuhakikishe suala hili linakwisha na mimi baada ya kumaliza Bunge hili nitafanya ziara kwenye Halmashauri kuhakikisha kwamba walimu ambao tutakuwa tumewapelekea kwenye Halmashauri wanapangwa zile sehemu za vijiji ambako hakuna walimu kabisa. (*Makofii*)

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Walimu wanapangwa maeneo ya pembezoni, shida kubwa ni kutokuripoti kutokana na mazingira. Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili ili iache ubaguzi kwa sababu inatunga mitihani bila kuangalia kuna shule hazina walimu wa sayansi hata mmoja wanapimwa na shule ambazo zina walimu wa kutosha. Sasa hii sio haki kwa watoto wa vijiji, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tatizo hili kuhakikisha wanafika kule?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli baadhi ya maeneo kuna mazingira magumu na sisi tunakiri na ni kweli walimu huwa hawaripoti na hasa alikotoka Mheshimiwa Mbunge kule Kasulu Kibondo nilitembelea mwaka jana nikakuta asilimia 40 tu ya walimu walikuwa wameripoti kule na hii inategemea na mazingira, nyumba na mambo mengine. Nimshauri tu Mheshimiwa Mbunge kwenye Halmashauri zenu mapokaa muwe na mikakati angalau ya kuboresha mazingira kama hayo.

Lakini na sisi kama Serikali tayari tumeanza kuboresha mazingira magumu kwenye Halmashauri. Kuna fedha tulikuwa tumeandaa ziende kwenye shule za mazingira magumu kwa ajili ya walimu lakini tumesema fedha hizo tuweze kununulia samani na nadhani Halmashauri ya Kibondo imo katika zile Halmashauri zenye mazingira magumu waweze kupata hizo fedha kwa ajili ya samani.

4 JUNI, 2013

**SPIKA:** Wizara hii inakuja sasa hivi msiondoe utamu kwenye maswali. Tuendelee Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 338

**Mikoa ya Lindi na Mtwara Kuzuiwa  
Kulima Pamba**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

**SPIKA:** Wizara hii inakuja sasa hivi msiondoe utamu kwenye maswali. Tuendelee Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika

- (a) Kwa nini Mikoa ya Lindi na Mtwara inazuwa kulima zao la Pamba?
- (b) Je, Serikali inafahamu kuwa zao la Pamba lilianza kulimwa kwenye Mikoa hiyo?
- (c) Je, Serikali sasa inaweza kuiruhusu Mikoa ya Lindi na Mtwara kulima zao hilo?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisitisha kilimo cha zao la pamba katika Mikoa ya Kusini baada ya kuonekana kwa funza mwekundu (*Red Bollworm*) katika maeneo hayo. Karantini hiyo ilihusisha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Wilaya ya Njombe, Kyela, Mbozi, Sumbawanga na Chunya kwa madhumuni ya kuzuia mdudu huyo kusambaa katika maeneo makuu ya uzalishaji wa pamba katika Kanda ya Magharibi na Mashariki mwa Tanzania.

Aidha, udhibiti wa kisumbufu hicho ni mgumu kutokana na baiolojia yake inayomwezesha kuishi chini ya udongo kama hakuna mimea ya pamba au hali ya hewa inayomwezesha kuishi. Sababu kubwa ya kuzuia kilimo cha pamba katika maeneo niliyoyataja ni kwamba gharama ya kumdhhibit funza mwekundu zilioneckana kuwa kubwa kuliko pamba inayopatikana hivyo Serikali iliamua kuzuia kilimo cha pamba wakati ikifanya utafiti wa kupambana na funza mwekundu.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafiti ni endelevu. Kwa kuwa matokeo ya utafiti wa kudhibiti funza mwekundu yameonyesha kuwa kuendelea na kilimo cha pamba kwa mazoea hakutakuwa na tija, Serikali inaangalia uwezekano wa kufanya marekebisho ya kanuni za sheria ya mazingira ili kuruhusu kufanyika kwa utafiti wa pamba aina ya "*Bt Cotton*" ambayo ina tija kubwa katika uzalishaji, pla ina ukinzani na magonjwa na visumbufu vya mimea. Mimi naamini matokeo ya utafiti huo yatatoa mwanya wa kilimo cha pamba kuanza tena katika Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mikoa ya Kusini ni mojawapo ya mikoa waanzilishi wa kilimo cha pamba nchini. Hata hivyo kutokana na kuwepo kwa mdudu huyo Serikali ilianza kushughulikia tatizo hilo kwa kufanya utafiti wa kudhibiti funza mwekundu katika mikoa ya Kusini katika msimu wa 2004/2005 na kumalizika msimu wa 2007/2008.

Utafiti huo ulilenga kuthibitisha kuwepo kwa funza mwekundu katika maeneo ya karantini, kutathmini kuenea kwake, madhara ya kiuchumi ya kulima pamba katika maeneo yaliyoathiriwa na funza mwekundu na mtazamo na maoni ya wakulima wa maeneo hayo kuhusiana na karantini hiyo.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utafiti huo yalionyesha kuwa funza mwekundu aliongezeka mwaka hadi mwaka wakati wa kipindi chote cha miaka mitatu ya utafiti. Matokeo haya yaliashiria kuwa pamba ikilimwa maeneo hayo funza huyo ataongekeka kwa kiasi kikubwa na

kusambaa katika maeneo mengi yanayolimwa zao la pamba nchini. Aidha, matokeo hayo pia yalionyesha kuwa kilimo cha pamba katika eneo ambalo kuna funza mwekundu kinaongeza gharama za uzalishaji ikilinganishwa kilimo hicho katika eneo lisilo na funza mwekundu. Kwa mfano mkulima analazimika kunyunyizia dawa mara 210 ikilinganishwa na mara 6 zinazohitajika.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana majibu ya Mheshimiwa Waziri ni ya kusikitisha kwa maana kwamba utafiti huu wa kudhibiti funza umefanyika kwa zaidi ya kipindi cha miaka 35 sasa. Tatizo hili limekuwepo pia *Mozambique* na wenzetu wamefanikiwa kudhibiti kwa nini hatutumii tafiti walizozifanya wao na wakadhibiti funza hao? Hilo la kwanza.

La pili, matatizo haya ya magonjwa ambayo yamekuwa hayatibiki Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekuwa kila mwaka mnatuambia wataalamu wetu wanafanya kazi kubwa, lakini kazi za utaalamu wao hazitupi matokeo yaliyokuwa na ufanisi. Kwa sababu kuna tatizo pia la ubwiliunga kwenye mikorosho wananchi wanalazimika kila mwaka kupulizia mikorosho na miembe ili kuweza kupata mazao. Kweli tumeshindwa kufanya utafiti wa magonjwa haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri naomba majibu yawe mafupi maana swali hili ni la kujaribu sana linaweza kutupiga semina hapa.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nimesema utafiti ni suala endelevu wala hakuna mwanzo na mwisho wa utafiti. Ndiyo maana nimesema tunafanya utafiti sasa wa kuangalia uwezekano wa kutumia *Bt Cotton*. Hii ni aina ya pamba ambayo inazalishwa kwa njia za bioteknolojia kutokana na utaalamu wa Uhndisigeni. Sasa utafiti huu unalenga kupata mbegu ambayo au aina ya pamba ambayo itakuwa na ukinzani wa magonjwa yote haya ambayo tunazungumza.

Mheshimiwa Spika, labda nimalizie tu kwa kusema hivi kama tukiruhusu kwamba kilimo hiki kifanyike moja itakuwa kwanza tunakwenda kinyume na mkataba wa Kimataifa wa kulinda mazao kwa kudhibiti kuenea kwa visumbufu nya mimea, mkataba ambao tulurihdia hapa hapa Bungeni mwaka 2005.

Labda nimuahidi Mheshimiwa Mangungu kwamba tutakachokifanya sasa wataalamu wangu watakuwa wanakwenda kufanya semina kuwaonyesha matokeo ya utafiti kwamba yamefikia wapi ili angalau twende pamoja katika utafiti huo.

**SPIKA:** Hilo swali toka naingia Bungeni linaulizwa kila mwaka. Kwa hiyo, naendelea na Mheshimiwa Agnes Mkanga.

Na. 339

#### **Ucheleweshwaji wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kilimo cha kitaalam kinahitaji pembejeo mbalimbali ikiwemo mbolea, lakini mara nyingi pembejeo hizo huchelewa kuwafikia Wakulima kukidhi msimu husika wa kilimo hicho:-

- (a) Je, kwa nini kunakuwa na ucheleweshwaji huo?
- (b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha Wakulima wanapata pembejeo hizo mapema?

#### **WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Agnes Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli wakulima wengi wamekuwa wakilalamikia uchelewaji wa pembejeo hususan mbolea. Tunapozungumzia upatikanaji wa pembejeo ni vema tukafahamu kwamba kuna aina (tabaka) mbili za pembejeo. Tabaka ya kwanza ni pembejeo ambayo ina ruzuku ya Serikali katika bei na tabaka ya pili ni pembejeo inayouzwa na wafanyabiashara kwa bei ya soko.

Pembejeo yenyeye ruzuku inaagizwa na kusambazwa kwa uratibu maalum na Makampuni na Mawakala walioeteuliwa ili kuhakikisha kwamba wakulima husika wanapata pembejeo hiyo kwa bei iliyopangwa na Serikali na kwamba wanapata unafuu wa bei kuititia ruzuku. Aina nyingine ni pembejeo ambayo inapatikana katika soko huria.

Kwa upande wa pembejeo yenyeye ruzuku ucheleweshaji ulikuwa unasababishwa na upatikanaji wa fedha za kuchapisha vocha ambapo Wizara ililazimika kusubiri bajeti ya Serikali ipitishwe ili taratibu za manunu zianze. Kwa upande wa pembejeo ya soko huria, wafanyabiashara wa pembejeo wamekuwa wanasiita kupeleka pembejeo vijijini wakati wa kiangazi kwa kuhofia gharama ya kuzihifadhi kwa muda mrefu kutokana na wakulima wengi kusubiri mpaka mvua inyeshe ndipo waanze kununua pembejeo.

Aidha, sababu nyingine ya kuchelewa kwa mbolea yenyeye ruzuku ni urasimu na ubadhifuru katika usambazaji wa vocha za pembejeo uliosababishwa na baadhi ya watendaji na Mawakala wasio waaminifu ambao wamekuwa wanasiababisha wizi na upotevu wa fedha na wakati mwingine pembejeo kutomfikia mkulima.

(b) Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 2012/2013 Serikali ilitumia utaratibu wa kufikisha pembejeo za kilimo kwa wakulima ambapo Mawakala wa Pembejeo wanateuliwa na Makampuni ya Pembejeo badala ya Kamati za Pembejeo za Wilaya. Lengo la kutumia utaratibu huu ni kuondokana na tatizo la Mawakala ambao huchelewa kupeleka pembejeo.

Kwa kuwa Kampuni ndizo zitakazoathirika zisipofikisha pembejeo mapema, imani yangu ni kwamba zitafanya jitihada ya kuwaflikishia wakulima pembejeo mapema. Hata hivyo utaratibu huu nao uligubikwa na changamoto za vocha kuchelewa kuwafikia wakulima kutokana na baadhi ya watendaji kutowajibika kikamilifu; Mawakala na watendaji wasio waaminifu kuwarubuni wakulima; na baadhi ya Makampuni kutofikisha pembejeo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto zilizojitokeza, Serikali imebuni mfumo mpya wa usambazaji wa pembejeo utakaotumika katika msimu 2013/2014 ambapo katika baadhi ya maeneo, wakulima kuititia vikundi na Vyama vya Ushirika watapata mikopo ya muda mfupi na yenye riba nafuu kwa ajili ya kununulia pembejeo.

Mfumo huu umejadiliwa katika semina ya usambazaji wa pembejeo iliyofanyika hapa Dodoma tarehe 28 mpaka tarehe 29 Mei, 2013 na kuonekana kuwa unaweza kuleta manufaa yanayotarajiwa pamoja na kuwa utajenga uwezo endelevu wa wakulima kujinunulia mbolea.

Semina hiyo iliwahusisha wadau mbalimbali wakiwemo Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wabunge, Wakulima, Wasambazaji wa Pembejeo, Taasisi za fedha (Mabenki) na wadau wengine.

Aidha, utaratibu mpya wa mkutano wa Bajeti yaani huu utaratibu tuliouanza sasa mwezi Aprili hadi Juni unatarajiwa kuharakisha upatikanaji wa fedha mapema ili uagizaji na usambazaji wa pembejeo uwahi kalenda ya kilimo.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mfumo uliotumika mwaka 2012/2013 uligubikwa na changamoto za wizi kutokana na watendaji kadhaa kutokuwa waaminifu.

4 JUNI, 2013

Je, katika huu mfumo uliobuniwa hivi majuzi Serikali imejiandaa vipi kwamba tatizo hili la wizi lisijitokeze tena?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**

Mheshimiwa Spika, wizi ni jambo ambalo linajitokeza kila wakati, kila mahali. Tulivyojiandaa ni utaratibu uliopo tu kwamba vyombo vyetu nya dola vyote vinavyoshirikiana wote tushirikiane kudhibiti maana wanaoiba ni watu hawa hawa, watendaji ni hawa hawa. Basi tushirikiane kama tulivyokuwa tunafanya katika misimu iliyopita, mimi naamini hata kwenye mfumo huu watakuwepo tu maana wanapitia kwenye vyama hivyo hivyo. Tutakachokifanya ni kuhakikisha kwamba tunatumia mfumo uliopo wa Serikali kuwakamata na kuwfakisha Mahakamani kila watakapofanya wizi huo.

Na. 340

**Hitaji la Maafisa Ugani Vijijini**

**MHE. REBECCA M. MNGONDO (K.n.y. MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA)** aliliza:-

Wafugaji wengi vijijini hufuga pasipo kupata ushauri wa wataalam (Maafisa Ugani):-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka Maafisa Ugani Vijijini?
- (b) Je, Serikali inasimamiae utendaji wa Maafisa Ugani hawa katika kupunguza kero za wakulima na wafugaji?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Anthony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wakulima na wafugaji wanapata huduma za kitaalam popote pale walipo nchini ili kufanikisha shughuli zao kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji.

Kwa upande wa kilimo, hadi kufikia mwezi Juni, 2012 Serikali ilikuwa imeshaajiri jumla ya Maafisa Ugani 7,974 katika ngazi ya Kata na Vijiiji.

Lengo la Serikali ni kuwa na Afisa Ugani mmoja kwa kila Kata na kila Kijiji nchini. Idadi hii bado ni ndogo ukilinganisha na jumla ya Kata na Vijiiji 15,082 vilivyomo nchini. Kufuatia hali hii bado tuna upungufu wa wataalam wa kilimo 7,108 kwenye Kata na Vijiiji nchini. Kwa upande wa mifugo Maafisa Ugani waliopo ni 5,197 ambao ni sawa na asilimia 32 ya mahitaji. Upungufu huu uliopo ni Maafisa Ugani 12,128 sawa na asilimia 68.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu huu, Serikali imeboresha mazingira ya vyuo vya kilimo na mifugo kwa kukarabati majengo na kuongeza udahili wa wanafunzi ambapo kwa sasa vyuo vya kilimo vina uwezo wa kudahili wanafunzi hadi 3,500 kwa mwaka na vile vya Mifugo vina uwezo wa kudahili hadi wanafunzi 2000 kwa mwaka.

Mpango wa Serikali kukabiliana na upungufu uliopo ni kuendelea kudahili wanafunzi katika vyuo hivi na kuwaajiri kulingana na hali ya upatikanaji wa fedha.

Aidha, jumla ya wataalam wa kilimo 1,514 ambao hawakupata nafasi za ajira mwaka 2012 na wahitimu 1000 wa mwaka 2011/2012 watakuwa mionganoni mwa waajiriwa wapya 1,804 watakaoajiriwa na kupelekwa vijijini ili kupunguza pengo liilopo.

(b) Mheshimiwa Spika, utendaji wa Maafisa Ugani hawa husimamiwa na Halmashauri za Wilaya husika chini ya Wizara ya TAMISEMI.

4 JUNI, 2013

Aidha, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvvi hushirikiana kwa karibu na Halmashauri za Wilaya katika kuandaa na kusambaza miongozo mbalimbali kuhusu utoaji wa huduma za ugani kwenye Halmashauri hizi, kusomesha wataalam na kuwapatia mafunzo rejea, kuandaa mpango wa ajira kwa kutangaza nafasi za ajira, kufanya usaili na kuwapangia vituo vyta kazi kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kadiri ya mahitaji yao.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa wakulima na wafugaji wanapata huduma za kitaalamu popote pale walipo, lakini changamoto ni upungufu wa Maafisa Ugani ambao kwa ujumla wake kama alivyosema Mheshimiwa Waziri ni 12,128 sawa na asilimia 68.

Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu kuwatumia wale wachache waliopo kwa kuwapa vitende kazi na hasa pikipiki ili waweze kutembelea vijiji vingi zaidi na kutoa huduma bora wakati Serikali inaendelea na utaratibu wake wa kuajiri na kusomesha Maafisa Ugani wapya.

Lakini swali la pili kwa kuwa njia ya kutoa elimu kwa njia ya elektroniki (*electronic media*) ni njia ambayo ni rahisi zaidi. Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu kutoa elimu kwa njia ya redio ambayo nina uhakika katika vijiji vyetu wakulima na wafugaji wana uwezo wa kumudu kuwa na redio moja ili wapate elimu bora ya ufugaji na ukulima?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, kwamba kuwapatia vitendeakazi suala hili tumekwishaanza kupitia miradi mbalimbali, kupitia ASDP, kupitia PADEP kitu tunachokifanya ni kuendelea kuwapatia vitendeakazi ikiwa ni pamoja na vyombo vyta usafiri na wakati mwingine pia kuwapatia vitendeakazi Mabwanashamba ambavyo wanahitaji pale wanapokuwa katika mashamba.

Lakini la pili linalofanana na hilo tunataka kuliboresha ni usimamizi wa mabwana shamba hawa au Maafisa Ugani kwa sababu kule waliko tunahitaji kusimamia kwa karibu na kufanya hivi lazima tushirikiane na Halmashauri na sisi wenyewe tukiwa Wizarani si rahisi. Kwa hiyo, ni yote mawili kwamba vitendea kazi pamoja na kuwasimamia ili waweze kutumiza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, la pili napenda tu nishukuru na nikubali ushauri wake na ushauri huu tunaendelea nao kupitia ukulima wa kisasa tunafanya kama Mheshimiwa Mbunge anavyopendekeza lakini nakubali kwa kifupi kwamba ushauri huu ni mzuri na tutaendelea kupanua elimu kwa wakulima kupitia vyombo mbalimbali. (*Makofi*)

Na. 341

### **Msongamano Mkubwa wa Mahabusu Magerezani**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna msongamano mkubwa wa mahabusu katika Magereza yetu hali inayoelezwa kuchangiwa na kuchelewa kwa upelelezi wa kesi na kusababisha Mahakama zishindwe kuamua kesi.

Je, Serikali inachukua hatua gani na za haraka kuondoa kero hii kubwa inayowasumbua wananchi?

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani ambao kwa sasa wanahifadhiwa wastani wa wafungwa na

4 JUNI, 2013

mahabusu 38,000 kwa siku ukilinganisha na uwezo wake Kisheria wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,552 na hivyo kusababisha kuwepo kwa msongamano.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua tatizo hili, Serikali kuititia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeshachukua hatua ya kuunda kikosikazi chini ya Mkurugenzi wa Mashitaka nchini, kushughulikia tatizo la msongamano Magerezani na kutoa mapendekezo yake kwa Serikali juu ya hatua za kuchukua. Aidha ni kweli kuwa zipo changamoto za upelelezi zinazochangia kukwama kwa baadhi ya kesi Mahakamani hasa kesi kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo na kwa kutumia maoni ya kikosi kazi na wadau wengine wa Haki Jinai, Serikali kuititia ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai (*DPP*) na Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (*DCI*) inafanya ukaguzi wa pamoja kwenye Magereza hapa nchini ili kuondoa kesi ambazo hazina ushahidi wa kutosha kuwapatia dhamana kwa utaratibu wa kuwekwa chini ya uangalizi wa Idara ya Huduma kwa Jamii washtakiwa ambao kesi zao zinadhamana ili wamebaki gerezani kwa kukosa ndugu wa kuwadhamini.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zilizochukuliwa na Serikali kuititia Jeshi la Polisi ni pamoja na kuongeza kasi katika kufanya vikao vya kusukuma kesi (*Case Flow Management*) katika ngazi zote za mfumo wa Haki Jinai, kufanya Ukaguzi wa Upelelezi (*Investigation Clinics*) kila baada ya miezi mitatu ili kuwabaini wapelelezi wazembe ili kujua kufanya vikao vya pamoja kati ya waendesha mashtaka na wapelelezi ili kujua changamoto zinazokabili idara hizi mbili na kuzitatau kwa pamoja kwa lengo la kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Aidha, elimu kwa wapelelezi na waendesha mashtaka nchini inatolewa kuhusu uelewa wa dhana ya *Civilianization* ili kuwajengea uwezo wa kiutendaji. Vilevile, majalada ya upelelezi wa kesi kubwa kama mauaji, kubaka, madawa ya kulevyaa na uhalifu kwa njia ya mtandao hutolewa kwa kuzingatia taaluma na uwezo binafsi wa

Mpelelezi. Jeshi la Polisi pia linatumia vikosi kazi vya wataalam waliobobebe katika upelelezi ngazi ya Taifa na Mkoa ili kukamilisha upelelezi mapema. (*Makof*)

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tumekuwa tukishuhudia watu wenyewe majina makubwa, matajiri na sasa mpaka wasanii kesi zao upelelezi ukipelekwa harakaharaka katika hali ya kustaajabisha. Umekwenda hivyo mpaka wafanyabiashara wa madawa ya kulevywa wakiwemo wapakistan ambao kesi yao ilienda kwa haraka na kupelekeea kupewa dhamana ili hali ikiwaacha Watanzania maskini wenyewe kesi za simu, kuku wakiendelea kusota magerezani.

Je, Serikali inabagua raia wake katika kutoa haki?

Swali la pili, kumekuwa na tabia chafu iliyooza kwenye Jeshi la Polisi la ubamikizaji wa kesi na ubadilishaji wa vielelezo. Tumeshuhudia madawa ya kulevywa yakibadilika na kuwa dona yanapofika Mahakamani na tumeshuhudia watu wakibambikiwa mpaka mafuvu ya vichwa Tanzania sasa hivi.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa Jeshi la Polisi katika jambo hili chafu na la kutisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu upelelezi na ubaguzi. Inawezekana kuna mifano ambayo ye ye anaifahamu ya kuwa kesi zimekwenda haraka na zikaashiria rushwa au ubaguzi.

Lakini ndani ya Serikali hakuna mpango wa kufanya ubaguzi kwa makusudi na lengo hasa la upelelezi ni kutafuta ushahidi wa kutosha ili haki itendeke. Kwa hiyo, kama kuna maelezo yoyote anayo kuhusu ukweli alio nao wa ubaguzi basi naomba anipatie ili tuufanyie kazi na tuweze kujua vipi. Lakini muhimu ni kuhakikisha kwamba upelelezi unafanywa kwa kila daraja wala ubaguzi usiwe sehemu ya kutoa matokeo ya upelelezi.

4 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, la pili la ubambikiaji kesi. Nakubaliana naye kwamba kuna elements sasa hivi kwenye Jeshi la Polisi ambazo zinakiuka maadili ya kazi ya Jeshi la Polisi. Kama tunavyoona Serikali na Jeshi lenyewe linachukua hatua tunaporidhika kwamba hili limefanyika na nakumbuka hivi karibuni tu kulikuwa na tukio hapa karibu Kilosa, Dumila na wale waliofanya vile tumewafukuza na kuwaondoa kwenye Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe wito kwa Jeshi la Polisi au askari wote kwamba Serikali haitavumilia uovu kama huu na tutachukua hatua ikiwemo kuwafukuza kazi lakini pia kuwafungulia kesi za jinai kwenye Mahakama za kawaida.

Na. 342

#### **Kusambaza Umeme katika Vijiji vya Jimbo la Kwela**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA** aliuliza:-

Umeme umekuwa ni kikwazo kikubwa cha shughuli za kiuchumi katika Ukanda wa Bonde la Ziwa Rukwa hususan katika vijiji vya Muze, Mtowisa, Mfinga, Milepa, Kaoze, Kipeta, Kilyamatuandua, Kilangawana, Kapenta na Nankanga:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika maeneo hayo?

(b) Je, ni lini Serikali itatumia vyanzo vya umeme vya Mto Nzovwe na Momba vyenye uwezo wa kutoa megawati 18 kwa pamoja na kusambaza umeme katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia *TANESCO* ilishafanya tathmini ya kupeleka umeme katika ukanda wa Bonde la Ziwa Rukwa. Mradi huu utahusisha vijiji vya Muze, Mtowisa, Mfinga, Milepa, Kaoze, Kipeta, Kilyamatuandua, Kilangawana, Kapenta na Nankanga. Mradi huu unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 5.44/- na kuunganisha wateja wa awali wapatao 1,505. Kwa sasa Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*) inatafuta fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika maeneo hayo.

(b) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Momba imeingia makubaliano na kampuni iitwayo *CAMsky* ya Marekani kwa ajili ya kuendeleza maporomoko ya Momba. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwaa kuanza kabla ya mwisho wa mwaka huu (2013). Uendelezaji wa maporomoko ya Mto Nzovwe unategemea upatikanaji wa mwendelezaji.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ufanuzi mzuri wa Naibu Waziri lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Serikali ilishapanga kupeleka umeme katika Mji mdogo wa Laela na kushushwa katika Kata ya Kaengesa, Sandamngano, Sandurura, Huwi Kalambazite na Lusaka. Je, kwanini isiflikishe Kata ya Miangalua na kijiji cha Ntunko ambacho ni kilomita nne kutoka Laela na kuna huduma kama ya Zahanati na Shule ya Sekondari?

Pili, ni lini sasa umeme utapelekwa Laela ukizingatia kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni Halmashauri ya siku nyingi lakini haina hata kijiji kimoja chenye umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Malocha kwa kweli anavyofuatilia miradi ya umeme katika Jimbo lake. Niwahakikishie wananchi wa Laela kwamba katika awamu hii ya utekelezaji wa *REA Phase Two* Laela itapata umeme ikiwa ni pamoja na mtiririko wa vijiji vyote ambavyo vimetajwa ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevitaja.

Hili analolisema la Kata ya Nyangarua ambayo iko kilomita nne tu tunaweza kuliangalia wakati wa utekelezaji kwa sababu zile scope za kazi zinakuwa zinabadilika hasa tukienda kwenye utekelezaji kwenye field kabisa. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane tuone nini tunaweza tukafanya kwa umbali mdogo wa kiasi hicho na kama kweli tutaona una tija kuwapelekea umeme tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, niwaondoe mashaka wananchi wa Leila na Jimbo lake kwa ujumla kwamba Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi nzuri na tutendelea kufanya msaada huu kwa wananchi ili waweze kupata huduma hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha na tumekopa. Nina tangazo moja tu la Mwenyekiti wa *CPA Branchya Tanzania*, Mheshimiwa Zungu anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa chama cha Wabunge wa Jumuiya ya Madola yaani *CPA Tanzania Branch* kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa na kikao muhimu katika chumba namba 133. Kwa hiyo, wajumbe wa Kamati wa *CPA Branch* watakuwa na kikao hicho.

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2013/2014 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii**

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDII:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kukubali kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii kwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia, kwa mara nyingine kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu nikiwa na afya njema. Pili ningependa kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe; Kaimu Katibu Mkuu Ndugu Selestine Muhochi Gesimba pamoja na Kamishna wa Elimu, Prof. Eustella Bhalalusesa.

Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali za elimu zilizo chini ya Wizara yangu; Viongozi katika ngazi mbalimbali, walimu na watumishi wengine wote, kwa ushirikiano walionipa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na maandalizi ya bajeti hii. Shukurani zangu pia ziwaendee viongozi wa vyama vyta wafanyakazi na vyama vyta wanataaluma, wanafunzi na washirika wa maendeleo, kwa ushirikiano wao katika kuiendeleza sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kutumia fursa hii kuwapa pole wale wote walipatwa na majanga, pamoja na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali yaliyotokea nchini kwetu hivi karibuni. Kwa namna ya pekee, ninachukua nafasi hii kutoa pole kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wote kwa ujumla, kwa kuondokewa na Mbunge wa Chambani, Marehemu Salim Hemed Khamis (*CUF*).

Aidha, ninachukua fursa hii kuwapa pole wananchi wote kwa ajali ya kuporomoka kwa ghorofa iliyotokea jijini Dar es Salaam tarehe 29 Machi 2013, pamoja na maporomoko ya udongo yaliyotokea katika machimbo ya Moshono katika Manispaa ya Arusha.

Vilevile, ninachukua nafasi hii kuwapa pole wakazi wa Arusha pamoja na Watanzania wote kwa ujumla kwa mlipuko wa bomu uliotokea katika kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi la Parokia ya Olasiti Arusha.

Tunawaombea kwa Mungu majeruhi wote waliooko hospitalini na majumbani ili waweze kupona haraka. Mungu mwenye rehema azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Aidha, Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu, wale wote walioondokewa na wapendwa wao kutokana na ajali hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, ninapenda sasa kuchukua fursa hii kufanya mapitio ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, majukumu ya kisera na ya kiutendaji, Utekelezaji wa Mpango wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kuwasilisha Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 na utekelezaji wake. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Sekta ya Elimu ilielekezwa kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 85(a) - Elimu ya Awali.

(i) Kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi ina darasa la Elimu ya Awali lenye madawati yanayolingana na mahitaji ya watoto wa elimu hiyo; na

(ii) Kujenga vyoo kwa ajili ya watoto wa Elimu ya Awali ili wasiingiliane na wale wa shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza maelekezo ya ilani ya uchaguzi katika eneo hili, jumla ya Shilingi bilioni tano (bil. 5) zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa madawati pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Ninapenda kuzikumbusha Halmashauri zote kutumia fedha hii kununulia madawati na vifaa hivyo ili kuinua ubora wa mazingira ya kufundishia na kujifunzia na Elimu ya Awali nchini.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(b): Elimu ya Msingi. Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa 'Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Pili' (MMEM II 2007

– 2011) na kuandaa na kutekeleza awamu ya tatu ya mpango huo (MMEM III 2012 – 2016).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza llani ya Uchaguzi, Serikali ilifanya tathmini ya MMEM II na kukamilisha andiko la ‘Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya III’ (MMEM III) ambalo liliidhinishwa na kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu mwezi Novemba, 2012.

Lengo la mpango huu ni kutoa Elimu ya Awali na Msingi iliyo bora kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule. Andiko la mpango huo lilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili kutoa fursa kwa wadau wa ngazi zote kulielewa kwa urahisi na hivyo kurahisisha utekelezaji wake.

Aidha, mlongozo 7 ya utekelezaji wa MMEM III iliandaliwa ili kuimarisha utekelezaji wa mpango. Andiko la MMEM III pamoja na miongozo yake itasambazwa na kutolewa mafunzo elekezi kwa wadau katika mwaka huu (2013) kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(c): Elimu ya Sekondari. Kusimamia kwa ukamilifu utekelezaji wa ‘Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili’ (MMES II 2010 - 2015), kuandaa na kutekeleza awamu ya tatu (MMES III).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hii, Serikali ilianda Hadimu za Rejea kwa ajili ya tathmini ya muda wa kati ili kubaini mafanikio ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya MMES na kuwezesha maandalizi ya Awamu ya Tatu ya MMES III. Aidha, mafanikio makubwa ya utekelezaji wa ‘Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari’ (MMES).

Awamu ya Kwanza yamejidhihirisha katika ongezeko la idadi ya shule na wanafunzi. Ili kukabiliana na changamoto zilizotokana na ongezeko hili, Serikali, kuitia ‘Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili’ (2010-2015) imeweka mkakati wa kuimarisha miundombinu ya shule

1,200 za sekondari za serikali kwa awamu tatu, ili ziweze kufikia kiwango kinachokubalika cha kuifanya kila moja kuwa shule iliyokamiliika (*functional school*). Awamu y kwanza ya ukarabati itajumuisha shule 264, na awamu ya pili itakuwa na shule 528. Aidha shule 408 zitaimarishwa katika awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la upungufu wa walimu katika shule zetu, walimu hupangwa katika kila Halmashauri kila mwaka kwa kuzingatia uwezo wa ajira na uwiano wa mahitaji katika Halmashauri husika.

Katika kutekeleza azma hii mwaka 2012/2013, jumla ya walimu 14,060 wakiwemo 7,835 wa ngazi ya shahada na 6,225 wa ngazi ya stashahada wallajiriwa na kupunguza pengo la walimu kutoka asilimia 50.2 hadi asilimia 36.6.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu wa vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kujifunzia, Serikali ilitoa Ruzuku ya Uendeshaji (*Capitation Grant*) ya wastani wa Sh. 13,266 kati ya Sh. 25,000 kwa kila mwanafunzi wa Shule za Sekondari za Serikali, hadi Machi, 2013. Aidha, Serikali iliendesha mafunzo kwa watendaji wapya 1,259 wa Halmashauri, ili kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kuinua ubora wa utoaji wa elimu katikangazi ya sekondari, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (*Japan International Cooperation Agency (JICA)*), ilitoa mafunzo kazini kuhusu mbinu bora za ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha kwa walimu 10,584 kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara. (*Makofii*)

Aidha, walimu 338 wa mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Morogoro, Mbeya na

Dodoma, walipata mafunzo kuhusu matumizi ya Vivunge  
vya Sayansi (*Science Kits*).

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(d): Elimu ya Ualimu.

(i) kusimamia kwa kamilifu utekelezaji wa Mkakati  
wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu (*Teacher  
Development and Management Strategy – TDMS*) katika  
utoaji wa mafunzo ya ualimu; na

(ii) kuandaa walimu wengi wa Elimu ya Awali na  
kuwapanga katika shule zinazohusika.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea kusimamia  
utekelezaji wa Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya  
Walimu ambao lengo lake kuu ni kuhakikisha kuwepo kwa  
walimu na wakufunzi mahiri na wanaotosheleza mahitaji  
katika ngazi za Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Elimu ya  
Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, Vyuo vya Elimu  
ya Ufundji pamoja na Vyuo vya Ualimu.

Katika kutekeleza azma hii, Wizara iliendelea  
kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vyuo vya ualimu nchini  
ambapo vyuo vya ualimu viliongezeka kutoka 105 (vya Serikali  
34) mwaka 2011/2012 hadi 122 (vya Serikali 34) mwaka 2012/  
2013 na hivyo kuongeza udahili wa wanachuo kutoka 43,258  
mwaka 2011/2012 hadi 49,715 mwaka 2012/2013.

Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya utekelezaji wa  
programu ya 'Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Elimu ya Msingi'  
(MWAKEM) ngazi ya shule, ili kuinua ubora wa mafunzo ya  
walimu kazini, ambapo imeonesha mafanikio na hivyo  
kuwezesha kufanya maandalizi ya upanuzi wa utekelezaji wa  
programu kitaifa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundzi, ilifanya mapitio ya Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu ngazi ya Cheti, ambao hapo awali ulijumuisha Elimu ya Awali. Mapitio haya yalibainisha umuhimu wa kuwa na Mtaala wa Elimu ya Awali pekee kwa kuzingatia mahitaji ya elimu ya sasa. Hivyo, kuanzia mwaka wa masomo 2012/13, Wizara ilianza kupokea wanachuo kwa ajili ya kusomea mchepuo huo katika Chuo cha Ualimu cha Singachini, ambapo jumla ya walimu wanafunzi 37 waliandikishwa kwa ajili ya mafunzo haya. Aidha, katika mwaka 2013/14 Wizara inatarajia kutoa mafunzo haya kwa walimu 1,000 katika Vyuo vya Ualimu vya Kabanga, Kinampanda, Mhonda, Mandaka, Nachingwea, Mpuguso Tarime pamoja na Singachini.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(e): Elimu ya Juu; Kusimamia kwa ukamilifu Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu. Katika kutekeleza lengo hilo Wizara illimarisha miundombinu katika Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki kupitia Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Wizara iliendelea na ujenzi wa kumbi za mihadhara sita na ukarabati wa madarasa saba na ofisi kwa ajili ya wanataaluma. Aidha, Wizara iliendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza katika Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam eneo la Buyu Zanzibar.

Katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Wizara iliendelea na ujenzi wa maabara, kumbi za mihadhara na ofisi kwenye idara za Uchumi-Kilimo na Biashara (*Agricultural Economics and Agribusiness*), Sayansi na Teknolojia ya Chakula (*Food Science and Technology*) na Uhndisi Kilimo. Wizara iliendeleza ujenzi wa jengo la ghorofa kumi litakalotumika kwa ajili ya vyumba vya semina, kumbi za mihadhara, maabara, maktaba na ofisi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Wizara ilijenga maabara ya biologija. Aidha, Wizara iliendeleza ujenzi wa mifumo ya majisafi na majitaka, mfumo wa umwagiliaji na jengo la kufanya majaribio, ili

4 JUNI, 2013

kuwawezesha wanafunzi kufanya mafunzo kwa vitendo katika Chuo Kikuu Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(f): Mafunzo ya Ufundii; Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo, mwaka 2012/2013, Wizara yangu ilikamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi wa miaka mitano utakaotekeliza kuanzia mwaka 2013/2014 hadi 2017/2018, wenyе vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuongeza udahili katika Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi;

b) Kuinua ubora wa Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi; na

(c) Kuweka mfumo bora wa ufuatiliaji na tathmini ya Elimu ya Ufundii na Mafunzo ya Ufundii Stadi.

Mheshimiwa Spika, Ibara 85(g): Wizara itatekeleza yafuatayo katika Elimu ya Watu Wazima yenye Manufaa:-

(i) Kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Elimu ya Watu Wazima yenye manufaa nchini kote;

(ii) Kuimarisha Mipango ya Elimu ya kuijendeleza ikiwa ni pamoja na Elimu Masafa na Ana kwa Ana;

(iii) Kuimarisha utoaji wa elimu nje ya mfumo rasmi kupitia Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Watoto Walioikosa (MEMKWA) kwa kushirikiana na wadau wengine;

(iv) Kuinua ubora wa Elimu ya Watu Wazima kupitia Mpango wa Uwiano Kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA); na

(v) kuimarisha uwezo wa watendaji katika usimamizi na menejimenti ya programu za elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Serikali ilikamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Watu Wazima Nje ya Mfumo Rasmi wa Mwaka 2012/13 – 2016/17, unaolenga katika kupanua upatikanaji wa fursa za elimu na hivyo kupunguza idadi ya wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu; kuinua ubora wa elimu itolewayo nje ya mfumo rasmi na kujenga uwezo wa watendaji katika kupanga, kuratibu, kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango huo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imekabidhiwa majukumu ya kuweka na kusimamia viwango vya ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi katika ngazi za Elimu ya Awali na Msingi; Elimu ya Sekondari; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo rasmi; Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi; Elimu ya Ualimu; Elimu ya Juu, Usajili wa Shule na Ukaguzi wa Shule na Vyuo vya Ualimu pamoja na Taasisi za kielimu zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia, ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa utoaji wa elimu kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini, pamoja na kufanya mapitio, kuandaa na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya Sera, Mipango, Sheria na Kanuni za Elimu zilizopo, kulingana na mabadiliko ya dhima na Dira ya Taifa; na kuandaa mikakati ya utekelezaji wake. Aidha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ndiye msimamizi mkuu wa masuala ya taaluma katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada zake za kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi nchini, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa takriban miaka kumi iliyopita, imekuwa ikitekeleza mipango mbalimbali ya elimu chini ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (*Education Sector Development Programme ESDP*), ambapo mafanikio na

changamoto zake zimekuwa zikitolewa taarifa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mipango hiyo ni Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya III (MMEM III); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya II (MMES II); Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu; Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (MMEJU) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU). Utekelezaji wa mipango hiyo, umeleta mafanikio mbalimbali na kuibua changamoto kadhaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali, inapenda kutambua mchango wa wadau wote wa elimu katika kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo ambao umefanikisha kuongeza fursa katika ngazi zote za elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai 2012 hadi Aprili 2013, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, imepata mafanikio yafuatayo:-

- (a) Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo – 2012 pamoja na mkakati wa utekelezaji wake ilikamilika kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali wa elimu;
- (b) Walimu 10,584 wa shule za sekondari walipata mafunzo kazini katika ufundishaji wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lughaa;
- (c) Walimu wapya 14,060 (wa Shahada – 7,835, wa Stashahada – 6,225) walipangiwa vituo vya kazi katika Halmashauri zote nchini na kufanya idadi ya walimu wote katika shule za sekondari nchini kuwa 65,529 na hivyo kupunguza pengola walimu kutoka asilimia 50.2 mwaka 2011/12 hadi asilimia 36.6 mwaka 2012/13;
- (d) Walimu 338 wa shule za msingi kutoka Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Morogoro, Mbeya na Dodoma walipata mafunzo ya

matumizi ya vivunge vyatya sayansi ili kuimarisha ufundishaji wa somo la sayansi;

(e) Wanafunzi 1,196 walipewa mafunzo ya ukutubi na uhifadhi nyaraka (cheti – 502, stashahada – 545 na mafunzo ya muda mfupi – 149);

(f) Udhili katika Vyuo vya Ualimu uliongezekwa kutoka wanachuo 43,258 (24,243 Vyuo vya Serikali) katika mwaka wa masomo 2012, ambapo Walimu wa Elimu Maalumu walikuwa 188 hadi wanachuo 49,715 (25,133 Vyuo vya Serikali) katika mwaka wa masomo 2013, ambapo wanachuo 332 walikuwa wa Elimu Maalumu;

(g) Walimu 100 kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi walipatiwa mafunzo kabilishi kuhusu mitaala ya Mafunzo ya Ufundidi Stadi na Utoaji wa Mafunzo kwa Kuzingatia Umahiri (*Competence-Based Education and Training*);

(h) Jumla ya vitabu 25,516 viliongezekwa katika maktaba za Taifa. Kati ya hivyo, 468 vilipatikana kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 1975 inayomtaka kila mchapishaji, kuwasilisha Maktaba kuu, nakala mbili za kila kitabu anachokichapisha, wakati 24,984 vilipatikana kwa njia ya msaada na 64 vilinunuliwa na hivyo kufanya idadi ya vitabu vyote katika Maktaba nchini kufikia 1,210,473;

(i) Wanafunzi 560,706 (wasichana 281,460), kati ya wahitimmo 886,946 wa Elimu ya Msingi, walichaguliwa kuijunga na Kidato cha Kwanza katika Shule za Serikali mwezi Januari, 2013;

(j) Wanafunzi 546 (wasichana 291) kati ya 2,850 wenyewe ulemavu wa aina mbalimbali walichaguliwa kuijunga na Kidato cha Kwanza katika shule za Serikali Januari, 2013. Hili ni ongezeko la asilimia 33.9 ya wanafunzi wenyewe ulemavu waliojiunga na elimu ya sekondari mwaka 2013 ikilinganishwa na waliojiunga mwaka 2012;

(k) Idadi ya wanafunzi waliogharimiwa masomo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliongezeka kutoka wanafunzi 93,176 mwaka 2011/2012 hadi 95,594 mwaka 2012/2013 ;

(l) Andiko la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya III (MMEM III) lilikamilika na kuidhinishwa na kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu mwezi Novemba, 2012 na kutafsiriwa katika Lugha ya Kiswahili ili kutoa fursa kwa wadau wa ngazi zote kulisoma na kulielewa;

(m) Andiko la Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (MMEU) wenye lengo la kujenga nguvu kazi yenye uwezo wa kuhimili ushindani wa soko la ajira, kwa kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi nchini, lilikamilika na kuidhinishwa na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu;

(n) Maandalizi ya miongozo sita kwa ajili ya utoaji wa Elimu ya Awali yalikamilika na kufikia hatua ya kuchapwa;

(o) Ujenzi wa maabara ya bayolojia katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ulianza na maabara ya Kompyuta ilijengwa katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Zanzibar;

(p) Madarasa matano yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja na maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kwa wakati mmoja vilijengwa katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara cha Moshi;

(q) Mabweni ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili yaliyoko Muhimbili na Chole yalifanyiwa ukarabati mkubwa;

(r) Mpango Kabambe (*Master Plan*) kwa ajili ya kuendeleza eneo la Mloganzila ulikamilishwa na michoro ya Hospitali iliandaliwa. Aidha, *Dar es Salaam Water and Sewerage Authority (DAWASA)* na *Dar es Salaam Water*

*Supply and Sewerage Corporation (DAWASCO)*, zilifanya upembuzi yakinifu ili kubaini uwezekano wa kuweka mtandoa wa maji ya visima pamoja na ya bomba kutoka mtambo wa maji wa Ruvu Juu;

(s) Vyuo vya Ualimu vitatu (Patandi, Vikindu na Bustani), vilikarabatiwa na ujenzi wa majengo mapya kufanyika ili kukiwezesha kila chuo kudahili wanafunzi wengi zaidi. Uwezo wa sasa wa Chuo cha Ualimu cha Patandi ni kudahili wanachuo 350. Baada ya kukarabatiwa kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanachuo 560. Uwezo wa Chuo cha Ualimu cha Vikindu ni kuchukua wanachuo 384 na baada ya kukarabatiwa kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanachuo 550. Uwezo wa Chuo cha Ualimu cha Bustani ni kuchukua wanachuo 240 na baada ya ukarabati kitaweza kuchukua wanachuo 700;

(t) Utafiti wa chanjo ya UKIMWI katika Programu ya Tanzania na Msumbiji iitwayo *Tanzania and Mozambique HIV Vaccine Programme (TaMoVacP)* uliendelea kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili, ambapo majoribio ya kubaini namna bora ya utoaji wa chanjo dhidi ya VVU yalifanyika katika Majiji ya Dar es Salaam, Mbeya pamoja na Maputo (Msumbiji);

(u) Utafiti wa kutambua muda ambao dawa ya *Artemether-Lumefantrine ALU* inatumia kuua vimelea vya malaria (*Malaria Parasites*) uliendelea kwa kutumia kipimo cha *Malaria Rapid Diagnostic Test (MRDT)*. Matokeo ya utafiti yameionesha ALU kuwa na ufanisi wa asilimia 100. Hivyo, *MRDT* imeingia katika Sera ya Taifa kwa ajili ya utekelezaji katika nchi nzima; na

(v) Wanafunzi 30 raia wa Uganda na 10 raia wa China wanaosoma katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Ardhi na Muhimbili na Watanzania 87 walioko Msumbiji, walidhaminiwa chini ya mpango wa kubadilishana wanafunzi baina ya Tanzania na nchi hizo mbili. Aidha, wahadhiri 31 walioko katika mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu

walidhaminiwa kuptitia Mpango wa *Deutscher Akademischer Austausch Dienst (DAAD)*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa katika utoaji wa Elimu nchini, Sekta ya Elimu imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

- (a) Kuinua kiwango cha ufaulu katika shule za msingi na sekondari;
- (b) Kukidhi mahitaji ya walimu na wahadhiri;
- (c) Kuimarisha upatikanaji wa vifaa vya kutosha vya kufundishia na kujifunzia, hususan vitabu vya kiada na vifaa vya maabara na karakana;
- (d) Kupunguza idadi ya watu wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);
- (e) Kupata vyanzo mbadala na endelevu vya kugharimia elimu, hususan mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;
- (f) Kuongeza fursa za Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi;
- (g) Kuimarisha miundombinu katika Vyuo vya Ualimu, Vyuo Vikuu na Vyuo Vikuu Vishiriki, pamoja na Vyuo vya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi;
- (h) Kuimarisha ukaguzi wa shule ili uweze kufanyika kwa asilimia 50 ya asasi zote za elimu na mafunzo kila mwaka; na
- (i) Kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalumu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa rasilimali zilizopo zinatumika kwa ufanisi na kuleta mabadiliko yenye

tija kwa Wananchi, Serikali iliamua kuwaweka pamoja wataalamu na wadau mbalimbali kutoka katika Sekta sita ikijumuisha Sekta ya Elimu. Wataalamu hawa waliunda vikundi-maabara kulingana na sekta zao kwa ajili ya kuchambua kwa undani vipaumbele vyta sekta husika, namna ya kuvitekeleza, kubaini watekelezaji na kuibua viashiria vyta kupima matokeo, ili kutekeleza kaulimbiu ya 'Pata Matokeo Makubwa Sasa' (*Big Results Now - BRN*).

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Elimu, Wataalamu 34 kutoka katika Idara za Serikali, Sekta Binafsi na Mashirika yasiyokuwa ya Serikali, walishiriki katika Kikundi cha Maabara cha Sekta ya Elimu. Maabara hiyo, iliweka kipaumbele katika kuinua ubora wa Elimu Msingi (*Basic Education*), ambapo ilijikita katika kubaini chanzo cha kushuka kwa ufaulu katika Elimu Msingi na Sekondari na kutafuta mbinu za kukabiliana nayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maongezi humu ndani yanakuwa marefu, halafu wengine kwa taarifa yetu kwenye TV mnaonekana kabisa mmegeuza viti vyenu mnaongea. Jana niliwaona wengine nikashangaa kabisa. Mheshimiwa Waziri endelea!

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Pamoja na changamoto zilizotajwa hapo awali, maabara hii ilibaini sababu zifuatazo kama chanzo cha kushuka kwa ufaulu:-

(a) Uhaba wa walimu, hususan kwa masomo ya Hisabati, Sayansi na *English*;

(b) Mazingira magumu ya kufanya kazi kutokana na ugumu wa kufikika na ukosefu wa huduma muhimu za kijamii;

(c) Utoro wa walimu na mchakato wa kufundisha na kujifunza usioridhisha ambapo ilibainika kwamba kwa wastani asilimia 53 ya muda wa masomo hautumiki kwa kuwafundisha wanafunzi;

(d) Kutotiliwa mkazo kwa ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(e) Uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu;

(f) Kutokuwepo kwa programu za mafunzo kazini ambazo zingewawezesha walimu kukabiliana na mabadiliko katika mitaala; na

(g) Udhaifu katika uongozi na usimamizi wa elimu katika ngazi ya shule.

Mheshimiwa Spika, ili kuahikisha kuwa kiwango cha ufaulu katika mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi na Sekondari kinapanda hadi kufikia asilimia 80 ifikapo mwaka 2015, wataalamu wa Kikundi - Maabarara cha Elimu wamependekeza yafuatayo:-

(a) Kufanya tathmini ya kitaifa ya uwezo wa watoto wa Darasa la Pili katika kumudu stadi za Kusoma, Kuhesabu na Kuandika (KKK) kabla ya kwenda madarasa ya juu;

(b) Kuzipanga shule katika makundi ya ubora kulingana na kiwango cha ufaulu katika mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi na Kidato cha Nne na kuzitangaza katika vyombo vya habari ili kuifahamisha jamii na kuipa fursa ya kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya elimu;

(c) Kutoa mafunzo kwa walimu wa Darasa la I na II kuhusu ufundishaji na ujifunzaji fanisi wa stadi za KKK;

(d) Kutoa mafunzo kwa walimu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Kiswahili, *English* na Hisabati kwa shule za msingi na masomo ya Kiswahili, *English*, Hisabati na Bayolojia kwa shule za Sekondari;

(e) Kuimarisha maslahi ya walimu, ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko yao kwa wakati;

(f) Kutoa motisha kwa shule zitakazoonesha ongezeko katika kiwango cha ufaulu;

(g) Kuimarisha miundombinu ya shule za Sekondari 1,200 ifikapo mwaka 2014;

(h) Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa Ruzuku ya Uendeshaji (*Capitation Grant*) katika Shule za Msingi na Sekondari; na

(i) Kuendesha mafunzo kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari za Serikali kuhusu menejimenti na utawala wa shule.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya kikundi-maabara cha Sekta ya Elimu yanafanyiwa kazi, Wizara iliteua kikosi kazi cha Wizara (*Ministerial Delivery Unit - MDU*) kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa kila siku wa maazimio ya kikundi-maabara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI). Pili, ilifanya mapitio ya miongozo ya usimamizi wa shule katika ngazi ya msingi na sekondari. Aidha, kikosi kazi hiki kimeanza kazi kwa kushirikiana na Tume ya Mpito ya Rais ya kusimamia uwasilishaji wa matokeo ya utekelezaji wa maazimio ya vikundi maabara (*Interim Presidents Delivery Bureau IPDB*), ambapo imebainisha maeneo ya kipaumbele yanayotakiwa kutekelezwa ndani ya miezi sita ili kufanikisha kupatikana kwa matokeo makubwa sasa (*Big Results Now*).

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/13 na kisha nitoe mwelekeo wa Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara kwa mwaka 2013/14.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 na kisha nitoe mwelekeo wa mapato na matumizi ya fedha za Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ilipanga kukusanya maduhuli ya Serikali, yenye thamani ya Shilingi 156,179,258,099. Bajeti ya maduhuli ya Idara ilikuwa Shilingi 5,079,865,300 na ya Taasisi ilikuwa Shilingi 151,099,392,709. Hadi tarehe 31 Machi, 2013, jumla ya Shilingi 99,640,714,509 zilikuwa zimekusanywa, ambazo ni asilimia 63.3 ya makadirio. Kati ya hizo, Shilingi 4,431,943,006 zilikusanywa na Idara; na Shilingi 95,208,771,503 zilikusanywa na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ilitengewa jumla ya Shilingi 724,471,937,000. Kati ya hizo, Shilingi 631,890,621,000 zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 92,581,316,000 zilikuwa ni za maendeleo. Hadi tarehe 31 Machi, 2013, jumla ya matumizi ya kawaida ya Wizara yalikuwa Shilingi 518,933,124,851, ambayo ni asilimia 82.1 ya makadirio na matumizi ya maendeleo yalikuwa Shilingi 45,785,445,106.00, ambayo ni asilimia 49 ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya jumla kuhusu matumizi ya fedha zilizopokelewa, naomba sasa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Kamishna wa Elimu ina majukumu ya kuweka na kudhibiti viwango vya ubora wa elimu na utoaji wa elimu katika ngazi za Awali; Msingi; Sekondari; Mafunzo ya Ualimu; Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Aidha, Ofisi ya Kamishna inaratibu ubora wa elimu kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini kuititia Ukaguzi wa Shule, Ukuzaaji Mitaala, Uendeshaji Mitihani, Huduma za Maktaba pamoja na Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu. Ofisi hii inajumuisha Vitengo vya Elimu Maalumu, Elimu kwa njia ya Redio, Usajili wa Shule, pamoja na Ithibati ya Vifaa vya Elimu na Masuala Mtambuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara kuititia Ofisi ya Kamishna wa Elimu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendelea kuratibu shughuli za taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Kamishna kwa kuendesha vikao vya taaluma na vikao kazi ili kujadili masuala ya uendeshaji wa elimu;

(b) Ilitoa Waraka wa Elimu Namba 5 wa Mwaka 2012 uliorekebisha mihula ya masomo ya shule ambapo Muhula wa Kwanza kwa ngazi zote za Elimu ya Msingi, Sekondari na Mafunzo ya Ualimu, utaanza juma la kwanza la mwezi Januari na kumalizika juma la kwanza la mwezi Juni; na Muhula wa Pili utaanza juma la kwanza la mwezi Julai na kumalizika juma la kwanza la mwezi Desemba kila mwaka, kuanzia mwaka 2013;

(c) Ilitoa Waraka wa Elimu Na. 4 wa Mwaka 2012, unaohusu utaratibu wa kutoa adhabu kwa mwanafunzi au mwanachuo anayeonesha utovu wa nidhamu akiwa mwaka wa mwisho wa masomo;

(d) Iliratibu shughuli za masuala mtambuka kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kutoa Elimu ya VVU, UKIMWI na Afya ya Uzazi shulenii;

(ii) Kufanya mapitio ya kitabu cha Shule Rafiki Kijinsia - Kiongozi cha Mwalimu wa Shule za Msingi;

(iii) Kuendesha mafunzo ya Mpango wa TUSEME ili kuwahamasisha wanafunzi na kuwajengea ujasiri wa kusema, hususan katika masuala ya kijinsia;

(iv) Kukamilisha andiko la kitaifa kuhusu masuala ya Usafi wa Mazingira na Maji Safi na Salama Shuleni (*School Water Sanitation and Hygiene - SWASH*);

(v) Kuendesha mafunzo kwa wadau wa elimu kuhusu kuingiza dhana ya ufundishaji wa Elimu ya Ujasiriamali katika masomo ya Elimu ya Msingi na Sekondari nchini;

(vi) Kukamilisha Mkakati wa Uendeshaji wa Elimu ya Kijiandaa na Kujikinga na Maafa na Majanga Shulen;

(vii) Kufanya utafiti kuhusu tabia hatarishi katika Afya ya Uzazi na Maambukizi ya VVU mionganoni mwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Vituo vya Ufundisti na kuandaa mwongozo wa namna ya kujiepusha na tabia hatarishi mionganoni mwa wanafunzi wa Vyuo Vikuu na Vituo vya Ufundisti;

(e) Iliendelea kusajili shule na Vyuo vya Ualimu na kutoa leseni za kufundisha kwa:-

(i) Kusajili shule 81 kati ya maombi 87 yaliyowasilishwa ambapo, 37 ni shule za sekondari (za Serikali 14); 4 ni za Awali na 40 ni za Awali na Msingi,;

(ii) Kusajili Vyuo vya Ualimu 6 visivyo vya Serikali kati ya maombi 12 yaliyowasilishwa;

(iii) Kuridhia maombi 51 ya kujenga shule, kati ya 94 yaliyopokelewa;

(iv) Kuthibitisha wenge shule na mameneja wa shule 67 kati ya 127 walioomba;

(v) Kutoa leseni za kufundisha 133 kati ya maombi 143 yaliyopokelewa kutoka kwa wataalamu wa kigeni na leseni 10 kati ya maombi 15 yaliyopokelewa kutoka kwa wataalamu wa Kitanzania ambao hawakusomea ualimu;

(f) Iliandaa vipeperushi kwa lengo la kutoa elimu kwa wadau wa elimu kuhusu taratibu za usajili wa shule na walimu;

(g) Ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 546 (wasichana 291) wenge ulemavu wa aina mbalimbali kwa ajili ya kujunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2013 ambapo wasioona ni 237 (wasichana 117); viziwi 175 (wasichana 80); wenge ulemavu wa akili 13 (wasichana 05); na wenge

ulemavu wa viungo 121 (wasichana 53). Idadi ya wanafunzi wenyewe ulemavu waliojiunga na Elimu ya Sekondari mwaka huu iliongezeka kwa asilimia 33.9 ikilinganishwa na mwaka 2011/2012;

(h) Ilinunua mtambo wa kisasa wa kuchapia vitabu vyatya maandishi ya nukta nundu (*Braille*) kwa ajili ya wanafunzi wasioona wa shule za msingi na sekondari nchini; na

(i) Ilianda na kutangaza vipindi vyatya elimu kupitia TBC Taifa kama ifuatavyo: Masomo ya Elimu ya Shule za Msingi kwa njia ya Redio (vipindi 600); na Elimu ya Ualimu kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji (vipindi 96).

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Msingi; Kitengo cha Elimu ya Msingi kina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo katika ngazi ya Awali na Msingi. Aidha, Kitengo cha Elimu ya Msingi kinasimamia ubora wa utoaji wa elimu kwa usawa kwa Darasa la I - VII, kwa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Elimu ya Msingi itolewayo nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Kitengo cha Elimu ya Msingi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji, upatikanaji na matumizi ya vifaa sahihi vyatya kufundishia na kujifunzia pamoja na miundombinu ya shule katika Elimu ya Awali Akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2013/2014 na Msingi katika mikoa 14 ya Tanzania Bara (Morogoro, Dodoma, Njombe, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Singida, Rukwa, Manyara, Mbeya, Mtwara, Simiyu, Tanga na Tabora), mwezi Oktoba, 2012;

(b) Ilipanga walimu wapya 13,633 wa ngazi ya cheti katika vituo vyatya kazi. Kati ya hao, walimu 13,592 walipangwa katika Halmashauri na walimu 41 walipangwa katika shule za msingi za mazoezi;

(c) Ilifanya ufuatiliaji wa uendeshaji wa Mitihani ya Darasa la IV, Mitihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi na Mitihani wa Ufundu Stadi, katika Halmashauri tisa ambazo ni Temeke, Ilala, Kinondoni, Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini, Bagamoyo na Kisarawe, ili kubaini wanafunzi wenye matatizo katika ujifunzaji, kwa mfano wasiojua KKK kwa Darasa la IV na waliofeli na sababu za kufeli ili kupata ufumbuzi wake;

(d) Ilifanya tathmini ya MMEM II ambapo ilibaini kwamba upungufu wa fedha uliathiri kufikiwa kwa malengo yaliyopangwa, ambayo ni kuongeza uandikishaji, kuinua ubora wa elimu, kujenga uwezo pamoja na uimarishaji wa taratibu za kitaasisi. Ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Tatu wa Mwaka 2012-2016 (MMEM III 2012 - 2016) ulianzishwa. Mpango huu unalenga katika kuongeza ujuzi, uhudhuriaji na uhitimu katika Elimu ya Msingi na kuandaa watoto kwa ajili ya maisha katika jamii yenye mila na desturi mbalimbali;

(e) Ilianda miongozo saba ya uendeshaji wa MMEM III pamoja na miongozo sita kwa ajili ya Elimu ya Awali. Miongozo hii iliidhinishwa na Kamati ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu na ipo katika hatua za kuchapwa;

(i) Iliratibu mpango wa chakula shulenii unaofadhiliwa na mpango wa chakula duniani (*World Food Programme – WFP*) kwa kufanikisha yafuatayo: Kutoa mafunzo ya uendeshaji kwa watendaji 354 wa mpango; na kutoa mafunzo kwa watendaji 180 kutoka Halmashauri za Meru, Arusha, Mbulu na Kongwa ambapo sasa wanaendelea na mpango wa Chakula na Lishe Shuleni wenyewe;

(f) Ililikamlisha Rasimu ya Kwanza ya Mwongozo wa Ufundishaji wa Somo la Sayansi kwa Vitendo;

(h) Ilitoa mafunzo elekezi kwa wasimamizi wa Elimu ya Awali ngazi ya Kata na Wilaya katika Halmashauri za Hai,

Siha, Monduli, Makete, Bagamoyo, Temeke, Mtwara (V) na Magu; na

(i) Iliendesha mafunzo ya kujenga uwezo na kutoa mwongozo wa namna ya kuimarisha ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, ambapo wataalamu 20, wakiwemo wakufunzi wa vyuo vya ualimu na maafisa kutoka Makao Makuu, walishiriki.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Elimu ya Sekondari kina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu katika ngazi ya Elimu ya Sekondari, pamoja na kusimamia utoaji bora wa elimu kwa usawa kwa kidato 1 – 6, kuweka viwango na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu ya sekondari itolewayo nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara yangu kupitia Kitengo cha Elimu ya Sekondari, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilianza Tathmini ya Mahitaji na Gharama za Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Shule 528, ambayo inatarajiwa kukamilika tarehe 30 Mei, 2013;

(b) Ilivezesha utoaji wa mafunzo kwa walimu 10,584 wa masomo ya Sayansi, Hisabati na Lugha ili kuinua ubora wa ufundishaji na ujifunzaji wa masomo hayo;

(c) Ilifanikisha utoaji wa mafunzo kwa watendaji 396 (watendaji 3 kutoka kila Halmashauri – Afisa Elimu Sekondari, Mhandisi na Afisa manunuzi) ili kuwajengea uwezo katika usimamizi na uendeshaji wa MMES II;

(d) Ilivezesha ufuatiliaji na tathmini ya matumizi sahihi ya fedha ya ruzuku ya MMES II, kwa kutumia Wakaguzi wa Ndani na wa Nje, kwenye Halmashauri zote;

(e) Iligharimia mafunzo ya kuwajengea uwezo Maafisa 17 wanaosimamia shughuli za MMES;

(g) Iliratibu kazi ya uchaguzi wa wanafunzi 560,706 (wasichana 281,460) katи ya 865,827 waliofanya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, kwa ajili ya kujunga na Kidato cha Kwanza Januari, 2013 kwa Shule za Serikali;

(i) Iliendesha mafunzo ya walimu wa sayansi kuhusu matumizi ya vivunge vya sayansi (*Micro Science-Kits*) kwa ajili ya shule 180 chini ya Mradi wa UNESCO kama ifuatavyo: Wawezeshaji 24 walijengewa uwezo wa namna ya kutoa mafunzo kwa kutumia vivunge vya sayansi kwa walimu; na jumla ya walimu 418 wa sayansi wa Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Tanga, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Morogoro, Mbeya na Dodoma kutoka shule 180 wakiwemo wakuu wa shule 80 wa shule zilizo katika Mradi wa Vivunge vya Sayansi kutoka Mkoa wa Tanga, Shinyanga, Mwanza na Morogoro, walipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya vivunge vya Sayansi;

(h) Iligharimia mafunzo ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa ajili ya walimu 450;

(i) Iligharimia uchapaji na usambazaji wa nakala 439,135 za vyeti vya wahitimu wa Kidato cha 4 na cha 6; na

(ii) Ilipangia vituo vya kazi walimu wapya 14,060, wakiwemo 7,835 wa ngazi ya shahada na 6,225 wa ngazi ya stashahada katika Halmashauri zote nchini na kupunguza pengo la walimu kutoka 50.2 hadi asilimia 36.6.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Ualimu inasimamia utoaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada. Vilevile, Idara huandaa na kupitia miongozo na viwango vya Elimu ya Ualimu na kufanya ufuutiliaji na tathmini ya uendeshaji na utekelezaji wa mtaala wa Elimu ya Ualimu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Idara ya Elimu ya Ualimu, iliandaan pendekero la kuunda Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania na kuliwasilisha kwa wadau. Aidha, ili kuhakikisha kwamba kumbukumbu za watumishi wa vyuo vya ualimu pamoja na shule za mazoezi zinatunzwa

ipasavyo, Wizara ilianza kuingiza taarifa zao katika Mfumo wa Kielektroniki wa kutunza Kumbukumbu za Watumishi, Wanachuo na Mali za Vyuo katika Vyuo vya Ualimu (*Teacher Education Staff and Students Inventory System – TESSIS*). Hadi Tarehe 30 Aprili, 2013 taarifa za watumishi wa Vyuo vya Ualimu 13 (Morogoro, Mpwapwa, Vikindu, Kinampanda, Tabora, Songea, Sumbawanga, Tukuyu, Ilonga, Mhonda, Mpuguso, Tandala na Shinyanga) zilikuwa zimeingizwa katika mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Elimu ya Ualimu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanachuo 5,446 ngazi ya Cheti na 4,338 ngazi ya Stashahada kwa ajili ya kuanza mafunzo ya ualimu na kufanya idadi ya wanachuo wote katika vyuo vya Serikali kuwa 25,133. Kati ya wanachuo hao, 332 ni wa Elimu Maalumu;

(b) Iliendelea kusimamia na kuimarisha michezo katika vyuo 12 vya Ualimu vya Serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la Liikunnan KehityshteytÖ Liikery (LIIKE) kutoka Finland kwa kuwezesha yafuatayo: Utoaji wa mafunzo ya awamu ya kwanza kwa wakufunzi 24 juu ya elimu ya afya na michezo kwa wiki mbili katika Chuo cha Ualimu Butimba – Mwanza; na maandalizi ya rasimu ya programu ya utoaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa wakufunzi wa Elimu kwa Michezo juu ya Elimu ya Afya na Michezo Awamu ya Pili;

(c) Iliandaa programu ya upanuzi wa utekelezaji wa Mkakati wa Elimu na Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Shule za Msingi (MWAKEM) Ngazi ya Shule na Kitaifa, ambapo utekelezaji wake utafanyika kwa awamu tatu; na

(d) Illichangia sehemu ya gharama za mafunzo kwa watumishi 225 wanaosoma Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ina jukumu la kukabiliana na ongezeko la watu wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu

kwa kutoa fursa ya kujiendeleza kielimu nje ya mfumo rasmi wa shule mionganini mwa vijana na watu wazima na kusimamia vituo vya magazeti ya elimu katika kanda.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi (*EWW/ENMRA*), ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliandaa na kuisambaza rasimu ya kwanza ya ripoti ya tathmini ya Elimu kwa Wote (*EWO*) kwa wadau wa elimu kwa lengo la kupata maoni kutoka kwa wadau kuhusu hali halisi ya utelekezaji wa malengo ya Elimu ya Watu Wazima kuanzia mwaka 2000 hadi 2012;

(b) Iliandaa zana za kukusanya *data* kwa ajili ya kufanya majoribio ya utafiti kuhusu jinsi walengwa wa programu za *EWW/ENMRA* walivyowezeshwa kushiriki katika shughuli za maendeleo kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni kupitia maarifa na stadi walizopata;

(c) Ilizindua Mpango Mkakati wa Elimu juu ya Haki za Binadamu ambao andiko lake litasambazwa kabla ya Mwezi Juni, 2013. Aidha, muhtasari wa andiko ulichapwa na kusambazwa katika Halmashauri zote ili kuuelimisha umma kuhusu haki zao na namna ya kuzipata;

(d) Ilifanya ufuatiliaji wa programu za *EWW/ENMRA* katika Halmashauri 13 za Handeni, Manispaa ya Moshi, Moshi Vijijini, Rombo, Bariadi, Mvomero, Urambo, Kondoa, Tunduru, Songea Vijijini, Serengeti, Manispaa ya Iringa na Njombe Mjini; na

(e) Ilifanikiwa uchapaji na usambazaji wa nakala 7,100 za magazeti, katika Kanda za Ziwa (nakala 5,000), Nyanda za Juu Kusini (nakala 1,100) na kanda ya Kusini (nakala 1,000) ili kuuarifu umma kuhusu matukio mbalimbali yanayohusu elimu, hususan Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi ina majukumu ya kubuni, kusimamia

na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, pamoja na kuhakikisha kuwa, elimu na mafunzo yanayotolewa yanazingatia ubora na mahitaji ya soko la ushindani na kwa walengwa wenye sifa stahiki, kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi na Vyuo vya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Iliratibu ujenzi wa vyuo vya ufundu stadi vya wilaya na mikoa ambapo maandalizi ya ujenzi wa vyuo vinne vya Mikoa ya Geita, Njombe, Simiyu na Rukwa yalifanywa kwa kila mkoa husika kutenga maeneo stahiki, kufanya mapitio na rejea ili kubainisha stadi zitakazofundishwa vyuoni na kufanya mazungumzo kati ya Serikali na Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kupata fedha za kugharimia ujenzi; na maandalizi ya ujenzi wa vyuo vitano vya Wilaya za Ukerewe, Namtumbo, Chunya, Ludewa na Kilindi yalifanyika kwa Wilaya husika kutenga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vyuo.

(b) Iliratibu zoezi la uimarishaji wa Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze kutumika katika utoaji wa mafunzo ya ufundu stadi. Zoezi hilo lilihusisha yafuatayo:-

(i) Kusambaza nakala za mitaala ya mafunzo ya ufundu stadi katika Vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi;

(ii) Kutoa mafunzo kabilishi kuhusu mitaala ya mafunzo ya ufundu stadi na utoaji wa mafunzo kwa mitaala inayozingatia umahiri kwa walimu 100 kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(iii) Kuwezesha wanafunzi 1,250 kujiunga na mafunzo ya ufundu stadi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(iv) Kuanza kwa ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vya Mputa na Muhukuru; na

(v) Kuanza ujenzi wa karakana katika vyuo 5 vya maendeleo ya wananchi (Ikwiriri, Mbinga, Nzega, Kisangwa na Handeni);

(c) Ilkamilisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (MMEU) ambao utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwezi Julai mwaka 2013/2014. Mpango huu unalenga katika kujenga nguvukazi yenye kuhimili ushindani wa soko la ajira kwa kuinua ubora wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu nchini ili kukidhi mahitaji ya sekta kuu za uchumi kama ilivyoinishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mpango huu pia unalenga katika kuimarisha udahili katika ngazi mbalimbali za Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili kujenga uwiano wa nguvu kazi katika ngazi mbalimbali kwa kila fani. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi utatekelezwa kwa ushirikiano baina ya Wizara mbalimbali ambazo kwa sasa zinamiliki vyuo vinavyotoa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi nchini. Jukumu kubwa la Wizara yangu katika mpango huu ni kuratibu utekelezaji wa mpango pamoja na ufuutiliaji na tathmini ya utekelezaji. Utekelezaji wa mpango huu utawezesha kutimizwa kwa Malengo ya Kitaifa ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu; na

(d) Iliratibu utekelezaji wa mradi wa ushirikiano baina ya Taasisi za Elimu ya Ufundu nchini na Vyuo vya Canada unaoitwa *Education for Employment (EFE)* kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika masuala ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kwa;

(i) Kuendesha warsha ya wadau wa mradi katika kutathmini utekelezaji wa mradi;

(ii) Kuendesha Kongamano la Tatu la Mradi wa EFE la Kimataifa kuhusu *Skills Development for a Competitive Tanzania*;

(iii) Kuandaa vigezo nya kutathmini ufanisi au utendaji kazi (*Key Performance Indicators*) wa taasisi za elimu na mafunzo ya ufundi stadi;

(iv) Kuandaa zana (*Instruments*) kwa ajili ya kukusanya taarifa zitakazotumika katika upimaji huo;

(v) Kuandaa majoribio ya ukusanyaji wa taarifa husika kwa kutumia zana mpya; na

(vi) Kuandaa andiko la Madi Awamu ya Pili ya Miaka Mitano (2013/2014 – 2017/2018) na kuliwasilisha kwa *Canadian International Development Agency – CIDA* kwa ajili ya kupata ufadhili.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Elimu ya Juu ina majukumu ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Sheria, Taratibu na Miongozo ya utoaji wa Elimu ya Juu, pamoja na kuhakikisha kuwa elimu inatolewa kwa kuzingatia ubora kulingana na mahitaji ya soko la ushindani na inawafikia walengwa wenyewe sifa stahiki kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mamlaka ya Elimu Tanzania na Vyuo nya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Elimu ya Juu ilitolewa katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki 50 nya Serikali. Kazi za msingi zinazofanywa na Vyuo Vikuu ni kufundisha na kufanya utafiti unaolenga katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini, pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na umma kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013 Wizara, kupitia Idara ya Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidhamini wanafunzi 30 raia wa Uganda wanaosoma katika Vyuo Vikuu nya Dar es Salaam, Chuo Kikuu Ardhi na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi – Muhimbili na wanafunzi wa Tanzania 88 walioko Msumbiji, chini ya utaratibu wa kubadilishana wanafunzi baina ya Tanzania na Uganda na Tanzania na Msumbiji;

- (b) Ilidhamini wanafunzi 10 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka China, chini ya mkatuba wa ushirikiano kati ya Tanzania na China;
- (c) Ilitoa ruzuku kwa wanafunzi wapya 450, na 1,450 unaoendelea na mafunzo ya shahada ya awali ya udaktari wa binadamu, meno, tiba ya mifugo na ufamasia;
- (d) Ilielimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji kupitia maadhimisho ya kitaifa na wiki ya vyuo vikuu nchini;
- (e) Ilidhamini mafunzo ya shahada za uzamili kwa wanataaluma 80 katika vyuo vikuu yya umma;
- (f) Ilidhamini wahadhiri 44 walioko katika mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kupitia Shirika la Huduma ya Ujerumani ya Kushirikiana Kitaaluma (- DAAD);
- (g) Iliratibu uteuzi wa wanafunzi 190 waliokwenda masomoni katika nchi za Algeria, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Korea ya Kusini, Uturuki, Misri na Serbia;
- (h) Iliwajengea uwezo wanataaluma 187 katika ngazi ya Uzamili na 191 katika ngazi ya Uzamivu ndani na nje ya nchi;
- (i) Iliratibu maandalizi ya kuunganisha taasisi 28 za Elimu ya Juu katika Mkongo wa Taifa;
- (j) Iligharamia mahitaji maalumu kwa wanafunzi wenye ulemavu katika vyuo vikuu vinne nchini;
- (k) Iliandaa Hadidu za Rejea kwa ajili ya kufanya Utafiti kuhusu Ulinganifu wa Mafunzo Yanayotolewa katika Vyuo Vikuu na Soko la Ajira;
- (l) Iliwasilisha andiko la *STHEP*kwa ajili ya kuomba ufadhili wa Awamu ya Pili ya *Adaptable Programme Lending (APL II)* kutoka Benki ya Dunia; na

(m) Ilikamilisha taarifa ya njia mbadala za kughamramia elimu ya juu itakayowasilishwa kwa wadau kwa ajili ya majadiliano.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Ukaguzi wa Shule ina majukumu ya kufanya ukaguzi wa Shule za Awali, Msingi, Sekondari, Elimu Maalumu, Vituo vya Ufundu Stadi, Elimu ya Watu Wazima na Elimu nje ya Mfumo Raskmi, pamoja na Vyuo vya Ualimu ili kuimrisha ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni na viwango vya utoaji elimu vilivywewka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Ukaguzi wa Shule, ilitekeleza yafuatayo:-

(i) Ilisimamia na kuendesha Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili wa mwaka 2012, ambapo watahiniwa 249,325 (wasichana 113,213) kati ya 386,271 (wasichana 187,244) waliofanya mtihani mwaka 2012 walifaulu. Hii ni asilimia 64.6 ya watahiniwa waliofanya mtihani; na

(ii) Iliwezesha utoaji wa mafunzo kabilishi kuhusu Mfumo wa Mawasiliano na Utunzaji wa Taarifa za Ukaguzi wa Shule (*Inspectorate Management Information System - IMIS*) kwa Maafisa Elimu wa Halimashauri 21 na Wakaguzi wa shule 43 ili kuimrisha mfumo wa mawasiliano na utunzaji wa taarifa za ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Sera na Mipango ina majukumu ya kutoa huduma za kitaalamu katika uandaaji, ufuutiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo na kuratibu shughuli za utafiti wa kielimu. Aidha, ina wajibu wa kuratibu uandaaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu pamoja na vikao vya pamoja vya wadau wa sekta ya elimu na kusimamia uandaaji na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati (*Medium-Term Strategic Plan*) wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara, kupitia Idara ya Sera na Mipango, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilikamilisha rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2012 na kuandaan mkakati wa utekelezaji wake;

(b) Iliimarisha ukusanyaji, uhifadhi na usimamizi wa takwimu na taarifa za elimu kwa kusimika hazinadata (*database*) katika Halmashauri 68; na

(c) Iliandaa Mkutano wa Pamoja wa Mapitio ya Sekta ya Elimu kwa mwaka 2012 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu uliofanyika kuanzia tarehe 25 hadi 27 Septemba, 2012. Aidha, mapitio ya Sekta yalifanyika na kuhitimishwa na Mkutano Mkuu (*High Level Meeting-HLM*) uliofanyika tarehe 16 Novemba, 2012 kwa kuwashirikisha Viongozi wa Serikali wanaouna Sekta ya Elimu na Wakuu wa Washirika wa Maendeleo, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na Mashirika ya Dini. Katika kikao hiki, Serikali, Washirika wa Maendeleo, pamoja na Mashirika yasiyokuwa ya Serikali, walitia saini mkataba kuhusu uimarishaji wa elimu (*Education Reform Compact - ERC*), ambapo maeneo makuu manne ya kipaumbele yalibainishwa kwa ajili ya utekelezaji katika mwaka 2013/2014, kama ifuatavyo:-

(i) Ubora wa Elimu - kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo, ikiwa ni pamoja na kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu;

(ii) Taratibu za Kitaasisi - Kuimarisha usawa katika mgawanyo wa rasilimaliwatu wenyewe sifa stahiki katika sekta ya elimu pamoja na kuwafanya wabaki katika ajira;

(iii) Kuimarisha Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo - Kupanua wigo wa ugharimiaji wa sekta ya elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ambapo taratibu za kuingia mkataba na *Global Partnership in Education (GPE)* utakaoiwezesha Tanzania kupata msaada wa Dola za Kimarekani milioni 94.8 zilifanyika; na

(iv) Kuimarisha Menejimenti ya Elimu – Kuimarisha uwajibikaji na ufanisi wa usimamizi ili kuinua ubora wa utoaji wa huduma za elimu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu inasimamia masuala ya utawala, ajira, maslahi na maendeleo ya watumishi, pamoja na Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara, kuptitia Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilijirri watumishi 270 (wakufunzi na walimu wa shule za mazoezi 221);

(b) Iliidhinisha vibali 528 vya ajira za wataalamu wa kigeni;

(c) Ilipandisha vyeo Watumishi wa Serikali 2,175 (walimu 1,662); na

(d) Iliendelea na zoezi la kuimarisha mfumo wa utunzaji kumbukumbu katika masijala, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali kina majukumu ya kuratibu na kuandaa utoaji wa habari za Sekta ya Elimu kwa Wananchi kuptitia kwenye vyombo vya habari na kushirikiana na wadau wengine wa Sekta ya Elimu katika kuhamasisha Wananchi kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kuptitia Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliandaa na kusambaza nakala 800 za kalenda na nakala 1,050 za shajara ili kuifahamisha jamii

kuhusu sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Elimu na Mafunzo;

(b) Ilianda makala 12 zinazohusu mafanikio, mipango na maendeleo katika Sekta ya Elimu ambapo zilichapwa kwenye magazeti mbalimbali;

(c) Iliratibu utoaji wa taarifa kwa wadau wa elimu kupitia tovuti ya Wizara (<http://www.moe.go.tz>) na kuifanyia mapitio Tovuti ya Wizara ili kuiimarisha;

(d) Ilifanikisha uandaaji na usambazaji wa nakala 1,250 za Jarida la Elimu ili kuuhamasisha umma kushiriki katika kutekeleza mipango ya maendeleo ya elimu; na

(f) Ilivezesha utoaji wa taarifa za maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa umma kupitia redio, televisheni, magazeti na mikutano kati ya Wanahabari na Watendaji Wakuu wa Wizara ambapo mikutano 10 ilifanyika na vipindi 18 vya redio na 12 vya televisheni vilirushwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala, Taasisi na Mabaraza yaliyo chini ya Wizara yangu yana wajibu wa kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini. Katika mwaka 2012/2013, kila Wakala, Baraza na Taasisi zilitekeleza kazi zilizopangwa kwa kuzingatia malengo na mipango ya elimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) ina jukumu la kutoa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu ya Kujiedeleza nje ya Mfumo Rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilipanua wigo wa utoaji wa mafunzo ya EWW kwa kuanzisha mafunzo hayo katika ngazi ya stashahada (*NTA Level 6*) kwa njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa (*UHM*), ambapo mafunzo yataanza rasmi mwaka wa masomo 2013/2014 yakiwa na wanafunzi wasiopungua 200);

(b) Ililikamilisha uandishi wa mihtasari kwa ajili ya masomo kumi na moja ya Hatua ya Tatu (sawa na Kidato cha 5 & 6) na kuanza maandalizi ya kuandika moduli za tahasusi (*combinations*) saba ili kuongeza fursa za utoaji wa Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi kwa njia ya *UHM*;

(c) Ilidurusu moduli za masomo ya hatua ya kwanza (Sawa na Kidato cha 1 na 2) na ya pili (sawa na Kidato cha 3 - 4) ili kuimarisha utoaji wa Elimu ya Sekondari nje ya mfumo rasmi kwa njia ya *UHM*. Aidha, ililikamilisha miongozo ya namna ya kuchambua vitabu vya fasihi vya masomo ya Kiswahili na Kiingereza hatua ya pili;

(d) Ilizanzisha programu tatu za ngazi ya Stashahada ambazo ni Maendeleo ya Jamii, Ujasiriamali (*Community Development, Entrepreneurship*) na Maendeleo ya Rasillimaliwatu (*Human Resource Development*) kwa kushirikiana na *Association of Business Managers and Administrators Ltd. (ABMA)* ya Uingereza, ambapo kozi hizi zitaanza kufundishwa rasmi Julai, 2013;

(e) Ilianda mafunzo ya muda mfupi ya Uchambuzi wa Data za Utafiti (*Research Data Analysis*), Uandaaji wa Andiko la Mradi (*Project Write-up*) na Matumizi ya Msingi ya Kompyuta (*Basic Computer Applications*) ambayo yataanza rasmi mwezi Julai 2013;

(f) Ilifanya uchambuzi wa vitabu vya kilimo viliviyowahi kuandikwa na TEWW, ikiwa ni maandalizi ya awali ya kampeni ya elimu kwa umma kuhusu dhana ya KILIMO KWANZA kwa jamii katika mikoa minane ya Tanzania Bara, ambapo Vitabu hivyo vitatumika katika kampeni hii;

(g) Ililikamilisha rasimu ya Mwongozo kwa Watoaji wa Elimu ya Sekondari kwa Njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa (*UHM*);

(h) Ilifanikisha kazi ya kutafsiri filamu ya *Mina Smiles* kutoka katika Lugha ya Kiingereza kwenda katika Lugha ya Kiswahili (*Mina Atabasamu*) ili itumike kama nyenzo ya

kufundishia jamii na kufanyia majoribio huko Bagamoyo kwa walengwa 37 walioshiriki kutoka vituo viwili. Aidha, iliwezesha usambazaji wa nakala za *DVD* na utoaji wa mafunzo kwa wawezeshaji 25 ili waweze kuitumia filamu hii katika kielimisha jamii juu ya umuhimu wa kisomo na hasara za kutokujua kusoma na kuandika;

(i) Illichapisha Toleo Namba 19 la Jarida la Elimu ya Watu Wazima (Journal of Adult Education – Tanzania) lenye makala saba za utafiti. Aidha, ilikamilisha maandilizi ya utafiti katika mikoa saba ya Tanzania Bara ili kuibua masuala ya jinsia yanayohusu ukandamizaji wa wanawake katika jamii. Matokeo ya utafiti huu yatachapishwa katika Jarida la Wanawake, Toleo Namba 6;

(j) Iligharamia mafunzo ya wahadhiri wawili katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu, 10 katika shahada ya uzamili, 6 katika shahada ya kwanza na 12 katika mafunzo ya muda mfupi; na

(k) Ilinunua kiwanja cha Ekari 13 katika Wilaya ya Kibaha - Mkoa wa Pwani kwa ajili ya ujenzi wa Chuo, ikiwa ni jitihada za kupanua miundombinu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kubuni na kuandaa mtaala na mihtasari ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari, Ualimu na Elimu Maalumu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara, kuititia Taasisi ya Elimu Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ililikamilisha uandishi wa Rasimu sita za Miswada ya masomo ya Elimu ya Awali na Rasimu saba za masomo ya Elimu ya Msingi;

(b) Ilitoa mafunzo ya stashahada ya mwaka mmoja katika kubuni na kutekeleza mtaala kwa wanafunzi 47 kutoka nchi za Afrika, Asia, Ulaya na Amerika kwa njia ya ana kwa ana na mtandao; na

(c) Ilifanya upembuzi yakinifu wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Mitaala na Utafiti wa Maendeleo ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania ina jukumu la kutoa na kusambaza huduma za maktaba nchini. Aidha, ina jukumu la kuanzisha, kuendesha, kuongoza, kuimarisha, kutunza na kuendeleza Maktaba za Umma, kuanzia Mikoa na kutoa mafunzo pamoja na kuendesha mitihani ya Taaluma ya Ukutubi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara, kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliwezesha kupatikana kwa vitabu 25,516. Kati ya hivyo, 468 vilipatikana kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 1975, inayomtaka kila mchapishaji kuwasilisha Maktaba Kuu, nakala mbili za kila kitabu anachokichapisha; vitabu 24,984 vilipatikana kwa njia ya msaada na 64 vilinunuliwa na hivyo kufanya idadi ya vitabu vyote katika maktaba nchini kufikia 1,210,473. Aidha, vitabu hivi vilisambazwa katika mikoa na wilaya zenye maktaba za Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania;

(b) Ilitoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba katika shule 22 na taasisi 7;

(c) Iliwezesha udahili wa wanafunzi 1,196 katika Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka (*School of Library, Archives and Documentation Studies – SLADS*) - Bagamoyo, ambapo ngazi ya Cheti walikuwa 502, Stashahada 545 na mafunzo ya muda mfupi 149; na

(d) Ilikamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike, yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 64, katika Chuo cha Mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka - Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu una majukumu makuu manne: Kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti katika masuala yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu na kuandaa na kusambaza makala na vitabu mbalimbali vya uongozi na uendeshaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Ilitoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa Viongozi 669 kati ya 900 waliolengwa na hivyo kutekeleza lengo kwa asilimia 74.5;
- (b) Ilitoa mafunzo juu ya mbinu bora za kusimamia Elimu ya Sekondari katika kata kwa Waratibu Elimu Kata 1,004 kutoka mikoa kumi ya Tanzania Bara (Pwani, Tanga, Manyara, Lindi, Iringa, Rukwa, Kigoma, Mara, Shinyanga na Dodoma);
- (c) Ilitoa mafunzo ya Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule na juu ya Elimu katika Majanga kwa Wasimamizi wa Elimu ngazi ya Kata na Wilaya kwa Halmashauri za Iringa, Mufindi, Njombe, Mbarali na Mbeya;
- (d) Iliendesha mafunzo juu ya mbinu za Uhamasishaji wa Jamii katika kupata Rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya shulekwa wilaya za Kusini Unguja, Kaskazini B, Chake Chake na Micheweni Zanzibar;
- (e) Ilikamilisha Moduli za kutolea mafunzo kwa Wajumbe wa Kamati za Shule za Msingi juu ya Usimamizi wa Elimu ya Msingi;
- (f) Ilikamilisha Moduli za kutolea mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata juu ya Usimamizi wa Elimu ya Sekondari;

(g) Ilikamilisha Moduli za kutolea mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi za Shule za Sekondari juu ya utekelezaji wa majukumu yao katika kuziongoza shule;

(h) Ilianda Moduli kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Usimamizi wa Elimu kwa wadau ngazi ya Shule, Kata na Wilaya;

(i) Ilifanya utafiti wa kubaini mahitaji ya mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata juu ya kusimamia elimu ya sekondari, Bodi za Shule za Sekondari na Kamati za Shule;

(j) Iligharimia mafunzo ya Watumishi 38 (3 mafunzo ya muda mrefu, 3 mafunzo ya muda mfupi na 32 mafunzo kabilishi) juu ya Mfumo wa Upimaji na Tathmini wa wazi wa Utendaji wa Kazi; na

(k) Ilifanikisha kupatikana kwa eneo lenye ukubwa wa Ekari 300 katika Wilaya ya Misungwi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha *ADEM* - Mwanza ambapo taratibu za kisheria zinafuatiliwa ili ununuzi uweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO* ina majukumu ya kutekeleza Programu za *UNESCO* nchini kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Wizara kuitia Tume ya Taifa ya *UNESCO*, ilitekeleza yafuatayayo:-

(a) Illichapisha nakala 760 za Tanzania and *UNESCO Magazine*, gazeti ambalo hutoa maelezo ya kazi zinazofanywa na Tume pamoja na fursa za ushirikiano zilizopo baina ya wadau na Tume. Aidha, Tume illichapisha nakala 1,000 za vipeperushi, 1,000 za Kalenda na 100 za Shahara (*Diary*) na kuandaa hazinadata (*database*) ya wadau ili kurahisisha mawasiliano;

(b) Ilifanikisha shule mia moja na tisa kujunga na mtandao wa *UNESCO (UNESCO Associated School Project)* ulioziwezesha shule hizo kupata msaada wa vionambali 109 (*Telescope*), kutoka shule rafiki zilizo katika mtandao huo;

(c) Iliwashirikisha wadau katika mikutano ya uandaaji wa Ripoti ya Utekelezaji wa Makubaliano ya Kupinga Ubaguzi katika Utoaji wa Elimu ya Mwaka 1960 au Mapendekezo Dhidi ya Ubaguzi katika Utoaji wa Elimu ya Mwaka 1960;

(c) Iligharimia mafunzo ya watumishi watatu; wawili walipata mafunzo ya Usimamizi wa Miradi nchini Uganda na mmoja alipata mafunzo ya Uongozi katika Afrika huko Addis Ababa; na

(d) Iliratibu utekelezaji wa miradi tisa ya ushirikishwaji wa *UNESCO*, ambayo ni:-

(i) Kuijengea uwezo Tume ya Taifa ya *UNESCO* ambapo vifaa ikiwemo mashine ya kutolea vivuli, nukushi (*fax*), kompyuta pakato na projekta vilinunuliwa;

(ii) Kuhifadhi lahaja za Lughya ya Kiswahili za Kimakunduchi na Kitumbatu ambazo ziko hatarini kutoweke, kwa ushirikiano na Baraza la Kiswahili la Zanzibar;

(iii) Kuanzishwa kwa Kituo cha Kitaifa cha Utafiti wa masuala ya kijinsia huko Tengeru Arusha, kwa ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;

(iv) Kuhamasisha watoto wa Elimu ya Msingi kupenda masomo ya sayansi kwa kuchunguza, kugundua na kutumia kionambali ambapo walimu na wanafunzi wa shule za msingi 15 kutoka Zanzibar na Tanzania bara walijengewa uwezo wa kutumia kionambali katika kujifunza elimu ya anga;

(v) Kuwajengea uwezo Maafisa Ugani 40 wa Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa na Njombe;

(v) Ununuzi wa vifaa vya maabara ya Lugha kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Zanzibar ili kuinua ubora wa ufundishaji wa lugha;

(vi) Kuwajengea uwezo wabunge 54 wa Kamati za Kudumu za Bunge za Ardhi, Maliasili na Mazingira na Huduma za Jamii, pamoja na waandishi wa habari 20 juu ya umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa maeneo ya Tanzania yaliyowekwa kwenye Orodha ya Urithi wa Dunia; na

(vii) Kuandaa, kuzalisha na kusambaza Toleo la Kiswahili la *video* ya 'Mina Atabasamu' (*Mina Smiles*) kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kutekeleza Sera ya Mitihani kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha, Baraza lina jukumu la kuendesha mitihani ya kuhitimu Elimu ya Msingi, Sekondari, Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada na Mtihani wa Maarifa na kusimamia uendeshaji wa mitihani itolewayo na bodi za nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara, kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2012 kwa watahiniwa 865,827 katи ya 1,050,000 walikuwa wametarajiwа kufanya mtihani huo;

(b) Iliwatahini jumla ya wanafunzi 583,869 wa Elimu ya Sekondari na Ualimu ambapo watahiniwa 481,412 walikuwa wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2012 na watahiniwa 21,314 wa Maarifa (*Qualifying Test - QT*) kwa mwaka 2012 na watahiniwa 52,612 walikuwa wa Kidato cha Sita na 28,531 wa Ualimu.

(c) Ilinunua trela mbili za lori ili kuongeza ufanisi katika usambazaji wa mitihani; na

(d) Ilipunguza ghamama za usahihishaji wa mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2012 kwa kuwawezesha watahiniwa kujibu maswali katika karatasi maalumu za *Optical Mark Reader (OMR)* na majibu yake kusahihishwa kwa kutumia skana maalumu, ambapo idadi ya wasahihishaji ilipungua kutoka 4,098 mwaka 2011 hadi 287 mwaka 2012 na siku za usahihishaji zilipungua kutoka 30 hadi 16.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Maendeleo Dakawa kina majukumu ya kuratibu shughuli za maendeleo ya taasisi zilizomo kwenye kituo ikiwemo Shule ya Msingi yenye wanafunzi 600 (106 wa Elimu ya Awali na 494 wa Elimu ya Msingi), pamoja na watumishi 15; Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Juu yenye wanafunzi 450 na watumishi 20; Chuo cha Ufundı Stadi chenye wanachuo 160 na watumishi 20; na Chuo cha Ualimu chenye wanachuo 784 wa diploma na watumishi 50. Aldha, kituo kina jukumu linge la kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa na miundombinu iliyokabidhiwa na Chama cha *African National Congress (ANC)* cha Afrika ya Kusini kwa ajili ya kulinda Historia ya Ukombozi wa Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Kituo cha Maendeleo Dakawa, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliratibu shughuli za maendeleo ya taasisi zilizomo katika kituo, ikiwemo Chuo cha Ualimu Dakawa, Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Dakawa, Chuo cha Ufundı Stadi Dakawa na Shule ya Msingi Dakawa;

(b) Ilisimamia utunzaji wa mazingira ya kituo yenye eneo la kilometra za mraba 28 kama ilivyokabidhiwa na *ANC*;

(c) Iliendelea kutunza kumbukumbu za kihistoria za Ukombozi wa Kusini mwa Afrika; na

(d) Iliendelea na maandalizi ya kuandaa muundo wa kisheria wa kituo.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania ina majukumu ya kutafuta na kubaini vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharimia maendeleo ya Sekta ya Elimu nchini, ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wadau wa elimu kuchangia kwa hiari katika Miradi ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliunda Kamati Maalumu ya kupitia mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ilioanzisha Mfuko, ili kuuwezesha Mfuko kuwa na vyanzo vya mapato vya uhakika na endelevu. Kamati hiyo iliandaa ripoti ya vyanzo mbadala vya kugharimia Elimu ya Juu na kutoa mapendekezo ya marekebisho ya sheria zilizounda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya mwaka 2004; Mfuko wa Elimu - 2001; Sheria ya Vyuo Vikuu 2005 na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundis 1997. Mapendekezo haya yaliwasilishwa Hazina na kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya utekelezaji; na

(b) Ilifanikisha upatikanaji wa shilingi bilioni 1.32 kama ahadi, fedha taslimu na vifaa, kwa njia ya harambee, matembezi ya hisani na chakula cha hisani. Lengo lilikuwa kukusanya Sh. bilioni 2.3. Aidha, fedha zilizopatikana zilitumika kwa ajili ya kutoa ufadhilli wa miradi 99 ya elimu yenye lengo la kuinua ubora wa elimu na kuongeza upatikanaji wake kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina majukumu makuu ya kusimamia ubora wa Elimu ya Juu, kutoa ithibati, kuratibu uanzishwaji wa Vyuo Vikuu na kuidhinisha programu zinazofundishwa ili zikidhi maendeleo ya Taifa na soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilifanya tathmini ya programu kumi za masomo za vyuo vikuu viwili na vyuo vikuu vishiriki vinne na kuidhinisha programu za masomo kama ifuatavyo: Chuo Kikuu Kishiriki

cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki - programu moja, *Sebastian Kolowa Memorial University (SEKOMU)* - programu mbili, *Mwenge University College of Education (MWUCE)* - programu moja, *Jordan University College JUCO* - Programu nne, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi programu moja na Chuo Kikuu cha Tumaini - MAKUMIRA programu moja;

(b) Ilivipa usajili wa muda Chuo Kikuu cha Kilimo na Sayansi Shirikishi cha Butiama na Chuo Kikuu cha Aga Khan Kampasi ya Arusha;

(c) Ilikamilisha rasimu ya kanuni za utekelezaji wa mfumo wa tuzo zinazotambulika kitaifa (*National Qualifications Framework - NQF*);

(d) Ilifanya tathmini ya kitaalamu katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki sita kwa lengo la kuvihuisha. Vyuo hivyo ni *Teofilo Kisanji University (TEKU)* - Kituo cha Dar es Salaam, *Tanzania International University* - Dar es Salaam, *Enkernforde University* - Tanga, *Tumaini University* - Iringa, *Tumaini University* - Kituo cha Mbeya na *Kampala International University (KIU)* - kituo cha Dar es Salaam;

(e) Ilifanya ukaguzi ili kuhakiki ubora katika maeneo mbalimbali ikiwemo udahili katika vyuo vinne, ambavyo ni *Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC)*, *University of Arusha*, *Jomo Kenyatta University* - Kituo cha Arusha na *Stephano Moshi Memorial University College (SMMUCO)*;

(f) Iliratibu warsha mbili za kutathmini mradi wa majaribio unaotekelezwa na nchi tano Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazolenga katika kuweka ulinganisho (*harmonization*) na kudhibiti ubora wa programu za masomo ya biashara katika vyuo vikuu, kwa kushirikiana na *Inter-University Council for East Africa (IUCEA)*;

(g) Ilielimisha umma juu ya majukumu yake kuitia televisheni, redio, magazeti na tovuti ya tume pamoja na

kuchapisha na kusambaza nakala 20,000 za kitabu cha 'Mwongozo wa Udhili' na vipeperushi mbalimbali vinavyowaelekeza waombaji jinsi ya kuomba kudahiliwa katika Vyuo Vikuu nya Elimu ya Juu nchini; na

(h) Iliratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi 44,715 (wa kike - 15,388) waliojunga na Elimu ya Juu katika Vyuo Vikuu kwa mwaka wa masomo 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundii lina majukumu ya kusimamia na kuratibu mitaala, ubora wa mafunzo, mitihani, tuzo, usajili na ithibati za vyuo nya elimu ya ufundu nya umma na binafsi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ililikagua vyuo 74, ambapo vyuo 16 vilipewa usajili wa kudumu, vyuo 53 vilipewa usajili wa muda na vyuo 5 vilipewa usajili wa matayarisho;

(b) Ililikagua vyuo 20 ambapo vyuo 9 vilipewa ithibati; na idara 29 zilitambuliwa kuwa na uwezo wa kuendesha mafunzo;

(c) Ililibaini na kuwasajili walimu 275 katika vyuo nya ufundu;

(d) Ilitoa mafunzo juu ya namna ya kuendesha mitihani kwa ajili ya vyuo 24 na mafunzo elekezi juu ya kutengeneza mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa mafunzo wa vyuo 15;

(e) Iliratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo 18 kupitia mfumo wa udahili wa pamoja ujulikanao kama *Central Admission System - CAS*;

(f) Ilitembelea vyuo 13 ili kudhibiti utekelezaji wa masharti ya ithibati; na

(g) Ilitoa mafunzo kwa wakufunzi 78 kutoka vyuo 26 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala mipya.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi Raia wa Tanzania wanaosoma katika Taasisi za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi na kukusanya marejesho ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilitoa mikopo kwa wanafunzi 95,594 katи ya 98,773 waliokuwa wameomba hadi tarehe 30 Aprili, 2013;

(b) Ilifanikisha urejeshwaji wa jumla ya shilingi 10,128,238,670 za mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Hii ni asilimia 56 ya lengo la shilingi 18,000,000,000 la mwaka 2012/2013; na

(c) Ilielimisha umma kuhusu Sera ya Uchangiaji Elimu ya Juu, utoaji na urejeshaji mikopo kupitia vipeperushi, magazeti, redio, televisheni, mikutano, warsha na maonesho.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi ina majukumu ya kuratibu, kudhibiti, kugharamia, kutoa na kukuza elimu na mafunzo ya ufundı stadi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilifanya maandalizi kwa ajili ya kuanza ukarabati wa Chuo cha Ufundı Stadi katika Wilaya ya Karagwe na ujenzi wa Chuo cha Ludewa kwa kufanya yafuatayo: Kuanza tathmini ya mahitaji ya kazi yote ya ukarabati (*conditional survey*) pamoja na maandalizi ya taratibu za kuwapata wazabuni katika Wilaya ya Karagwe na kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kutenga

eneo la ujenzi wa Chuo cha Wilaya na kuainisha mahitaji na stadi zitakazohitajika;

(b) Ilitekeleza mpango wa mafunzo ya ufundi viwandani kuititia *Skills Enhancement Programme (SEP)* katika viwanda kumi ambavyo ni Kampuni ya Ranchi za Taifa Kongwa - Dodoma; Hoteli ya Mt. Meru Arusha; Kiwanda cha Kamba za Katani (*Tanzania Cord - TANCORD*) cha Tanga; Kiwanda cha Sukari cha Kagera; Machinjio ya Kizota - Dodoma; Nabareza Ranchi - Manyara; Dodoma Hoteli - Dodoma; na MR Hoteli - Iringa;

(c) Ilifanya utafiti wa soko la ajira nchi nzima ili kubaini mahitaji ya mafunzo ya ufundi stadi kisekta, hususan stadi zinazohitajika na wawekezaji (*Potential and Emerging Skills*) na zinazoendana na mahitaji ya maeneo vitakapoengwa vyuo vipyta vya mikoa na wilaya, ambapo stadi zinazohitajika zilibainishwa. Aidha, iliandaliwa orodha ya stadi hizo kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi kwa kila kanda. Utafiti huu uliwezesha kubaini stadi zinazohitajika katika vyuo vitakavyojengwa katika Mikoa ya Geita, Njombe, Simiyu na Rukwa; na

(d) Ilifanya maandalizi ya ujenzi wa vyuo vinne vya Ufundi Stadi vya mkoa katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe na Rukwa kwa kufanya yafuatayo: Kupatikana kwa maeneo yaliyopimwa na kupatiwa hati miliki ambapo upimaji na taratibu za upatikanaji wa hati miliki unaendelea; kukamilika kwa zoezi la kufanya mapitio na marejeo ili kuainisha stadi zitakazofundishwa katika vyuo vya ufundi stadi vya mkoa katika mikoa husika; na kukamilisha taratibu za kupata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank - AfDB*) kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Mikoa husika.

Mheshimwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendeleza ushirikiano na wafadhili mbalimbali katika kugharamia utafiti, mafunzo na miundombinu. Maeneo mbalimbali ya utafiti na mafunzo yaliwezesha kwa ushirikiano na ufadhilli kutoka mataifa mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la *Sida*, Serikali ya Kifalme ya Norway, Serikali ya Ujerumani kupitia Shirika la *Deutsche Gese Inter (GIZ)*, Serikali ya Denmark kupitia *Danish International Development Agency (DANIDA)*, SHIRIKA la Rockefeller na Ford; Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza; Chuo Kikuu cha Bolton, Chuo Kikuu cha Michigan State (Marekani); Serikali ya Ufaransa kupitia *CORUS*, Shirika la Volkswagen, Tume ya Ushirikiano ya Ulaya na Shirika la Kimataifa la Utabiri wa Hali ya Hewa;

(b) Ilidahili wanafunzi 13,769 wa Shahada ya Kwanza kati ya 15,112 waliolengwa, 2,800 wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu kati ya 2,987 waliolengwa na 120 wa Stashahada kati ya 283 waliolengwa. Udahili wa wanafunzi wa shahada za awali haukufikia malengo yaliyotarajiwa kutokana na ufaulu mdogo wa wahitimu wa Kidato cha Sita kwa mujibu wa viwango vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(c) Iliiwezesha Bima ya Afya kuendelea kuwa chanzo cha mapato yanayosaidia uendeshaji wa Kituo cha Afya ambapo mapato hayo yalikiwezesha chuo kupata mkopo wa ukarabati na upanuzi wa kituo hicho;

(d) Ililikamilisha ushauri katika maeneo yafuatayo: Tathmini ya mabadiiliko ya Tabia nchi kwa maji ya Mto Wami; uchunguzi wa udongo wa miradi minne ya Dar es Salaam; na uchunguzi wa udongo katika upanuzi wa Hospitali ya AgaKhan;

(e) Ilifanya utafiti katika maeneo yafuatayo: Kuendeleza Mkakati wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi na Tahafifu; Kuingiza Teknolojia ya Ujenzi katika Maeneo Oevu katika Kilimo cha Mijini na Uvuvi wa Samaki ili Kuongeza

Uzalishaji kwa kutumia Majitaka Yaliyorejeshwa; Programu ya Usalama wa Chakula: Kuimarisha Usalama wa Chakula kwa Kuongeza Thamani na Menejimenti ya Wadudu Waharibifu wa Mazao na Magonjwa Yanayoenezwa kupitia Viumbe; Tathmini ya Matumizi ya Taarifa za Fedha katika Kupanga na Kuandaa Bajeti: Uchunguzi Kifani wa Halmashauri za Wilaya Teule; na Kuimarisha Mifumo Asilia ya Uvumbuzi katika Kilimo kwenye Mabonde ili Kuimarisha Uzalishaji na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Chuo hiki kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanafunzi 1,228 (196 wa fani ya sayansi); katи ya 1,250 waliolengwa (250 wa fani ya sayansi);

(b) Ilipokea mapendekezo ya Kiufundi na Gharama (*Technical and Financial Proposal*) kwa ajili ya kujenga jengo la Kitivo cha Sayansi za Jamii na Humanitia na kuendelea na maandalizi ya kumpata Mshauri Elekezi;

(c) Ilishirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususan kwa shahada za uzamili na uzamivu kwa kuwagharimia jumla ya wahadhiri 32 katika mafunzo ya shahada za uzamili na 60 katika shahada za uzamivu ndani na nje ya nchi. Ilishirikiana na NORAD katika utafiti wa maendeleo endelevu ya Jamii na Utafiti kuhusu elimu ya ualimu kwa nchi za Afrika Kusini mwa Sahara.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya Elimu na Ualimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka 780 mwaka 2011/2012 hadi wanafunzi 1,036 mwaka 2012/2013 ambapo 200 ni wa fani ya sayansi;

(b) Ilianza ujenzi wa maabara ya bayolojia chini ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu;

(c) Ilitoa ushauri wa kitaalamu katika mpango uitwao *Education Quality Improvement Programme (EQUIP)* ulioko Shinyanga unaofadhiliwa na Shirika la Oxfam. Mradi huu unalenga katika kuimarisha elimu katika Wilaya ya Shinyanga Mjini;

(d) Ilifanya ukarabati wa vyumba vya madarasa, kumbi za mihadhara, mabweni, mifumo ya umeme na maji, pamoja na ofisi za wafanyakazi; na

(e) Iliendelea kugharamia masomo ya wahadhiри katika ngazi za uzamili na uzamivu ambapo mhadhiri mmoja aligharimiwa mafunzo katika ngazi ya uzamili na watano katika ngazi ya uzamivu kwa ushirikiano na washirika mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za kilimo, mifugo, mazingira na maendeleo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliongeza udahili kutoka wanafunzi 7,228 mwaka 2011/2012 hadi 9,789 mwaka 2012/13;

(b) Ilikamilisha utoaji wa elimu na ushauri kwa wakulima wa Wilaya ya Mvomero na Kilolo kwa kupitia mafunzo ya muda mfupi na kuongeza mapato ya ndani;

(c) Ilikamilisha ujenzi wa ukumbi wa miadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 250 kwa wakati mmoja na kuanza kuutumia;

(d) Iliendeleza ujenzi wa maabara, kumbi za miadhara na ofisi kwenye Idara za Uchumi-Kilimo na Biashara (*Agriculture Economics and Agribusiness*), Sayansi ya Chakula na Teknolojia (*Food Science and Technology*) na Uhndisi Kilimo (*Agriculture Engineering*), chini ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu;

(e) Ilifanya utafiti juu ya Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Tahafifu (*Climate Change Impact Adaptation and Mitigation - CCIAM*) katika maeneo yenye ikolojia tofauti yaliyoko kwenye Milima ya Uluguru Morogoro na Nyanda za Juu Kusini, kwa ushirikiano na Serikali ya Kifalme ya Norway;

(f) Iliendelea na utafiti wa uenezaji wa teknolojia ya uzalishaji wa mbuzi wa maziwa katika ngazi ya kaya; na

(g) Ilifanya utafiti kuhusu kuimarisha ubunifu katika maliasili na Mlolongo wa thamani ya Kilimo kwa Wakulima Wadogowadogo (*Enhancing Pro-poor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value Chains - EPINAV*) katika Wilaya za Mvomero na Kilosa, kwa ushirikiano na Serikali ya Kifalme ya Norway.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara ambacho ni sehemu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina majukumu ya kufundisha, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ushirika, maendeleo ya jamii, biashara, oganaizesheni, ujasiriamali na masuala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliongeza udahili wa wanafunzi kutoka 3,941 mwaka 2011/12 hadi 4,300 mwaka 2012/13;

(b) Ilifanya utafiti kuhusu matumizi ya vocha za pembejeo (*Warehouse Receipt System*) ili kupata njia mbalimbali za kuwajengea uwezo wa kifedha wakulima wadogo wadogo;

(c) Ilifanya utafiti wa matumizi ya TEHAMA katika kuimarisha ujifunzaji kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu katika vyuo vya *MUCCOBS* na *SAUT* ili kupanua matumizi ya Teknolojia mionganoni mwa wanafunzi;

(d) Ilitoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uendeshaji kibiasara wa Kituo cha Kimataifa cha Mabasi cha Nyangamufuni (*Nyangamufuni International Bus Stand*) Mjini Moshi;

(e) Ilitoa ushauri wa kuandaa andiko mradi kuhusu Ukarabati wa Kiwanda cha Tumbaku kinachomilikiwa na *Songea Namtumbo Co-operative Union*;

(f) Ilbijenga madarasa matano yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja na kukarabati ghorofa mbili za jengo la makazi katika kampasi ya Moshi; na

(g) Ilbijenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 100 kwa wakati mmoja katika Kitivo cha Kizumbi na kubadilisha bweni moja kuwa darasa; na kutengeneza meza 350 na viti 250 kwa ajili ya matumizi ya darasani.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kina majukumu ya kutoa Elimu ya Juu kwa njia ya Masafa na Ana kwa Ana; kutafiti, kutoa ushauri wa kitaalamu na kueneza maarifa kupitia vituo vyake vilivyopo mikoani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilijenga maabara ya Kompyuta katika kituo cha Zanzibar; na kuandaa chumba kwa ajili ya Maabara ya Kompyuta katika vituo vya Mtwara na Kinondoni;

(b) Ilikamilisha jengo la ofisi katika kituo cha Mtwara na wigo katika kituo cha Shinyanga na kufanya ukarabati katika majengo ya ofisi za vituo vya Simiyu na Mara;

(c) Iliongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada za uzamili na Uzamivu hadi 2,391 ikilinganishwa na lengo la kudahili wanafunzi 1,300 kwa mwaka. Hili ni ongezeko la udahili kwa asilimia 45.6;

(d) Iliweka progamu 111 katika mfumo wa kielektroniki wa *MOODEL* ili wanafunzi waweze kuzitumia kwa urahisi. Aidha, ilikiunganisha chuo na vitabu vya kielektroniki vya *African Virtual University (AVU)* na *TESSA, Massachusetts Institute of Technology (MIT)* pamoja na majarida mbalimbali; na kuweka utaratibu wa kuwawezesha wanafunzi kupata kompyuta pakato (*Laptops*) kwa bei nafuu ya Dola za Kimarekani 300, kwa kushirikiana na serikali ya wanafunzi;

(e) Iliweka intaneti isiyotumia waya (*Wireless Internet*) katika Vituo 19 vyenye Maabara za Kompyuta;

(f) Iliendeleza utafiti katika maeneo ya usalama wa matumizi ya TEHAMA; ufugaji wa kuku wa kienyeji; udhibiti wa utupaji taka ovyo kwa kuweka vifaa vya kutupia takataka Chuoni na maeneo ya jirani Jijini Dar es Salaam; matumizi ya maji ya Ziwa Victoria kupitia Mpango wa *ViCRes*; matumizi ya simu za viganjani katika kujifunzia; na mafanikio na matatizo ya matumizi ya ujifunzaji kwa njia ya kielektroniki (*e-learning*); na

(g) Kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 10 chini ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Ardhi kina majukumu ya kufundisha, kutafiti na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika nyanja mbalimbali zikiwemo za maendeleo ya ardhi, nyumba, mazingira na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara, kupitia Chuo Kikuu cha Ardhi ilitekeleza yafuatayo:-

- (a) Ilikamilisha michoro kwa ajili ya ujenzi wa hosteli za wanafunzi;
- (b) Iliendeleza utafiti katika maeneo ya upimaji wa athari za marekebisho na urasimishaji mali katika maisha ya watu wenyewe kipato duni Tanzania, kwa kutumia uchunguzi kifani wa Dar es Salaam (*Assessing the impact of Regularisation and Property Formalisation on the Livelihoods of the Poor in Tanzania, the Case of Dar es Salaam*).
- (c) Ilikamilisha utafiti katika mipango Shirikishi ya Matumizi ya Ardhi katika kusuluhisha migogoro kati ya wakulima, kwa kutumia uchunguzi kifani wa Kijiji cha Kwitete katika Wilaya ya Serengeti (*Participatory Village Land use Planning to Resolve Conflicts between Crop Growers: experience from Kwitete Village, Serengeti District*), ambapo umuhimu wa kuwashirikisha watumiaji wa ardhi katika kuandaa mipango ya matumizi yake ulidhihirika kwa kuwa kunatoa fursa kwa watumiaji kutatua matatizo yao wenyewe. Aidha, ilibainika kuwa watumiaji wa ardhi au rasilimali za ardhi wana mbinu mbalimbali za kimila ambazo zinaweza kutumika katika kutatua matatizo na kusuluhisha migogoro ya matumizi ya ardhi; na
- (d) Ilikamilisha utafiti katika Ushirikishaji wa Jumuiya katika Usimamizi wa Mazingira kwa kutumia uchunguzi kifani wa Manispaa ya Kinondoni - Dar es Salaam (*Community Participation in Environmental management: the Case of Kinondoni Municipality - Dar es Salaam*), ambapo ilidhihirika kuwa mfumo wa usimamizi wa ukusanyaji taka mijini una upungufu. Aidha, ilifahamika kuwa taasisi rasmi zina mfumo mzuri wa ukusanyaji taka kuliko ule wa jumuiya mbalimbali

za Wananchi na kwamba kila mhusika akizingatia kutimiza wajibu wake kwa kufuata sheria na taratibu za kushughulikia uzoaji taka na wadau wakishirikiana ndioy mkakati sahihi wa kuongeza ufanisi wa ukusanyaji taka mijini.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kina majukumu ya kufundisha, kutafiti, kutibu na kutoa ushauri na huduma za kitaalamu katika maeneo ya tiba na afya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2012/2013, Wizara kuititia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilifanya ukarabati wa mabweni ya wanafunzi ya Muhimbili na Chole;

(b) Ilianza kuandaa Mpango Kabambe kwa ajili ya kuendeleza eneo la Mloganzila na kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo hilo ili kuwezesha kuanza kwa ujenzi wa hospitali ya kufundishia;

(c) Ililikamilisha hati za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi na kuzituma Jamhuri ya Korea ya Kusini kwa ajili ya uhakiki, kwa kushirikiana na mshauri elekezi wa mradi kutoka Jamhuri ya Korea Kusini (*BAUM Architects, Engineers and Consultants Inc*);

(d) Iliandaan andiko la mradi (*project write-up*) likiainisha gharama halisi ya fedha itakayohitajika kwa ajili ya ujenzi wa kampasi ya chuo itakayokuwa na kumbi za miadhara, maabara za kufundishia, mabweni ya wanafunzi, jengo la utawala, nyumba za wafanyakazi na miundombinu mingine muhimu na kuliwasilisha Serikalini na kwa wawakilishi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii mnamo tarehe 31 Desemba, 2012 kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi;

(e) Iliendelea na utafiti wa kujua muda ambao dawa ya *Artemether-Lumefantrine (ALU)* inatumia kuua vimelea vya malaria (*Malaria Parasites*) kwa kutumia kipimo

cha Malaria *Rapid Diagnostic Test (MRDT)*. Aidha, *MRDT* imeingia katika Sera ya Taifa kwa ajili ya utekelezaji katika nchi nzima. Matokeo ya utafiti yameionesha *ALU* kuwa na ufanisi wa asilimia 100; na

(f) Iliendeleza utafiti wa chanjo ya UKIMWI katika programu ya Tanzania na Msumbiji ya utafiti wa chanjo dhidi ya VVU iitwayo *Tanzania and Mozambique HIV Vaccine Programme (TaMoVac)*, ambapo utafiti wa kubaini namna bora ya utoaji wa chanjo ya majoribio dhidi ya VVU ulifanyika katika Majiji ya Dar es Salaam, Mbeya pamoja na Maputo (Msumbiji), kama ifuatavyo:-

(i) Washiriki 120 wa hapa nchini na vijana 24 nchini Msumbiji walishiriki katika Mradi wa *TaMoVac-01*, ambapo usalama wa chanjo ulizidi kuthibitishwa na uchambuzi wa takwimu kuhusu uwezo wa chanjo kutengeneza vichocheo vya kinga dhidi ya VVU unaendelea;

(ii) Utafiti wa *TaMoVac-II* ulianza rasmi mnamo Januari, 2013 ukihusisha washiriki 160 kutoka Tanzania (Dar es Salaam na Mbeya) na wengine 38 kutoka Maputo (Msumbiji); na

(ii) Mafunzo kwa ajili ya Wataalamu wa Kitanzania wanaoshiriki katika utafiti katika maeneo haya yanaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe kina majukumu ya kutafuta, kukuza, kuhifadhi na kueneza maarifa na stadi za menejimenti kwa njia ya mafunzo, utafiti na huduma za kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu Mzumbe ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanafunzi wapya 3,715 katika programu mbalimbali (cheti, stashahada na shahada ya kwanza 1,531, shahada ya uzamili 2,169 na uzamivu 15);

(b) Ilikamilisha ujenzi wa maktaba ya kampasi ya Mbeya mwezi Februari, 2013, ambapo vifaa vya maktaba vinategemewa kununuliwa kabla ya mwisho wa 2012/2013;

(c) Ililipia kiwanja cha Iwambi, Mbeya kwa Shilingi bilioni moja katika Manispa ya Mbeya kwa ajili ya kupanua wigo wa utoaji wa elimu;

(d) Ilikamilisha utafiti katika maeneo 12 na kutoa ushauri katika maeneo 18 ya menejimenti, uongozi na sayansi ya jamii;

(e) Illichapisha vitabu vitatu, makala ya kufundishia moja na makala nyingine 17; na

(f) Iligharimia mafunzo ya watumishi 12 wa ngazi ya shahada ya uzamili na 15 katika shahada ya uzamivu.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dodoma kina majukumu ya kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Iliendelea na ujenzi wa maabara na madarasa katika Chuo cha Sayansi za Asili na Hisabati (wanafunzi 5,000) na Chuo cha Sayansi za Ardhi (wanafunzi 3,000) ambao unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2013;

(b) Iliendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ambayo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2013;

(c) Iliendeleza utafiti katika maeneo ya mazingira, rasilimali, uchumi na tabianchi na kuwajengea uwezo wanataalamu katika utafiti kwa ushirikiano na Vyuo vya Utafiti wa Kilimo vya Mlingano na Ilonga, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo, Madagascar, *Council for*

*Development of Science Research in Africa (CODESRIA), Tume ya Sayansi na Teknolojia;*

(d) Ilidahili wanafunzi 4,191 wapya wa shahada ya kwanza, 393 wa shahada za uzamili na 22 wa shahada ya uzamivu. Upungufu wa wanafunzi wa shahada za awali umetokana na kushindwa kukidhi vigezo husika;

(e) Iliendelea na ujenzi wa Kituo cha Uchunguzi wa Maradhi wa Tiba ambao unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2013; na

(f) Ilitoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika maeneo yafuatayo: Kupendekeza njia za kuwahamasisha wateja katika kulipia huduma katika Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu; kuandaa Andiko la Mradi kwa ajili ya *Dodoma Urban Water and Sanitation Authority (DUWASA)*; kufanya tathmini za kukamilika kwa mradi wa *World Vision, Tanzania*; Usimamizi wa Wanyama Pori (*Wild Life Management Areas – AMA*); kutathmini 'Mipango ya Uwandani kwa ajili ya Mamlaka ya Mbuga za Wanyama Tanzania (*Tanzania National Park Authority - TANAPA*); kufanya utafiti na kutoa ushauri kuhusu michakato ya uchaguzi na menejimenti katika nchi teule za Afrika ya Mashariki, kwa ajili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, *Inter-Governmental Authority for Development (IGAD)*, Soko la Pamoja la Nchi zilizo Mashariki mwa Afrika pamoja na Afrika ya Kati (*Common Market for Eastern and Central Africa*); kuandaa Mpango wa Menejimenti ya Utalii katika Visiwa vya Pemba na Unguja kwa ajili ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi – Zanzibar; kufanya tathmini ya Huduma za Malezi ya Awali ya Mtoto – Zanzibar kwa ajili ya Wizara ya Huduma za Jamii, Vijana, Jinsia na Watoto – Zanzibar; na kugharamia ununuzi wa samani za ofisi, nyumba, kompyuta na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kina majukumu ya kuendesha mafunzo katika fani za Sayansi za Jamii; kutoa mafunzo ya uongozi;

kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili wanafunzi 160 wa programu za Cheti, 475 wa programu za Stashahada na 207 wa programu za Shahada ya Kwanza;

(b) Iligharimia mafunzo ya wanataaluma 14 (11 - Shahada za Uzamivu, 3 - Shahada za Uzamili) na wafanyakazi waendeshaji 3 (1 - Shahada ya Uzamili, 1 - Cheti katika Ukutubi na 1 - Cheti katika Utunzaji wa Kumbukumbu);

(c) Iliendeleza ujenzi wa hosteli moja ya wanafunzi, Kivukoni, Dar es Salaam itakayokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 640; na

(d) Ilianza kuendesha Mafunzo ya ualimu wa Stashahada na Shahada katika Jiografia na Historia, na Kiingereza na Kiswahili kwa kudahili wanafunzi 41.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi Arusha kina majukumu ya kutoa elimu na mafunzo ya ufundu katika fani za magari, ujenzi, mitambo, umeme, barabara, sayansi na teknolojia ya maabara, eletroniki na mawasiliano ya anga; kwa kiwango cha cheti na stashahada. Aidha, chuo hufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo yake ya taaluma na kitaalamu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo cha Ufundi Arusha ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Ilidahili jumla ya wanafunzi 500 wa mwaka wa kwanza (474 - Ufundi Sanifu ngazi ya NTA - 4, na 26 – Shahada ya Kwanza katika fani ya Uhndisi Ujenzi na Umwagiliaji);

- (b) Ilanzisha programu tatu za Ufundu Sanifu (*NTAs 4-6*) katika fani za Teknolojia ya Uchongaji Mawe na Usonara, Habari na Kompyuta na Sayansi ya Kompyuta;
- (c) Iliaziri Jumla ya wafanya kazi 44 (wanataaluma 30 na waendeshaji 14);
- (d) Iliendesha kozi ya awali (*Pre-Entry Course*) ya kujunga na Chuo kwa ajili ya wasichana, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania ambapo washiriki 90 walihuduria. Kati ya hao, 88 walifaalu na kujunga na masomo ya Ufundu Sanifu kwa mwaka wa masomo 2012/2013;
- (e) Iligharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wanataaluma 12 (Shahada ya Uzamivu 4, Shahada ya Uzamili 6 na Shahada ya Kwanza 2); na ya muda mfupi 3;
- (f) Ilifanya ukarabati wa Karakana ya Idara ya Uhndisi Umeme;
- (g) Iliendelea na shughuli ya kumalizia ujenzi wa jengo la Ujenzi na Umwagiliaji (*Civil and Irrigation Building*) ambapo umwagaji wa zege la ghorofa ya mwisho umekamilika na kazi za kuweka madirisha, milango, plasta na kupaua zinaendelea;
- (h) Ilanza kazi ya kuchimba visima vitatu kwa ajili ya maji ya kuendeleza Shamba la Mafunzo ya Kilimo na Umwagiliaji la Oljoro kwa kutoa matangazo ya kutafuta mkandarasi wa kazi hiyo, kwa kushirikiana na *Japan Food Aid Counterpart Fund*;
- (i) Iliendeleza mikakati ya mapambano dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI (*HIV/AIDS*) kwa Wanajumuiya wa Chuo kwa kusambaza vipeperushi vya kuelimisha juu ya UKIMWI kwa wanajumuiya (wanafunzi) na kupima afya kwa hiari kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali *Tanzania Youth Alliance (TAYOA)* na Madaktari wa Halmashauri ya Jiji la Arusha; na kuwaelimisha watumishi na familia zao, kuhusu upimaji wa hiari na ushauri na unasihi

katika Siku ya Familia ya Chuo cha Ufundu Arusha (*ATC Family Day*), kwa kushirikiana na Hospitali ya Mkoa ya Mount Meru;

(j) Iliendeleza ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundu vilivyo nchini na vya kimataifa kama ifuatavyo:-

(i) Kushirikiana na *Japan International Cooperation Agency (JICA)* kuititia wataalam wa Kijapani wawili wanaojenga uwezo wa wakufunzi katika kufundisha Uhandisi Ujenzi na Umwagiliaji kwa vitendo;

(ii) Kuendeleza ushirikiano na vyuo vya Ufundu Barani Afrika chini ya uratibu wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA)*;

(iii) Kushiriki katika kongamano lilloandaliwa na CAPA nchini Zambia;

(iv) Kuchaguliwa kuwa mwenyeji wa kongamano la vyuo vya ufundu Afrika chini ya uratibu wa CAPA Novemba, 2013 ambapo maandalizi yameshaanza;

(v) Kushirikiana na Chuo cha Camosun cha nchini Canada, kuititia Mradi wa *Education for Employment (EFE)*, ambapo msaada wa kununua baadhi ya vifaa vya maabara ya uchongaji madini ya vito na usonara umetolewa; na

vi) kushiriki katika mradi uitwao Programu ya Elimu ya Ufundu na Utegemezaji wa Soko la Ajira (*Technical Education and Labour Market Support Programme - TELMS*) unaofadhiliwa na Serikali ya Italia ambapo jumla ya wanafunzi wa kike 128 walipata ufadhili wa ada (kila mmoja Sh. 180,000). Aidha, wanafunzi sita wa kike waliofanya vizuri katika masomo yao, walizawadiwa kompyuta pakato kila mmoja;

(k) Ilifanya utafiti wa kutengeneza mitambo midogo ya kufua umeme wa maji (*Hydroturbine Machines*)

pamoja na kutengeneza mashine ya kupukuchua mahindi, kuyachambua kwa ukubwa na kuyafungasha; na

(l) Ilitoa huduma za ushauri wa kitaalamu kuhusu ujenzi wa vituo vyta kufua umeme vyta Kasansa (Katavi), Likwela (Mbinga), Matombo (Morogoro), Rungwe na Matamba (Makete), upimaji wa udongo kwa ajili ya ujenzi wa majengo na mabwawa, pamoja na matengenezo ya vifaa katika Hospitali ya Mount Meru.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mipango na bajeti ya elimu ya mwaka 2012/2013, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Ofisi ya Kamishna itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuandaa Nyaraka na Miongozo ya Elimu ili kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo, Sheria ya Elimu na Kanuni za uendeshaji wa elimu nchini;

(b) Kusimamia na kuratibu ukamilishaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo;

(c) Kuendelea kuratibu shughuli za taasisi za kitaalamu na kitaaluma zilizo chini ya Ofisi ya Kamishna wa Elimu;

(d) Kuratibu shughuli zote za Masuala Mtambuka katika ngazi zote za utoaji wa Elimu na Mafunzo, ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha mwitikio kuhusu Elimu ya VVU na UKIMWI, baina ya wanafunzi na wafanyakazi katika ngazi zote za elimu;

(ii) Kuendelea kutekeleza Mradi wa Maji, Afya na Usafi wa Mazingira na Maji Safi na Salama Shuleni (*School Water, Sanitation and Hygiene - SWASH*) kwa kutoa mafunzo

kwa wawezeshaji katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya kuhusu kutumia mwongozo wa maji safi na salama katika kutoa elimu ya afya shuleni; kuunda vikundi vya uhamasishaji na klabu za maji, afya na mazingira shuleni na kutoa elimu ya usafi wa mazingira na matumizi sahihi ya vyoo shuleni;

(iii) Kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa elimu kuhusu Elimu ya Kujienda na Kujikinga dhidi ya Maafa na Majanga shuleni;

(iv) Kutoa elimu ya mazingira kwa wadau wa elimu kuhusu namna ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi kuititia *Africa Adaptation Programme*; na

(v) Kuendesha Programu ya TUSEME shuleni ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujitambua, kujiamini na kuwa jasiri katika kuzungumzla masuala mbalimbali shuleni na katika jamii;

(e) Kufanya uchaguzi wa wanafunzi wenye ulemavu watakaofaulu mtihani wa kuhitimu Elimu ya Msingi mwaka 2013 kwa ajili ya kuijunga na Elimu ya Sekondari Januari, 2014;

(f) Kuinua ubora wa utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu kwa kununua na kusambaza vitabu vya kiada na vifaa maalumu vya kufundishia na kujifunzia, ikiwa ni pamoja na visaidizi (*Assistive Devices*) kwa ajili ya watoto wenye ulemavu;

(g) Kujenga uwezo wa Lugha ya Alama kwa walimu wanaofundisha viziwi;

(h) Kuwajengea uwezo walimu wanaorekebisha matamshi kwa watoto viziwi na wenye ulemavu wa akili;

(i) Kuandaa mwongozo wa kuanzisha kituo cha huduma za elimu kwa watu wenye ulemavu;

(j) Kuandaa na kutangaza vipindi 600 vya masomo ya Elimu ya Msingi kwa njia ya Redio na vipindi 96 vya Elimu ya Ualimu kuhusu mbinu za ufundishaji;

(k) Kusajili shule na vyuo vya ualimu na kutoa leseni za kufundishia kwa wageni na Watanzania ambao wanataka kufanya kazi ya kufundisha lakini hawana taaluma ya ualimu;

(l) Kuendesha vikao vinne vya Kamati ya Ithibati ya Vifaa vya Elimu ili kujadili Miswada 100 ya vitabu vya shule; na

(m) Kuwajengea uwezo wa kitaaluma na kitaalamu watumishi watano wa Ofisi ya Kamishna wa Elimu kwa kuwapatia mafunzo ili kuinua ubora wa utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Msingi: Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Kitengo cha Elimu ya Msingi, itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kufanya ufuatiliaji wa uandikishaji wa watoto katika Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi sambamba na upatikanaji na matumizi ya vifaa sahihi vya kufundishia na kujifunzia, pamoja na ujenzi wa miundombinu ya shule, ikiwemo vyumba vya madarasa, nyumba za walimu na vyoo;

(b) Kuendesha mafunzo ya wavezeshaji 50 kuhusu ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na kuratibu mafunzo ya walimu kazini katika stadi za KKK;

(c) Kuratibu upangaji wa walimu wapya wa Daraja la 'A' katika Halmashauri, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI);

(d) Kuratibu uchapaji wa andiko na miongozo ya MMEM III na kuisambaza kwa wadau;

(e) Kugharimia uchapaji na kusambaza miongozo sita ya uendeshaji wa Elimu ya Awali, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto na Mpango wa Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali;

(f) Kuratibu Mpango wa Lishe Shuleni unaofadhiliwa na *World Food Programme (WFP)* na kukamilisha Mpango wa Kitaifa wa Lishe Shuleni;

(g) Kuwajengea uwezo wasimamizi na waendeshaji wakuu wote wa Elimu ya Awali ngazi ya mkoa, wilaya na kata kuhusu miongozo ya Uendeshaji wa Elimu ya Awali na Mpango wa Mafunzo Kazini kwa Walimu wa Elimu ya Awali;

(h) Kukamilisha Mwongozo wa Ufundishaji wa Sayansi kwa Vitendo;

(i) Kugharimia uchapaji na kusambaza nakala 1,000,000 za vyeti vya kuhitimu Elimu ya Msingi;

(j) Kutoa mafunzo kwa walimu juu ya maadili ya walimu (*Teachers Professional Code of Conduct and Ethics*) na Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 katika wilaya sita za Mbarali, Iringa Vijijini, Mufindi, Makete, Njombe na Mbeya Vijijini;

(k) Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Shule Inayomjali Mtoto na kuwaelekeza walimu jinsi ya kutumia njia rafiki katika ufundishaji, katika Wilaya za Mbarali, Iringa Vijijini, Mufindi, Makete, Njombe na Mbeya Vijijini; na

(l) Kupanua Mpango wa *TUSEME Clubs* ili kuwawezesha watoto, na hasa wasichana, kusema juu ya haki zao katika Wilaya za Mbarali, Iringa Vijijini, Mufindi, Makete, Njombe na Mbeya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Sekondari: Katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Kitengo cha Elimu ya Sekondari itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari katika Halmashauri;

(b) Kutathmini mahitaji halisi ya miundombini ya Shule za Sekondari 408 katika Halmashauri 86 na kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha ya ruzuku katika Halmashauri;

(c) Kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu 8,400 wa masomo ya sayansi, Hisabati na Lughaa;

(d) Kutoa mafunzo kwa wakuu wa shule kuhusu usimamizi wa elimu ngazi ya shule;

(e) Kufanya tathmini ya matokeo ya mitihani ya Kidato cha 4 na 6;

(f) Kufanya ufuatiliaji kuhusu kiwango cha uwiano wa walimu kimasomo katika Halmashauri zote na kupanga walimu wapya wa ngazi za stashahada na shahada katika Halmashauri kulingana na mahitaji, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI);

(g) Kuratibu mashindano ya uandishi wa insha ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi zilizo Kusini mwa Afrika;

(h) Kuratibu zoezi la uchaguzi wa wanafunzi watakaoingia kidato cha 1 na 5;

(i) Kusimamia uendeshaji wa Shule ya Sekondari ya Sayansi Miono inayotarajiwa kuanza mwezi Julai, 2013;

(j) Kukamilisha uainisho wa gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi katika Elimu ya Sekondari; na

(k) Kugharimia uchapaji na kusambaza nakala 507,191 za yeti vya kuhitimoo Kidato cha 4 (462,212) na 6 (44,979).

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ualimu: Katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Idara ya Elimu ya Ualimu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuratibu udahili wa jumla ya wanachuo 15,601 (8,690 wa Cheti na 6,911 wa Stashahada) na kufanya jumla ya wanachuo wote katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali kuwa 25,300 ukilinganisha na 25,133 wa mwaka 2012/13;

(b) Kuendesha Mafunzo ya Waelimisha Walimu (*Teacher Educators*) kwa Wakufunzi 580 wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali ili kuwajengea uwezo wa kuendesha Mafunzo ya Ualimu kwa ufani;

(c) Kupanua utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo ya Walimu Kazini kwa Shule za Msingi (MWAKEM) kwa awamu tatu;

(d) Kulipa sehemu ya gharama za masomo kwa watumishi 255 wanaosoma Shahada ya Kwanza Chuo Kikuu Huria na 45 wa Uzamili katika Vyuo Vikuu mbalimbali;

(e) Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Bodii ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania;

(f) Kutekeleza Mkakati wa Menejimenti na Maendeleo ya Walimu uliohuishwa;

(g) Kuendesha mafunzo kwa wakufunzi 28 wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali kuhusu stadi za kufundisha Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(h) Kuendesha mafunzo kazini kwa wakufunzi 350 wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali wanaofundisha masomo ya Sayansi, Hisabati na *English*;

(i) Kuendesha mafunzo ya Elimu kwa Michezo kwa Wakufunzi 30 wa vyuo vya Ualimu vya Serikali kwa kushirikiana na Shirika lisilo la Kiserikali la LIIKE la Finland;

(j) Kuendesha mafunzo kwa wakufunzi 180 wa Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA kama rejea na mbinu ya kufundishia na kujifunzia katika Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu; na

(k) Kukarabati vyuo saba vya Ualimu vya Serikali (Kitangali, Sumbawanga, Mpuguso, Kabanga, Tandala, Tarime na Murutunguru).

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi itafanya yafuatayo:-

(a) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya Elimu ya Watu Wazima katika Halmashauri 10 ili kubaini changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa Programu za *EWW/ENMRA* na hivyo kuunda mikakati ya kukabiliana nazo;

(b) Kusambaza seti tatu za miongozo ya uanzishaji na utekelezaji wa Mpango wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana katika Halmashauri nane (Ilala, Kinondoni, Temeke, Dodoma (M), Illemela, Bagamoyo, Songea (M) na Mkuranga), zilizo chini ya Mpango wa 'Ndiyo Ninaweza' ili kuimarisha ubora wa utoaji wa Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi;

(c) Kufanya utafiti juu ya hali halisi ya kisomo nchini katika Halmashauri za Wilaya 40 ili kujua idadi ya wasiojua Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) na kuimarisha programu zinazotolewa;

(d) Kuziwezesha Halmashauri za Wilaya tisa kutekeleza Programu ya 'Ndiyo Ninaweza' kwa kuzipatia vifaa na mafunzo;

(e) Kuratibu mipango ya Elimu ya Watu Wazima kwa ushirikiano na Mashirika ya Umoja wa Mataifa nchini; na

(f) Kuchapa na kusambaza nakala 10,000 za Magazeti Vijijini katika kanda na kutoa huduma za uchapaji kwa asasi za kielimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kugharimia mafunzo ya wanafunzi wapya 450 na wanaoendelea 1,450 (Madaktari wa Binadamu, Meno na Tiba ya Mifugo) kwenye Vyuo Vikuu vya ndani kupitia Bodi ya Mikopo;

(b) Kudhamini wanafunzi wanaogharimiwa chini ya Mpango wa *IUCEA* ambapo wanafunzi watano Raia wa Uganda wanaosoma; Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili wanne na Chuo Kikuu Ardhi mmoja na Watanzania 88 wanaosoma Msumbiji, chini ya utaratibu wa kubadilishana wanafunzi baina ya Tanzania na Uganda na Tanzania na Msumbiji;

(c) Kuendelea kutekeleza Mkataba wa Ushirikiano kati ya Tanzania na China kwa kudhamini wanafunzi 10 Raia wa China katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

(d) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu dhana ya uchangiaji wa gharama za Elimu ya Juu na fursa za Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi, kupitia vyombo vya habari na Maonesho ya Taasisi za Elimu ya Juu;

(e) Kugharimia mahitaji maalumu ya wanafunzi wenye ulemavu katika Vyuo Vikuu vinne nchini;

(f) Kugharimia mafunzo ya Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa wahadhiri 44 kupitia Mpango wa DAAD;

(g) Kuratibu uteuzi wa wanafunzi 190 kwa ajili ya nafasi zinazotolewa na nchi rafiki ambazo ni Algeria, China, Cuba, Urusi, Uingereza, Korea ya Kusini, Uturuki, Misri, Mauritius na Serbia;

(h) Kukamilisha na kuanza kuutumia mwongozo wa gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi wa Elimu ya Juu (*Student Unit Cost Framework*);

(i) Kusimamia utekelezaji wa uanzishaji wa Chuo Kikuu cha Kilimo na Sayansi Shirikishi cha Butiama;

(j) Kukamilisha majukumu ya Awamu ya Kwanza ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu hasa katika ujenzi wa kumbi za miadhara katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam; maabara katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam na miundombinu ya majisafi na majitaka katika Chuo Kikuu Ardhi, utakaowezesha wanafunzi 36,344 kupata madarasa ya kusomea na walimu 1,640 kupata sehemu za ofisi na kuendelea kugharimia mafunzo ya wanataluma 156 katika ngazi ya Uzamili na 142 katika ngazi za Uzamivu;

(k) Kuratibu uanzishwaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu utakaogharimiwa na Benki ya Dunia kwa kuandaa miongozo itakayotumika katika ugharimiaji na majukumu mbalimbali kwa ajili ya taasisi za Elimu ya Juu; na

(l) Kuratibu maandalizi ya Muswada wa Sheria utakaobadilisha Sheria ya Mamlaka ya Elimu Tanzania na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuanzisha Mfuko wa Elimu utakaoyaimarisha mamlaka kifedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Idara ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuratibu ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi vinne vya mikoa na vitano vya wilaya;

(b) Kuendelea kuratibu zoezi la uimarishaji wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viweze pia kutumika katika utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi;

(c) Kuendelea kuwahamasisha wanafunzi wa kike na wenyewe ulemavu katika Shule za Sekondari ili wajunge na Elimu ya Ufundini Mafunzo ya Ufundini Stadi baada ya kuhitimu Elimu ya Sekondari;

(d) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Ufundini Mafunzo ya Ufundini Stadi (MMEU); na

(e) Kusimamia utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi wa *Education for Employment* ambao utadumu kwa miaka mitano kwa sekta za maeneo ya Madini na Utalii kuanzia Julai, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Idara ya Ukaguzi wa Shule, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kukagua asasi za elimu 10,684 kati ya 20,981 na kutoa ushauri wa kitaaluma na kitaalamu;

(b) Kusimamia na kuendesha mtihani wa Kidato cha Pili wa mwaka 2013;

(c) Kuwezesha ukarabati wa ofisi 11, ununuzi wa samani kwa ajili ya ofisi tisa za ukaguzi wa shule za Kanda na Wilaya na ununuzi wa magari tisa kwa ajili ya ofisi za ukaguzi wa shule;

(d) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi wa shule wapya 200 watakaoteuliwa kujinga na Idara; na

(e) Kukamilisha taratibu za kuwezesha Idara ya Ukaguzi wa Shule kuwa Mamlaka ya Ithibati na Udhibiti katika ngazi ya Elimu Msingi.

Mheshimiwa Spika, Sera na Mipango. Katika mwaka 2013/14, Wizara kuititia *Idara ya Sera na Mipango*, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kuhusu utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo pamoja na mkakati wa utekelezaji wake;

(b) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Pata Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now – BRN*) zitakazotekeliza katika Sekta ya Elimu;

(c) Kuendelea kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na usimamizi wa takwimu na taarifa za elimu kwa kununua kompyuta na kusimika hazinadata (*database*) katika Halmashauri mpya 40;

(d) Kufanya mapitio na kuandaa michoro na miongozo kwa ajili ya ujenzi wa shule 528 na ukarabati wa vyuo vya ualimu saba (Kitangali, Sumbawanga, Mpuguso, Kabanga, Tandala, Tarime na Murutunguru);

(e) Kufanya mapitio ya muda wa kati wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu; na

(f) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwtu, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuajiri watumishi 1,010 (walimu 180);

(b) Kuidhinisha vibali vya wataalamu wa kigeni 570 katika Sekta ya Elimu;

- (c) Kupandisha vyeo watumishi 1,288 (walimu 1,117);
- (d) Kuthibitisha kazini watumishi 78;
- (e) Kuimarisha utunzaji kumbukumbu za watumishi, kupitia mfumo wa kielektroniki uitwao *Lawson* na kurekebisha taarifa zote za kiutumishi kwa watumishi wote; na
- (f) Kuratibu utekelezaji wa mpango wa mafunzo pamoja na kuwapatia watumishi wapya mafunzo elekezi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kuandaa machapisho mbalimbali yakiwemo nakala 1,000 za kalenda, 1,200 za shajara na nakala 1,000 za Jarida la Elimu ili kuufahamisha umma juu ya sera na mipango mbalimbali ya maendeleo ya Elimu na Mafunzo;
- (b) Kuandaa na kutangaza vipindi 15 vya Redio na tisa vya TV, pamoja na makala 10 katika magazeti ili kuhamasisha umma kushiriki katika mipango mbalimbali ya maendeleo ya elimu;
- (c) Kuratibu ushiriki wa Wizara katika maadhimisho na maonesho mbalimbali ya kitaifa; na
- (d) Kufanya mapitio ya taarifa katika Tovuti ya Wizara pamoja na kuanzisha *blog* ya elimu itakayoelimisha jamii kuhusu mafanikio, changamoto na mabadiliko yanayotokea katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Wakala, Mabaraza na Taasisi, itatekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), itatekeleza yafuatayo:-

- (a) Kudahili wanafunzi wapya wa Programu ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu (*Adult and Continuing Education Studies*) katika ngazi ya Cheti 250 (Morogoro), Stashahada 400 na Shahada 300 (Dar es Salaam) ili kuongeza walimu, wasimamizi na viongozi wataalamu wa Elimu ya Watu Wazima nchini;
- (b) Kudahili wanafunzi wapya 400 wa ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu kwa njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa (UHM), ili kupanua wigo wa utoaji mafunzo;
- (c) Kusambaza mwongozo wa uendeshaji wa Vituo vya Elimu ya Sekondari kwa njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa katika Wilaya zote za Tanzania Bara, kusajili na kuratibu vituo hivyo ili kuwezesha wawekezaji na waendeshaji wa masomo hayo kufuata utaratibu uliowekwa;
- (d) Kuandika moduli za hatua ya tatu (sawa na Kidato cha V na VI) za masomo kumi na moja ya *English, French, Basic Applied Mathematics, Advanced Mathematics, History, Geography, Kiswahili, General Studies, Economics, Commerce na Accounts* ili kuongeza fursa ya utoaji wa Elimu ya Sekondari nje ya mfumo rasmi kwa njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa kwa walengwa wengi;
- (e) Kupanua wigo wa mpango tarajali wa Elimu Changamani baada ya Elimu ya Msingi (*Integrated Post-Primary Education - IPPE*) katika Wilaya tano za Njombe Vijijiini, Iringa Vijijiini, Mbeya Vijijiini, Mbarali, Mufindi na Jiji la Mwanza kwa kushirikiana na Shirika la *UNICEF*;
- (f) Kuandaa na kuendesha mpango tarajali wa elimu mbadala (*Alternative Education*) kwa wasichana waliopata mimba wakiwa shulenii katika Wilaya za Shinyanga Vijijiini na Kahama kwa kushirikiana na Shirika la *UNESCO*;

(g) Kuendesha Kampeni ya KILIMO KWANZA katika Mikoa minane ya Tanzania Bara ili kuinua kiwango cha ufahamu wa dhana hii kwa jamii; na

(h) Kuelimisha jamii juu ya masuala ya Elimu ya Watu Wazima na Masuala Mtambuka kwa kufanya utafiti na kutoa taarifa za utafiti huo katika majarida ya kitaalamu ya *Studies in Adult Education* (nakala 300) na *Journal of Adult Education* (nakala 300) pamoja na jarida la Sauti ya Wanawake (nakala 500) na vitabu vya kuelimisha umma.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kufanya utafiti juu ya uimarishaji wa Elimu ya Awali na Msingi;

(b) Kufanya mapitio ya mitaala ili kuinua ubora wa elimu katika ngazi ya Elimu ya Awali na Msingi;

(c) Kutoa mafunzo kazini kwa walimu wa shule za msingi 550 na walimu wa Shule za Sekondari 550, wakufunzi wa vyuo vya ualimu 550 na Maafisa Elimu 300;

(d) Kuandika vitabu vya kiada kwa ajili ya Elimu ya Awali na Msingi;

(e) Kutoa mafunzo ya Cheti na Stashahada katika kubuni na kutekeleza mitaala; na

(f) Kujenga Kituo cha Mafunzo ya Mitaala na Utafiti wa Maendeleo ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini;

(b) Kutoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa walengwa 300 wa cheti, 350 wa stashahada na 200 wa mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya wafanyakazi wa maktaba za umma, shule, vyo na taasisi nyingine nchini;

(c) Kuendeleza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi wa kike ili kuimarisha utoaji wa Mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka; na

(d) Kuinua ubora wa huduma za Maktaba kwa watu wazima na watoto katika mikoa 21, kwa kuongeza machapisho 50,000.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu, katika Vituo vya ADEM - Bagamoyo na Mwanza, kwa viongozi 900 wa Idara mbalimbali za Elimu pamoja na wafanyakazi kutoka katika Mashirika yasiyo ya Kiserikali (*NGOs*) na Mameneja na Wamiliki wa Shule zisizo za Serikali;

(b) Kutoa mafunzo kwa Wajumbe 5,000 wa Kamati za Shule za Msingi juu ya usimamizi wa Elimu ya Msingi nchini;

(c) Kutoa mafunzo ya awali ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wa Shule Wapya wa Shule za Sekondari 1,500 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara;

(d) Kuendesha mafunzo ya Wakuu wa Shule za Sekondari 4,200 juu ya Misingi ya Menejimenti ya Shule (*Education Management Tool Kit*);

(e) Kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi za Shule za Sekondari 4,000 juu ya usimamizi wa Shule za Sekondari;

4 JUNI, 2013

(f) Kutoa mafunzo kwa Waratibu Elimu Kata 2,286 wa Tanzania Bara juu ya usimamizi wa Elimu ya Sekondari;

(g) Kutoa mafunzo kwa Maafisa Elimu wapya 120 wa ngazi ya Halmashauri;

(h) Kutoa mafunzo ya awali ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa ajili ya Wakaguzi wa Shule 240;

(i) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Maofisa Elimu 264 wa Wilaya na Mikoa kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara; na

(j) Kugharimia mafunzo kazini kwa watumishi 37 wa Wakala ili kuinua ubora wa utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO*, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kushirikisha wadau katika kupanga na kutekeleza Programu za *UNESCO* katika Nyanja zote za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi ya Jamii na Habari na Mawasiliano; na

(b) Kuchapisha na kusambaza nakala 700 za toleo la 10 la Jarida la Tanzania na *UNESCO*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,000,000 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwaka 2013;

(b) Kuendesha Mitihani ya Kidato cha Nne (watahiniwa 480,000) na Maarifa (*Qualifying Test – QT* – watahiniwa 25,000) mwaka 2013, Kidato cha Sita (watahiniwa 52,000) na Ualimu (watahiniwa 21,000) mwaka 2014. Matarajio

ni kusajili jumla ya watahiniwa 578,000 kwa ajili ya mitihani hiyo; na

(c) Kuimarisha usalama na utunzaji kumbukumbu za taarifa mbalimbali kwa kujenga Kituo cha Data (*Data Centre*) kwa ajili ya kutunza taarifa kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Kituo cha Maendeleo Dakawa, itatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuendelea kusimamia taasisi zilizomo katika kituo, ikiwemo Shule ya Msingi, Shule ya Sekondari ya Kidato cha 5 na 6 ya Wasichana Dakawa;

(b) Kuimarisha miundombinu kwa ajili ya kukifanya Kituo cha Maendeleo cha Dakawa kuwa kitovu cha Sayansi na Teknolojia ya Habari ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(c) Kukamilisha taratibu za kuandaa muundo wa kisheria wa kituo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha taratibu za kubadilisha Sheria ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya mwaka 2001 ili kuupatia Mfuko wa Elimu vyanzo vya mapato vya uhakika na endelelevu;

(b) Kuendelea na uchangishaji wa rasilimali ili kupata shilingi bilioni 2.3 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 30 ya wasichana kwenye Halmashauri nane za Wilaya za Geita, Lushoto, Kasulu, Kibaigwa, Lindi, Musoma, Songea na Manyara;

(c) Kuandaa maandiko ya miradi 12 ya Elimu na kuyawasilisha kwa wadau mbalimbali wa elimu wa ndani na nje ya nchi ili kupata fedha kwa ajili ya kugharimia miradi hiyo; na

4 JUNI, 2013

(d) Kuendelea kufadhili Mpango wa *Pre-Entry* kwa wanafunzi wa kike wanaojiunga na vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua na kutathmini mipango ya kuanzisha au kuhuisha vyuo vikuu 10 ili kudhibiti ubora wa elimu itolewayo na vyuo vikuu nchini;

(b) Kuendelea kuratibu na kusimamia udahili wa wanafunzi wapatao 50,000 wanaojiunga na vyuo vikuu ili kufikia lengo la kuwa na jumla ya wanafunzi wapatao 300,000 kwenye Taasisi za Elimu ya Juu nchini ifikapo mwaka 2015;

(c) Kuendelea kuratibu na kuandaa Maonesho ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ili kuuelimisha umma kuhusu malengo, maendeleo na mchango wa Taasisi za Elimu ya Juu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini; na

(d) Kuanzisha ofisi tatu za kanda ili kusogezza huduma karibu na wadau wa Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukagua, kusajili na kutoa ithibati kwa vyuo vya ufundi 40 ili kudhibiti ubora wa elimu;

(b) Kubaini na kusajili walimu 400 katika vyuo vya ufundi;

(c) Kuratibu udahili wa wanafunzi 40,000 katika ngazi ya cheti, stashahada na shahada katika vyuo vilivyo sajiliwa na Baraza;

(d) Kusimamia vyuo vya ufundi 20 katika kutengeneza mfumo wa kuhakiki ubora wa mafunzo; na

(e) Kuidhinisha mitaala 40 ya ngazi za cheti, stashahada na shahada pamoja na kuratibu mafunzo ya walimu 20 juu ya kufundisha kwa kutumia mitaala inayozingatia umahiri, katika vyuo vya ufundi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa Mikopo kwa wanafunzi 98,025 wa Elimu ya Juu wakiwemo waombaji 35,649 wapya na wanafunzi 62,376 wanaoendelea;

(b) Kukusanya marejesho ya mikopo ya Shilingi bilioni 28.8 katи ya shilingi bilioni 44.2 zinazotakiwa kukusanya;

(c) Kuendelea kutoa elimu kwa umma juu ya wajibu wa kila mtu kuchangia Elimu ya Juu, taratibu za utoaji mikopo pamoja na urejeshwaji wake; na

(d) Kufungua Ofisi ya Kanda ya Ziwa - Mwanza na kuziimarisha Ofisi za Kanda za Zanzibar na Dodoma kwa kuziunganisha na Mfumo wa Utoaji Mikopo uliopo Makao Makuu ya Bodi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanza ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Korogwe, Karagwe, Kihonda (Morogoro) na Songea ili kuongeza udahili wa wanafunzi;

(b) Kuanza ujenzi wa Vyuo vipyta vinne vya Ufundi Stadi vya Mkoa katika Mikoa ya Simiyu, Njombe, Geita na Rukwa;

(c) Kufanya maandalizi ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya katika Wilaya za Kilindi, Ukerewe,

Namtumbo, Ludewa na Chunya kwa kumpata mshauri elekezi na mkandarasi na kuandaa michoro;

(d) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa walimu 414 (wanawake 121) wa Vyuo vya Ufundisti visivyo vya Serikali pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(e) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa washiriki 140 (wanawake 46) katika vituo 48;

(f) Kufanya mapitio ya mitaala mitano ya Ufundisti ili utoaji wa Elimu na Mafunzo uzingatie Umahiri (*Competence-Based Education and Training - CBET*) badala ya *Trade Test* ya sasa;

(g) Kuimarisha Vyuo vya Ufundisti ili viwe vya kisasa kwa kukarabati Vyuo vya Ufundisti vya Mkoa katika Mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Mtwara na Chuo cha Walimu wa Ufundisti Morogoro pamoja na kuweka mitambo ya kisasa ya kufundishia ili kwenda sambamba na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia;

(h) Kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya *VETA* na Kituo cha Uwekezaji cha Taifa, Shirika la Taifa la Nyumba pamoja na Shirika la Viwanda Vidogovidogo ili kuwawezesha wahitimu wa ufundisti kupata ajira; na

(i) Kuendeleza mpango wa kutoa mafunzo ya ufundisti viwandani au katika kampuni uitwao *Skills Enhancement Programme (SEP)* kwa ajili ya viwanda au makampuni saba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa fani ya Sayansi na Uhandisi wa mwaka wa kwanza kutoka kiwango cha sasa cha wanafunzi 1,005 hadi 1,258 kufuatia ukamilishaji wa majengo ya mihadhara na maabara;

(b) Kuongeza udahili kutoka wanafunzi 2,800 hadi 3,500 katika ngazi za uzamili na uzamivu;

(c) Kuendeleza ushirikiano na washirika mbalimbali wa maendeleo katika kugharimia utafiti, mafunzo, ukarabati na ujenzi wa miundombinu; na

(d) kuendeleza utafiti katika maeneo yafuatayo: Uimarishaji wa teknolojia mpya ya kutengeneza juisi kutoureka na ndizi na kuifanya teknolojia na huduma hiyo kuwa ya kibashara; mabadiiliko ya Tabia-Nchi na Huduma za kiikolijia na usalama wa chakula; na kupanua uwezo wa kitaalamu kuhusu uhandisi wa rasilimali maji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi 1,250 (250 wa fani ya sayansi);

(b) Kununua vifaa vya maabara;

(c) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunza kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu;

(d) Kununua samani za maktaba na vitabu vya kufundishia;

(e) Kujenga Jengo la Kitivo cha Sayansi za Jamii na Humanitia;

(f) Kupanua Jengo la Kitivo cha Elimu kwa ajili ya kuongeza ofisi za wahadhi;

(g) Kujenga Jengo la Utawala kwa ajili ya ofisi za wafanyakazi waendeshaji;

(h) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA;

(i) Kushirikiana na vyuo na taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususan kwa shahada za uzamili na uzamivu;

(j) Kujenga kituo cha afya ili kuwa na jengo maalumu la kutolea huduma za afya;

(k) Kujenga jengo la maabara na madarasa katika shule ya sekondari ya mazoezi;

(l) Kuajiri jumla ya wafanyakazi 51 (walimu 22 na waendeshaji 29);

(m) Kupata ardhi nyingine kubwa zaidi kwa ajili ya upanuzi wa chuo;

(n) Kukarabati miundombinu ya umeme na barabara;

(o) Kuimarisha viwanja vya michezo; na

(p) Kutengeneza Mpango Kabambe (*master-plan*) wa chuo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kutoka 1,036 mwaka 2012/13 hadi 1,200 mwaka 2013/2014;

(b) Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja;

(c) Kuanza ujenzi wa jengo la utawala, hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000, shule ya mazoezi, maabara mbili za sayansi (Fizikia na Kemia) na jengo jipya la maktaba;

(d) Kuendelea kuimarisha mazingira ya kufundishia kwa kufanya ukarabati na upanuzi wa madarasa, kumbi za mihadhara, maktaba, maabara, mabweni, ofisi za wafanyakazi, mifumo ya maji, barabara, mfumo wa umeme, mawasiliano pamoja na mandhari ya nje ya majengo ya Chuo;

(e) Kuajiri wafanyakazi wapya 94 (wanataaluma 55 na waendeshaji 39); na

(f) Kuendelea kugharimia masomo ya wahadhiri katika viwango vya shahada za uzamili na uzamivu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kuanzisha shahada mpya za kwanza 10 na za uzamili 10, pamoja na masomo 15 yasiyokuwa ya shahada, ili kuongeza idadi ya wanafunzi kutoka 8,115 waliopo hadi 14,498;

(b) Kufanya utafiti wa msingi na tumizi (*basic & applied research*) ambao utasaidia katika kutatua matatizo ya jamii na kuongeza tija;

(c) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA ili kufanikisha shughuli za 107 mafunzo, utafiti na ushauri kwa wadau mbalimbali, pamoja na kazi za kiutawala;

(d) Kufufua vitengo vya uzalishaji vilivyopo kampasi ya Solomon Mahlangu ili viweze kuzalisha na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika mapato ya ndani;

(e) Kujenga miundombinu mipyä na kukarabati iliyopo ili kuimarisha ufundishaji;

(f) Kuendelea kutekeleza utafiti wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi na Tahafifu (*Climate Change*

*Impact Adaptation and Mitigation - CCIAM) na Mlolongo wa thamani ya Kilimo kwa Wakulima Wadogowadogo (Enhancing Propoor Innovation in Natural Resources and Agricultural Value Chains - EPINAV) kwa ushirikiano na Serikali ya Ufalme ya Norway; na*

(g) Kukamilisha ujenzi wa kumbi za mihadhara, ofisi na maabara chini ya Mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi, itatekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4,300 mwaka 2012/2013 hadi 4,700 mwaka 2013/2014;

(b) Kuendelea kugharimia mafunzo ya wahadhiri 20 katika ngazi za uzamili na uzamivu;

(c) Kuimarisha utafiti na uchapishaji wa makala mbalimbali kwa mfano, makala za vyama vya ushirika, maendeleo ya ushirika, utunzaji wa mazingira na upunguzaji wa umasikini, ili kuelimisha jamii;

(d) Kuimarisha vituo vinne vya kanda (Mtwara, Iringa, Mwanza na Singida) vinavyotoa elimu ya vyama vya ushirika, maendeleo ya ushirika, utunzaji wa mazingira na mikakati ya kupunguza umasikini;

(e) Kuimarisha kiwango cha huduma za utafiti na ushauri kwa kushirikiana na vyuo vingine vya ndani na nje ya nchi, hususan Chuo cha Ushirika cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Stirling cha Uingereza, Chuo Kikuu cha Malawi, Chuo Kikuu cha Zambia na *Humber Institute of Technology and Advanced Learning (HITAL)* cha Canada;

(f) Kukamilisha mipango ya uenezaji wa elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochaea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara

ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vyta Ushirika na Shirikisho la Vyama vyta Ushirika; na

(g) Kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ili kukiwezesha chuo kuwa Chuo Kikuu Kamili.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa Maabara za Kompyuta katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Mtwara, Mara na kituo cha Kinondoni;

(b) Kujenga au kukarabati Jengo la Mitihani, ofisi na maabara ya sayansi katika vituo vya Mikoa ya Shinyanga pamoja na Makao Makuu Bungo;

(c) Kukarabati majengo ya Chuo kwa Awamu ya II katika Mikoa ya Kagera, Mara, Kilimanjaro, Shinyanga na Zanzibar;

(d) Kuongeza udahili wa wanafunzi ili ufikie 9,000 kwa Shahada ya Kwanza na Cheti, na 2,817 kwa Shahada za Uzamili na Uzamivu kwa mwaka;

(e) Kuendelea kuweka vitabu vya masomo yote ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwenye mfumo wa dijitali ili wanafunzi waweze kuvitumia kwa urahisi;

(f) Kuwashawishi wachapishaji wa Tanzania kuchapisha vitini vya masomo bila kutegemea fedha toka Chuoni, kwa makubaliano maalumu na Chuo;

(g) Kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 10 chini ya mradi wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu;

(h) Kusimika intaneti isiyotumia waya (*wireless internet*) katika Vituo 10 vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania;

(i) Kuendeleza utafiti katika maeneo yafuatayo: Usalama wa matumizi ya TEHAMA; uimarishaji wa ufugaji wa kuku wa kienyeji, Ilima – Mbeya; uimarishaji wa taratibu za kukusanya na kuzitupa takataka za mijini; matumizi ya ardhi na maji ya Ziwa Victoria; matumizi ya simu za viganjani katika kujifunza; mafanikio na matatizo ya kujifunza kwa njia ya kielektroniki (*e-learning*); na kuanza kutoa mafunzo ya ualimu kwa njia ya Ana-kwa-Ana na Masafa kwa nchi za SADC kwa ngazi ya Stashahada na Shahada.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Chuo Kikuu Ardhi, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kukamilisha ujenzi wa *Lands Building* na kuanza ujenzi wa *Lands Building Annex*;

(b) Kuanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya maabara mbalimbali (*Multi-purpose Laboratory Building*) na jengo la Studio, kwa ajili ya wanafunzi wa Shahada za Usanifu Majengo na Mipango Miji na Vijiji;

(c) Kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli za wanafunzi na nyumba ya Makamu Mkuu wa Chuo na upanuzi wa maktaba;

(d) Kuendeleza miundombinu ya TEHAMA na kuanza ujenzi wa Kituo cha Wanafunzi;

(e) Kuendeleza utafiti katika maeneo yafuatayo: Mazingira, udhibiti wa majitaka na mabadiliko ya tabianchi; kufuatilia tabia ya matabaka yaliyoko chini ya ardhi (*plates tectonic*); kusaidia kutengeneza miundombinu ya upimaji (*survey reference points*); mipango-miji na vijiji; nyumba na makazi; na kufanikisha mchango wa matokeo ya utafiti uliokwishafanya na chuo katika maeneo mbalimbali katika kuimarisha sera za Serikali na utendaji kazi wa kitaalamu;

(f) Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi za umma na binafsi katika maeneo yafuatayo:

Uandaaji wa taarifa za uimarishaji wa hali za majiji na miji ya Tanzania na utekelezaji wake kwa kushirikiana na Mtando wa majiji Tanzania; utathmini na usimamizi bora wa ardhi; upimaji viwanja, mabwawa, njia za umeme, gesi, maji na barabara; na ujenzi wa nyumba na miundombinu na masuala yahusuyo makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi 520 wa shahada ya kwanza na 300 wa shahada ya Uzamili;

(b) kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya maji, umeme na barabara ya kiwango cha lami.:

(c) Kuanza kwa ujenzi wa hospitali ya Mloganzila itakayotumika kwa ajili ya kufundishia na kutoa huduma za afya kwa wananchi;

(d) Kufanya uchambuzi wa takwimu za utafiti wa chanjo ya majoribio dhidi ya VVU katika programu ya utafiti ya TaMoVac-01, na kuendelea na utafiti wa *TaMoVac-II*; na

(e) Kuendelea kugharimia mafunzo ya wataalamu katika Shahada za Uzamivu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu Mzumbe, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 4,324 katika programu mbalimbali (cheti - 429, stashahada - 446, shahada ya kwanza - 1,350, shahada ya uzamili - 2,069 na shahada ya uzamivu - 30);

(b) Kukarabati vyumba vya maktaba na maabara ya kompyuta na kuvifanya kuwa madarasa, na kuweka vifaa na samani katika maktaba mpya ya Kampasi ya Mbeya;

(c) Kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tano katika Kampasi ya Dar es Salaam na kuliwekea samani na vifaa;

(d) Kuanza ujenzi wa madarasa na kumbi za mihiadhara katika Kampasi ya Mbeya na Kampasi Kuu Mzumbe;

(e) Kugharimia mafunzo ya watumishi 12 katika ngazi ya shahada ya uzamili na 15 katika ngazi ya shahada ya uzamivu;

(f) Kuchapisha vitabu 10, makala za kufundishla 4 na makala nyingine 40; na

(g) Kukamilisha utafiti katika maeneo 25 na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo 35 ya menejimenti, uongozi na sayansi ya jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi wapya 8,000 katika shahada ya awali na 400 katika shahada za uzamili;

(b) Kuanza ujenzi wa vyo vya Sayansi za Asili, Hisabati na Sayansi za Ardhi; na kukamilisha ujenzi wa maabara na madarasa;

(c) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka;

(d) Kuendeleza utafiti katika maeneo ya mazingira, rasilimali, uchumi na tabianchi;

(e) Kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 katika Chuo cha Elimu, na kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa Chuo cha Tiba kitakachokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 4,500;

(f) Kugharimia ununuzi wa samani za madarasa, ofisi, mabweni, maabara na kompyuta, vifaa yya kufundishia, pamoja na ununuzi wa magari 15;

(g) Kuweka miundombinu ya umeme na TEHAMA katika vyuo vya Sayansi za Asili, Hisabati na Sayansi za Ardhi;

(h) Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa barabara za ndani na zinazounganisha skuli kwenye maeneo yasiyofikika; na

(i) Kuanza ujenzi wa nyumba za wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Katika mwaka 2013/14, Wizara kuititia *Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere*, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili wanafunzi 2,550 wa programu mbalimbali (500 wa Cheti, 1,000 wa Stashahada na 1,050 wa Shahada ya Kwanza);

(b) Kugharimia mafunzo ya watumishi 18 wapya (wanataaluma 13 na waendeshaji 5);

(c) Kuendeleza ujenzi wa hosteli ya wanafunzi katika Kampasi ya Kivukoni; na

(d) Kuajiri wanataaluma 28 na wafanyakazi waendeshaji 22.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara kuititia Chuo cha Ufundi Arusha, itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kudahili jumla ya wanafunzi 550 wa mwaka wa kwanza (Cheti 25 Stashahada 495, Shahada 30);

(b) Kuanzisha programu tatu katika ngazi ya Stashahada (*Ordinary Diploma au NTAs 4-6*) kama ifuatavyo: Diploma ya Ualimu katika Masomo ya Sayansi (*Diploma in Science Education*); Teknolojia ya Magari na Mitambo Mikubwa; *Biomedical Engineering*. Aidha, mitaala ya programu ya *Hydro-Electric Power Systems* itaandaliwa kwa ajili ya kuanzisha mafunzo katika kituo cha kuzalisha umeme cha Kikuletwa.;

(c) Kuhuisha mitaala 18 ya programu zilizopo za Ufundsi Sanifu (*NTAs 4-6*);

(d) Kuendesha kozi ya Mafunzo ya Awali (*Pre-entry course*) ya kujunga na Chuo kwa ajili ya wasichana, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania;

(e) Kuajiri wanataaluma 30 na wafanyakazi waendeshaji 17;

(f) Kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanataaluma 15 na wafanyakazi waendeshaji 10;

(g) Kufanya ukarabati na kununua vifaa vya karakana na maabara;

(h) Kufanya ukarabati na kuendesha Kituo cha kuzalisha Umeme cha Kikuletwa;

(i) Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Uhandisi Umwagiliaji na kununua samani kwa ajili ya jengo hilo;

(j) Kuendeleza shamba la Mafunzo ya Kilimo na Umwagiliaji la Oljoro;

(k) Kuendeleza ushirikiano na nchi wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundsi vilivyo nchini na vya kimataifa, kama ifuatavyo:

*Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA); Technical Education and Labour Market Support Programme (TELMS) inayofadhiliwa na Serikali ya Italia; na Japanese International Co-operation Agency (JICA);*

(l) Kuandaa kongamano la kimataifa la Vyuo vya Elimu ya Ufundı ambavyo ni wanachama wa *Commonwealth Association of Polytechnics in Africa (CAPA)*;

(m) Kuendelea kufanya utafiti wa kutengeneza mashine ya kupukuchua na kuchambua mahindi kwa ukubwa na kasha kuyafungasha; na

(n) Kuendelea kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu kuhusu ujenzi wa vituo vya kufua umeme, upimaji wa udongo kwa ajili ya ujenzi wa majengo na mabwawa, matengenezo ya vifaa katika hospitali ya Mount Meru, pamoja na matengenezo na ufungaji wa taa za kuongoza magari barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, ninapenda kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa Sekta ya Elimu, ikiwa ni pamoja na Washirika wetu wa Maendeleo, viongozi wa ngazi mbalimbali na Wananchi wa Tanzania kwa ujumla ambao wamechangia katika kufanikisha utekelezaji wa mipango ya elimu na Mafunzo ya Ufundı. Baadhi ya Washirika wetu wa Maendeleo ni Serikali za Algeria, China, Cuba, India, Japani, Kanada, Marekani, Misri, Norway, Pakistan, Poland, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumanı na Uturuki.

Mheshimiwa Spika, aidha, mashirika yaliyochangia katika kufanikisha Programu za Elimu ni pamoja na *Aga Khan Education Services, Airtel, Barclays Bank, Benki Kuu, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Taifa ya Biashara, Book Aid International, British Council, CAMFED, Care International, Children International, Children's Book Project, CIDA, COL, Commonwealth Secretariat, CRDB, DAAD, DANIDA, DfID, EDC, FEMINA, Ford Foundation, GIZ, ILO, International Reading Association, Irish Aid, JICA, JOVC, KOICA, Mwananchi Communications, NMB, NORAD, OPEC,*

*Oxfam, Peace Corps, Plan International, Rockefeller, Shirika la Volkswagen, Sida, Sight Savers International, TENMET, Tigo, Umoja wa Nchi za Ulaya (European Union EU), UNAIDS, UNDP, UNESCO, UNESCO Institute for Life Long Learning (UIL), UNFPA, UNICEF, USAID, VODACOM (T), VSO, WFP, WhiteDent, Winrock International na World Vision.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii ya jumla ya Shilingi 689,681,055,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/14 ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Katika maombi haya:-

(a) Shilingi 98,715,863,400 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Idara ambapo: Shilingi 44,248,528,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 54,467,335,400 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

(b) Shilingi 518,367,140,600 zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Taasisi. Kati ya hizo, Shilingi 188,171,668,000 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 330,195,472,600 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Katika fedha ya matumizi mengineyo, Shilingi 306,000,000,000 ni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu.

(c) Shilingi 72,598,051,000 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, Shilingi 18,830,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 53,768,051,000 ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe binafsi na kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara kwa anwani ya <http://www.moe.go.tz>.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri na hoja imeungwa mkono. (*Makofi*)

Tunaendelea, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mwalimu Mhita; nategemea leo hutalia humu ndani. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. ZABEIN M. MHITA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii na kwa kuwa muda wa dakika 30 hautoshi, naomba Taarifa hii iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Magaret Sitta, naomba kuwsilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundikwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundikwa kujiridhisha na utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Kamati ilifanya ziara katika taasisi mbalimbali za Wizara hiyo ikiwemo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimibili (*MUHAS*), Mradi wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Bahari Zanzibar na Tawi la Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Kamati ya Waziri Mkuu ya Kuchunguza Matokeo ya Kidato cha Nne ya Mwaka 2012. Ili kupata Taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne ya Mwaka 2012, Kamati ilikutana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mithiani Tanzania. Maoni kuhusu matokeo hayo, pamoja na maoni na mapendekezo yanayolenga kuboresha utoaji wa elimu nchini ni sehemu ya Taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 26 - 28 Machi, 2013, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilikutana Dar es Salaam kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 iliyowasilishwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Waziri ilikuwa na maeneo mahususi yafuatayo:-

- Utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii katika bajeti ya Wizara ya Mwaka 2012/2013;
- Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013; na
- Makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, katika rejea ya maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, napenda kulitaarifu Bunge hili kwamba, Serikali imezingatia na kufanya kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mbalimbali, lakini bado maeneo yafuatayo yanatakiwa kufanyiwa kazi zaidi:-

- Mfumo wa Kuhudumia Walimu nchini (*Teachers Service Delivery Scheme*) ambao unahusisha vyombo zaidi ya kimoja kuhudumia walimu;

- Utoaji posho maalumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu (*Retention Scheme*);
- Kuwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kuwa Wakala ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;
- Serikali kuhusisha taasisi zingine katika kutoa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini; na
- Kuimarisha Urejeshwaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu iliyotolewa tangu mwaka 1991.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Sh. 724,471,937,000.00 ziliidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Kati ya fedha hizo, Sh. 631,890,621,000.00 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya Kawaida (*Recurrent Expenditure*) na Sh. 92,581,316,000.00 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo (*Development Expenditure*). Hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2013, Wizara ilikuwa imetumia Sh. 478,788,304,199.86, sawa na asilimia 76 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 44,631,132,329.00, sawa na asilimia 48 kwa ajili ya shughuli za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa fedha kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo hauridhishi kwani hadi kufikia robo ya mwisho ya kipindi cha bajeti, asilimia 48 tu ya Bajeti ya Maendeleo ilikuwa imetumika.

Mheshimiwa Spika, hali hii imeathiri utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Wizara ikiwemo Mradi wa Chuo Kikuu cha Sayansi za Bahari Zanzibar iliyotengewa jumla ya Sh. Bilioni 1.1 na Mradi wa Tawi la Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Zanzibar iliyotengewa jumla ya Sh. bilioni 1.4, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2013 fedha hizo zilikuwa hazijatolewa.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, malengo ya maendeleo katika Wizara hii hayakufikiwa kama iliyopangwa. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali izingatie

malengo ya Bajeti ya Wizara yaliyowasilishwa na kuidhinishwa na Bunge hili kwa kutoa fedha kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Elimu nchini zilibainika kama ifuatavyo:-

- (i) Bajeti pungufu isiyokidhi mahitaji ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii;
- (ii) Mfumo wa kuhudumia walimu unaohusisha vyombo zaidi ya kimoja na hivyo kusababisha urasimu katika upatikanaji wa haki za walimu nchini;
- (iii) Mfumo unaotumika kuajiri Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali nchini kwa kutumia Sekretarieti ya Ajira, unasababisha uhaba wa wahadhiri katika Vyuo Vikuu hivyo;
- (iv) Utendaji kazi usioridhisha wa Idara ya Ukaguzi wa Elimu nchini kutokana na ufinyu wa Bajeti;
- (v) Matumizi ya Lugha ya kufundishia na kujifunzia nchini yanayoainishwa na Sera ya Elimu na Mafunzo bado ni changamoto;
- (vi) Ongezeko la Uhitaji wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini; na
- (vii) Kasi ndogo ya ujenzi wa Chuo Kimoja cha VETA kwa kila Wilaya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii imekusudia kukusanya mapato yenyeye Jumla ya Sh. 171,518,704,660.00. Aidha, Wizara imeomba kuidhinishiwa Jumla ya Sh. 689,681,055,428.00 ambazo Sh. 617,083,004,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Expenditure*) na Sh. 72,598,051,428.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo (*Development Expenditure*) kwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina wa taarifa ya mgawanyo wa fedha katika Bajeti ya Wizara hii na kubaini kwamba, mgawanyo huo kwa kiasi haukuzingatia mambo muhimu katika utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji. Kamati ilishauri kuhamisha fedha katika baadhi ya vifungu vya Wizara (*Budget Reallocation*) ili kuiwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kwa kuongeza tengeo la shilingi bilioni 7.8 kufikia angalau shilingi bilioni kumi dhidi ya mahitaji halisi ya shilingi bilioni 13.8 katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, kumudu utekelezaji wa majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati iliwasilisha mambo muhimu katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, kwa ajili ya kufanyiwa kazi zaidi. Mambo hayo ni pamoja na:-

- Kuiwezesha Idara ya Ukaguzi wa Elimu kifedha kwa kupewa agalau shilingi bilioni kumi;
- Kutenganisha fedha za Matumizi ya Kawaida ya Wizara na fedha ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu;
- Kuharikisha uanzishwaji wa Mfuko Maalumu wa Elimu kuhudumia mikopo ya elimu ya juu nchini; na
- Kuwezesha upatikanaji wa fedha za Miradi ya Chuo Kikuu cha Sayansi ya Bahari shilingi bilioni 1.1 na Tawi la Chuo cha Mwalimu Nyerere Zanzibar shilingi bilioni 1.4 kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kabla ya tarehe 30 Juni, 2013. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 22 Mei, 2013, Kamati pia ilipata nafasi ya kukutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye ni Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kujadili umuhimu wa kuongeza kasi ya kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabili Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilisha kujadili Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Kamati inatoa maoni na ushauri katika kuboresha utolewaji wa elimu nchini katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, inasimamia utekelezaji wa shughuli za taasisi mbalimbali za Elimu ambazo ni Vyuo vya Ualimu nchini, Vyuo Vikuu vya Serikali, Baraza la Mitihani Tanzania (*NECTA*), Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*), Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi (*VETA*), Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*), Taasisi ya Elimu Tanzania (*TIE*) na Elimu ya Watu Wazima.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida (*Recurrent Budget*) imekuwa ikijumuisha fedha za kuendeshea shughuli za Wizara, ikiwemo kuhudumia vyuo na taasisi tajwa pamoja na fedha za Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Pamoja na takwimu kuonesha kiasi kikubwa cha fedha hutengwa kwa Wizara hii, sehemu kubwa ya fedha hizo hutumika kwa ajili ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na kubakisha kiasi kidogo kutumika kwa Wizara **MWAKA**, **BAJETI YA**, **BAJETI**, **ASILIMIA**, **BAJETI YA**  
**KUTEKELEZA**, **MAJUKUMU** yake, **JEDWALI**, **HIFADHATU** na **ZAFIDI**.  
**MATUMIZI** **KWA BODI** **ZINGINE**  
**YA KAWAIDA** **YA MIKOPO** **ZAFIDI**  
**BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA YA WIZARA YA ELIMU** **ZAFIDI**  
**YA UFUNDI**: **IKIJUMUISHA** **BAJETI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU**  
**YA JUU NA BAJETI YA MATUMIZI YA TAASISI ZA WIZARA (2008-2013)**

2008/09	236,026,325,000	120,227,294,000	50.9	115,799,031,000
2009/10	373,577,867,000	120,345,042,600	32.9	253,232,824,400
2010/11	520,918,355,000	243,266,608,000	46.6	277,651,747,000
2011/12	519,639,819,000	319,816,362,000	61.51	99,823,457,000
2012/13	627,729,233,000	306,629,806,100	48.8	321,099,416,900
2013/14	617,083,004,000	306,629,808,100	49.7	311,099,416,900

## Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Aprili, 2013

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikisababisha utekelezaji hafifu wa baadhi ya shughuli nyingine za Wizara, ikiwemo kuhudumia Vyuo Vikuu vya Serikali na Taasisi zingine za Wizara. Kamati inaitaka Serikali itenganishe Bajeti ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini na Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Wizara hii imekuwa ikikwama kutokana na ukosefu wa fedha za utekelezaji wa Miradi hiyo, ikiwemo Mradi wa Chuo cha Sayansi za Bahari Zanzibar. Kamati inaitaka Serikali iwezeshe Wizara kutekeleza Miradi ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu kwa kipeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa Chuo cha Sayansi ya Bahari Zanzibar, ulianza mwaka 2002 na hadi kufikia mwaka 2013 haujakamilika. Aidha, zimetumika fedha nyingi kiasi cha takribani shilingi bilioni sita kuweka jamvi ambalo limekaa muda mrefu hadi nondo zake kushika kutu. Imeamuliwa ujenzi wa Mradi utekelezwe kwa awamu. Kutokana na ukosefu wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka 2012/13 kukamilisha ujenzi wa awamu iliyopo, Mkandarasi anataka kuondoka katika eneo la mradi. Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Fedha zilizoidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni 1.1 zipelekwe mara moja kukamilisha jengo husika lianze kutumika;
- Serikali inapotekeleza miradi mikubwa ianze kutekeleza kwa awamu kwa kujenga jengo moja na kukamilisha, badala ya kutumia fedha nyingi kutandaza jamvi kubwa, hali inayoleta upotevu wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotembelea Mradi wa Tawi la Chuo cha Mwalimu Nyerere Zanzibar, ilisikitishwa na ujenzi wa Jengo la Utawala la Chuo liliojengwa kwa kiasi kikubwa chini ya kiwango. Kamati inaitaka Serikali kurekebisha upungufu uliopo katika jengo hilo mapema iwezekanavyo na kutoa taarifa ya urekebishi hilo. Aidha, mkandarasi aliyetekeleza Mradi huu na Wasimamizi wake wakiwemo Wahandisi kutoka Serikalini wachunguzwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo ya Kamati kwa Wizara, imejidhihirsha kwamba maelekezo ya Kamati yamedharaaulika, kwani Jengo hilo la Utawala la Chuo limefunguliwa rasmi kabla ya mrejesho wa maagizo ya Kamati. Kamati inaitaka Serikali kutoa mrejesho wa utekelezaji wa maagizo ya Kamati mapema iwezekanavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ili kusimamia viwango vya Elimu inayotolewa nchini, sambamba na ongezeko la taasisi mbalimbali takribani 20,000 zinazotoa elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu, Kamati inasisitiza yafuatayo:-

- Serikali iiwezeshe Idara ya Ukagazi wa Elimu nchini kuwa wakala unaojitegemea ili kutekeleza majukumu yake kikamilifu; na
- Serikali iiwezeshe Idara hii kifedha angalau shilingi bilioni kumi kwa mwaka (2013/2014) na vifaa. Aidha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kutekeleza jukumu la Ukagazi wa Elimu zitumike kwa kuzingatia madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya lugha ya kufundishia na kujifunzia yanayoainishwa katika Sera ya Elimu nchini; Kamati imebaini kwamba, lugha ya kufundishia na kujifunzia inaleta changamoto kubwa katika suala zima la utoaji elimu nchini. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti kupata ufumbuzi wa suala hili muhimu, ili kuwa na taifa lililoelimika na lenye maarifa ya kukabiliana na

mazingira yake. Aidha, Sera ya Elimu iwe wazi katika suala la lugha ya kufundishia na kujifunzia kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali mpaka Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo yanayosababisha Walimu kutohudumiwa ipasavyo, ni mfumo uliopo wa kuhudumia walimu (*Teachers Service Delivery System*). Walimu wanahudumiwa na vyombo zaidi ya kimoja na kusababisha adha nyingi, ikiwemo urasimu katika kupanda madaraja, kuijendeleza kimasomo, utekelezaji wa malipo ya haki zao mbalimbali kama mishahara na likizo. Kamati inasisitiza kwamba, Serikali iangalie upya Mfumo wa Kuhudumia Walimu haraka iwezekanavyo ili kukabiliana na adha zinazowakabili walimu nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali kulipa madeni ya walimu nchini ya shillingi billioni 52 (mwaka 2009 - 2012), bado kuna idadi ya walimu takribani 502 (2012/2013) waajiriwa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis, ambao madai yao yalikataliwa kutokana na kutokidhi vigezo vya malipo. Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Taarifa za madai ya walimu ambayo yamekataliwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ulipaji ziwafikie wahusika mapema iwezekanavyo ili waweze kukidhi vigezo vinavyohitajika kwa malipo; na
- Serikali iwe na mpango endelevu wa kulipa madai ya walimu kadiri yanavyojitokeza ili kuondokana na tatizo la mlundikano wa madai ya walimu.

Mheshimiwa Spika, imedhihirika kwamba upungufu wa walimu hasa katika maeneo ya vijijini, unasababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mazingira magumu katika kutekeleza majukumu ya walimu. Kamati inashauri Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo, mchakato wa kutoa posho ya mazingira magumu kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ili kuwafanya wabaki katika mazingira hayo na kuipenda taaluma yao. Aidha, taarifa ya matumizi ya posho ya shillingi 500,000 kwa mwalimu anayeishi

katika mazingira magumu iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2012/2013 itolewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kujenga Chuo Kimoja cha VETA katika kila Wilaya, Kamati inashauri hatua hiyo ya Serikali ipewe nguvu za kutosha kifedha ili kuongeza idadi ya Vyuo hivyo nchini, vitakavyohudumia idadi kubwa zaidi ya wahitimu wa Elimu ya Msingi na Sekondari ambao hawakubahatika kuendelea na masomo. Aidha, *Skills Development Levy* inayopelekwa kuhudumia mafunzo ya ufundi iongezwe kutoka asilimia mbili kwenda asilimia nne, kuwezesha VETA ikiwemo Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, kutoa huduma ya mafunzo hayo kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeamua kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*Folk Development Colleges - FDC*), kutoa mafunzo ya Ufundu Stadi ya VETA, Kamati inashauri Serikali iviboreshe Vyuo hivyo ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi. Aidha, Serikali itoe taarifa kuhusu hatua zilizochukuliwa kuhusu utekelezaji wa suala hili kwa kuzingatia umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudni kubwa ya Serikali ya kutenga takribani shilingi bilioni 306 kuhudumia Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Kamati imebaini kwamba, utaratibu unaotumika kutoa mikopo hiyo, haukidhi mahitaji ya wanafunzi wanaotoka katika familia zenyen kipato duni. Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Serikali iboreshe mfumo wa kupata wahitaji wa mikopo (*Means Testing*) ili kuweza kujumuisha watoto wanaotoka katika familia zenyen vipato duni;
- Juhudi za makusudi zitumike kuongeza makusanyo ya mikopo iliyokwishatolewa tangu mwaka 1991, kwani kiasi cha takribani shilingi bilioni 8.8 (Februari, 2013) zilizokusanywa na Bodi kati ya matarajio ya shilingi

bilioni 18 zilizotarajiwa kukusanya kwa mwaka 2012/2013 ni ndogo; na

- Serikali ianzishe Mfuko Maalumu wa Elimu kwa kuunganisha Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Sheria ya Mamlaka ya Elimu Tanzania kwa ajili ya kutoa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini. Mfuko huo maalumu utabainisha vyanzo vya mapato kuhudumia mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali hutumia muda na fedha nyingi kusomesha wataalamu hadi kufikia ngazi ya Uprofesa. Kutokana na umri wa kustaafu kwa mtumishi wa umma kuwa miaka 60, wataalamu hawa hutumika kwa muda mfupi na kulazimika kustaafu. Aidha wataratibu unaotumika kuajiri **Na Jaaisti Wahadhiri Manitaji Upunguru Waliopo halisi** wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali wa Kutumia Sekretarieti ya Ajira, umesababisha upungufu mkubwa wa wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali nchini kama ilivyofafanuliwa katika Jedwali II.

#### **Jedwali II: Mgawanyo wa Wahadhiri katika baadhi ya Vyuo Vikuu vya Serikali nchini**

1.	Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili	245	506	261
2.	Chuo Kikuu Dodoma	597	1,350	753
3.	Chuo Kikuu Mzumbe	288	400	112
4.	Chuo Kikuu cha Ardhı	235	343	108
5.	<b>Jumla</b>	<b>1,365</b>	<b>2,599</b>	<b>1,234</b>

#### **Chanzo: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı – Aprilı, 2013**

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri ifuatavyo:-

- Suala la kuajiri Wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Serikali litemkelezwe na Vyuo Vikuu kwa kufanya usaili wa

Wahadhiri, pamoja na kutumia utaratibu uliokuwa ukitumika wa kuwaandaa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao kuwa wahadhiri; na

- Wahadhiri ngazi ya Uprofesa waongezewe vipindi vyatika mikataba ya kazi kadiri ya uwezo wao wa kutoa huduma hiyo, baada ya kustaaifu.

Mheshimiwa Spika, Kundi la Watu Wenye Ulemavu ni kundi muhimu linalohitaji mazingira rafiki kuwezesha upatikanaji wa elimu kwa kundi hilo ili kukabiliana na mazingira ya kila siku. Kamati inaitaka Serikali kuwa na mkakati wa makusudi wa kuboresha mazingira ya utoaji elimu kwa Watu Wenye Ulemavu nchini.

Mheshimiwa Spika, imejidhiihishaa kwamba, kumekuwepo na upungufu wa upatikanaji wa huduma ya majisafi na vyoo shulenii hasa katika maeneo ya vijijini, hali inayohatarisha afya za wanafunzi katika maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kwamba, vibali vyatika ujenzi wa shule vinavyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii, viainishe wazi kwamba, ujenzi wa shule uanze kwa kujenga vyoo na kuwezesha upatikanaji wa majisafi kabla ya kujenga madarasa ya shule na shule iandikishwe baada ya kutimiza masharti hayo. Hatua hii itawezesha upatikanaji wa huduma hizo muhimu mashulenii.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupata Taarifa ya Matokeo mabaya ya Mtihani wa Kidato cha Nne 2012, ilipata nafasi ya kuwasikiliza Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii - Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania - Dkt. Joyce Ndalichako, tarehe 17 Mei, 2013 Mjini Dodoma. Kamati ilibaini yafuatayo:-

- Kwa miaka mingi tangu mwaka 1980, Baraza la Mitihani Tanzania limekuwa likitumia utaratibu wa

kupanga alama za mitihani kwa kuangalia matokeo ya somo moja moja (*Flexible Grade Ranges*), utaratibu uliondelea hadi mwaka 2012 kwa kuzingatia mazingira ya kielimu.

- Kutokana na vikao vilivyofanyika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı mwaka 2012, Wizara iliagiza kwamba, utaratibu uliokuwa unatumika miaka yote katika kupanga matokeo kwa mfumo wa *Flexible Grade Ranges* uachwe na badala yake Baraza litumie utaratibu mpya wa aina moja ya kupanga alama za mitihani za masomo yote kwa usawa (*Fixed Grade Ranges*); na
- Ulipotumika utaratibu huu mpya wa kupanga alama za matokeo ya Kidato cha Nne 2012 ndipo yalipopatikana Matokeo ya Ufaulu wa asilimia 34.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaona kwamba, haikuwa busara kutangaza matokeo hayo yanayotokana na utaratibu mpya wa alama bila ya ushirikishwaji mpana wenye kuzingatia athari ambazo zingejitokeza. Kamati inasubiri Taarifa Kamili ya Tume ya Waziri Mkuu kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kushirikiana na Kamati yangu kila tunapohitaji ushauri wako na pia kwa kunipa nafsi hii kuwasilisha taarifa ya Kamati yangu. Aidha, namshukuru Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı - Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı - Mheshimiwa Philipo Mulugo na Watendaji wote wa Wizara hii, wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu Mkuu - Ndugu Selestine Gesimba, kwa kushirikiana na Kamati.

4 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Stephen Ngonyani - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, kwa kushirikiana nami katika kuiongoza vyema Kamati.

Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wa Kamati, kwa busara na umakini katika kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta - Mwenyekiti, Mheshimiwa Stephan Hilary Ngonyani, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Ritta Louise Mlaki, Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mheshimiwa Ezekia Dibogo Wenje, Mheshimiwa Dkt. Antony Gervase Mbassa, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pagalile Rwakatare, Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Zabein Mhaji Mhita, Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mheshimiwa Hassnain Mohamed Murji, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood na Mheshimiwa Christowaja Gelson Mtinda.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, akiwemo Katibu wa Kamati hii, Ndugu Stella Mlambo na Ndugu Pili Omari, chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge - Dokta Thomas D. Kashililah, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99, Kanuni ndogo ya (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, napenda kuchukua nafasi hii kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tumeonya mara nydingi juu ya hatari inayoinyemelea Taifa letu kutokana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kuharibu mfumo wetu wa elimu. Tunasikitika kwamba maonyo yetu yote, ushauri na nasaha tulizotoa zilibezwa kwa kishindo ndani na nje ya Bunge hili. Sasa si maonyo wala utabiri tena, kuporomoka kwa mfumo wetu wa elimu ni dhahiri.

Mheshimiwa Spika, leo hii asilimia zaidi ya thelathini ya Watanzania hawawezi kusoma wala kuandika. Wengi wa vijana wanaomaliza katika vyuo vyetu vya elimu ya juu hawaajiriki wala hawawezi kujajiri. Katika utafiti uliofanywa na shirika moja linalojihusisha na ajira Jijini Dar es Salaam unaonesha kuwa ni theluthi moja tu ya wahitimu katika vyuo vya elimu ya juu nchini wanaoweza kuajirika, kwa maana ya kushindana katika soko la ndani la ajira.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka saba ya utawala wa Rais Kikwete, kiwango cha ufaulu katika ngazi ya msingi na sekondari kimeendelea kushuka huku kiwango cha kufeli kikipanda kwa kasi kubwa. Kwa mujibu wa takwimu za Serikali zinazopatikana kwenye kitabu cha takwimu za elimu, *Basic Statistics in Education in Tanzania*, katika kipindi hiki, kiwango cha kufeli kimepanda kutoka asilimia 10.7, Rais Kikwete alipoingia madaraka hadi asilimia 50 mwaka 2010 alipomaliza awamu ya kwanza ya utawala wake.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya utawala wa Rais, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, umepandisha kiwango cha kufeli hadi asilimia 65.5 katika mwaka 2012, kabla ya kubatilishwa kisiasa kwa matokeo ya kidato cha nne na kuwa asilimia 56.9.

Wataalam wa masuala ya elimu wanabashiri kwamba, kwa kuwa hakuna hatua zozote za maana zinazochukuliwa na Serikali hii katika kurekebisha mambo, kiwango cha kufeli kinaweza kupanda hadi kufikia asilimia 95 kama hakutakuwa na ujanja ujanja wa kufuta matokeo na kuyapanga upya kama Serikali hii ya CCM ilivyofanya siku chache zilizopita.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, nilisema Tanzania ni vyema ikawekwa kwenye kitabu cha maajabu ya dunia yaani, *The Guiness Book of Records* kwa kuchagua baadhi ya watoto wasiojua kusoma na kuandika kuingia kidato cha kwanza na mwaka huu hii *standardization* ya kisiasa ni kituko kingine ambacho sijui Jumuiya ya Kimataifa inatuelewaje, kwa kuwa hata baada ya kufanya *standardization* ya kisiasa bado kiwango cha wanafunzi waliopata sifuri ni kikubwa sana na hajjawahi kutokea katika historia ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sababu za kuperomoka kwa mfumo wetu wa elimu zinajulikana na zimeainishwa katika tafiti mbalimbali zilizofanywa na mashirika mbalimbali na Serikali yenye. Vile vile, mapendekezo juu ya hatua za kuchukua zimeainishwa sana na watafiti mbalimbali wakiwemo wataalam wa Serikali yenye.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, mwaka 2011, Serikali iliunda Kamati iliyokuwa na wajumbe kumi chini ya Uenyekiti wa Ndugu Francis M. Liboy wa Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kuchunguza sababu za kushuka kwa kiwango cha ufaulu wa mtihani wa Taifa wa kidato cha nne mwaka 2010. Kamati ilitoa ripoti nzuri yenye kurasa 137 ambayo ilisifiwa sana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa yake, Kamati illainisha sababu nyngi zilizosababisha matokeo mabaya ya kidato cha nne ya mwaka 2010, zikiwemo sababu za kimfumo, uwezo wa usimamizi wa utekelezaji wa mitaala, upatikanaji wa vifaa na uboreshaji wa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa ya Kamati hiyo,

utaona kwamba, sababu za kufeli na mapendekezo yaliyotolewa yanaakisi kwa kiasi kikubwa, sababu na mapendekezo yatakayotolewa na Tume ya Waziri Mkuu inayoendelea kumalizia kazi yake, kama yalivyodokezwa na Mheshimiwa Lukuvi katika taarifa yake aliyoitoa hapa Bungeni hivi karibuni, isipokuwa katika suala la kufuta na kupanda upya matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, utangulizi wa taarifa hii ulandikwa na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Profesa Hamisi O. Dihenga na Dibaji ilandikiwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa ya Kamati hii haijawahi kutolewa hadharani hadi iliposambazwa hivi karibuni kwenye mitandao ya kijamii na wadau wakereketwa wa elimu. Sasa, ni wajibu wetu kama Kambi ya Upinzani kuhoji mambo yafuatayo:-

(i) Kwa nini Serikali ilificha taarifa ya Kamati iliyounda kuhusu matokeo ya kidato cha nne ya mwaka 2010?

(ii) Kwa nini Serikali iliunda Kamati nyingine kufanya kazi ile ile iliyofanywa na Kamati ilioundwa na Serikali hiyo hiyo, chini ya usimamizi wa Waziri Mkuu huyo huyo na Waziri wa Elimu huyu huyu aliyepo leo?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haiamini kwamba, kuperomoka kwa mfumo wetu wa elimu ni kwa bahati mbaya, wala Kambi ya Upinzani haiamini kwamba Serikali hii haina uwezo wa kirasilimali na kimiundombinu wa kutatua matatizo ya elimu.

Mheshimiwa Spika, tunachoamini katika Kambi ya Upinzani ni kwamba kuperomoka kwa mfumo wa elimu hapa nchini, ndio taswira halisi ya kushindwa kiuongozi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Inabidi Watanzania wenzetu

waelewe kwamba hawa mliowakabidhi Serikali hawawezi na kuendelea kuwaamini ni kuiweka elimu na nchi yetu rehani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, aidha, tuisahau kwamba uwepo wa CCM madarakani kunategemeana sana na idadi kubwa ya wananchi kuendelea na elimu duni. CCM wanajua kwamba uwepo wa idadi kubwa ya watu walioelimika vizuri ni kuhatarisha uwepo wake madarakani. Kwa hiyo, kuharibu mfumo wa elimu kunafanya makusudi ili chama hiki kiendelee kubaki madarakani kiujanja ujanja. Serikali imezoea kufanya mambo mepesi na kukwepa mambo mazito katika Taifa hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wa elimu; tumetoa angalizo kwa miaka mingi sana kwamba mfumo we Mfumo wa elimu umepitwa na wakati. Pia watoto wetu wanaanza shule ya msingi kwa kuchelewa sana 6-9 na wanakaa shulenii kwa muda mfupi miaka saba, darasa la kwanza hadi la saba.

Mheshimiwa Spika, kiwango cha wastani duniani cha kukaa shulenii *compulsory* ni miaka tisa, lakini watoto wetu wanakaa miaka saba pekee. Matokeo yake wanamaliza wakiwa wadogo na bila kuwa na maarifa na stadi za msingi za kuwafanya wajitegemee. Ndio maana tumekuwa tukitoa mapendekezo kwamba mfumo wetu wa elimu upitiwe upya ili:-

(i) Watoto waanze shule mapema. Kama tulivyopendekeza katika ilani ya CHADEMA ya Mwaka 2005 na 2010, watoto waanze shule wakiwa na umri usiozidi miaka sita.

(ii) Wigo wa elimu ya msingi upanuliwe ili watoto wakae shulenii kwa elimu ya lazima kwa muda usiopungua angalau miaka tisa kama ilivyo katika nchi zingine katika bara la Afrika.

(iii) Elimu ya msingi lazima iunganishwe na elimu na mafunzo ya ufundi ili vijana wetu wamalizapo elimu ya

msingi, wawe na maarifa na stadi za kufanya kazi itakayowafanya wajitegemee popote walipo kama ilivyositisizwa katika kipindi cha utawala wa awamu ya kwanza chini ya uongozi wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya, kwamba, mawazo yetu hayajawahi kusikilizwa kwa sababu ama ya vivu wa kisiasa au kuogopa kuipa CHADEMA sifa kwa ubunifu. Matokeo yake tumeendelea kuwa na mfumo wa elimu uliopitwa na wakati na leo sote tunaona matokeo ya kuperomoka kwa mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika hali ambayo si ya kawaida, hatimaye Serikali sasa imeamua kukubaliana na maoni ya CHADEMA na Sera mpya ya Elimu imependekeza kubadili mfumo wetu wa elimu ikiwemo kupanua wigo wa elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya jumla, napenda sasa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani katika sekta na ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Awali; wataalam wa elimu wanatuambia kwamba, elimu ya awali ndio ngazi muhimu zaidi katika elimu kwa kuwa ndio inayotoa msingi wa elimu katika ngazi zinazofuata. Kwa hiyo, wataalam wa elimu duniani wamekuwa wakitoa wito kwa Serikali kuwekeza katika elimu ya awali. Kwa kweli nchi zilizowekeza vya kutosha katika elimu ya awali ndizo zenye mafanikio makubwa zaidi kielimu duniani kuliko zile zisizowekeza katika elimu ya awali.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, hapa kwetu elimu ya awali hajapewa kipaumbele cha kutosha na hii inajidhirisha kwenye randama kwa kuwa hakuna bajeti iliyo tengwa kwa ajili ya elimu ya awali. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Ufundji ya mwaka 1995, inaelekeza kwamba watoto wote wanapaswa kuititia elimu ya awali kabla ya kujunga na elimu ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Sera hii pia inaelekeza kwamba kila shule ya msingi lazima iwe na darasa la elimu ya awali. Hata hivyo, kwa mujibu wa kitabu cha takwimu za elimu kinachotolewa kila mwaka na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı *BEST*, ni asilimia 39.9 pekee ya watoto wenyewe stahili ya kuijunga na elimu hiyo, wanaojiunga na elimu hiyo na kiwango hiki kimekuwa kikishuka badala ya kuongezeka. Kwa mfano, katika mwaka 2012, kiwango cha uandikishaji katika elimu ya awali kilishuka kwa asilimia 3.2 kutoka watoto 1,069,208 mwaka 2011 hadi watoto 1,034,729 katika mwaka wa 2012.

Mheshimiwa Spika, hali ya Walimu katika elimu ya awali pia ni mbaya kwani, kwa wastani, Mwalimu mmoja anafundisha watoto 114 kinyume na kiwango kinachopaswa cha Mwalimu mmoja wanafunzi 25. Hali ni mbaya zaidi katika baadhi ya Mikoa kama vile Dodoma, Kigoma na Morogoro ambapo Mwalimu mmoja hufundisha watoto zaidi ya 600! *Tazama BEST* 2012, ukurasa wa 13.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya hotuba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundı aliyeisoma hivi punde haina mikakati yoyote ya maana itakayoweza kututoa hapa tulipo na hata rasimu ya sera mpya haioneshi mikakati ya kuboresha elimu ya awali.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Msingi na Sekondari; pamoja na kwamba tumefanikiwa kama Taifa kupanua uandikishaji wa watoto katika elimu ya msingi na sasa tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza udahili katika elimu ya sekondari, ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi hizi umeendelea kuwa dhaifu kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana kwamba, Serikali ya CCM imeshindwa kutekeleza mapendekezo mbalimbali ya kitaalam ambayo yamekuwa yakinolewa katika kuboresha elimu inayotolewa katika ngazi za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Spika, maoni hayo ni pamoja na

kuongeza idadi ya Walimu wenye sifa stahiki, kuchochea motisha na mori wa kazi ya ualimu, pamoja na kuboresha mazingira ya kujifunzia. Baadhi ya tafiti za Kimataifa zinaonesha kwamba, ni asilimia nne pekee ya shule za sekondari zenye sifa au zinakidhi vigezo vya chini vya kuwa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, ndio kusema kwamba, ni shule 160 pekee kati ya zaidi ya shule 4000 za sekondari nchini zenye kustahili kuitwa shule za sekondari. Kwa maneno mengine, shule za sekondari zinazostahili kuitwa sekondari hapa nchini hazizidi shule 160. Haishangazi basi kwamba watoto wanaopitia shule za umma za sekondari wanafeli kwa kiwango cha kutisha tunachokishuhudia leo.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kutoa wito kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo ya wataalam wa elimu katika kuboresha mfumo wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Elimu ya Ufundu; ndio mhimili wa kutoa maarifa na stadi za kuweza kujitegemea. Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, kuna vyuo vya ufundu vipatavyo 248 hapa nchini vinavyomilikiwa na taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Mshirika ya Watu Binafsi na Taasisi za Kidini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, vyuo hivyo kwa pamoja vina uwezo wa kuchukua wanafunzi wasiozidi 50,000 katika ngazi ya cheti ukilinganisha, kwa mfano, na wanafunzi 973,812 waliomaliza elimu ya msingi kwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wanafunzi 513,876 walichaguliwa kuijunga na elimu ya sekondari, sawa na asilimia 52.8 ya waliomaliza elimu ya msingi. Ndio kusema watoto 459,936 waliomaliza elimu ya msingi mwaka 2012, sawa na asilimia 42.2, waliingia mitaani bila maarifa na stadi za msingi za kuwafanya wajitegemee.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu za hapo juu utaona

kwamba, vyuo vyetu nya elimu ya ufundi bado ni vichache na havikidhi haja ya mahitaji yaliyopo. Ndio maana CHADEMA ikaweka katika ilani yake mpango wa kuunganisha elimu ya msingi na elimu ya ufundi ili kila mwanafunzi anayepitia elimu ya msingi apate fursa ya kupata mafunzo maalum ya ufundi kabla ya kumaliza ili aweze kupata maarifa na stadi zitakazomwezesha kujitegemea, kujajiri, kuajirika na kupata utamaduni na tabia ya kupenda kazi. Bahati mbaya Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi haina mpango huu na kutokana na wivu wa kisiasa imeshindwa kunakili sera ya CHADEMA na kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu; nchi yetu imepanua elimu ya juu katika ya miaka ya hivi karibuni na hasa katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne ya Rais Kikwete. Kwa sasa tuna vyuo vikuu 28, vyuo vikuu vishiriki 22 na vituo na taasisi zenye hadhi ya elimu ya juu zipatazo 14.

Mheshimiwa Spika, kati ya vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki vilivyopo nchini 36 sawa na asilimia 72, vinamilikiwa na kuendeshwa na mashirika na taasisi binafsi na Serikali inamiliiki na kuendesha vyuo 14 pekee, sawa na asilimia 28 ya vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki vyote nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, naomba nichukue nafasi hii kupongeza sana taasisi na mashirika binafsi na hasa taasisi za dini kwa kutoa mchango mkubwa kwa sekta ya elimu ya juu hapa nchini. Kwa kuwa vyuo hivi vinasomesha vijana wa Kitanzania wanaolipa kodi kwa Serikali hii, ni muhimu sana kuweka utaratibu utakaohakisha kwamba, vyuo nya binafsi vinapata ruzuku maalum ya Serikali katika kuchangia na kupunguza makali ya gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, jambo hili lilielezwa vizuri na kwa kina katika ilani ya CHADEMA ya mwaka 2010 na tutalizungumza tena katika ilani ya CHADEMA ya mwaka 2015 hadi kitakapoeleweka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupanua wigo wa

elimu ya juu hapa nchini, ubora wa elimu inayotolewa katika taasisi hizi bado ni wa wasiwasi mkubwa. Kuna viashiria vingi vinavyoonesha kwamba ubora wa elimu ya juu nchini mwetu sio wa kuridhisha. Kiashiria kimojawapo ni uwezo wa vyuo vyetu kuhimili ushindani wa Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Vyuo vyetu vingi havionekani kabisa katika ligi ya mashindano ya vyuo vikuu duniani. Kwa mfano, kwa miaka takribani mitano mfulizmo ni vyuo viwili pekee vinavyoonekana katika vyuo bora 100 barani Afrika katika Mpango wa Kupima Vyuo Vikuu, *World University Ranking*, uliofanywa na mashirika ya *Times Higher Education* Uingereza, Shanghai China na *Webometrics*.

Mheshimiwa Spika, Vyuo hivi ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ni bora Tanzania ni cha 1,618 kati ya vyuo 2000 duniani vilivyoshindanishwa mwaka 2012. Vyuo vikuu vyetu sio miongoni mwa vyuo vikuu bora 1,000 duniani.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu nydingi zinazokwamisha ubora wa elimu ya juu ambazo zimeelezwa vizuri katika maandiko ya wataalam wa elimu nchini na nje ya nchi. Naomba kwa leo nitaje mambo mawili nayo ni ubora wa Walimu (Wahadhiri) na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa Mwalimu wa chuo kikuu uliyebobea sharti uwe na shahada ya uzamivu *Ph.D* katika eneo husika la kitaaluma. Katika Walimu 3,755 waliopo katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu hapa nchini, ni Walimu 649 pekee wenye shahada za uzamivu sawa na asilimia 17! Upungufu huu unatokana kwa kiasi kikubwa na Serikali kutokutoa kipaumbele katika kusomesha Walimu wa vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo vyuo vikuu vingi vinategemea zaidi fedha za wafadhili wa nje katika kusomesha Walimu wake, ambazo hazina uhakika. Ndio maana katika llani ya CHADEMA ya mwaka 2010 tulisema

na tutasema tena mwaka 2015, kwamba Serikali iwekeze fedha za kutosha katika kusomesha Walimu wa vyuo vikuu ili wapate viwango vinavyokubalika Kimataifa. Hali ipo hivyo hivyo katika upande wa utafiti. Fedha zinazotolewa kwa ajili ya utafiti ni kidogo sana na tafiti nyingi za vyuo vikuu zinategemea ufadhili wa nje.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uhaba mkubwa sana wa fedha za maendeleo na hata za matumizi mengineyo yaani *OCs* kwa vyuo vya elimu hapa nchini. Hali inayopelekea majengo ya vyuo vyetu hasa vile vya zamani kama UDSM, Ardhi, Sokoine, Mzumbe na Muhimbili kuonekana machakavu kwa kuwa ukarabati haufanywi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya ongezeko la wanafunzi haliendi sambamba na ujenzi wa madarasa, vyoo, maktaba na mabweni. Matokeo yake wanafunzi wanaishi kwa tabu sana huku afya zao zikiwa mashakani. Kwa wengine hali ya ufinyu wa sehemu za kulala vyuoni huwafanya wafanye matendo maovu yasiyokubalika katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazopelekwa kwenye vyuo vyetu ni kidogo mno na zinapungua kadiri siku zinavyokwenda huku idadi ya wanafunzi ikiongezeka. Hali hii sio tu inaleta migomo isiyo ya lazima bali pia inawaweka watendaji wa vyuo hivyo njia panda.

Mheshimiwa Spika, anguko la elimu nchini na mustakabali wa Taifa. Ni mwaka mmoja tu umepita tangu Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA itoe angalizo kali kwa Serikali juu ya kasi kubwa ya kuporokoka kwa Elimu ya Tanzania na hivyo kuitaka Serikali kuchukua hatua madhubuti ili kuliepusha Taifa na balaa hilo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali hii ya CCM imeendelea kupuuza ushauri mzuri inayopewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na matokeo yake ni kwamba, anguko la kipindi hiki ni kubwa kuliko maanguko yote yaliyowahi kutokea katika Historia ya Tanzania ambapo

asilimia 56.9 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa kidato cha nne mwaka 2012 walipata alama sifuri baada ya kukarabatiwa yaani *standardization*.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya mtihani wa Kitaifa wa kidato cha nne mwaka 2012 yanaakisi kiwango cha juu cha kudorora kwa elimu nchini na matokeo ya Serikali ya CCM kuipuuza elimu. Pamoja na juhudhi kubwa za Serikali kubatilisha matokeo hayo bado ukweli umebakie pale pale kama ambavyo wataalam wa elimu walivyobashiri na kuonya zoezi hilo kuwa halina tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya awali ambayo asilimia 65.5 walipata sifuri sasa imekuwa 56.9 yaani punguzo la asilimia 8.6 wakati wale wa daraja la nne waliokuwa asilimia 33.5 sasa imekuwa 28.1 sawa na ongezeko la asilimia 5.4 huku wale wa daraja la pili asilimia 1.8 na sasa ni 2.8 sawa na ongezeko la asilimia moja. Kwa wale wa daraja la kwanza walikuwa asilimia 0.5 na sasa ni 0.9 sawa na ongezeko la asilimia 0.4.

Mheshimiwa spika, kimsingi ukilinganisha matokeo haya utaona kwamba, hayana tofauti ya maana *no significant difference* na yale ya awali kwa sababu daraja la kwanza hadi la tatu bado hawajafikia asilimia 10. Hawa ndio wanaotegemewa kujunga na elimu ya kidato cha tano!

Mheshimiwa Spika, vile vile ni asilimia 33.5 tu ndio wamepata daraja la nne au theluthi ya watahiniwa wote ukilinganisha na asilimia 28.1 ya awali. Kwa ujumla asilimia 56.9 (57) ya watahiniwa wote wamepata daraja la sifuri ukilinganisha na 65.5 ya awali.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi bado asilimia 90.5 ya watahiniwa wamepata daraja la nne na sifuri katika matokeo mapya ukilinganisha na yale ya awali ya asilimia 93.6. Kwa maana hiyo, bado zaidi ya nusu ya watahiniwa wote wa 2012 wamepata daraja sifuri au wamefeli hata baada ya mabadiliko ya ripoti ya awali ya Tume. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, matokeo mapya yanakubaliana na mapendeleko na ushauri wa wadau mbalimbali wa elimu Tanzania kwamba, matokeo ya awali hayakuwa na kasoro zozote na kwamba mfumo uliotumika haukuwa sababu ya matokeo hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna punguzo la asilimia ya walifeli kwa asilimia 8.6 na hivyo kuwa asilimia 56.9 bado matokeo haya ni mabaya kuliko matokeo yote ya kidato cha nne kwa nchi hii toka tumepata uhuru. Vile vile kama tatizo ni matumizi ya mfumo mpya wa *ku-grade*, vipi hata haya yamekuwa mabaya kuliko ya mwaka 2011 yaliyotumia mfumo wa *flexible grading* na siyo *fixed?* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa uchambuzi huu ni wazi sasa kuwa ukweli ni lazima usemwe hata kama utauma namna gani ili Taifa lisonge mbele kwa kuwa ni dhahiri kuwa, watoto wetu walifeli kwa sababu ya mfumo wetu wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapenda kuionya Serikali kuwa mchezo huu wa kisiasa uliochezwa ili kupunguza hasira za wananchi ni mchezo mchafu ambao haulipeleki Taifa letu mbele kwa kuwa hauelezai vyanzo vya matatizo makubwa yanayosababisha anguko la elimu nchini na mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kuna ushahidi wa kutosha kwamba, Serikali inahusika sana kusababisha anguko kuu la matokeo ya kidato cha nne 2012 na ushahidi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Novemba, 2012, Kamishna wa Elimu Profesa E. P. Bhalalusesa alimwandikia Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa yenye kichwa cha habari; Yah: Utaratibu wa Matumizi ya Alama za Maendeleo ya Mtahiniwa na Viwango vya Ufaulu katika Mitihani ya Taifa. Katika barua hiyo, Kamishna wa Elimu alisema hivi, "Kutokana na maelezo ya barua yako, Wizara

imeridhia mapendekezo ya uwiano wa alama za maendeleo ya wanafunzi CA na alama za mtihani wa mwisho kubadilishwa kutoka alama 50:50 na kuwa 30:70.

Wizara inaridhia pia alama 15 zitokane na mtihani wa kidato cha pili kwa wanafunzi wa kidato cha nne. Aidha, Wizara inataka mlete mchanganuo wa jinsi alama 15 zilizobakia zitakavyopatikana ili kuleta uelewa wa pamoja. Vivyo hivyo mchanganue mgawanyo wa alama za maendeleo ya mwanafunzi kwa kidato cha sita"

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Desemba, 2012, mwezi mmoja baadaye Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı, Selestine Gesimba alimwandikia barua Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania kama ifuatavyo:-

"Yah: Maagizo ya kuhusu Utaratibu wa Matumizi ya Viwango vya Ufaulu katika Mtihani wa Kidato cha Nne na Sita. Tafadhali rejea kikao cha tarehe 10/12/2012 kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Wizara kuhusu somo tajwa hapo juu.

Baada ya kupitia mapendekezo mliyowasilisha pamoja na majadiliano katika kikao husika naelekeza yafuatayo yafanyike.

(i) Viwango vya Ufaulu vilivyopendekezwa na Baraza la Mitihani Tanzania vitumike kwa mitihani ya kidato cha nne 2012 na kidato cha sita kwa mwaka 2013 tu.

(ii) Viwango vya kutunuku *grade range* vifanyiwe kazi zaidi ili kupunguza au kuondoa mlundikano (*bunching*) wa alama katika kundi moja.

(iii) Baraza la Mitihani Tanzania lifanye utafiti kuhusu matumizi ya alama za maendeleo kwa O-Level/na A -Level/na kutoa mapendekezo mapya ya matumizi ya alama za maendeleo yaani *Continuous Assessment*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maagizo haya ufanyike mapema ili mapendekezo yaliyowasilishwa yaweze kuanza kutumika katika mwaka wa fedha 2013/2014."

Mheshimiwa Spika, mjumbe mmojawapo wa kikao kinachotajwa na barua hii, ni Profesa Sifuni Mchome ambaye alikuja kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kuchunguza Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa kidato cha nne mwaka 2012 na kupendekeza matokeo hayo yafutwe.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine walikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii; Mheshimiwa Philipo Mulugo, Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii; Selestine Gesimba, Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii na Profesa E. P. Bhalalusesa, Kamishna wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, wote hawa ni maafisa wa Serikali ambao walishiriki kikamilifu kufanya maamuzi na kutoa maagizo ya kubadili mfumo wa kupanga matokeo ya kidato cha nne 2012 ambao sasa wanakimbia kivuli cha maamuzi yao na kulibebesha Baraza la Mitihani la Tanzania mzigo wa uvivu wao wa kufikiri na woga wa kuchukua hatua za kuwajibika kwa kujuzulu kwa kushindwa kusimamia elimu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inakichukulia kitendo cha Serikali kulitupia Baraza la mitihani mzigo ili kuhalalisha makosa iliyoyafanya na kusababisha wanafunzi wa kidato cha nne 2012 kupata alama sifuri kwa zaidi ya asilimia 60, wakati Serikali ndio iliyokuwa ikitoa maagizo kwa Baraza la Mitihani, ni usaliti wa hila kwa Baraza la Mitihani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha uamuzi wa Serikali wa kuyafuta matokeo ya kidato cha nne yaliyopitishwa na Bodii ya NECTA, chini ya uongozi wa Profesa Rwekaza Mukandala ulikwenda kinyume kabisa na misingi ya utaalam na weledi yaani *professionalism* na kwa misingi hiyo haukuwa na uhalali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu mbele ya Bunge hili, *standardization* iliyofanywa na Serikali kwa matokeo ya kidato cha nne inakwenda kumsaidia vipi mwanafunzi ambaye hakuandika chochote katika karatasi ya mtihani zaidi ya kuchorachora picha za ajabu na kuandika matusi? Pia, je, marekebisho haya, yanakwenda kusaidia vipi familia ambazo ziliathirika na matokeo haya kwa watoto wao kujua kutokana kufeli mtihani huo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa vyovyyote vile mchakato wa uliobadili matokeo ya kidato cha nne hauna tija kwa Taifa kwa kuwa unaturudisha nyuma. Itakumbukwa kwamba sababu zilizopelekea Serikali kuitisha matumizi ya viwango vipyta vya ufaulu katika mitihani ya kidato cha nne na sita 2012/2013 ni kwamba mfumo wa zamani ulikuwa haupandishi ubora wa elimu yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba uamuzi wa Serikali ya CCM kurudi kwenye mfumo wa zamani wa kupanga matokeo, una lengo la kuendelea kudidimiza elimu ya nchi yetu jambo ambalo halikubaliki.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Bdi ya *NECTA* kwamba kwa kuwa Serikali imelazimisha mabadiliko ya matokeo ya kidato cha nne, kinyume na miiko ya weledi wa Bodi hiyo, basi Bodi hiyo ijiuzulu ili kulinda heshima yake ya utaalam na weledi kwa kutoruhusu maamuzi ya kisiasa kuathiri utendaji wa kitaalam. Aidha, kwa kufanya hivyo, Serikali itapata funzo la kuwajibika inapofanya makosa ya wazi kama haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kauli ya Serikali iliyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 3 Mei, 2013 na Mheshimiwa William Lukuvi kuhusu taarifa ya awali ya Tume ya Taifa ya Kuchunguza Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, 2012 ilisema hivi:

"Maamuzi ya Baraza la Mawaziri yanalenga kutenda haki kwa Walimu na wanafunzi ambao juhudii zao za

kufundisha na kujifunza zimepimwa kwa kutumia mfumo mpya ambao hawakupata fursa ya kushirikishwa na kuandaliwa".

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haioni uhalisia wa kauli hii wala haioni nia ya dhati ya Serikali kuwasaidia wananchi kupata elimu bora kwa haki na kwa usawa, kwani ni hivi majuzi tu katika Mkutano wa Kumi wa Bunge, ambapo hoja binafsi ya Mheshimiwa James Mbatia kuhusu udhaifu ulioko katika sekta ya elimu nchini ilibezwa na Serikali kwa kutolewa majibu mepesi kinyume na kanuni za Bunge na hatimaye kuyazima maazimio ya Bunge ya kuinusuru elimu ya Tanzania yaliyokuwa yamependekezwa katika hoja hiyo.

Mheshimiwa Spika, ni katika mkutano huo huo wa Bunge ambapo hoja binafsi ya Mheshimiwa Joshua Nassari kuhusu Baraza la Mitihani linavyoathiri elimu ya Tanzania iliondolewa katika orodha ya shughuli za Mkutano wa Kumi wa Bunge bila ridhaa ya mtoa hoja kinyume na kanuni ya 58(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, maazimio yaliyokuwa yameainishwa katika hoja zote mbili nilizofanyia rejea hapo juu yalikuwa na tija sana katika kuuboresha mfumo wa elimu hapa Tanzania na pia yalikuwa yanatoa suluhu kwa tatizo la kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi ambalo linaongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Serikali ya CCM chini ya mwavuli wa wingi wa Wabunge wake Bungeni, cha kuzivuruga hoja hizi na hivyo kusababisha maazimio ya Bunge juu ya hoja hizi kutoteklezwa, ni udhaifu mkubwa sana kwa chama kinachotawala cha CCM na Serikali yake na ni ushahidi uliokamilika kwamba elimu kwao sio kipaumbele cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, niwe mkweli na muwazi kwamba, Serikali ambayo elimu sio kipaumbele cha Taifa, haiwafai Watanzania kwa karne hii. Hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani

inaionya Serikali kuacha kabisa kufanya mzaha na elimu ya Taifa hili kwani ikiendelea kufanya mchezo na elimu kama ilivyo sasa, italiingiza Taifa kwenye msiba mkubwa wa umasikini mkuu ambao matanga yake hayaishi leo wala kesho bali ni ya miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawapa angalizo wananchi wote wa Tanzania kwamba, haya yote yanatokea kwa kuwa Serikali ya CCM hajaiweka elimu kuwa kipaumbele cha Taifa na kwamba umefika wakati wa kufanya mabadiliko makubwa ya mfumo wa utawala kwa kuchagua chama chenye nia ya dhati ya kuleta mabadilko kitakachounda Serikali inayojali elimu ya watoto wao na bila shaka chama hicho hakiwezi kuwa CCM tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gharama za elimu nchini; wote tunatambua kuwa kupata elimu ni haki ya kila Mtanzania. Vile vile, tunatambua kuwa soko huria limeshamiri katika sekta zote nchini ikiwemo elimu. Lakini kinachosikitisha, wote tunaelewa kipato cha Watanzania wengi na Mwalimu Nyerere alionya kuwa tukishabaguana katika elimu tutakuwa na matabaka na kimsingi hapo ndipo tulipofika. Haiwezekani Serikali ishindwe kudhibiti gharama za elimu hapa nchini katika ngazi zote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, inawezekanaje mwenye shule aamue kupandisha ada kwa shilingi milioni moja ghafla? Inawezekanaje vyuo vya elimu ya juu vilipishe wanafunzi wao fedha nyngi kuliko kiwango kinachotolewa na Bodi ya Mikopo? Mfano, chuo cha St Joseph Songea wanapaswa kulipa chuo shilingi 2,750,000/= huku Bodi ya Mikopo ikiwapatia sh. 1,043,000/= hivyo kujikuta wakilipa sh. 1,707,000/=.

Mheshimiwa Spika, hivi ni watoto gani wa wakulima wataweza kulipa fedha hii? Kibaya zaidi vijana hawa wanasona masomo ya sayansi yaani *Bachelor of Science*

*and Technology in Agriculture.* Je, tutafanikisha Kilimo Kwanza kama tunapoteza vijana wenye uwezo wa kusomea taaluma hii? (*Makof!*)

Mhesimiwa Spika, sambamba na shule binafsi umejitokeza utata mkubwa kuhusiana na ongezeko kubwa la ada kwa shule ya Serikali ya *Arusha School* tofauti na wenzao wa Olympio. Wazazi na walezi wameandika barua kwa watendaji wa Wizara Iakini hadi ninapozungumza hawajajibowi na hawaalewi hatma ya watoto wao.

Mhesimiwa Spika, swalii la kujiuliza, kama shule hii iko chini ya Wizara, ni kwa nini ada zinapanda kiholela na ni kwa nini kwa shule hiyo tu na sio zote? Ni vyema Serikali iangalie utaratibu mzima wa kugharamia elimu hapa nchini ili wazazi, walezi na wadau wote wa elimu waelewe vizuri.

Mhesimiwa Spika, changamoto katika Sekta ya Elimu na tatizo la kupanga vipaumbele vya bajeti ya elimu. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Haki Elimu 2011, hali ya mazingira katika shule zetu kuanzia elimu ya awali mpaka sekondari ni mbaya kwa kujifunzia.

Mhesimiwa Spika, uwiano wa Mwalimu mwenye sifa kwa mwanafunzi, elimu ya awali umebaki kuwa 1:124 badala ya 1:25; uwiano wa matundu ya vyoo kwa wanafunzi msingi unakadiriwa kuwa 1:56 badala ya 1:25 kwa wavulana na 1:55 badala ya 1:20 kwa wasichana. Mrundikano wa wanafunzi darasani ni mkubwa mno, wastani kwa nchi nzima ni 1:70 badala ya 1:40, uhaba wa madawati unafikia asilimia 49.1 kwa sasa ikiwa ni upungufu wa takribani madawati 1,879,806 kati ya 3,893,338 yanayohitajika.

Mhesimiwa Spika, shule za sekondari pia zinaathiriwa na changamoto za namna hii pamoja na tatizo la uhaba wa mabweni, maabara, vitabu na Walimu wa masomo ya sayansi. Pia hamasa ya mioyo ya Walimu kujitolea na kuridhika na ualimu iko chini sana. Changamoto hizi zinatupa ishara

kuwa shule zetu za umma msingi na sekondari si shule ambazo zinaweza kumfanya wanafunzi afundishwe na ajifunze ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, ni jambo ola kushangaza kuona hata shule za vipaji maalum kama Mzumbe hawana vyoo hali iliyopelekea vijana hawa kuacha masomo na kuandamana hadi kwa Mkuu wa Mkao. Kama shimo moja la choo linatumika kwa wanafunzi 150 hivi kweli tunawapeleka wapi watoto wetu?

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa changamoto hizi zina uhusiano wa moja kwa moja na upangaji wa vipaumbele vyetu na maamuzi ya matumizi ya rasilimali za Taifa. Ikiwa tunataka kutoka hapa tulipo kwenda mahali bora zaidi ni lazima upangaji wa bajeti katika sekta ya elimu uangaliwe kwa makini sana kwa kuwashirikisha wadau wote wa sekta ya elimu ili kutatua changamoto za sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka sasa Serikali kuacha visingizio vya uhaba wa bajeti na wahisani kukwamisha utekelezaji wa mipango ya kuikwamua elimu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa mapendekezo yafuatayo katika upangaji wa bajeti katika Sekta ya Elimu, 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wanafunzi kutojua kusoma na kuandika; hili bado ni tatizo kubwa na hadi sasa Serikali hajawa na mkakati maalum wa kuondoa tatizo hili. Shule za msingi kwa madarasa yote bado zina wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika. Hali hii imejitokeza pia katika baadhi ya shule za sekondari licha ya Serikali kudai itawabaini na kuwaondoa.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili lazima lianze kufanyiwa kazi kwa kuwa na mpango maalum wa kuwasaidia wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika. Mpango huu lazima uwashirikishe wadau wote wa Sekta ya Elimu hasa wazazi ili watambue majukumu yao katika kuondoa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa elimu ya awali ni msingi wa mwanafunzi katika kujifunza kusoma na kuandika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inataka kuona bajeti hii ikitilia mkazo uwekezaji katika elimu ya awali hasa kuwa na Walimu bora na vifaa nya kujifunzia na kufundishia. Uwekezaji katika elimu ya awali utachangia sana kuondoa tatizo sugu la kuwa na wanafunzi wasiojua kusoma na kuandika katika shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuwa ni majuzi tu Waheshimiwa Wabunge wamepitia Rasimu ya Sera ya Elimu na msisitizo umewekwa kwenye elimu ya awali, lakini cha ajabu bado mkakati wake hauoneshi ni jinsi gani itawaandaa Walimu wa shule hizi. Utaratibu wa sasa ni Walimu wale wale wa msingi hufundisha na awali.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kwa kuwa watoto hawa wana mahitaji maalum na hivyo wanahitaji Walimu maalum walipita katika vyuo maarufu kama Montesori ili kuwalea vizuri watoto hawa wajitambue na kupenda shule hasa ikizingatiwa hapa ndipo ubongo wa mtoto unapokuwa kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba, katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi, MMEM III, Serikali imeazimia kuanzisha fungu maalum katika bajeti ya elimu, *separate budget line* kwa ajili ya elimu ya awali na kutenga asilimia 20 ya matumizi yake ya kawaida kwa ajili ya sekta ya elimu, huku asilimia 60 ya fedha zitakazotengwa kwa ajili ya sekta kuelekezwa katika elimu ya awali na msingi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inataka Serikali kutekeleza mpango huu katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa fedha na Wataalam wa Idara ya Ukaguzi wa Shule; ripoti ya tathmini ya Mpango

wa pili wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM); inaonesha kutofikiwa kwa malengo ya ukaguzi wa shule, hivyo kuziacha shule nyingi bila kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ya kutofikiwa kwa malengo ya ukaguzi ni uhaba wa fedha unaosababisha upungufu wa vitendea kazi na wataalam wa ukaguzi. Mwaka 2011/2012, shule za msingi zilizokaguliwa ni 3,061 tu kati ya 7,200 zilizopangwa kukaguliwa (sawa na asilimia 42.5). Aidha, sekondari 935 (43.3%) zilikaguliwa katи ya 2,100 zilizopangwa kukaguliwa.

Mheshimiwa Spika, hii ni kusema kwamba ni asilimia 19.1 pekee katи ya shule za msingi nchini ambazo hukaguliwa na asilimia 21.4 tu ya sekondari ambazo hukaguliwa kwa mwaka. Tafsiri hapa ni kuwa uwezo wa fungu la ukaguzi katika bajeti ni kukagua asilimia 20 tu ya shule zake zote, asilimia 80 ya shule hazipati fursa ya kukaguliwa kutokana na uhaba wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, athari za shule kutokaguliwa ni nyingi, utendaji wa Walimu kutopimwa, utekelezwaji wa mitaala, maendeleo ya shule na wanafunzi kutopimwa. Kama ukaguzi haufanyiki kwa nini tunashangaa wanafunzi kufeli au kumaliza elimu ya msingi na kufaulu mitihani ilihali hawajui kusoma na kuandika?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali katika bajeti ya Elimu ya 2013/2014 kutoa kipaumbele katika kuimarisha ukaguzi wa shule. Aidha, Serikali itenye fungu la kutosha kwa ajili ya ukaguzi, kwa kuwa tumeona athari ya shule kutokaguliwa katika matokeo mabaya ya wahitimu wa darasa la saba, kidato cha pili na cha nne 2012 na tusingependa kuona haya yakijirudia.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kitengo kimekuwa hakitengewi fedha za kutosha, watumishi wake ambao kimsingi wanapaswa kuwa mashulen ikuhakiki ufundishaji na ufundishwaji, wameishia kukaa ofisini kwa kuwa hawana

vitendea kazi vya kuwafikisha huko. Kwa mfano, kanda yenye shule za sekondari 430 na vyuo vya ualimu kupatiwa shilingi milioni nne kwa mwaka ni jambo lisloelezeka na ni kichekesho kwani fedha hii haitoshi ukarabati wa magari mawili ya kanda achilia mbali mafuta! Hivi kama kazi mojawapo ya ukaguzi ni kufuatilia na kuhakiki ubora wa elimu na bila kufika na kuona na kutoa ushauri kwa watoa maamuzi ni vigumu sana kujua kinachoendelea ndani na nje ya madarasa yetu.

Mheshimiwa Spika, ni kwa muda mrefu sasa Serikali kupitia Wizara hii iliahidi kuanzisha Wakala wa Ukaguzi na jambo hili likakolezwa na Rais Dkt. Kikwete wakati wa mkutano wake na viongozi wa shule binafsi *TAMOGOSCO* kule Mbeya 31 Aprili, 2013.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni lini sasa Wakala huu utaanza? Hii ni kwa kuwa Wakaguzi huishia kutoa ushauri na si kutekeleza au kuchukua hatua kwa ule upungufu wanaokutana nao.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa fedha za ruzuku shulen; ili kuinua ubora wa elimu Serikali iliazimia kutoa ruzuku kwa kila mwanafunzi kupitia MMEM na MMES; sh. 10,000/= kwa mwanafunzi shule ya msingi na sh. 20,000/= kwa mwanafunzi wa sekondari kila mwaka. Hata hivyo, mujibu wa utafiti uliofanywa na Haki Elimu 2012, ni wastani wa sh. 6,025/= tu ambazo hufika shulen badala ya sh. 10,000/=, kwa msingi na wastani wa sh. 14,178/=, pekee badala ya sh. 20,000/= zilizoahidiwa kwa kila mwanafunzi wa sekondari.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekwamisha shughuli nyingi za maendeleo ya mwanafunzi shulen, vitabu havinunuliwi kwa wakati, nyenzo za kufundishia na fedha za uendeshaji wa shule hazitoshi. Katika baadhi ya shule hasa katika Mkoa wa pwani, fedha za *capitation grants* zinazopelekwa ni sh. 2,000 kwa mwanafunzi wa shule ya msingi.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi, licha ya kuwa kidogo

mno kwa mahitaji, bado zinakatwa tena kwa ajili ya michezo ya UMITASHUMTA na hivyo kiasi kinachobakia hakiwezi kufanya chochote. Matokeo yake ni kwamba, wazazi wanalahimishwa kulipa michango mbalimbali ya shule, jambo ambalo ni kero kubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kutenga kiwango kamili cha sh. 10,000/= na sh. 20,000/= kwa mujibu wa ahadi na kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatolewa zote kwa shule husika. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuzingatia mfumuko wa bei wakati wa kutoa fedha za ruzuku kwa kuwa mfumuko wa bei umekuwa ukiathiri pia uwezo wa shilingi katika kufanya manunuvi.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa upangaji wa kiwango hiki cha ruzuku ulifanyika 2002 - 2006 wakati mfumuko wa bei ukiwa katika wastani wa 4.4%, wakati leo wastani wa mfumuko wa bei ni takriban asilimia 14.9% (Tazama Taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*NBS*) Septemba, 2012), hii ikiwa ni mara tatu zaidi ya wastani wa mfumuko wa bei wa kipindi fedha za ruzuku zilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, upangaji na usimamizi wa fedha za umma. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Fedha iliyotolewa tarehe 9 Juni, 2011, Serikali ilitoa ahadi ya kupunguza bajeti ya matumizi ya kawaida ili kuongeza bajeti za miradi ya maendeleo. Hata hivyo, bado Wizara ya Elimu imeendelea kutenga fedha nyingi katika matumizi ya kawaida huku eneo la matumizi mengineyo likiendelea kutengewa fedha nyingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha bajeti ya matumizi ya kawaida ya Wizara imeongezeka kutoka bilioni 523.8 mwaka 2011/2012, hadi bilioni 631.9 mwaka 2012/2013, sawa na ongezeko la asilimia 20; wakati fedha za matumizi mengineyo ya posho, mafuta, safari, samani na ukarimu ikiongezekaa kutoka bilioni 207 mwaka 2011/2012 hadi bilioni 386 mwaka 2012/2013 sawa na ongezeko la asilimia 86.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Bajeti ya matumizi ya kawaida imeshuka kutoka shilingi bilioni 631.9 kwa mwaka 2012/2013 hadi kufikia shilingi bilioni 617.08 huku bajeti ya matumizi mengineyo (posho, mafuta, safari, samani na ukarimu) ikipungua kidogo kutoka shilingi bilioni 386 kwa mwaka 2012/2013 hadi kufikia shilingi bilioni 384.6 kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, licha ya kupungua kidogo kwa matumizi mengineyo tofauti ya bilioni mbili, bajeti ya maendeleo ambayo ndio roho ya elimu yetu imeporomoka kutoka shilingi bilioni 92.6 kwa mwaka 2012/2013, hadi kufikia shilingi bilioni 72.6 kwa mwaka 2013/2014 tofauti ya shilingi bilioni 20. Lengo la kupunguza matumizi mengineyo na yasiyo ya lazima, ilikuwa ni kuongeza bajeti ya maendeleo ili kuleta maendeleo katika sekta ya elimu. Kwa maana hiyo, lengo hilo halijatimizwa.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya sekta ya elimu umekuwa si mzuri pia. Licha ya Serikali kudai kuwa haina fedha za kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya elimu, bado kumekuwa na usimamizi mbaya wa hata zile fedha kidogo zinazopangwa. Kwa mfano, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011, ilibaini kuwa fedha zilizotolewa kwa miradi ya MMEM na MMES hazikutumiwa na Halmashauri kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kuachana na matumizi ya kawaida yasiyo ya lazima katika bajeti ya 2013/2014 na badala yake fedha hizo zitumike kutatua changamoto muhimu kama urekebishaji wa maslahi ya Walimu kama vile nyumba, mishahara na posho ya mazingira magumu ya kazi na ukaguzi wa shule.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itasaidia kurudisha morali wa ufundishaji na kupunguza matatizo ya ufaulu nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwana CHADEMA inaitaka Serikali kuwa na tabia ya kupanga bajeti kwa kuainisha vipaumbele vichache vinavyotekerezka. Hii ni kwa

sababu Serikali haiwezi kutatua matatizo yote kwa wakati mmoja, hivyo ni muhimu Serikali ijenge utamaduni wa kuteua vipaumbele vichache katika bajeti kwa kila mwaka wa fedha ili kutatua changamoto za sekta ya elimu.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii lazima ieleze bayana mikakati ya Wizara kuboresha usimamizi na ufanisi wa fedha za umma hasa katika kuhakikisha fedha zinafika kwa walengwa kwa wakati, zinatumika kama zilivyopangwa na zinatumika ipasavyo kwa mantiki ya kuleta thamani iliyokusudiwa (*value for money*).

Mheshimiwa Spika, maslahi na stahili za Walimu nchini; tofauti na Kauli Mbiu ya Serikali hii ya CCM ya "Maisha Bora kwa Kila Mtanzania", sasa Serikali imeyafanya maisha ya Watanzania kuwa magumu zaidi kwa kutoboresha maslahi na mishahara ya Walimu. Aidha madai ya Walimu yamezidi kujilimbikiza jambo linalowafanya Walimu wazidi kuishi kwa tabu.

Mheshimiwa Spika, madai haya ni ya tangu 2007 na mwaka 2009, Serikali ilifanya uhakiki wa madai ya Walimu na kupata jumla ya shilingi bilioni 52 ambapo shilingi bilioni 32 ni madai ya mishahara na shilingi bilioni 20 ni madai yasiyo ya mishahara kama vile likizo, uhamisho, matibabu, gharama za masomo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi sana kulipa madai yasiyo ya mishahara. Madai ya mishahara yameendelea kulipwa kwa kasi ndogo sana. Kwa mfano, katika uhakiki wa mwaka 2009 katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, jumla ya Walimu 364 waliodai jumla ya shilingi milioni 417 ni Walimu 25 tu wamelipwa jumla ya shilingi milioni 40 hadi sasa. Mfano huu wa kasi ndogo ya kulipwa ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuwalipa Walimu haki yao kwani kwa kutowalipa kunaweza kuwa sababu kubwa ya kuperomoka kwa elimu kama tunavyoshuhudia sasa kutookana na Walimu kuvunjika

moyo kwanza kwa kulipwa mishahara midogo sana ukilinganisha na kada nyingine za utumishi wa umma, lakini pia licha ya kupunjwa, Walimu hawalipwi stahili zao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kuingia madarakani 2005, aliunda Tume kadhaa ikiwa ni pamoja na Tume ya Kuboresha Mishahara ya Watumishi wa Umma iliyoongozwa na Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza badala ya kuboresha mishahara ya watumishi wa umma, tarehe 1 Disemba 2009, Serikali kuitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliandaa waraka namba C/AC.44/45/01/84, wenye kichwa cha habari kisemacho "Utaratibu wa kuwabadilisha kazi *recategorization* kupandisha cheo Walimu wa shule za Serikali ambao wamejiendeleza kielimu".

Mheshimiwa Spika, waraka huo unaagiza kuwa Walimu ambao walishajiriwa na Serikali wakienda masomoni wanaporudi kutoka masomoni, wafanyiwe utaratibu wa kupandishwa vyeo kwa majina *recategorization*, lakini mishahara yao waliyofikia iondolewe na badala yake warudishwe nyuma hadi kwenye mishahara ya Walimu wanaoanza kazi. Kwa maana nyingine ni kwamba umri wa Mwalimu kukaa kazini unafutwa *deletion of seniority in service*.

Mheshimiwa Spika, kwa ufanuzi ni kwamba, Walimu wamegawanyika katika makundi au kada tatu zifuatazo:-

(i) Walimu; hawa ni Walimu wenye elimu ya kidato cha nne na mafunzo ya ualimu katika ngazi ya cheti na wanaajiriwa ili kufundisha katika shule za msingi. Mwalimu anayeajiriwa kwa mara ya kwanza katika kada hii *Pre-service*, huanza na mshahara wa ngazi ya *TGTSB* na hupanda mpaka ngazi ya mshahara wa *TGTS E* ambayo ndiyo ukomo (*Bar*) wake.

Hawezi kupanda tena kwenda cheo kingine cha

mshahara mpaka atakapofungua ukomo huo kwa kuongeza kiwango chake cha elimu kutoka ngazi ya kidato cha nne na mafunzo ya ualimu ya ngazi ya cheti kwenda kiwango cha elimu ya kidato cha sita na mafunzo ya ualimu ya ngazi ya Stashahada *Diploma* au Shahada *Degree* ya chuo kikuu. Ataendelea kuwa Mwalimu wa shule za msingi kwa kupewa majukumu yanayoendana na kiwango chake cha elimu.

(ii) Maafisa Elimu Wasaidizi; hawa ni Walimu wenyе elimu ya kidato cha sita na mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Stashahada *Diploma* na wanaajiriwa ili kufundisha katika shule za sekondari au katika vyuo vya ualimu vya ngazi ya cheti. Walimu hawa wanapoajiriwa kazini kwa mara ya kwanza *Pre-service*, huanza na mshahara wa ngazi ya *TGTS C* na hupanda vyeo vya mshahara mpaka ngazi ya *TGTS F* ambayo ndiyo ukomo *Bar* wake. Hawezi kupanda tena kwenda cheo kingine cha mshahara mpaka atakapofungua ukomo huo kwa kuongeza kiwango chake cha elimu kutoka kidato cha sita na mafunzo ya ualimu ya ngazi ya Stashahada yaani *Diploma* na kufikia kiwango cha elimu na mafunzo ya ualimu ya kiwango cha Shahada yaani *Degree* ya Chuo kikuu.

(iii) Maafisa Elimu; hawa ni Walimu wenyе elimu na mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Shahada yaani *Degree* ya chuo kikuu na wanaajiriwa ili kufundisha katika shule za sekondari na katika vyuo vya ualimu vya cheti na *Diploma*. Walimu hawa wanapoajiriwa kwa mara ya kwanza (*Pre-service*), huanza na cheo cha mshahara cha *TGTS D* na hupanda mpaka cheo cha mshahara cha *TGTS I* ambayo ndiyo ukomo (*Bar*) wake. Hawezi kupanda tena cheo cha mshahara mpaka atakapoongeza kiwango chake cha elimu kutoka Shahada yaani *Degree* kwenda Shahada au Stashahada ya uzamili yaani *Masters Degree/Post Graduate Diploma*.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa waraka unaolalamikiwa na Walimu ni kwamba:-

Mheshimiwa Spika, Mwalimu wa shule ya msingi

mwenye mshahara wa *TGTS E* (sh.720, 000/=), akijiendeleza kielimu na kupata *Diploma*, abadilishiwe muundo kwa kuitwa Afisa Elimu Msaidizi daraja la II, lakini mshahara wake ushushwe kutoka sh. 720,000/= mpaka sh. 370,000/= ambayo ni *TGTS C*, daraja ambalo Mwalimu wa *diploma* anayeajiriwa kwa mara ya kwanza huanzia na kama mwalimu huyo huyo alikuwa amejiendeleza kutoka cheti na kwenda *Degree* badala ya *Diploma* basi anapewa cheo cha jina kwa kuitwa Afisa Elimu daraja la II lakini mshahara wake unashushwa kutoka Tsh. 720,000/= mpaka Tsh. 532,000/= ambayo ni *TGTS D*, daraja ambalo huanzia Mwalimu mwenye *degree* anapoajiriwa kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, wakati huo endapo Mwalimu huyo aliyejiendeleza kielimu alikuwa na *Diploma* na alikuwa bado hajafikia ukomo wa mshahara kwa mujibu wa kiwango chake cha elimu, tukimwita ni Mwalimu X, anaposhushwa mshahara kwenda sh. 532,000/= au sh. 370,000/=, mwalimu Y ambaye hajajiendeleza kielimu anapandishwa mshahara wake kwenda sh. 930,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya Walimu nchini kupinga kwa nguvu zote Waraka huo, Serikali iliwasanganya Walimu kwamba, imefuta waraka huo kwa kuandika waraka mwingine wenye namba CAC.44/45/O1/A/121 wa tarehe 20 Disemba 2011 kwa kichwa cha habari kile kile na maudhui kandamizi kuliko hata waraka ule wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuhuishwa kwa waraka namba C/AC.44/45/01/84 kwa kutumia waraka namba CAC.44/45/O1/A/121, tazito linaloendelea sasa ni kwamba, Walimu wote waliojiendeleza kielimu, badala ya kupandishwa madaraja ya mishahara, sasa wanafanyiwa *recategorization* mpya na wanabakizwa kwenye madaraja yale yale na wanatakiwa kukaa kwenye madaraja hayo kwa muda wa miaka mingine mitatu zaidi ndipo wapande madaraja ya mshahara. Huu ni uonevu na ubaguzi mkubwa sana kwa walimu wanaojiendeleza.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kama kuna Walimu

wawili, Mwalimu X na Mwalimu Y, ambao walajiriwa pamoja na wanapanda madaraja ya mishahara pamoja na wana kiwango cha elimu kimoja tuseme *Diploma* na kama mwaka wao wa kupandishwa madaraja ni 2013, tofauti inayojitokeza kama ifuatavyo:-

Ikiwa Mwalimu X amejiendeleza kielimu na kupata *degree*, wakati Mwalimu Y hajajiendeleza kielimu wote wawili wako kwenye daraja la mshahara la *TGTS-E* lenye mshahara wa sh. 748,000/= kwa mwezi. Kwa mujibu wa Waraka namba CAC.44/45/O1/A/121, Mwalimu Y ambaye hajajiendelea kielimu anaruhusiwa kupanda kutoka *TGTS E* 748,000/= kwenda ngazi ya mshahara *TGTS F* yenye mshahara wa sh. 930,000/= kwa mwezi na mwalimu X ambaye amejiendeleza kielimu anabasilishiwa muundo kwa kuondoa jina la Afisa Elimu Msaidizi na kupewa jina la Afisa Elimu daraja la II lakini anazuilliwa kupanda daraja la mshahara, atabaki kwenye msahahara wa *TGTS-E* (Tsh. 748,000/=) kwa muda wa miaka mingine mitatu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa vyovoyote vile, mpango huu wa Serikali ya CCM ya kuwabana Walimu wasinufaikie na matunda ya elimu yao hata pale wanapojobana na kujisomesha katika mazingira magumu kwa kutowapandisha madaraja ya mishahara ni udhalimu na unyonyaji dhidi ya Walimu na sumu mbaya itakayoiua elimu ya Tanzania kwa kuwa huwezi kuzungumzia elimu bila kuwagusa Walimu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuandikwa kwa waraka huu kandamizi, utaratibu uliokuwa ukitumika kuwapandisha Walimu madaraja ya mishahara ulizingatia zaidi umri wa Mwalimu kazini, utendaji wa kazi uliokuwa bora pamoja na kiwango chake cha elimu. Aidha, Mwalimu alipojiendelea kielimu alistahili kupanda cheo kutoka kada moja kuingia kwenye kada nyingine bila kujali ni mwajiriwa wa muda mrefu au ni mwajiriwa wa hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukandamizaji huo, wapo Walimu ambao watastaafu wakiwa bado hawajapata manufaa ya elimu yao waliyojiendezea na wakati huo huo

Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya juu tayari imeshaingiza makato ya 8% kwenye mishahara yao kama marejesho ya mkopo wakati elimu hiyo haina tija kwa walimu kimapato.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inaitaka Serikali kuwatendea haki Walimu waliojiendeza kielimu kwa kuwapandisha madaraja ya mishahara haraka iwezekanavyo ili kuwapa motisha wa kufanya kazi kwa bidii na pia kuwavutia Walimu wengine kujiendeza kielimu ili kuinua ubora wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kabla ya tarehe 1 Disemba, 2009; utaratibu uliokuwa unatumika kuwapa Walimu miundombinu na kuwapandisha madaraja haukuwa ukilalamikiwa kama huu ulioletwa na waraka namba C/AC.44/45/01/84 na waraka namba CAC.44/45/O1/A/121.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kufuta mara moja nyaraka zote mbili zilizotajwa hapo juu na kurejea kwenye utaratibu wa kuwapandisha Walimu madaraja ya mishahara uliokuwepo kabla kwa kuwa nyaraka za sasa ni kandamizi na zinalenga kuwakatisha Walimu tamaa ya kujiendeza kielimu na hivyo kuwaongezea umaskini na kuendelea kudidimiza elimu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, namba 8 ya mwaka 2002, kifungu cha 6(4) kama ilivyorekebishwa na Sheria namba 18 ya 2007 na Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003, kifungu cha 6(h), mwenye mamlaka ya kuwapandisha Walimu madaraja ni Tume ya Utumishi wa Walimu *TSD*, lakini sasa hivi tangu nyaraka za kuwakandamiza Walimu zilipoanza kuandikwa na serikali, Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji ndiyo wanaowapandisha na kuwashusha Walimu madaraja ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni nani mwenye mamlaka ya kisheria ya kuwapandisha Walimu madaraja ya mishahara na ni sheria ipi inatumika kuwapandisha Walimu madaraja ya mishahara?

Mheshimiwa Spika, wapo pia Walimu wa shule za msingi waliojiendezea kielimu na wamekuwa wakihamishiwa shule za sekondari, bila kulipwa haki na maslahi yao ya uhamisho kwa madai kuwa Idara ya Shule za Msingi na Idara ya Shule za Sekondari zote ziko chini ya mwajiri mmoja ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri, Manispaa na Jiji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili; inawezekana vipi shule za msingi na shule za sekondari kuunganishwa pamoja wakati katika Wizara ya Elimu, Makao Makuu, idara hizi zimetengana na kila moja inajitegemea? Je, utunzaji wa kumbukumbu za Walimu hawa utakuwaje ikiwa taarifa za Walimu wa shule za msingi ziko Idara ya Msingi, Wizarani wakati walimu wenyewe wamehamishiwa sekondari?

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa nini Walimu wa shule za msingi wanapohamishwa kutoka kituo kilichokuwa cha shule ya msingi na kwenda kituo cha shule ya sekondari, hawalipiwi fedha za uhamisho?

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuwakandamiza Walimu wanaojiendezea kwa kutowapandisha madaraja ya mishahara, bado Serikali hii ya CCM imeendelea kuwabagua Walimu kwa kuwalipa mishahara tofauti Walimu wenye kiwango kimoja cha elimu. Kwa mfano, Mwalimu mwenye shahada ya kwanza akiajiriwa kufundisha shule ya Sekondari huitwa Afisa Elimu Daraja la II na huanza na ngazi ya mshahara *TGTS-D* (sh. 532,000/=), wakati Mwalimu mwenye kiwango hicho hicho cha elimu akiajiriwa katika chuo cha ualimu huitwa mkufunzi na huanza na mshahara wa *TGTS-E* (sh. 720,000/=).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

inayoongozwa na CHADEMA inaitaka pia Serikali kulieleza Bunge hili kama hii ni haki na inatumia vigezo gani kuwalipa Walimu wenyewe kiwango kimoja cha elimu mishahara tofauti.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali haipendi kukubali ushauri wetu, basi naomba wachukue ule wa Kamati ambao kimsingi unafanana sana na ule ambao tumeutoa.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Walimu na manufaa yake kwa Walimu; madhumuni ya kuanzishwa kwa Chama cha Walimu (CWT) yalikuwa ni kutetea maslahi ya Walimu. Hata hivyo, kwa siku za karibuni kumekuwa na malumbano ambayo yanapelekea baadhi ya Walimu kutaka kujitoa.

Mheshimiwa Spika, Walimu lazima wafahamu kuwa umoja ni nguvu na waelewe kuwa hakuna watumishi wengi hapa nchini zaidi yao. CHADEMA inaanini kuwa penye wengi hapakosi matatizo, hivyo ni vizuri CWT wakae pamoja na kuangalia matatizo yao ya ndani ili waweze kutatua matatizo lukuki yanayowakabili Walimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vitabu vya elimu na mchango wake katika kukuza au kupunguza ubora wa elimu; vitabu ni nyenzo muhimu sana katika utoaji wa elimu. Vitabu vya kiada na ziada vinapaswa kuwa na ubora unaokubalika ili elimu itakayopatikana katika vitabu hivyo iweze kuwa bora pia. Kwa mantiki hiyo, vitabu vina nafasi kubwa sana katika kuboresha elimu, lakini pia vitabu viliyoandikwa kiholela bila kuzingatia viwango na mitaala husika vina nafasi kubwa pia ya kuperomosha ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa vitabu katika kuboresha elimu, Serikali kuititia waraka wake namba mbili wa mwaka 1998, iliunda Kamati ya kuidhinisha vitabu na vifaa vya elimu (*EMAC*) ili kutoa ithibati baada ya kujiridhisha kuwa machapisho ya vitabu yamekidhi viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kuidhinisha kitabu, unaanza kwa sekretarieti kuwapa watathimini kuititia

Miswada ya vitabu inayoletwa na mchapishaji. Kwa bahati mbaya sana watathimini hawa huwa hawapatikani kwa njia ya ushindani ulio wazi, jambo linaloashiria rushwa na ujisadi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hali ya kutokuwa na uwazi katika kuwapa watathimini Miswada ya vitabu halina afya hata kidogo katika kupata machapisho yenyewe ubora. Ikumbukwe kuwa mapendekezo ya watathimini ndiyo huwasilishwa katika kikao cha *EMAC* kwa ajili ya kuitishwa au kukataliwa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa Mtathimini anayepitia Muswada wa kitabu kwa njia isiyo ya ushindani wa wazi inatoa mwanya wa uteuzi wa kirafiki usiozingatia ujuzi wa somo, ambapo hatima yake ni kuwa na vitabu vinavyodanganya wanafunzi. Mfano mzuri ni kitabu cha Uraia darasa la saba kilichochapwa na kampuni ya *Educational Books Publishers* ambacho katika ukurasa wa 145 kinadanganya watoto kuhusu uwepo wa shirika la *GATT* ambalo limekufa na kuzikwa miaka kumi na nane iliopita.

Mheshimiwa Spika, aidha, kitabu cha *40 Big Lies in Civics for Tanzania schools* kilichoandikwa na mwandishi nguli na mtafiti Huruma K. Joseph kinafafanua kwa kirefu makosa mbalimbali ambayo baadhi yake yamebarikiwa na *EMAC*.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni hatua gani zimechukuliwa kwa uzembe unaofanywa na watathimini wa Miswada ya vitabu na ubabaishaji wa wajumbe wa *EMAC* katika utungaji wa vitabu?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wachapishaji kuwa Sekretarieti ya *EMAC* imekuwa ikiikalia Miswada ya vitabu isiyowekewa asali na kugoma kuiwasilisha katika vikao vya Kamati licha ya kukidhi alama zinazotakiwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaweza kuthibitisha Miswada ambayo imekaa kwenye ngazi ya sekretarieti takribani miaka mitatu sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaweza kuthibitisha pasipo shaka Muswada uliokataliwa *reject* katika ngazi ya sekretarieti ingawa alama zake zilitosha kupata ithibati yenye masharti *conditional approval*. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ichunguze na kuchukua hatua madhubuti kwa Maafisa wanaoendekeza ubinafsi huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ambayo inapaswa kukaa vikao vinne kwa mwaka, imekuwa wakati mwingine ikikaa kikao kimoja kwa mwaka. Hii imesababisha kuwepo kwa wachapishaji ambao wanaamua kuingiza vitabu sokoni bila kuwa na ithibati ambavyo baadhi vimekuwa na makosa yanayotisha.

Mheshimiwa Spika, ushahidi juu ya hili ni kitabu cha uraia kidato cha pili kilichotolewa na kampuni ya Nyambari Nyangwine kinachoainisha Wenyeviti wa Vijiji kuwa eti theluthi yao ni wajumbe katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya, *Civics for secondary schools book Two page 41* na kile cha historia darasa la sita cha *Adamson Educational Publishers*, kinachoonesha makao makuu ya Tanzania kwa sasa yapo Nairobi, Historia darasa la saba ukurasa wa 84.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa vitabu hivi vyta kiada visivyo na ithibati ya *EMAC* ni dhahiri vinamweka katika hali mbaya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundu kutokana na kauli yake ndani ya Bunge lako Tukufu, kuwa vitabu vyote vinavyotumika katika shule za msingi, sekondari na vyuvo vya ualimu vinaithibati ya *EMAC*. Kauli hii ya Waziri aliitoa pale alipokuwa akijibu hoja ya Mheshimiwa James Mbaitia juu ya udhaifu katika mfumo wa elimu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataki kujua kama huo ndio bado msimamo wa Waziri ili Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iweze kuwasilisha kama ushahidi vitabu vya kiada zaidi ya thelathini (30) vya Kampuni ya *Adamson Educational Publishers*, ambavyo vimekuwa vikitumika mashulenii bila kuwa na ithibati.

Mheshimiwa Spika, moja ya maajabu ya vitabu hivi

vya Adamson ni kupotosha historia kwa kumtaja Mohammed Shamnte kuwa ndiye aliyebla kiongozi wa *ASP* na si Sheikh Abeid Amani Karume (Historia darasa la sita, ukurasa wa 28) na kwamba eti utawala wa kijerumani Tanganyika ulianza wakati wa vita vya majimaji (Historia darasa la sita, ukurasa wa 28). Kambi Rasmi inataka kujuua kama Mheshimiwa Waziri anabariki uozo huu au anatangaza kupiga marufuku matumizi ya vitabu hivi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa ili kufuta mizaha hii katika elimu mambo yafuatayo yafanyike:-

(a) Serikali ipanue idadi ya wafanyakazi katika sekretarieti angalau kila somo liwe na mjumbe mmoja katika sekretarieti;

(b) Vikao vya *EMAC* vikae kama inavyotakiwa, yaani mara nne kwa mwaka;

(c) Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa wajumbe wa sekretarieti na Kamati pale inapoonekana kuna ukiukaji wa maadili au uzembe wa makusudi unaopelekea kuidhinisha vitabu vyenye makosa yasiyovumilika;

(d) Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ambalo hupitia na kuidhinisha miswada unayoondikwa kwa lugha ya kiswahili kabla ya kupelekwa sekretarieti, ishindanishwe na Taasisi zingine za Kiswahili kama vile Taasisi ya Uchunguzi ya Kiswahili (TUKI) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA). Hii itasukuma kufanya kazi kwa ufanisi kuliko sasa ambapo hupitisha maneno ya Kiswahili yanayolalamikiwa na wadau;

(e) Inayowasilishwa kwake. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ushindani wa wazi katika kuwapata watathimini wa *EMAC*; na

(f) Aidha, muda wa kujadili Miswada ya vitabu pamoja na mapendekezo ya watathimini ni kidogo sana, jambo ambalo linazidi kudhoofisha ubora wa vitabu. Kikao

cha *EMAC* chenye wajumbe kumi na wanne huupitia Muswada wenyе kurasa hadi 200 kwa dakika zisizozidi kumi. Baada ya kuupitia Muswada hujadiliana kwa dakika 10 - 20.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo muhimu ya kuboresha Sekta ya Elimu nchini; ili kuboresha sekta ya elimu nchini, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

(i) Serikali ianzishe Bodi ya Wataalam wa Ualimu (*Tanzania Teachers' Professional Board – TTPB*) kama ziliyo taaluma nyingine kama uhasibu (*NBAA*), uhandisi, utabibu na kadhalika. Ili bodi hii iwe inaratibu na kupanga vigezo vya mtu kuitwa Mwalimu katika ngazi ya ujuzi wake.

Bodi hii pia itahusika na kusimamia nidhamu na maadili ya taaluma ya ualimu nchini na pia itahusika na ukaguzi wa shule ili kuona kama Walimu wanazingatia mwongozo wa taaluma yao. Chombo hiki kiwe na mamlaka kisheria kuwasajili walimu na kuwapa leseni za kufundisha.

(ii) Serikali iongeze kiwango cha ufaulu kwa wanaotaka kuijunga na vyuo vya ualimu baada ya kuhitimu kidato cha nne, kutoka daraja la nne hadi daraja la tatu kwa ngazi ya cheti. Aidha, wanaotaka kuijunga na vyuo vya ualimu baada ya kuhitimu kidato cha sita, wawe na ufaulu wa daraja la pili badala ya daraja la tatu kama ilivyo sasa. Hii itasaidia kupata Walimu wenyе uwezo mkubwa kitaaluma na hivyo kuinua ubora wa elimu yetu.

(iii) Serikali iweke usawa wa mishahara kwa wahitimu wenyе viwango sawa vya elimu, kwa mfano, cheti, stashahada na shahada kati ya Walimu na watumishi wa kada nyingine. Hii itasaidia vijana waone ualimu kama fani nyingine.

(iv) Serikali iweke utaratibu wa kuwapa motisha Walimu kwa kuruhusu watoto wa Walimu wasiozidi watatu kusoma bure katika shule za sekondari na wapewe mikopo bila masharti ya kusoma katika vyuo vya elimu ya juu ikiwa

watakuwa wamefaulu na kuwa na sifa ya kujunga na elimu ya sekondari na vyuo hivyo ili kuwaondolea Walimu mizigo mikubwa ya kulipa ada za sekondari na vyuo pamoja na kodi za nyumba kwa kutumia mishahara midogo wanayolipwa.

(v) Serikali ianzishe chombo cha Udhibiti wa Elimu na Mafunzo ya Ufundzi (*Tanzania Education and Training Regulatory Authority – TETRA*) kitakachoweka viwango vya ubora wa elimu kwa mujibu wa mitaala iliyopitishwa na Serikali, kudhibiti utungaji, usahihishaji na upangaji wa matokeo ya mitihani, kudhibiti gharama za elimu ada na michango mingine baina ya shule na taasisi nyingine za elimu za umma na binafsi ili kuwa na mfumo mmoja wa elimu unaoeleweka kuliko sasa ambapo kuna tofauti kubwa za kimfumo baina ya shule na taasisi za elimu binafsi na zile za umma.

Mheshimiwa Spika, hakuna nchi yoyote iliyօendelea hapa duniani bila kuwekeza kwenye elimu. Malaysia inajivunia maendeleo yake kwa kuwa iliwekeza kwa vitendo katika elimu na ndio maana nchi nyingi ikiwemo Tanzania imekwenda kujifunza kwao mambo mbalimbali. Wakati umefika sasa wa Serikali ya CCM kuwekeza kimkakati katika elimu na si kwa maneno.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika sana kuona Sekta ya Elimu iko katika sekta sita za vipaumbele kupitia *Big Results Now*, lakini kinachosikitisha sioni bajeti ya mwaka huu ikijibu changamoto za elimu hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa asilimia zaidi ya 50 inakwenda kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ieewe maana ya msemo huu; *if education is expensive, try ignorance*, yaani kama elimu ni ghali, jaribu ujinga. Imefika wakati sasa wote kwa pamoja kama Taifa tuseme Elimu Kwanza mengine baadaye na hivyo nguvu zetu zote zielekezwe kwenye elimu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, kuperomoka kwa elimu hapa nchini, pamoja na sababu nyingi zilizotajwa

na Tume mbalimbali za uchunguzi, kuna tatizo pia la kiuongozi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Ni dhahiri vile vile kwamba, hatuwezi kupiga hatua mbele kwa kuendelea na viongozi wale wale ambao matatizo yalitokea mikononi mwao. *Problems can not be solved by the same level of thinking which created them - Malcom X.*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno mengine, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundii Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Naibu wake Mheshimiwa Philipo Mulugo, watumie busara zao na kujipima kama kweli pamoja na majanga makubwa yaliyotokea katika elimu ambayo madhara yake yatadumu kwa vizazi vingi, wanastahili kuendelea kuongoza Wizara hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wahenga walisema ada ya mja hunena, lakini Mwungwana ni kitendo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado ina imani kwamba, Waziri wa Elimu na Naibu wake wataonesha uungwana na uzalendo zaidi kwa nchi yetu kama watawajibika kutoptana na hitilafu zilitotokea katika sekta ya elimu hapa nchini, hata kama makosa na hitilafu hizo hawakuzifanya wao wenye moja kwa moja. Lakini kwa ajili ya kuonesha uwajibikaji wa kiuongozi na kuonesha kwamba wanajali misingi ya utawala bora na pia kulinda heshima yao mbele ya jamii, hawana budi kuwajibika kwa dhamana waliyopewa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo si fedheha hata kidogo bali ni ushujaa na ukomavu katika uongozi. Rais Mstaafu Alli Hassani Mwinyi alifanya hivyo alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa makosa yaliyofanywa na watu wengine, lakini aliwajibika na kulinda heshima yake na hatimaye alikuja kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wadau wote wa Elimu wakiwajibika kikamilifu kwa majukumu waliyopewa, kutakuwa na mabadiliko mazuri makubwa sana katika Mfumo wa Elimu yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, na Watanzania wote wanaopenda kuona Taifa letu likisonga mbele kwa kasi

ya kumwondoa adui ujinga na kuona Serikali inaboresha mfumo wa elimu kwa kuwekeza kwa vitendo katika elimu. Hotuba yangu hii inapatikana katika Tovuti ya CHADEMA [www.chadema.or.tz](http://www.chadema.or.tz).

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Nashukuru. Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo mawili, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, saa saba hii watakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Msekwa, kwa hiyo, wanakaribishwa.

Halafu pia kuna tangazo la Mheshimiwa Jenista Mhagama Katibu wa *Caucus* ya CCM, kwamba Wabunge wote wa CCM kwa leo saa saba baada ya kusitisha Bunge, kutakuwa na kikao cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM, katika ukumbi wa Pius Msekwa. Sasa sijui Pius Msekwa ipi, mtapanga wenyewe huko.

Waheshimiwa tunaweza kuwa na wachangiaji kama watano asubuhi hii, tunaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu, Mheshimiwa Margaret Sitta ambaye, atafuatiwa na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina na Mheshimiwa Naomi Kaihula. Baada ya hapo, tutaangalia wengine kama watafikiwa. Mheshimiwa Margaret Sitta!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa heshima ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika hoja iliyowasilishwa siku ya leo. Pili, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kusimama ndani ya Bunge hili siku ya leo na wakati huo huo nawashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mimi ni Mwenyekiti, naunga mkono taarifa yetu na nampongeza sana aliyewasilisha kwa niaba yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia *Hansards* za mwaka jana, nikaona jinsi ambavyo nilichangia, nimeona ni vizuri nirudie baadhi ya mambo niliyozungumzia mwaka jana kutokana na umuhimu wake na kwa uzuri wake yako mengine ambayo pia yamezungumziwa au yamo ndani ya taarifa yetu ya Kamati ya Huduma za Jamii.

Mheshimiwa Spika, la kwanza kabisa, naiomba Wizara kupitia Waziri wake, atakapokuwa anahitimisha hoja yake kesho, atueleze hapa ndani ya Bunge hili, hivi tunavyozungumza kwamba, mfumo wa kuhudumia Walimu haufai, ndiyo unaosababisha Walimu wengi kushindwa kupanda Madaraja kwa wakati, lakini wakati huo huo kuwa na *arrears* nyingi, kwa mfano, Walimu wa Tabora wanaidai Serikali kwa upande wa *arrears* zaidi ya bilioni 1.9. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Walimu kwa mfano wa Dodoma, wanadai kupandishwa madaraja, Walimu zaidi ya 700 kwa Mkoa wa Dodoma. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie kesho atakapokuwa anahitmisha, hivi Serikali inaridhika na mfumo wa kuhudumia Walimu uliopo sasa? Maana yake hatukuona chochote ambacho kimezungumzwa katika hotuba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaendelea, nijibu kwa kifupi hotuba ya Upinzani, si kweli kwamba Serikali haijafanya chochote kwa upande wa elimu. Tutende haki, kitu kikubwa hapa ilikuwa ni uboreshaji, lakini ukisema kwamba, Serikali ya Mapinduzi haikufanya chochote si kweli.

Mheshimiwa Spika, jambo la muhimu nilitengemea sana katika hotuba ya Upinzani, ingejikita zaidi jinsi ya kutoa mapendekezo ya kuboresha, lakini kugandamiza gandamiza hapana, kwani Serikali imechukua hatua nyingi sana katika kurekebisha, kitu kikubwa ni kuongeza elimu, *access*, kitu kikubwa mngetoa *suggestions* jinsi ya kuboresha, ingekuwa ni vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, la pili, baada ya kumtaka Waziri atueleze kama Serikali inaridhika na mfumo wa kuhudumia Walimu.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningemwomba Mheshimiwa Waziri kwa kesho katika kuhitimisha hotuba yake, atuambie, kama anaridhika na mfumo wa Idara ya Ukaguzi inavyofanya kazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia takwimu katika kitabu cha Wizara yaani *BEST*, katika mwaka wa fedha 2011/2012, walikuwa wamepanga kukagua Vyuo vya Walimu 105, na Vyuo vya Walimu ndijo eneo la kutilia mkazo sana katika kuboresha elimu, lakini katika Vyuo 105 ambavyo vilipangwa kukaguliwa mwaka huu wa fedha uliopita, ni Vyuo 30 tu ambavyo vilikaguliwa, ambayo ni sawasawa na asilimia 28.6 tu.

Mheshimiwa Spika, wakati huo walikuwa wamepanga kukagua Vyuo vya Ufundı 216, lakini wakaweza kukagua Vyuo 39 tu ambayo ni sawasawa na asilimia 18. Hii inaonesha wazi kabisa Idara ya Ukaguzi haifanyi kazi ipasavyo kutokana na uhaba wa fedha, lakini pia, haina meno, sidhani kama Halmashauri zinasikiliza hata taarifa au zinasoma taarifa za ukaguzi. Kwa sababu wao ndijo wanaowasaidia mafuta na wao ndijo wanaowasaidia mahali pa kukaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakapokuwa anahitimisha, tunaomba atuambie hapa, hivi kweli Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa Idara ya Ukaguzi kujitegemea kwa kuwa Wakala, ipewe meno zaidi ifanye kazi vizuri zaidi. Naomba sana hili suala kesho lizungumziwe. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni suala la Wataalam wetu katika Taasisi za Elimu za Juu, tulipita *MUHAS* na sehemu nyingi tu, tukakuta kwamba Wataalam wanastaifu baada ya miaka 60, lakini baada ya hapo wanatoka katika Vyuo au Taasisi za Serikali, wanakwenda kwenye Taasisi binafsi na kuziacha Taasisi za Serikali hazina Wataalam.

Sasa tulikuwa tunaiomba Serikali na nitaomba na hili kesho Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha ituambie, je, haoni umuhimu wa kutoa madaraka yallyo katika Sekretarieti kuajiri wataalam na kuwapa madaraka Vyuo vyenyewe viajiri, lakini pia, haioni busara ya kuwaruhusu kupata mikataba ya miaka miwili miwili mpaka uwezo wao kufanya kazi ushindikane, afya zao jinsi zitakavyowaruhusu ili Taasisi zetu za Serikali zisikose Wataalam.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni mahitaji makubwa ya mikopo kwa ajili ya vijana wetu wa Chuo Kikuu, ni wazi kwamba, hata Serikali ifanyeje kwa kutumia fedha zake kama inavyotenga kwa kupitia Wizara ya Elimu, haiwezekani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara itakapokuwa inahitimisha ituambie, ina mkakati gani wa kutekeleza Azimio ambalo lilipita hapa Bungeni, hoja binafsi ilipita Bungeni na ikakubaliwa ya kuanzisha mfuko maalum ambaao utakuwa na vyanzo mbalimbali kwa kuhuisha Sheria mbili, iliyoanzisha TEA, yaani Mamlaka ya Elimu Tanzania na iliyoanzisha Bodi ya Mikopo. Ili vijana wengi zaidi na hasa wanaotoka kwenye familia duni, waweze kupata mikopo. Tunaomba kujuu mkakati uliopo kutekeleza hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia nafikiria katika hilo hilo la Wizara ya Elimu pengine ingefikiria pia kwamba, katika upatikanaji wa fedha katika Mfuko huo, lingine liangaliwe kwa upande wa kupata Levy, kuna *Skills Development Levy*, ambayo inatolewa na waajiri wenye wafanyakazi zaidi, nadhani ya saba, ambayo inakwenda Serikalini asilimia sita.

Mheshimiwa Spika, sasa najua asilimia mbili inakwenda VETA ambapo hapo hapo ningeomba kwamba, badala ya kwenda asilimia mbili VETA, iende asilimia tatu ili kusaidia vijana wetu wa ufundi waendelee zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini napendekeza kwamba, katika Mfuko huo muangalie uwezekano wa asilimia tatu

nyingine hii, badala ya kwenda Serikalini moja kwa moja, iende kwenye Mfuko huo wa Vijana wa Chuo Kikuu ili waweze kupata mikopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumzia ni suala la uhaba wa maji na vyoo katika Shule zetu za Msingi na Sekondari hasa za Kata hizi tulizozianzisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Waziri, tungeomba sasa, Kamishna, kabla hajaandikisha shule, la kwanza kabisa awaambie waanze kujenga vyoo na wahakikishe kwamba kuna visima, kwa sababu sasa hivi wengi, hata pengine na sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge hapa, tunakwenda kuomba, niandikishie shule yangu, unakuja kukuta ina madarasa mawili, nyumba ya Mwalimu, lakini kwa upande wa wanafunzi, hakuna vyoo, hakuna maji. Tunaomba iwekwe kama masharti, kwamba kabla hujaanza kujenga shule, anza vyoo, weka kisima, hiyo itakuwa imesaidia.

Mheshimiwa Spika, niliona niyataje kwanza hapo haraka haraka halafu niendelee kufafanua zaidi, bado narudi kwenye upande wa chombo kimoja, niliona niyamalize hayo hata kengele ikilia, niwe nimeshayasema.

Mheshimiwa Spika, Walimu wote wa Tanzania, wako karibu 236,544, kwa taarifa nilizopewa. Kutokana na wingi wa Walimu, si rahisi kuwashudumia ukichanganya na watumishi wengine, ndio maana Serikali hii hii ya Tanzania ilianzisha chombo cha Tanzania *Teachers Service Commission*.

Mheshimiwa Spika, tunaomba, *Teachers Service Commission* irudishwe, najua wasiwasi ni Halmashauri, kwamba kurudisha madaraka Mikoani au *D by D* wanayosema, kurudisha madaraka kwa wananchi, hiyo ndio wasiwasi wao, kwamba hivi mamlaka ya wananchi...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Said Mtanda atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu. Pia nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema Waislam wanaamini katika elimu kuititia Aya ile inayosema *Iqra Bismirabbika* mpaka mwisho, lakini pia hata Wakristo wanaamini katika elimu, kwa sababu wanasesma; mshikeni au mkamateni sana huyo elimu, msimuache aende zake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Chama cha Mapinduzi kinaamini sana ndiyo maana kimesema katika Katiba yake nitajielimisha kwa kadri ya uwezo wangu na nitatumia elimu yangu kwa manufaa ya wote. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, nadhani iko haja ya kuwekeza kwa kiasi kikubwa sana katika sekta hii ya elimu. Hatujafanya hivyo kwa sababu mwaka jana tulipitisha Bajeti hapa, tulipitisha shilingi bilioni 92 kwa ajili ya fedha za maendeleo, lakini hadi leo tunazungumzia Bajeti mpya, ni asilimia 48 tu ya fedha hizo ndio zimepatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, naomba kutoa msisitizo zaidi kwamba, bajeti hii haitoshi, lakini kama hiyo haitoshi, mwaka huu fedha za maendeleo zimeshuka kutoka bilioni 92 hadi bilioni 72. Sasa hatuwezi kwenda mbele na tutatumia fursa hii kumsema sana Dkt. Kawambwa, lakini Kawambwa hawezи kufanya maajabu kama hatapatiwa fungu la kutosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mwalimu wangu, Susan pale

alikuwa akitueleza hapa, anasema angependa Dkt. Kawambwa leo awajibike, lakini nasema, wako watu wengine ambao tunastahili kwanza kuwajibisha kabla hata hatujafika kumzungumzia Dkt. Kawambwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2011/2012, kutokana na ubovu wa haya matokeo, wapo waliohusika na kuna bwana mmoja Mkuu wa Idara ya Komputa pale Baraza la Mitihani anaitwa Joseph Mbewe na katika Tume ya uchunguzi iliyoundwa mwaka 2012 na Waziri Kawambwa, ametajwa, awajibishwe kwa sababu ndiyo waliohusika, hawa nao mbona hawatajwi. Tunaangalia tulikoangukia, badala ya kuangalia tulikojikwaa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe mfano mmoja dhahiri kuonesha kwamba, leo hii naomba Waziri akimaliza hapa na kesho tutakapoingia kwenye majumuisho, Bodil inayosimamia Baraza la Mitihani lazima ivunjwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna Kamati inayoitwa Kamati ya Kutunuku madaraja haya A, B, C, D, nayo ivunjwe kabla ya Bunge hili kwisha hapa. Nasema hivi kwa sababu moja, zimeshindwa kulisimamia Baraza la Mitihani, kwa vigezo vifuatavyo:-

Kwanza, Baraza la Mitihani kuna kitu kinachoitwa *continuous assessment* maana hata mimi ni Mwalimu, inatakiwa 50% ya *continuous assessment* ijumlishwe katika alama za mwisho za mtahiniwa, lakini hili halifanyiki. Hilo la kwanza.

La pili, kuna kitu kinachoitwa *cut off point*, yaani kupanga madaraja kwamba wewe upate A, au B au C. Sasa kwa miaka mingi sana kuna udhaifu mkubwa katika hili na kuna mkakati maalum hapa. Sasa niwatajie mfano mdogo sana wa masomo mawili na naomba mniwie radhi kwani sina nia ya kuleta ubaguzi wa kidini na si muumini wa hayo.

Mheshimiwa Spika, nita-sight mfano wa mawili tu, moja linaitwa *Bible Knowledge* na lingine linaitwa Elimu ya

Dini ya Kiislamu. Watahiniwa wa somo la *Bible Knowledge* wakipata alama kuanzia 80 kwao inahesabiwa ni A, lakini watahiniwa wa somo la elimu ya dini ya Kiislam wanahesabiwa hiyo 80 kuwa ni daraja B na haya siyasemi mimi, *report* ya taarifa ya uchunguzi wa Baraza la Mitihani ya mwaka 2012, iko wazi na hii aliunda Waziri na hapa atakuja atasema.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hilo sasa ilisababisha mwaka 2011 vijana wengi waliosoma somo la Elimu ya Kiislamu waandamane pale Kidongo Chekundu na walipigwa mabomu, waliambiwa wanahatarisha usalama wa nchi, lakini Waziri kwa uungwana wake na kwa uwezo wake aliunda Tume hii na ikaja na *report* ifuatayo:-

Elimu ya Dini ya Kiislamu, matokeo ya mwanzo A ilikuwa ni sifuri, lakini baada ya hii *report* kupitia na kuhakiki upya ikaonekana matokeo mapya A zipo mbili, B ilikuwa ni sifuri lakini walivyohakiki kupitia hii Kamati B zikawa nne, C ilikuwa ni sifuri, lakini zikaongezeka kuwa 79, D zilikuwa saba, zikaongezeka kuwa 282, *failure* walikuwa 731, lakini baada ya matokeo ya pili wakapatikana 335. Hao waliohusika wakiwemo hawa watu wa Kamati ya kutunuku madaraja haya, ndiyo wa kwanza kuwajibika leo hii hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema kwamba, lazima Bodi inayosimamia Baraza la Mitihani ivunjwe na Kamati inayotunuku nayo ivunjwe kwa sababu hawa ndiyo tatizo la kwanza na hawa ndiyo watendaji waliopo pale. Tunamlamu Kawambwa kwa kwenda kutangaza matokeo ambayo hawa ndiyo walivoyachakachua. Nataka niseme kwamba Kawambwa namfahamu, ni mtu mwadilifu, ni mtu mpole, lakini upole wake haina maana kwamba hana uwezo wa kazi hii. Hilo la kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, la pili, nirudi katika Mkoa. Hiki kitabu mlichotupa, kitabu hiki ukifungua katika ukurasa wa 119 tumesema tutakarabati shule, sasa mgawanyo huu haueleweki na haya ndiyo tunayoyasema humu. Ukiangalia Mkoa wa Kilimanjaro shule zilizotajwa ni 69, lakini Mkoa wa

Lindi 31, Mkoa wa Dodoma 42, Mkoa wa Mtwara 41. Jedwali hili lifutwe liletwe jedwali lingine lenye mgawanyo sawa wa ukarabati wa shule katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nasema sera mpya ya elimu...  
(*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Na Pwani!

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Kibaha kwa Hamoud, hakuna kitu! Utanisamehe sana rafiki yangu Selasini, katika hili jedwali wewe una shule 22, Jimbo moja hilo.

Mheshimiwa Spika, nasema jedwali hili lifutwe kwa manufaa ya nchi na iletwe *proposal* mpya na mgawanyo unaozingatia haki na maslahi ya watu wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine ni sera mpya, lazima iseme sasa kwamba, yapo maeneo *disadvantaged*, lazima yapewe kipaumbele na lazima Serikali ije na mkakati wa kufanya empowerment ya maeneo hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano, Wilaya yote ya Lindi ina Shule za Sekondari 27, Walimu wa somo la Sayansi wako 28, maana yake *ratio* ni kwamba, kila shule moja ina Mwalimu mmoja isipokuwa shule moja ndio itapata Walimu wawili. Halafu mnakuja mnatangaza hapa kwamba, Lindi ndiyo wanaongoza kwa kufeli, tunaongoza kwa kufeli au ninyi ndiyo mnatuletea mazingira haya?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, muda umekwisha!

**MHE. SAIDI MOHAMED MTANDA:** Mheshimiwa Spika, niongezee dakika chache.

**SPIKA:** Haiwezekani! Mheshimiwa Ntukamazina atafuatiwa na Mheshimiwa Naomi Kaihula na Mheshimiwa Abia Nyabakari.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze Waziri pamoja na timu yake kwa kutuletea rasimu nzuri ya sera pamoja na mikakati mizuri ya utekelezaji. Lakini kama ambavyo nimekuwa nikisema sisi Watanzania ni hodari sana wa kuandaa sera, mikakati na mipango mizuri, lakini utekelezaji unatushinda. Utekelezaji unatushinda kwa sababu hatuna uzalendo, hatuna uwajibikaji na pia hatuna uadilifu, hatuna *seriousness* wala *commitment, business as usual*.

Mheshimiwa Spika, lakini inategemea kwamba, katika mbinu ambayo tumeichukua sasa hivi ya *big results now* ya kufuatilia na kusimamia utekelezaji nadhani ndiyo tutaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI lazima tubadilike na tutekeleze sera hii na *change mind set* ya wafanyakazi yaani wafanyakazi wabadilike.

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba sasa nichangie kidogo katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, tunakubaliana kwamba elimu ni kipaumbele cha kwanza katika vile vipaumbele sita ambavyo tumejiwekea kufikia nchi ya ahadi yaani nchi ya uchumi wa kati na kwa sababu hiyo ni lazima tuhakikishe kwamba elimu inapewa bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, Sera yenye inakiri kwamba, katika nchi yenye uchumi wa kati, jamii inakuwa ni jamii ambayo imeelimika sana na jamii ambayo inapenda

kuijendeleza. Sasa itapenda kuijendeleza namna gani kama kwa mfano, hatuwezi kuwa na maktaba ambayo itasaidia wananchi kuijendeleza.

Mheshimiwa Spika, sasa tunahitaji mapinduzi yaani *we need a revolution, a revolution* kutoka kwenye *business as usual* kwenda kwenye uwajibikaji wa hali ya juu. Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, tunaomba tupate *Brigedia Generals, Brigedia Generals* wa kusukuma maendeleo yaani Mawaziri wawe *Brigedia Generals*.

Mheshimiwa Spika, sasa nawapa cheo hicho kwa sababu nilishampa Waziri Mkuu Cheo cha *Economic Major General* sasa kwa kuwa Mawaziri ni wadogo wanakuwa *Brigedia Generals*, akina Mheshimiwa Mwanri na Mheshimiwa Majaaliwa watakuwa Makanali. Lazima tubadilike na tulete mabadiliko makubwa sana katika kuhakikisha kwamba tunaendeleza elimu.

Mheshimiwa Spika, elimu imeporomoka na viashiria vipo vingi, ufaulu mdogo na wananchi wanaojua kusoma na kuandika sasa hivi ni chini ya 50%, lakini kwenye miaka ya 80 tulikuwa tumefikia 95%, lakini sasa hivi ni kama 45%. Baadhi ya watoto wanaomaliza shule ya msingi hawajui kusoma na kuandika, Walimu wenyewe ni vihiyo na kwa hiyo tunakuta kwamba elimu imeshuka. Bajeti ya Elimu ni ndogo sana na sisi Wabunge lazima tuisaidie Wizara hii ili kuhakikisha kwamba tunapata bajeti nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika shule zetu za Ngara na kwingine hazina Maktaba, hazina vitabu, hazina maabara, hazina nyumba za Walimu, hazina *hostel*, maslahi ya Walimu ni duni, madarasa hayatoshelezi wala hakuna ukaguzi wa shule. Hayo yote yanaashiria kwamba, elimu yetu imeshuka na vyuo vikuu vyenyewe ni hoi sana. Vyuo vikuu vinapewa fedha kidogo za *OC* yaani matumizi ya kawaida, wanapewa fedha kidogo cha maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwenyekiti wa *MUHAS* yaani Chuo Kikuu cha Muhimbili, nimemwagiza *Vice*

*Chancellor wangu ampatie Bursar yaani bwana fedha wa MUHAS, ampatie posho ya viatu, kwa sababu zile corridor za Hazina zinamaliza viatu kwa ufuatiliaji kwa wanaofuatilia disbursement, kwa hiyo nimewagiza Vice Chancellor ampatie posho ya viatu.*

Mheshimiwa Spika, lazima tukubaliane kwamba bila Maktaba hatuwezi kuwafanya wananchi wajendeleze, sasa Maktaba ya Taifa ina nia nzuri ya kusambaza Maktaba kwenye Wilaya na kwenye Vijiji, lakini wanapatiwa fedha kidogo sana. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Elimu iipatie Maktaba fedha za kutosha ili iweze kusambaza Maktaba katika Wilaya na katika sehemu mbalimbali za vijiji.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama Mwalimu *by professional* bila kuzungumzia matokeo ya mwaka jana yaani matokeo ya mitihani ya kidato cha nne. Matokeo ya mwaka jana ni janga la Kitaifa. Mimi kama Mwalimu *by professional* nasema kwamba sikubaliani na kufutwa kwa mitihani, kama tunafuta mitihani basi watoto warudie mitihani yaani *wa-resit*, hii ya *standardisation* ni siasa, *standardisation* ni siasa na ni danganyatoto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii inanikumbusha maneno ya busara ya Gavana wa Mwisho wa Tanzania Sir Richard Turnbull wakati Nyerere anamsindikiza kwenye meli alimwambia maneno machache akasema *Mr. President you can politicize everything but not education*, yaani unaweza kufanya kila kitu kiwe siasa lakini siyo elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *standardisation* ni siasa, sisi kama Walimu *by profession* mahali popote duniani kama mtihani unafutwa, watoto wanarudia mtihani kwa sababu ufaulu wa mwaka jana ndiyo hali halisi, badala ya kufuta mitihani tushughulikie yale matatizo yaliyosababisha kuwa na mitihani mibovu. Kwa hiyo, hiyo nimeona niitoe hivyo kama Mwalimu *by profession*.

Mheshimiwa Spika, sisi sote tunahusika, tusimlaumu Mheshimiwa Dkt. Kawambwa peke yake, Taifa linahusika kwa

kutohakikisha kwamba tunakuwa na utamaduni wetu. Watoto wetu wamezama katika utamaduni wa Marekani kwa kuangalia filamu za *Hollywood* za Marekani. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Marekani inapata fedha nydingi sana kutohana na filamu za *Hollywood*, kwa sababu huu ni mkakati wa Marekani wa kueneza utamaduni wake dunia nzima, inaitwa *American Cultural Globalisation*.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahusika kwa kutoa bajeti ndogo, wazazi wanahusika kwa kutofuatilia maendeleo ya watoto wao, Walimu ndiyo kabisa, kwa hiyo, tuna matatizo makubwa sana katika elimu yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nimeshasema kwamba, tusiingize siasa kwenye mitihani, mitihani inapofutwa inarudiwa. Tukifanya mambo ya *standardization*, tunaweka a *precedence*, watoto watakapofanya vibaya watakuwa wanashinikiza Serikali kufanya *standardization*, kwa sababu wanajua hawarudii mitihani.

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusu matokeo ya mitihani, mimi kama *senior citizen*, hili Baraza limeanza tangu mwaka 1973, lakini sijawahi kumwona Waziri wa Elimu anatangaza matokeo ya mitihani, siyo kazi yake bali ni kazi ya Baraza kutangaza matokeo ya mitihani. Nawaomba Waheshimiwa Mawaziri msiingie jikoni, kwani mkiingia jikoni mtaungua.

Kazi ambayo mnatakiwa kuifanya ni mteue watendaji wazuri na Wajumbe wazuri wa Bodi baadaye muwaache *wa-manage, let the Managers manage*, msiwaingilie bali muwape *autonomy* ya *ku-manage*. Kazi yenu ni *eyes on hands off*. Kwa hiyo, *it was unfortunate* kwangu nilipoona Waziri anatangaza matokeo hayo nilisikitika sana kwa sababu siyo kazi yake....

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Ahsante sana muda umekwisha, mambo makubwa, lakini muda umekwisha. Mheshimiwa Naomi Kaihula, atafuatiwa na Mheshimiwa Abia Nyabakari, sina hakika kama mtu mwingine wa nne atapata nafasi. Mheshimiwa Naomi Kaihula!

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili kuweza kuzungumzia masuala ya elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi kama *senior citizen* na kama Mwalimu hasa namshukuru Mungu kwamba, nimefundisha kuanzia kipindi cha Mkoloni, kipindi cha uhuru mpaka kipindi hiki, *almost 40 years* nipo katika *profession*. Suala la elimu katika nchi yetu limekuwa likinigusa katika ngazi mbalimbali, nimefundisha kuanzia shule ya msingi, sekondari na vyuo. Kwa hiyo, hii miporomoko na mikanganyiko ya elimu nimeiona na nime-experience mimi mwenyewe. (*Makofî/ Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo nataka kuzungumzia, kwanza, napenda nizungumze kwamba, katika nchi yetu kwa ambao tunaipenda nchi yetu, sisi ni wamoja, mnakumbuka ndugu zangu kuna wakati niliwaambia kwamba, ni lazima tukimbia mapepo kwa sababu mahali ambapo hapana pepo tutakuwa tunazungumza lugha inayoeleweka ya kuendeleza nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, inakuwaje tunapokuwa nje sisi sote tunaacha vyama, tunaona mambo yanayoonekana? Tukifika humu watu wanabadilisha tena wanaanza mitindo mingine, lazima tuseme ukweli kwa sababu ukweli utatuweka huru. Nawaambia kabisa kwamba ukweli hatuwezi tukaukimbia, ukweli una tabia moja ya kwamba unakuja kujilipiza kisasi kwa sababu utajijulisha tu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie moja, kwanza napenda niseme kwamba, nashukuru sana katika Bunge la Vyama Vingi, Vyama Vingi kunakuwa na Chama Tawala kinachoongoza lakini kunakuwa na Vyama vya

Upinzani na kazi ya Vyama vya Upinzani katika demokrasia ya vyama na katika utawala bora, samahanini kwani nimesoma pia siasa na nimebobea, ni kwamba kama kile Chama cha Upinzani ambacho kinatazama ile Serikali inafanya nini, kikilaza damu nchi imekufa, nchi inakufa kabisa jamani mnajua, ndugu zangu tumesoma wote wengine katika Chuo cha Kivukoni.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Upinzani ni lazima kifanye kazi kusudi watu wale wanaofanya kazi waweze kwenda inavyotakiwa. Namshukuru Mungu kwa sababu angalau sasa hivi Chama cha Upinzani kikuu kinaweza kufanya kazi hii na ndiyo maana nasema hivi, nakubaliana kabisa na yaliyoelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini Serikali ilivyokuwa inatueleza, ilikuwa inazidi kuji-expose jinsi ambavyo imeshindwa kutimiza wajibu, imeji-expose jinsi inavyoshindwa kutimiza wajibu katika muda huu mrefu, niwaambie! Sasa Chama cha Upinzani CHADEMA kikaleta *speech* nzuri na kwa kweli nashangaa mpPENDWA wangu Madam Sitta rafiki yangu.

Mheshimiwa Spika, sisi tumetoa mapendekezo, angalia kwenye kitabu chetu, mwisho naomba nimwonyeshe, ni ukurasa wa ngapi, ni ukurasa wa 51, tumetoa mapendekezo, tena imeandikwa wazi mpPENDWA wangu, tumeandika mapendekezo muhimu ya kuboresha sekta ya elimu nchini, tumetoa dada yangu. Pia kila wakati tunapotoa *speech* yetu tumekuwa tukitoa mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, tunaomba jamani tuachane na mapepo, tufanye kazi yetu kama tunavyofanya kwenye Kamati, unajua kazi tunayofanya kwenye Kamati, huwa tunakuwa wamoja, tunaangalia hiki na kile. Ni kweli kwamba wanapewa fedha kidogo, lakini pia inawezekana hata hiso fedha kidogo walizopewa wanazipangaje? wanazitumiaje? Je, kuna usimamizi wa kutosha? Ndiyo vitu ambavyo Chama chetu cha Upinzani kimekuwa kikieleza hapa Bungeni kwamba jamani lazima tuangalie jinsi gani tunavyosimamia. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, bila kupoteza muda, napenda niseme kwamba, naunga mkono hii hotuba ya Upinzani kwa kiwango kikubwa chote, tujaribu kuangalia tutakapotoka hapa na tunapokuwa tumeondokana na zile siasa na jazba, tutaona kwamba kuna mambo ambayo yatasaidia nchi yetu. Nawashukuru kwa kuwa mmenisikiliza. (Makof)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nichangie kwa mambo mengine ambayo hayaona kwamba yapo na yanaendelea, lakini cha kushangaza kabisa na humu ndani naona sura za Walimu wakongwe wengi tu.

**WABUNGE FULANI:** Tupo.

Mheshimiwa Spika, lakini vitu vya ajabu vinatendeka humu. Kitu cha kwanza kushuka au kuperomoka kwa elimu katika nchi yetu, kwani tunasikia sasa hivi? Hatusikii sasa hivi, lakini ni hatua gani tumechukua? Kwa mfano, tunajua kabisa kimojawapo kikubwa kinachochangia kuperomoka ni kwa ajili ya kutowajali watoa elimu, hatuwajali! Walimu hatuwajali! Sasa usipowajali Walimu, hivi unafikiri hao Walimu watakaa wakatoa elimu ya kutosha au usipomjali, tuseme mtu anayetunza watoto wako nyumbani, unafikiri atatunza watoto vizuri? (Makof)

**MBUNGE FULANI:** Hawezi!

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Hawezi! ukimpa maziwa atakunywa yeye kwa sababu unamwambia wewe ushinde njaa. Kwa hiyo, ni lazima umtunze yeye kwanza ili kusudi aweze kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, sasa ni kwa jinsi gani tunapaswa tuwatunze? Siwezi kuyarudia yote kwa sababu yaliyosemwa ni kweli, wana madai, mazingira magumu na nini, lakini kitu kingine kimoja ambacho hata baba yetu wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alituachia, alisema hivi: "Ni lazima tujali *quality*, ubora zaidi ya wingi." Hata hivyo, kwa makusudi kabisa tumeendelea kufanya siasa katika kufungua shule,

kabla hata hatujapata Walimu wa kutosha na majengo ya kutosha. Ukienda kwenye mazingira yale ni machafu, hakuna madawati wala nini.

Mheshimiwa Spika, nashangaa kila wakati na najiuliza hivi hawa Wakaguzi kama kweli walifanya kazi yao ilikuwaje wakafungua shule ambayo haina *desk*? Unakuta watoto wamekaa chini kabisa, hakuna *desk* hata moja, ilikuwaje? Hakuna vyoo kabisa na tunajua kwamba, mojawapo ya misingi ni lazima vyoo viwemo, lakini hakuna, imefunguliwaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa watu wanaposema, watu wawajibike sisi tunakaa kuwasaidia, tusiwasaidie. Nawambieni katika utawala bora, tunaanzia juu kuwawajibisha kwenda chini kwa sababu inamaamisha yule wa juu hakufanya kazi yake sawasawa. Wewe wa juu unapaswa uwe macho usilale, ushuke.

*In fact* yule wa juu akiwajibika kwa kawaida ya utawala bora inamaanisha mstari unashuka kwa wahusika, lakini huwezi kuanzia huku chini. Kama ye ye wa juu angechukua nafasi ya kuwawajibisha, sawa atawawajibisha wa kule chini, lakini kama ye ye hakufanya kazi akaaja akaonwa na watu wengine inabidi awajibike. Nchi yetu tuiponye, huu ni ugonjwa, siyo katika Wizara ya Elimu tu, bali ni katika mambo mengi, tuwawajibishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, inakuwaje katika shule vitu vya msingi kama vitabu vya kiada na ziada havipo, halafu mtu anasema watoto walichaguliwa kuingia *form one* hawajui kusoma wala kuandika? Yes, ndiyo! Watajuaje, wengine hawajakiona kitabu? Hawajakiona kitabu, nawaambieni na inashangaza na hasa wale watoto wa maskini ndiyo kabisa maana yake hawajui hata duka liko wapi na wanunue wapi. Mnasemaje? (Kicheko/Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Kwa muda nilionao naweza kumwita Mheshimiwa Abia Nyabakari na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mkristo na mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii. Katika chumba hiki kila siku kuna watu wakisimama lazima waseme kwamba, wao ni wasomi. Nafikiri hatuna wasomi wengi kama walio ndani ya Chama Tawala. Naomba niseme kama watu waliotutangulia wangkuwa hivi tusingefika mahali hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mtume Muhamad (*Swalallahu Alayh Wasalam*), alikuwa na Maswahaba, wote hawakuwa na elimu na alitembea nao na alifanya kazi nao. Si hivyo tu, Yesu Kristo, alichagua Mitume 12 wakiwakilisha tabia za wanadamu 12, walikuwemo akina Petro na Yohana na hawakuwa na elimu, ili wakakilishi tabia za watu waweze kuwaelewa. Sasa mkisema sisi wasomi ndiyo tunaoweza kuingoza nchi, hivi kweli humu kwenye Chama Tawala hakuna wasomi wengi kuzidi nyie? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mithali 14:8 inasema: "Akili ya mwenye akili ni kujua njia yake, lakini upumbavu wa wapumbavu ni udanganyifu." Kasomeni. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ikitenda haki itathibitika. Biblia inasema: "Wafalme wakitenda yasiyo haki ni machukizo, maana kiti cha enzi huthibitika kwa haki". Serikali inatoa *syllabus* ili elimu yetu ya Tanzania iweze kuwa *uniform*, lakini sasa Mwalimu huyo huyo anafundisha somo, anatunga mtihani, anafanya mambo yote yanaishia kule, mpaka mitihani sjui ya muhula na nini huko. Sasa najiuliza mtambaini vipi kwa wakati huyu Mwalimu kwamba, uwezo wake wa kufundisha ni mdogo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, twambieni, mnajiridhishaje kwamba, mwanafunzi aliye kule Rukwa na

yule aliyeko katika Wilaya ya Buhigwe kule Kigoma na wa Tandahimba kwamba, elimu zao zinakwenda sambamba katika mfumo huo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa Serikali pia kuweka mfumo wa kuhudumia Walimu nchini ambao unahuishisha vyombo vingi, nasema huo ni ubatili. Mkae mliangalie hili tena kwani nafikiri linaleta mchanganyiko katika utendaji wa kazi. TAMISEMI humo humo, sijui Utumishi humo humo, Elimu na Mafunzo ya Ufundı humo humo, hivi mtamwajibisha nani hapa? Waziri gani anatakiwa awajibike? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kama mfumo huo utaendelea, mtaendelea kufukuza Mawaziri na Mawaziri na nasema mkianzia na Waziri wa Utumishi wa Umma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri Serikali ingeunda chombo kinachohudumia shule za msingi na sekondari kwani naona shule zimekuwa nyingi sana. Chombo hicho kijitegemee chenyewe kusimamia hiyo kazi. Si hivyo tu, wawekewe chombo cha Ukaguzi kitakachokuwa na muundo kama ule wa CAG, naunganana na Margaret Sitta katika hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pia wangeanzisha Tume ya kutunga mitihani ya kila muhula, kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu ili kuwafanya hao Walimu wazembe wanaokaa wanafuma mikeka, kusukana, kufuma vitambaa na kuomba ruhusa zisizokuwa za msingi, waweze kuwajibika katika kazi. Muda mwingi Walimu wanakuwa wanaranda randa tu wakijua kwamba, nitatunga mtihani hapa, kwa hiyo sina shida, hawaoni umuhimu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, utoaji wa posho maalum kwa Walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu. Naionba Serikali iweke utaratibu mwingine wa ziada, kwa mfano, Mwalimu anayefundisha kule Kara analazimika kuchukua boti kwa sh. 10,000/= kwenda mpaka Kasanga, alale pale kwa sh. 10,000 na hapo bado hajala. Kesho yake Mwalimu huyo anapanda gari kwa sh. 10,000/= aende Sumbawanga maana hakuna barabara ya kukatizia hapo

kwenda Nkasi, alale hapo na kesho yake aende Nkasi kwa nauli ya sh. 6,000/= alale huko huko kama ni siku mbili, bado hajala, kisha arudi kwa utaratibu huo. Naomba hili Serikali iliangalie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Walimu wanaweza wakaenda huko bila hata kujua kama mshahara umeingia au haujaingia, maana hakuna mtandao na barabara ndiyo hizo hazipitiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Walimu wa Rukwa wanailaumu Serikali kwamba haiwaendelezi kielimu. Hata hivyo, niliwaambia kwamba, tulieni kwani inawezekana waliopo wanaohusika na nafasi hiyo labda kwa wakati wao nao hawakupata elimu stahiki, ndiyo maana hawaoni umuhimu wa elimu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu, Idara ya Elimu ya Sekondari hawana gari katika Manispaa jamani. Ile gari ya elimu ya msingi imechakaa na gari nyininge za ukaguzi sasa zinakwenda upande. Tunaomba Serikali itukumbuke, kama kuna fedha kidogo ya ziada, tunaomba msitusahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijasahau kabisa jambo muhimu katika Wilaya ya Nkasi, naiomba sana Serikali iweke utaratibu wa kufanya mitihani katika maeneo ya mwambao kama Makirando, huko watoto wetu wanapakiwa ndani ya boti kama samaki wanaokwenda kuuzwa, wanatolewa kituo hiki wanapitishwa huko, ukiuliza eti unaambiwa Wakaguzi wameshindwa kwenda kwa sababu ya maji. Hivi wao ndiyo wana roho kuliko watoto wetu? Tunaomba Serikali msije mkatubebesha mawe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nawaomba Walimu wangu wa Sumbawangwa, watu wanapopita wakiwashawishi eti wapinge maisha magumu kwa kuweka sahihi, huko ni kutomjua Mungu. Mungu mwenyewe alisema umaskini hautakoma na akaongeza kwamba hatutakula chakula kwa mtu bure, bali kwa taabu na masumbufu. Mtu anaposema muweke sahihi, huyo hamjui Mungu ambaye

alisema kwa jasho la uso wako utakula mpaka utakaporudia ardhi. Sasa nawaomba Walimu wa Sumbawanga wawe makini katika kufanya kazi, maana Biblia inasema asiyeweza kufanya kazi kwa bidii, huyo umaskini hautakwisha nyumbani mwake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, siyo hicho tu bali nawaomba Walimu wangu hasa wa Rukwa ninaowapenda, Biblia inasema; "Usiandamane na mikutano kutenda uovu wala usitie ushahidi katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana. Haya mashetani sijui yanakalia wapi maana yake... (*Kicheko*)

Sasa nimwite msemaji wetu wa mwisho kwa mchana huu, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine.

**MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hii hoja ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini mambo yafuatayo ni lazima tuyarekebishe kwa sababu tuko hapa kuishauri Serikali na wala siyo kuiandama.

Mheshimiwa Spika, nianze na jambo la kwanza ambalo linahoji elimu ni nini? Mtaalam mmoja aliwahi kueleza maana ya elimu, nakubaliana naye na naomba ninukuu: "Elimu ni urithishaji wa maarifa, mila, desturi, mienendo na falsafa ya jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine."

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la elimu ni kumtayarisha mwanajamii ili awe mtumishi mwema katika jamii yake. Katika daraja hizi mbili jamii na msomi, jamii ni muhimu zaidi kuliko msomi, lakini msomi pia ana ngazi muhimu katika jamii yake.

Elimu ikitolewa kwa lugha sahihi hutoa fikra sahihi zenyе uwanja mpana wa kufikiri na kuleta mabadiliko katika jamii." (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimetumia nukuu hii kutaka kuwaambia Wabunge wenzangu kwamba, sasa hivi tuko katika mpito, kuna mapinduzi ya kila aina; uchumi, elimu na kadhalika, hivyo haiwezekani tukaanza kulaumu kwamba, Serikali hajafanya chochote. Ndiyo maana nauliza wenzetu kwamba, ni kipi kilikuwa kitangulie hasa katika shule za Kata, ni kupeleka Walimu au vifaa?

Mheshimiwa Spika, kwanza tunajenga madarasa, tukimaliza kujenga madarasa tunatafuta wanafunzi, tukimaliza kutafuta wanafunzi ndiyo tunapeleka sasa Walimu. Utaajiri Walimu pasipokuwa na madarasa na wanafunzi? Watazeeka bila kufanya kazi, hivyo ni lazima tukae tufikiri na hilo. (Makof)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kitengo cha *EMAC – Educational Material Approval Committee*, ambacho kiko katika Wizara ya Elimu. Mheshimiwa Susan Lyimo, mwalimu wangu, siyo kwamba nampinga, hiki chombo kwa kweli zamani kilikuwa ni kitengo cha hovyo, lakini sasa hivi kimerekebishwa na kinafanya kazi vizuri sana. Ninachoomba ni kwamba, kiwezeshe kifedha ili kiweze kufanya kazi kwa uadili na hali kadhalika kitoe vitabu bora.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri awezeshe hiki kitengo cha *EMAC* ili kifanye kazi vizuri kwa sababu sasa hivi tuna Kamishina mzuri wa Elimu, tena Profesa, yule mama tumpe ushirikiano. Mheshimiwa Waziri ampatie yule mama ushirikiano na naamini ataleta mabadiliko katika mfumo huu wa elimu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa Wizara; napendekeza, kusimamia Wizara hii ya Elimu yenyewe halafu na Mafunzo ya Ufundı kwa maana ya vyuo vya *VETA*. Nasisitiza kwamba ili tuweze kuleta ufanisi mkubwa zaidi, ni vizuri vyuo vya *VETA* vikahamishwa kutoka katika Wizara hii vikapelekwa chini ya

Wizara ya Sayansi na Teknolojia na hapo tutaleta mwendelezo mzuri kabisa. *What is technology?* Nini maana ya sayansi? *Technology is an application of science.* Sasa kwa nini vyuo vya VETA visiende katika Wizara ya Sayansi na Teknolojia?

Mheshimiwa Spika, lugha ya kufundishia; napenda kusisitiza kwamba, wapo ndugu zetu kwa mfano, mzee wangu Ntukamazina, anasema ni lazima tutoe elimu kwa lugha ya Kiingereza. Hawa ni watu ambao wamesoma enzi za Mwalimu Nyerere, wakasomeshwa Marekani, Ufaransa, Uingereza na kadhalika. Wale watu ambao wamesoma katika nchi za Russia na China, wana mawazo ya kimapinduzi. Ni lazima tuthamini lugha ya kufundishia iwe Kiswahili na hapo tutaepukana na matatizo mengi na tutafanya kazi nzuri sana katika utoaji wa elimu. Kwa nini tusiamue?

Mheshimiwa Spika, naomba kutamka hadharani kabisa kwamba, elimu yetu inashuka kutohana na mfumo wa elimu ambao tunautumia. Sasa hivi tunapaswa tubadilike. Nawashauri Watanzania wenzangu wajifunze lugha; Kichina, Kifaransa na kila lugha, lakini tutoe elimu yetu kwa lugha ya Kiswahili, hapo tutaleta mwendelezo mzuri sana na tutakuwa tunakuza utamaduni wetu na kuepukana na kasumba ambazo hazina maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo moja ambalo naomba nilisisitize. Siku moja nilisema lugha ya kujua ndiyo lugha ya mawasiliano ya kujifunza. Lugha ya kwako ndiyo lugha ya kujijua, yaani kujielewa. Lugha ya kujielewa ni lugha yetu ya Kiswahili, ndiyo maana siku moja niliwaambia tunaweza tukawa tunaomba hata sala zetu kwa Mungu kwa kutumia lugha ya kigeni kwa sababu tunapomwombwa hatuombi *direct* tunapitia kwa wazee, waganga na wahenga ndipo Mungu anapokea na kujibu kuitia kwa watu hao. Sasa tukisali kwa njia hizo wale wazee wanaweza wakaelewa lugha ya Kiswahili, lakini kuwasiliana na Mungu kwa lugha ya Kiingereza hawawezi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nyie hamjasoma lugha ndiyo

maana mnacheka, hamjui. Si ndiyo! Mngekuwa mnajua msingeguna hivyo! Kwa hiyo, ni lazima tuthamini lugha yetu ya Kiswahili ili tufikiri kwa kutumia lugha yetu hiyo na hapo tutapata maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba niliongelee pia suala la matabaka katika elimu. Hapa kwa kweli tunatakiwa tuweke utaratibu kabisa kwamba, hizi shule za *English Medium, Academy* na za Kimataifa ziweze kutoa mihtasari au kufundisha kwa kutumia mitaala ya Tanzania. Hapo tutakuza utamaduni wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kwa ufupi Sera ya Elimu. Sera ya Elimu kama itatekelezeka, italeta mabadiliko makubwa katika nchi. Hata hivyo, naomba mambo yafuatayo yafundishwe; kwanza, sera itamke hadharani kuwa inamjenga mwanajamii ili aweze kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri na wala siyo wa kulalamika. Somo la maadili lijumuushe mada zifuatazo: Upendo, udugu, uzalendo, Utaifa, umoja, mshikamano, ujasiriamali, utamaduni wetu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa pawepo na Shirika la Uchapaji wa Vitabu ambalo litasimamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba kuhitimisha kwa kusema kwamba, elimu yetu tukiamua kujengwa katika misingi ya kufikiri, hekima na busara, Watanzania wote kwa pamoja tukaithamini, umoja wetu na kila mmoja atoe mchango wake na si kulalamika, tukajitambua, naamini Tanzania yenye elimu bora itawezekana.

Mheshimiwa Spika, tukikaa tunalalamika kwamba, Serikali haijfanya chochote kile, hebu fikiria wakati tunapata uhuru watu waliokuwa wamesoma *Masters* walikuwa ni wawili tu; mwalimu Nyerere na mwenzake mmoja. Sasa hivi tuna watu wengi na *Masters* ziko mpaka uchochoroni, *Ph.D* ziko mpaka uchochoroni, mnasema hakuna chochote kilichofanyika kuititia Chama cha Mapinduzi! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba tuamini kabisa kwamba Chama cha Mapinduzi ndicho kimewafikisha hapo mlipo na kimewakomboa na kuwaleta mpaka hapo ulipo. Kwa hiyo, mkithamini na mwendelee kuiheshimu Serikali ya Chama cha Mapinduzi, itafanya makubwa. Mwendelee kutoa ushauri wenye maana siyo wa kubeza tu, maana mkibea mtafanya hivyo kwenye mitandao.

Matokeo yake, mnapotosha wanafunzi wetu na hawasomi, sasa hivi badala ya kukaa na kufikiri ili walete maendeleo katika jamii muda mwiningi wako kwenye mitandao wakitukana matusi tu. Hao ndiyo wasomi wetu, muda mwiningi sana wako huko na baadhi ya wanasiwa wanakimbia kwenye vyuo huko kufanya siasa ambazo ni uchwara. Naomba kwa kweli turekebishe mambo kama hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ya kwangu yalikuwa ni hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante na kengele yenye we imegongwa.

Waheshimiwa Wabunge, baadaye tukirudi watakaofuata katika kuchangia ni Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Agness Hokororo, Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Thuywaiba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mheshimiwa Sarah Msafiri, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Joseph Selasini na Mheshimiwa Yahya Kassim. Hao ndiyo watakaofuatia hivyo, wajandae.

Waheshimiwa Wabunge, utaratibu wetu wa kuchangia tumeu-computerize, kwa hiyo, nikifika najua wewe umechangia mara ngapi, wewe mara ngapi na wewe mara ngapi. Kuna wengine wanasema namsikiliza Lukuvi, namsikilizaje Lukuvi na mimi nina kompyuta? Acheni vitu vidogo vidogo, nina kazi hapa na kuna utaratibu, tukiangalia tunajua umechangia ama hujachangia, umechangia mara mbili au ngapi na upo kwenye Wizara uliyoomba, kama hukuomba hupati nafasi.

Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge liliarishwa mpaka Saa 11. 00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Majadiliano mchangiaji wetu wa kwanza hapa ni Mheshimiwa Assumpter Mshama na ajandae Mheshimiwa Hokororo na Mheshimiwa Margaret Mkanga.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi nikiwa wa kwanza kuchangia katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda moja kwa moja katika tatizo kubwa. Tumekuwa na tatizo la Sekta hii kwa muda mrefu katika mjadala huo, nadhani Wizara husika itakuja na muafaka wa nini kifanyike ili kuondoa tatizo la elimu. Nitaanza na tatizo la mfumo mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupeleka katika mfumo wa elimu tulionao. Mfumo wetu una matatizo makubwa ambayo sekta moja inakuwa na vipengele zaidi ya vitano. Kwanza, ukienda katika Wizara au tuseme Sekta ya Elimu, utakuta Wizara kama tano zinaunganishwa pale, kuna Wizara ya Utumishi, ambayo inahusika na mambo ya ajira, kuna TAMISEMI ambayo ni utekelezaji na utendaji, kuna Wizara ya Elimu yenyewe inayoshughulika na sera na mwongozo, kuna Wizara ya Fedha ambayo inahusika ni namna gani watu watapata mishahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vigumu sana Wizara moja au kitengo kimoja kuongozwa na watu zaidi ya watano. Hivi tunapoongelea kufeli kwa wanafunzi, tunapoongelea

matokeo kuwa mabaya tunamshika namna hapa, nani mhusika halisi wa Wizara hii, matokeo yake hatuna mtu wa kumkamata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Elimu hainunui madawati, Wizara ya Elimu haihusiki na utaratibu wa kupandisha vyeo Walimu, ni nani anayehusika katika tatizo la kufelisha au la kupata matokeo mabaya. Hivyo, naiuliza Serikali imeona kitu gani baada ya kubadilisha mfumo uliokuwepo au imepata *impact* gani yaani imefanikiwa nini katika kubadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwa nini tusirudi katika ule mfumo wa zamani. Kwa mfano, niongee, unapokuwa unatengeneza raundi, lakini raundi yenye we imematikatika ni ngumu sana kupata kitu kizima na ndicho kinachotupata katika Wizara ya Elimu. Hivyo, naomba turudishe utaratibu kama ulivyokuwa zamani ili tuweze kupata matokeo mazuri na hii iendane na kwamba, unapokuwa umeanzisha kitu na umepima hakiwezekani, hebu tujaribu kuangalia nini kifanyike tuweze kurudi katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la Wizara ya Elimu yenye we, katika mwaka 2010 kuna utafiti ulifanyika **Movet Pest** pamoja na Chambi Chachage walifanya tafiti na Wizara yenye we ikatahakiki tarehe 14 Julai, 2010. Lakini kitu ambacho kilikuwa kimeongelewa pale ni kuona nini tatizo katika Wizara ya Elimu, kukaonekana matatizo ni kwamba Walimu hawawezi kupata *morale* wa kufundisha kama hawawezi kupewa *incentive* yaani hawana motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikaonekana kuna mambo ya kufanya kama vilewapewe nyumba za kuishi, wapewe posho ya usafiri, kupandisha haraka mishahara hasa wale Walimu ambao wanafundisha katika *remote area* yaani zile sehemu za pembezoni, wapewe hata *leave* za kwenda masomoni, wapewa kozi za mara kwa mara, wapewa fursa za kwenda kusoma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika mfumo tulionao;

Mwalimu anayefundisha Dar es Salaam na yule anayefundisha kwenye Jimbo langu la Nkenge katika Kijiji cha Nkaka, anapewa mshahara sawasawa na mtu anayekaa kwenye taa, anayepata huduma ya maji, anayepata hata mtandao wa simu kwa urahisi, anakwenda benki kirahisi, hawa walimu hawawezi kufundisha. Lazima tutengeneze utaratibu unaoweza kufanya Walimu wajisikie kwamba tunawatambua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu alikuwa anasema Walimu wanaichukia Serikali, nasema Walimu hawaichukii Serikali, Walimu hawatendewi haki. Siwezi kuwa nakaa katika vijiji vya pembezoni, napewa mshahara sawasawa na Mwalimu anayekaa Dar es Salaam, bila kufanya hivyo hatuwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tafiti ilivyofanyika wenzetu wanachama wa *SADC* waliamua kuongeza kitu. Mfano, Malawi wao wanatoa nyumba kwa kila Mwalimu anayekwenda kufundisha kijijini, anakuta nyumba ipo pale. Uganda wao wamemwongeza Mwalimu asilimia 30 kwenye mshahara wake, hicho ni kivutio cha kumfanya Mwalimu aende kufundisha katika sehemu za pembezoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Mozambique* wao wametoa mara mbili ya mshahara kama alikuwa anapata 400,000, anapata 800,000 hii inaongeza motisha kwa Mwalimu kwenda kufundisha katika sehemu ambazo hazina huduma za kijamii za kueleweka. Lesotho wao walitoa *Maloti* 275 ambazo ni sawa na 60,000 za Tanzania kwa ajili ya Mwalimu kuweza kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Mwalimu mmoja anayefundisha Kakunyu kwenye Jimbo langu anatembea kilomita 120 kwenda Wilayani. Lakini hujampa *transport allowance*, hujamwekea kitu chochote je, huyu Mwalimu atafundisha kwa *morale*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ya Elimu au hizi Wizara zote ziangalie, kuna haja ya kuendelea kukaa

pamoja, kwa nini tusifanye kitu kimoja kikubwa, Wizara ya Elimu ikawa na Wizara nzima kuanzia vidudu mpaka Chuo Kikuu, anashughulika mtu mmoja, hivyo tutaweza kumkamata mtu asiyeweza kuwajibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya ziara katika Jimbo langu, nilipofanya ziara katika Jimbo langu nilitembelea Walimu tu. Nataka nikwambie walichoongea Walimu, wanasema wanapoandika barua zao za matatizo inaweza ikachukua miezi mitatu, hajajibwa, unategemea huyo mwalimu atatoa matunda mazuri? Anapokuwa amepandishwa cheo, anaweza kutumikia cheo kile kile hata miaka mitatu hajaweza kupata mshahara wa cheo kipywa, huyo mwalimu atakubali kweli kuipenda Serikali iliyopo madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kwamba, Walimu sisi ndiyo tunaowafanya wasiweze kuipenda Serikali yao na wasiweze kuwatendea vizuri wale watoto wetu na wanao-*suffer* ni watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka nikiongelee ni utaratibu wa kufundisha. Hebu niulize wanasema watoto wamefeli, lakini mtoto anapokuwa ameanza shule ya awali mpaka darasa la saba anajifunza kwenye Kiswahili, asubuhi moja anajikuta yupo kidato cha kwanza, anatakiwa masomo yote ajifunze kwenye Kiingereza na Kiswahili kwenye somo moja tu. Hivi huyu mtoto at-a-concentrate kuelewa nini kinafundishwa pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiamue kwamba, Kiswahili kiwe cha nyumbani na Kiingereza kiwe cha kufundishia shulenii au tuamue kama ni Kiswahili twende kwenye Kiswahili. Kumbuka ubongo wa mtoto unashika kuanzia miaka mitatu, mpaka miaka kumi na nne yaani shule ya awali mpaka darasa la saba, ubongo ndipo unaweza kutengeneza kitu. Lakini anapokwenda tena ghafla, anashtuka asubuhi moja masomo manane yote yanafundishwa wa Kiingereza na Mwalimu anayemfundisha

mwenyewe amepitia kwenye mfumo huo huo ambao siyo wenyewe nguvu ya elimu ya kutosha. Sidhani kama tunaweza kutengeneza elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika mchango wangu ninachoomba Serikali iangalie upya *system* nzima ya elimu. Tuache kushika au kuwa na ugomvi na Walimu wakati Walimu hatuwatendei haki. Nakumbuka Walimu wengi Tanzania wapo vijijini, lakini vijijini huko huko hawana utaratibu wa maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itengeneze utaratibu wa kuwafanya Walimu waweze kuipenda kazi yao. Kwa mfano, leo mtoto anapopata *division four* ambaye hakushinda, wanamuuliza hata ualimu umeshindwa kuupata. Hivi kweli tunapeleka Walimu ambao yaani mtu *reject* yaani ambaye hawezি chochote angalau Ualimu, tunategemea kupata matokeo mazuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Hokororo na ajande Mheshimiwa Margareth Mkanga.

**MHE. AGNESS E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende moja kwa moja katika kuchangia hotuba ili yopo mezani. La kwanza kabisa naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali za kupunguza upungufu wa Walimu, lakini bado kuna kazi kubwa ya kuifanya kwa sababu kwenye

Wilaya ya Masasi kwa sasa hivi kwa mfano, mahitaji ya Walimu wa Sekondari ni 839 na Walimu tuliokuwa nao ni 412. Kwa hiyo, upungufu ni Walimu 427.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Walimu wa wanasayansi tunao 78, upungufu wa Walimu wa sayansi ni 260. Kwa shule za msingi wanaotakiwa ni walimu 1,480 na waliopo ni 1, 030 pungufu 450.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msisitizo wangu hapa ni kwamba, tunapogawa Walimu kwenye nchi hii, basi hata na sisi tunaonekana kwamba ni wa pembezoni tusiendelee kubakia kuwa pembezoni kwenye kila sekta. Walimu hawa wa Sayansi tunawahitaji na Mkoa wa Mtwara tunawahitaji sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki iliyopita hapa nchi nzima ilikuwa suala la uwekezaji wa gesi kwenye hii Mikoa ya Kusini na hususan Mtwara. Sasa kama hatutapatiwa hawa Walimu wa sayansi kuanzia sasa na matarajio yetu ni kwamba, tunakwenda kwenye uchumi wa katil sidhani kama tutakuwa tunatendewa haki tusipoandaliwa kuanzia sasa watoto wa shule za msingi na sekondari tukaingia wote kama nchi kwenye huo uchumi wa katil.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo changamoto nyiningine kubwa kwenye Wilaya ya Masasi, wote tunatambua tukio lilitokea tarehe 26, Idara ya Elimu kwa ujumla wake hawana ofisi, liletukio la kuchomwa moto kwa ofisi za Serikali, Idara ya Elimu hawana majengo na wao sasa wote wanajibanza kwenye ofisi za CWT, hawawezi kufanya kazi, hata tukikaa hapa kwa masaa 48 tukawataka Walimu na Idara hizo zifanye kazi. Naiomba sana Serikali yangu kuangalia kwa jicho la huruma kwa sababu nyaraka zote za Walimu, vitendea kazi na kila kitu kinachohusiana na Walimu kwenye Wilaya yetu ile ziliungua moto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye eneo hilo hilo la Mkoa wa Mtwara. Pamoja na kwamba tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu tumepata hiyo

rasilimali, lakini bado nasikitika pia kwenye Sekta ya Elimu bado sisi wa pembezoni tutaendelea kuwa wa pembezoni na hapa naomba nijikite kwenye ile rasilimali ambayo tulipewa tangu enzi za Baba wa Taifa, shule, kongwe za wasichana katika Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanisikitisha sana na hapa naomba Serikali yangu iangalie kwa makini. Katika shule za wasichana Mtwara, Mtwara *Girls* shule niliyosoma, Shule ya Wasichana Masasi, uwezo wa shule zile ni mkubwa kuliko zinavyotumiwa sasa na Serikali. Haitusaidii, haitusaidii Watanzania na haitusaidii wananchi wa Mkoa wa Mtwara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye shule ya Masasi wasichana uwezo wa shule ile inatakiwa iwe na wanafunzi 480, inasikitisha sasa hivi kuona ina wanafunzi 55 tu na tena ina michepu minne. Kwa wastani hapa kila michepu pengine unaweza kuwa na wanafunzi 10, lakini shule ile ina mabweni tisa, lakini yanayotumika ni mawili, mabweni mengine yote yamefungwa, madarasa yote yamefungwa, maabara hazitumiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na Mtwara *Girls*, uwezo wake ni kuchukua wanafunzi 540, sasa hivi ina wanafunzi 95. Mabweni 10 ya Mtwara *Girls* yamefungwa na sasa Mkuu wa shule alivyoona kwamba, buibui wanaendelea kuharibu, ameruhusu watoto wote wakae kwenye mabweni 10, kwa hiyo kila bweni lina watoto sita na madarasa yamefungwa, maabara zipo, miundombinu pale ipo. Sidhani kama maamuzi ya Serikali kupeleka watoto kidato cha tano na sita kwenye hizi shule za wasichana ilikuwa inatutendea haki sisi wananchi wa Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa siku tutaachwa, watoto wa kike wa Mtwara, shule ambazo sasa hivi wanazitumia ni za *day*, ni shule zetu za Kata. Naipongeza Serikali kwa ujenzi wa shule za Kata, lakini kuna haja gani ya watoto wa Mtwara kuendelea kusoma kwenye hizo shule za vibatari hizo za Kata, wakati tuna shule kongwe za bweni

Mtwara. Kulikuwa na haja gani kuchagua watoto wachache kutoka Tanzania wakati watoto wasichana wa Mtwara wangeweza kusoma na wakafaulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, enzi zetu sisi tulikuwa wasichana 350 na kati ya hao kwenye darasa moja tulikuwa tunafaulu tunakwenda *form five* na *form six*, sasa hivi elimu imeshuka kwetu na tunaendelea kunyooshewa vidole kwamba kila siku Mtwara na Lindi tumekuwa wa mwisho. Mazingira yetu ni mabaya na bado hatuangaliwi kwa jicho la huruma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana upungufu wa miundombinu uliokuwepo Masasi *Girls* kwa sababu ni shule kongwe, vyoo pamoja na uzio sawasawa na Mtwara *Girls*, ni vyema Serikali ikafanyia ukarabati, ikaboresha na shule zile sasa, hatukatai tuwe na kidato cha tano na cha sita, lakini ni vyema ikaanza kidato cha kwanza mpaka kidato cha sita ili watoto wanaotoka kule kama ambavyo tulisoma sisi na wao pia waweze kusoma kwenye mazingira mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Idara ya Ukaguzi, Wabunge wengi wamekuwa wakichangia hapa, lakini niseme, mwaka jana nilichangia hapa kuhusu Idara ya Ukaguzi na Wabunge wengi walichangia na Wizara ilitwambia kwamba ipo kwenye mchakato kuifanya Idara ya Ukaguzi kuwa Mamlaka. Mchakato huu unakwisha lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Halmashauri za Wilaya huko fedha za Ukaguzi haziendi. Wilaya ya Masasi walipokea milioni 2.5 tu kati ya milioni 82, Ruangwa senti ziro ambako pia Naibu Waziri wa Elimu wa TAMISEMI anatoka. Lakini hilo liende sambamba pia na miradi ambayo inagawanywa huko. Kwenye hiki kitabu ile miradi ya ukarabati wa shule, basi hizi rasilimali tunazosema zinagawanywa, basi tugawiwe wananchi wote, tupate.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiki kitabu kwenye shule zitakazokarabatiwa Wilaya ya Masasi ni nne tu, lakini tunasema kwenye zile mbili ambazo TAMISEMI waliziongeza

mbili zinatajwa Masasi ni Chanika Nguo na Namwanga, lakini ndiyo hizo mbili zilikuwepo kwenye mradi uliopita zile kati ya 260 na kwenye hiyo orodha ya sasa hizo mbili nazo pia zipo. Kwa hiyo zinafanya kuwa nne, Wilaya ya Masasi ina Majimbo mawili, lakini kwenye Majimbo mengine na Wilaya nyingine shule zaidi ya 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeshangaa sasa huu utaratibu unapangwa na nani, kwa sababu kama ni Mawaziri, nimeshangaa hata anapotoka Naibu Waziri kule Ruangwa ana shule sita, lakini mbili zilitajwa kwenye awamu ile ya kwanza. Kwa hiyo, kwa ufupi ni kwamba, sasa hivi ana nne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni nani anapanga kama ni watendaji wetu watutendee haki, waangalie Tanzania hii na Mikoa yake yote, siyo kuangalia kwamba Mkoa mwingine unapata shule nyingi na Mikoa mingine inapata shule mbili, haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie tatizo lingine. Tumekuwa tukilalamika hapa kwamba, wapo watoto ambao hawajui kusoma na kuandika kwenye shule zetu. Naomba sana kuishauri Serikali kwamba, mfumo tunaotumia sasa hivi hasa wa mitihani ni vyema ukarekebishwa. Wabunge hapa tumekuwa tukichangia inatusaidia nini kuwapa watoto maswali ya *multiple choice*, mtu ye yote anaweza akafanya, akiwa amefumba macho anafanya mtihani na anafaulu *a hundred percent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo mfumo hatusaidii, wale watoto ambao hawajui kusoma na kuandika, uzoefu mdogo nilioufanya huko tumewapa mtihani bila maswali na wamefaulu. Kwa hiyo, siyo vyema pia kuilaumu Serikali, tufike mahali tutafute chanzo na tutafute dawa tuondoe hilo tatizo. Mfumo wa mitihani yetu bado haututii moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa. Sasa namwita Mheshimiwa Margareth Mkanga, ajiandae Thuwayba Muhamed na Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ambayo ni muhimu sana kwani elimu ni mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na elimu maalum ambayo inashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa aina zote tu ambazo zinafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu maalum hii miaka ya hivi karibuni ililetwa zana au kuna zana inayoitwa elimu jumuishi kwamba, watoto hawa wasomeshwe katika madarasa na maeneo ambayo na wenzao wengine ambao sio wenye ulemavu wawepo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na dhana hii, lakini ningeomba kwa sababu ni miaka miwili, mitatu, minne iliyopita ifanyiwe tathmini ili tuone kama dhana hii kweli inatusaidia. Nasema hivyo kwa nini? Kwa mfano, kwa watoto viziwi, wanapokwenda maeneo ya sekondari, hali inakuwa mbaya zaidi, afadhali shule za msingi ambapo Walimu wa lugha ya alama wanakuwepo, lakini katika /eve/ya sekondari hawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kwamba Kamishna wa Elimu anachagua wangapi kwenda sekondari, lakini *performance* yao mwishoni mwa Kidato cha Nne, inakuwa ni zero au hakuna kati ya wale wanaopata zero kwa sababu hawana Walimu wa kuwawezesha kuelewa masomo ya lugha ya alama. Kwa hiyo naomba iangaliwe hii ili wawe na shule zao maalum, sio kuwabagua lakini kuwatenga wenyewe ili wahudumiwe vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo njia pekee ya kuwawezesha kwa kweli kupata masomo sawasawa na huko nyuma ndivyo iliyokuwa. Tusiige dhana za kutoka nje bila

kuwa na maandalizi ya kutosha, hatuna maandalizi ya kutosha, kwa hiyo hapa badala ya kuwaendeleza, ni sifuri ndizo tunazozitengeneza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru lakini kwa lugha ya alama hiyo hiyo, Wizara imesema kwamba Walimu wataimarishwa na nini. Naomba sio wale tu wanaokwenda kuijendeleza baada ya kuwa Walimu huku kwa kupenda kwao kuwashudumia watoto wenyewe ulemavu, lugha ya alama ifundishwe kwenye vyuo ili hawa Walimu wanapotoka pale wakienda kukumbana na mtoto kiziwi wasibabaike kumsaidia. Tutawapata lini wa kutosha tukitegemea tu kwamba wale wanaojitolea na hawa watoto bado ni wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Wizara imeeleza hapa inajitahidi mwaka hadi mwaka *enrolment* ya kwenda Kidato cha Kwanza ni kubwa, ina maana hata shule za msingi sasa watoto wenyewe ulemavu wanaosoma ni wengi na huu ni mwamko wa wazazi na Serikali kuweza kutoa maelekezo ya kutosha kwamba sasa watoto wengi hawafichwi. Kwa hilo nishukuru, wanakwenda mashulenii, lakini tuwaandalie mazingira mazuri, vinginevyo tunajidanganya tu na watakuwa wanakwenda kukaa, wakanywa uji, wakarudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika hili elimu maalum, ukurasa wa 81, naishukuru sana Serikali imeeleza kwamba itafanya mambo mengi sana mwaka huu. Hiyo imenipa picha kwamba, Kitengo hiki sasa maana yake kina majukumu mengi, kinapanuliwa majukumu mengi tu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara, elimu maalum kuifanya kitengo tu chini ya Kamishna iache. Elimu Maalum iundiwe Idara ili iweze kujipanua kama ambavyo Wizara yenyewe inaipa kazi zingine za ziada hapa, hili nimelisema siku nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kuna tatizo gani, Kitengo kinakuwa ni kijitengotengo tu watu wawili, watatu, wane au watano, hapana! Ifanyeni Idara kusudi ijiiamarishe kwa

sababu hawa watoto wenye ulemavu wa aina zote ni wengi na mambo yao ni maalum na yana gharama na kwa kweli ni mengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiondoka hapo naishukuru Wizara imesema, imenunua mashine ya kutengeneza vitabu vya nukta nundu naipongeza sana. Kwanza ni wafadhili tuwashukuru na Wizara basi imelifanya hilo, lakini ninaloomba vikorombwezo vinavyotakiwa na mashine hiyo viambatanishwe haraka iwezekanavyo. Kuna karatasi maalum, kuna wino maalum yaani sijui kuna nini, sio mradi mashine tu hapo, tusipongeze kuwa na mashine itakayokaa pale miaka na vitabu havitengenezwi kwa sababu *accessories* zake zingine zitakuwa bado hazijatimizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusu *TEA*. *TEA* ni Taasisi ambayo tuliiunda kabisa kisheria, tukaipa madaraka ya kuweza kusaidia taasisi zingine za elimu kutoa misaada na nini. Lakini njia moja ya kupata fedha hawa, muda wote imekuwa ni kuombaomba ufadhili na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sheria iliyoindua *TEA* tuiangalie tena, irekebishwe ili iipe *TEA* mamlaka ya kuwa na vyanzo vingine vya mapato vilivyo vikamilifu ili waweze kufanya kazi zao sawasawa za kusaidia mikopo ya wanafunzi za kusaidia vifaa na mambo kama hayo. Vinginevyo Taasisi hii sasa tutaiona tu kama haina kazi na ruzuku kutoka Serikalini inapungua mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, naomba wameshazungumza wengi posho maalum, posho ya mazingira magumu ya ufundishaji nchini kwa Walimu walioko pembezoni. Hapa naonjeza kwa Walimu wote wanaofundisha watoto wenye ulemavu, wanafanya kazi ya ziada, kumsaidia mtoto ambaye saa zote anatoka mate tu, wanabeba Walimu kumsaidia, sio mzazi tena kule nyumbani. Tena wazazi wengine ndio wanawasukumia kwamba, ehee hebu nenda shulenii angalau Walimu wakanisaidie, wapewe jamani posho ya mazingira maalum wana kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale nasema wanafanya kazi ya Mungu, yaani ya Mungu kabisa ya kujitolea mpaka unawahurumia. Wengine inabidi wachukue visenti vyao kuwarudisha nyumbani kwa nauli, asubuhi kuwafuata, nini hiki? Tuwe na utaratibu maalum kwanza wa kuwapa posho wao na kuhakikisha watoto wanafikajefikaje shulenii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine limekwishazungumzwa ni A, B, C, D, wakati wa mitihani. Hivi kwa nini hapo kidogo tunalegea? Sisi wengi humu hatukusoma katika A, B, C, D, eti kwamba ndio unajibu mitihani. Unapewa swalila insha uelezee sawasawa ukokotoe hesabu sawasawa sio *tick tick*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamjenga mwanasayansi gani kwa *tick tick*. Tunamjenga mwanafasihii gani kwa ku-*tick tick*, tunamjenga Mwanasheria gani kwa ku-*tick tick*, kwa nini tunatega kazi. Sawa walimu ndivyo hivyo, lakini basi na Wizara itoe maelekezo utungaji wa mitihani usiwe wa hobelahobela mno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *multiple choice* naishangaa sana. Mwishoni mwa ufundishaji wangu ilikuja hiyo *multiple choice*, nilikuwa mbishi, nikitoa mawili mengine yote *essays* watu wakune vichwa. Watu wafikiri ili kesho na kesho kutwa waweze kutafakari vitu, sio kupewa tu hivi hivi tu mkononi, kwa hiyo naunga mkono alichosema mwenzangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla naungana mkono na wenzangu. Jamani enzi tulizosoma sisi elimu ilikuwa inaeleweka unatoka asubuhi unakwenda kufanya nini, mitihani itakuwaje na vitu kama hivyo. Si vibaya kurudisha yale mengine mazuri ya wakati ule tukayaingiza kwenye mfumo wa elimu ya sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sera tulioiona juzi jana, izingatie yale mazuri yote ya wakati ule, maadili, usafi, wanafunzi kukaguliwa na nini, yote yale yalikuwa

yanamjenga mtoto, tusije tukawalaumu wanaondoka hawajui kusoma kuandika, hawana tabia nzuri na nini, lakini tunawaandaaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, lakini naomba haya ya elimu maalum yazingatiwe, mengine nimechoka kusema kila mwaka nayasema hayo hayo inachosha sasa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Thuwayba, wajiandae Mheshimiwa Serukamba na Mheshimiwa Kapteni John Komba.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, lakini kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ni msingi wa maendeleo na kila nchi zinazoendelea zilijiwekeza katika elimu na ndiyo maana wakapata wataalam wake na pia wakaweza kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijikite katika Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani, moja katika kazi yake kubwa lifanye kazi zake kwa uadilifu. Linahitajika lifanye kazi hiyo kwa uadilifu pia ndilo linalostahiki kutunga mitihani, ndilo linalostahiki kusahihisha na ndilo linalostahiki kusimamia na sio kuwavunja moyo wanafunzi pamoja na wazazi wao. Nasema hivi kwa sababu, tukiangalia katika *grades* za mitihani hazifanani wala hazioani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue mfano wa somo la lugha na tuna lugha nne hapa Tanzania tunazozifanyia mtihani. Tuna lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu. Lakini ukiangalia uwiano wao sio wa kawaida. Tuchukulie mfano somo la Kiswahili daraja A ni 75, *English* 80, Kifaransa 80, Kiarabu 81, imezidi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika daraja B

Kiswahili 65, Kiingereza 65, Kifaransa 70, Kiarabu 70. Ukienda daraja la C Kiswahili 50, Kiingereza 52, Kifaransa 55, Kiarabu 60. Ukienda katika daraja D Kiswahili 35, Kiingereza 35, Kifaransa 40 na Kiarabu 40, uwiano hapa uko wapi? Nauliza Baraza la Mitihani hapa uwiano uko wapo, ukilitazama somo la Kiarabu limepaa vibaya, sielewi kwa nini likawa linapaa namna hii wakati masomo yote haya ni ya lugha na yote tunayahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Sitta pale anawahitaji Wakalimani wa Kiarabu. Sasa ikiwa nyinyi hapa mnawafelisha watoto watoto hawa wote ni wa Kitanzania, wote wanataka elimu, wote wanataka kujiedeleza, kwa nini Baraza la Mitihani mnafanya vituko kama hivi, nataka kujua sababu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, naitaka Serikali isimamie Baraza kuunda mwongozo wa ufaulu wa wanafunzi na usio badilika badilika. Pili, kuwe na uwiano wa maksim unaofanana kwa masomo yote. (*Makof!*)

Ushauri wangu wa pili, Bodi ya *NECTA* ivunjwe, haitakikani kabisa kuwepo kwa sababu Bodi hii haimsaidii Waziri. Bodi hii ilivyokuwa haimsaidii Waziri inafanya mambo yake kiwenyewe wenyewe tu, haiwezekani mambo kama haya yanatokea, isiende ikamtaarifu Waziri. Wengine wanatoka wanakwenda kusaini tu, wakishakusaini hao wanatoka hawasubiri mikutano wanakwenda zao, ina faida gani Bodi hii kukaa iondoshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije katika *format* za mitihani. *Format* za mithani baadhi ya shule hazipelekwi, baadhi ya shule hazifiki kwa wakati, baadhi ya shule ndizo zinapelekwa. Mwaka jana waliofanya mtihani wamefika mpaka katika *hall* wanafanya mtihani *format* ya Kiarabu hawaijui na hili linatokea kwa upande wa pili wa Kisiwa wa Tanzania, upande wa Zanzibar hazipelekwi kwa wakati kwa nini? Tunataka tulijue suala hili kwa sababu hazipelekwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haitoshi kuna vitabu hivi

vya *literature*, vitabu vya *poem*, vitabu vya *plays*, hasa kwa lugha ya Kiswahili unaweza ukasomesha, ukafika katikati ukaambiwa hiki kitabu sicho, wakati huku umeshawafanya watoto mpaka uhakiki, ushawasomesha kila kitu, unaambiwa kitabu sicho, kwa nini hatuletewi *format* halafu mnasema Wazanzibar wanafeli, Wazanzibar hawafeli bali mnawafelisha. Kwa sababu mtoto huyu huyu wa Kizanzibar akienda nchi za nje ana-prove *wonderkwa* nini Tanzania afeli, hilo haliwezekani kuna jambo na nataka Baraza la Mitihani lituambie. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nije katika Bodi ya Mikopo, Bodi ya Mikopo isifanye kazi zake kwa mazoea. Kwa sababu sasa hivi sio kama zamani kwamba, watoto wote wanaomaliza masomo yao mwezi wa Juni au Julai, Agosti wanaanza tena au Septemba aaha! Sasa hivi unaweza ukamaliza masomo yako especiallywale wanaokwenda nje wanaweza wakamaliza Januari, Februari au Machi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya kwa uthibitisho, kuna mwanafunzi alikuwa anamaliza masomo yake mwezi wa Januari, Januari hii tuliyokuwa nayo 2013. Ameleta barua yake, kwa sheria zilivyo mtoto aliyesoma nchi za nje anatakiwa barua aipeleke kwa muambata wa elimu katika *Embassy*, lakini mtoto huyu ameipeleka toka tarehe 27 Agosti, 2012, barua ninayo hii hapa ushahidi, nitampa Mheshimiwa Waziri. Amelipeleka barua hii kwa muambata wa elimu ili apate fedha yake Januari akimaliza kimasomo arudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hakupelekewa, mtoto huyu ikabidi akae kule mpaka mwezi Aprili, tarehe 17 ndio aliporudi lakini hajapewa fedha kutoka Bodi ya Mikopo, ingawa Bodi ya Mikopo, kuna Mkurugenzi namshukuru sana Mkurugenzi Elias, ambaye tulikuwa tunashughulikia hii *issue*, alimwambia muambata anaitwa Mr. Manongi kule China kwamba, ampe fedha huyu mtoto ili aweze kurudi kuja zake nyumbani, lakini hajafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SMS* tulizokuwa tukiwasiliana

na Mr. Manongi hizi hapa ninazo nitacionesha. Sasa ikiwa tunakwenda namna hii na fedha zinatolewa kwa nini hazipelekwi hizi fedha kwa hawa watoto ili ukifika muda wao wa kurudi, wakarudi. Namwomba Mheshimiwa Waziri afanye safari aende akawaangalie watoto wa watu katika nchi mbalimbali mlikowapeleka, hawa Waambata wana matatizo na huyu wa China ndio mwenye matatizo hasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije nizungumzie kuhusu mambo ya ukaguzi. Idara ya Ukaguzi naomba ipewe mamlaka yake kamili kwa sababu hii ndiyo Idara ambayo inayoweza kuileta juu elimu katika nchi, lakini mkiipuzia haiwezekani elimu ikaja juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu mimi ni mwaliimu, tena *Professionally* na nimefanya kazi hii kwa miaka mingi sana. Jumla ya Wakaguzi tuliokuwa nao mpaka sasa hivi ni 1,160, tunataka kuwaongeza wengine 200, lakini hata hivyo hawatoshi.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Thuwayba na sasa namwita Mheshimiwa Serukamba, wajiandae Mheshimiwa Kapteni John Komba na Mheshimiwa Sara Msafiri.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi. Tatizo la elimu ni kubwa sana. Nitaanza kwa kusema mwaka 1983 Marekani walikuwa na tatizo kubwa sana la elimu, wakaunda Kamati na kuna *famous report* wanaiita "A Nation at Risk".

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Elimu wakati ule alisema maneno yafuatayo, ningeomba niyanukuu kabla sijaendelea na ninachotaka kusema. Anasema: " *Our purpose has been to help define the problems afflicting American education and to provide solutions, not search for scapegoats.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na Waheshimiwa viongozi tutambue tatizo la elimu ni kubwa katika nchi yetu na sidhani kama kuna mtu hapa tunadhani tukimbebesha mzigو huu, totalitatua tatizo la elimu. Tatizo ni letu wote, tatizo ni la sisi viongozi, tatizo ni la wazazi, tatizo ni la wananchi, tatizo ni la wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana la msingi, tatizo ijullikane tulifanyie kazi kwa pamoja, lakini na viongozi wafanye wajibu wao katika kutekeleza wajibu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamerikani kwa nini waliamua kuunda ile Tume ni kwa sababu walikuwa wanaona *position* yao katika elimu duniani inapungua. Kwa hiyo na sisi tunasema, tumegundua tumepata matatizo makubwa watoto wetu wamefeli, njia tunazotumia sioni kama tunatatua tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunda Tume nashukuru sana, lakini Tume hii tuweke watu ambao tuna uhakika nao, watu ambao wana *credibility* kwenye *society* yetu, watu ambao wanajua maana ya elimu, tusiweke watu ambao wako hapa kwa sababu ya matumbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeunda Tume nzuri na nitasema mtu mmoja, kwenye Tume ile kuna mtu anaitwa Profesa Mchome. Profesa Mchome huyu ameshiriki kwenye vikao vya kuongeza kutengeneza *standard* mpya za mitihani. Ameshiriki kwenye kikao, jambo jema. Matokeo yamekuja

mabaya huyu huyu anakwenda Serikalini kusema, unajua watu wamefeli sana kwa sababu tulibadilisha *standardization, what kind of a person.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijailaumu Serikali kupandisha *standards*, ndio dunia tunayokwenda, lakini kwa nini hatuwezi ku-*take responsibility* ya maamuzi yetu. Watoto wamefeli ni tatizo la elimu nchini, ni wakati umefika kama Serikali, tukae tujiulize hali yetu ikoje. Tusipojiangalia iko wasiwasi tutazalisha jambo la ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yuko mwanafalsafa mmoja alisema: "*We raising a new generation of American that is scientifically and technologically illiterate.*" Tusipokuwa waangalifu tunaua *generation* hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani wakati muafaka tukae na hiyo Tume ifanye kazi sio ya kwenda kuangalia matokeo, matokeo yale hata ungeyafuta kama matatizo bado yapo, ukawatungia mtihani rahisi kuliko wote bado watu wangelifeli. Habari ya kulaumu *NECTA* hapa, tunalaumu *NECTA* kwa sababu gani.

Jamani sijui kama mnajua pale *NECTA*, Mwenyekiti wa Bodii Professa Mkandala ambaye anaheshimika duniani. Katibu wa *NECTA* ni Mama, ni Daktari ambaye hata viwango vyake vya ufaulu duniani bado hatujavifikia. *University* amepata *first class*, amekwenda *Ph.D* amepata *first class* leo tunakaa tunam-doubt. Hii *Society* gani hii, nakubali matatizo yapo lakini nasema matatizo lazima tuyatatue na hatuwezi kuyatatua kwa kulaumiana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo elimu yetu kuna nini, Wizara ya Elimu inashughulikia elimu, TAMISEMI inashughulikia elimu, nani mwenye *authority* haya? Angalia matatizo ya elimu, kuna matatizo ya vitabu, maabara, madarasa tuhangaike na haya.

**MBUNGE FULANI:** Kweli!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Tuangalie tatizo la Walimu, haki zao tunawalipa vizuri, mishahara yao wanapata vizuri, stahiki zao wanapata vizuri, wanakaa maeneo mazuri, tuyaangalie yote haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia vyuoni tunaandaje Walimu wetu? Ukienda Singapore ambayo inasifika duniani kwa maendeleo makubwa, anayepata *division one* ndiye anakwenda kwenye Ualimu. Sisi leo wanaopata *division four* ndiyo tunawapeleka kwenye Ualimu. Yote haya tujilize vizuri lakini hatuwezi kwa sababu hatujajiandaa kuwalipa Walimu vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema kama Taifa umefika wakati tumemaliza miaka 50, tukae chini na mimi nasema ile Tume iliyoundwa wala sioni kama inaweza ikatusaidia sana. Tutafute Tume ya watu wazuri, wasomi wa ndani na nje ya nchi yetu, tuwatengenezee *term of references* nzuri, wauangalie upya mfumo wetu wa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuangalie bajeti ya elimu ikoje. Mwaka jana pesa walizoomba hawakupewa, inawezekana mwaka huu wakaomba na wasipewe zote. Matokeo yakitoka tunatafuta mtu wa kumtupia lawama? Haiwezekani! Kama ni suala la *standardization* imekuwa hivyo miaka yote toka tunasoma sisi *standardization* zilikuwepo. Nachotaka kusema, hali ya elimu ni tete, lazima tukae kama Taifa tuache kulaumiana, tutafute majawabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuangalie hali ya vyuo vikuu vyetu. Hatuwapi pesa za kutosha, hawawezi kufanya

*research* za kutosha, hawa mnataka wa-produce watu wazuri. Tujiulize swali moja. Leo iko *crisis*, angalia wanaomaliza vyuo vikuu wote tunajua *product* inayotoka, tunahakika wanaajirika, wameelimika vyta kutosha? Yote haya inatakiwa hiyo Tume ianzie *kindergarten* mpaka *university* ituambie karne ijayo tunaendaje kwenye elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaosoma *Masters* watanisamehe, wanaosoma *Masters* Tanzania kwenye *universities* zetu, asilimia 70 wanaandikiwa *Thesis*.

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Hawa ndio wasomi wetu. Hata kama hatutaki kuusikia ukweli huu. Kwa hiyo, nasema tatizo la elimu ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekani wakati ule wanahangaika na hili suala la elimu, walifika sehemu wakawa wanaenda kuuliza wale wanafunzi waliomaliza *university* hebu jamani nyie mliowaajiri hawa mnasemaje? Wengine wanakutwa hawawezi, hawana *capacity* ya kufikiri vizuri, ya kusoma *fast* kwenye *computation*, yote hawana. Nasema tufanye maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni suala la lugha. Naomba sasa tuamue tunaenda kwenye lugha gani? Kama ni Kiswahili tukubaliane twende kwenye Kiswahili lakini mkiniliza mimi, mimi siamini kwa dunia tunayokwenda ili tuweze kuwa *competitive* na tuweze kushindana duniani, hatuwezi kuepuka Kiingereza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo Mwanafalsafa mmoja alisema miaka thelathini ijayo China ingeweza kuwashinda Marekani lakini anasema jambo moja kubwa litakalowafanya wasiwashinde Marekani ndani ya miaka thelathini ijayo ni lugha. Lazima wafanye Kiingereza kama lugha ya kwanza. Mimi nasema tuamue kwenye suala la lugha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuamue kwenye suala la hesabu. Hapa tunaangalia na kujuliza maswali. Hivi nani ameuliza matokeo ya hesabu yalikuwaje? Asilimia 59 ya watoto waliofanya mtihani wamepata zero kwenye hesabu. Tatizo ni kubwa, tuache siasa ...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Kapt. Komba, Mheshimiwa Sara Msafiri na Mheshimiwa Kibona wajlandae.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nichangie hotuba ya Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sijui kama wale wa Nyasa wanansikia kule maana hawana redio, lakini wataambibi kwamba nimesemasema maneno hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze ku-*react* na hotuba hii ya Kambi ya Upinzani ya CHADEMA. Inatulaumu, inajifanya inasikitika, ni kama vile machozi ya simba yanataka kumtafuta mtu. Hivi jamani kweli anayefanya vijana hawa wanaonekana hawasomi, wako mitaani, wanakuwa na elimu ndogo ni CCM au CHADEMA?

**MBUNGE FULANI:** CHADEMA.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Kila wakati CHADEMA wanatumia wanachuo kuandamana mitaani, barabarani, wanatumia wamachinga kuandamana barabarani, leo mnazungumza elimu inashuka, haya ndiyo yanafanya elimu ishuke. Acheni watoto wasome lakini kila siku mnaandamana mnatumia vyuo vikuu, mnachukuwa sekondari,

mnaandamana mnachukua wamachinga, hii elimu itakwendaje jamani? Halafu mnasema jamani CCM mmeshindwa tuchukueni sisi. Kumbe lengo lenu ni madaraka, sio kuzungumzia elimu hapa. Hawa jamaa wanakisebusebu na kiroho papo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi muwakane, sisi kwetu tumewakana...

**MBUNGE FULANI:** Unataka Uwaziri wewe.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Sisi kwetu tumewakana kwa sababu kampeni za Udiwani zinafanyika sisi kule Mbinga tumekataa, tumeпита peke yetu, CHADEMA tumewakataa, kwa hiyo na nyie muwakatae kwa sababu lengo lao ni kutawala si maendeleo ya nchi hii. Mimi sitaki Uwaziri nakwambia kitu cha ukweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye upande wa elimu. Mimi nimesoma zamani na zamani ulikuwa huwezi kwenda *primary school* mpaka uende shule ile ya awali ujifunze kuandika, kusoma na kuhesabu zile KKK ndiyo uingie darasa la kwanza, siku hizi hakuna. Kwa hiyo, nafikiri ule utaratibu wa zamani ni mzuri naomba Mheshimiwa Waziri mrudie utaratibu ule ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuangalie, maana sasa hivi tunamlamu Waziri kwamba elimu imeshuka, sijui nini imeshuka lakini mtu hawezi kutumikia mabwana wawili. Huyohuyo awe chini ya Wizara ya Elimu, huyohuyo awe Wizara ya TAMISEMI, haiwezekani elimu ikapanda, turekebishe, turudishe Elimu na mambo yake na TAMISEMI na mambo yake ndipo tutakwenda. Kujikwaa sio kuanguka. Turudi, tuangalie tumejikwaa wapi twende tukaanzie pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni elimu Nyasa. Nimeona kuna shule zimeorodheshwa kwamba zinakarabatiwa au zitatengenezwa lakini kwa mfano kule Nyasa shule zile ziko upande wa Wilaya ya Mbinga. Sasa hela

zikienda Wilaya Mbinga, hivi ni kweli zile hela zitakuja Nyasa ili shule zitengenezwe? Nina wasiwasi zitazama Mbinga,haziendi Nyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia vilevile kwa mtani wangu Magufuli, yeye Wilaya yake ni Chato lakini pesa zinapelekwa Mkoa wa Kagera. Naomba sana hawa waliofanya utaratibu huu, pengine walifikiri ni zamani, tuache kufanya kazi kwa mazoea. Sasa hivi Chato iko Mkoa wa Geita, Nyasa iko peke yake inajitegemea na Wilaya ya Mbinga inabaki peke yake. Kwa hiyo, rekebisheni makosa haya, hela mtapeleka Mbinga hazitakwenda Nyasa, hela mtapeleka Kagera hazitakwenda Chato. Hapa namsemea Waziri ambaye hayupo lakini kwa kweli nimesoma kwenye hilo kabrasha. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Hela ya Kondoia inakwenda Chemba?

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu upande wa Wilaya yetu pia, sisi Nyasa hatuna *high school* hata moja. Kwa hiyo, naomba, ziko shule ambazo naifikiri ni vizuri watu wakaacha kukaa maofisi wakatembelea maeneo haya. Tuna shule ya St. Paul, tuna shule inaitwa Lundo, tuna shule inaitwa Kingerikiti, hizi shule tungependa zipandishwe hadhi zikawa katika hadhi ya kuwa *high school* badala ya kuwa sekondari na zinakidhi matakwa yote. Naomba maofisa wa Wizara waende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni ukaguzi, wenzangu wengi wamesema, ni kweli, zamani Idara ya Ukaguzi ilikuwa inaogopwa kuliko *DEO* mwenyewe au *REO* mwenyewe. Akafika Mkaguzi pale Mwalimu anatetemeka na anafanya kazi, anaanda mitaala yake, anaanda *lesson notes* vizuri kwa sababu anakaguliwa. Siku hizi hakuna, wanapuuzwa watu hawa. Naomba sana tukitaka kuirudisha elimu, tuimarishe Idara ya Ukaguzi ama sivyo tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Walimu. Hawa Walimu tutawaonea bure, ooh hawapendi nini, jamani mimi niseme, elimu ni zaidi ya CCM, ni zaidi ya CHADEMA, ni zaidi ya *CUF*, ni zaidi ya NCCR- Mageuzi, achana na hii habari, elimu tuifanye ni tunu ya Taifa, ni zaidi ya kila kitu. Tusizungumzie CHADEMA hapa, tusizungumzie CCM, tuzungumzie Taifa hili bila elimu ni zero. Kwa hiyo, ninaomba sana Walimu wapewe mahitaji yao, wanafunzi wapewe haki zao, wafanyakazi wa elimu wapewe haki zao, ndipo tutawenza kusukuma Taifa hili kwenda mbele. Hakuna cha UCHADEMA hapa, hakuna cha UCCM hapa, tunazungumzia elimu kwa Taifa la Tanzania, hakuna taifa la CCM wala CHADEMA. (*Makof!*)

**MBUNGE FULANI:** Ila Serikali ni ya CCM.

**MHE. KAPT. JOHN D. KOMBA:** Ila Serikali ni ya CCM. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba sana, mtakapo-*windup* naomba mtusaidie kule Nyasa tupate vyuo vya ufundi. Hatuna chuo hata kimoja, hata chuo cha kuvua samaki hakuna. Kwa hiyo, naomba tuleteeni kule chuo cha ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, namshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa ambaye alitufanyia *fund raising* ya kujenga angalau shule ya wanawake kule Nyasa. Tunakushukuru sana na zile hela tulizozipata tutaelekeza huko na naomba Waziri, Naibu Waziri mtuambie shule hiyo mtaisajili lini ili mwakani tuanze kuwaelemisha watoto wa kike kuanzia *form one* na kuendelea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache, naomba niunge mkono hoja sio mia kwa mia lakini mrekebishe haya. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba kuwatambua Walimu kutoka Kibaha Vijijini, wageni wa Mheshimiwa Abuu Jumaa. Karibuni sana Dodoma.

Sasa namwita Mheshiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Kibona ajiandae.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi ili kuweza kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa, naomba niseme kwamba bajeti iliyotengwa kwenye Wizara ya Elimu, ni ndogo sana. Mahitaji ya Wizara hii ni makubwa, Taifa haliwezi kuendelea kama hakutakuwa na wataalam wa kilimo, kama hakutakuwa na wataalam wa utafiti, kama hakutakuwa na wataalam wa habari na wanasayansi na wataalam wengine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani? Mwaka jana Wizara ya Elimu ilitengewa bajeti ya maendeleo shilingi bilioni 92.5/= . Ni asilimia 44 tu ya pesa ndiyo iliyotoka. Mwaka huu kutoka bajeti ya shillingi bilioni 92.5, Wizara imetengewa shilingi bilioni 72/= pungufu ya shilingi bilioni 20/= . Tunaenda wapi, mbona tunarudi nyuma? Changamoto ndiyo kama hivi tuyvoziona, Wabunge wenzangu wameongea. Ninaomba sana Serikali yangu itazame upya, iongeze pesa kwenye Wizara ya Elimu. Elimu ndiyo kila kitu, elimu ndiyo urithi pekee wa mtoto wa kike na mtoto wa maskini. Ninaomba sana Serikali yangu itazame upya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee Idara ya Ukaguzi. Malalamiko mengi sana ya Walimu na madai mengi sana ya kushuka kwa elimu mengine hayasababishwi na upungufu wa fedha, kunahitaji tu Wakaguzi wapite, wafanye *supervision* kwa Walimu, waangalie madarasa na waangalie hali ya elimu lakini Idara ya Ukaguzi imesahaulika kila mwaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema hivi kwa sababu gani? Mwaka 1982, Wizara ya Elimu iligatua majukumu yake ikazipa Halmashauri jukumu la kusimamia elimu ya msingi. Mwaka 2009, Wizara ya Elimu ikagatua majukumu yake ikawapa Halmashauri na fedha zote hizi unazoziona tunazopitisha hapa, hazibaki Wizara ya Elimu

zinaenda kwenye Halmashauri. Mwaka jana *almost* shilingi bilioni tatu zimekwenda kwenye Halmashauri. Hata hiki kitendawili cha kushuka kwa elimu, mimi nasema ukitazama vizuri, Wizara ya Elimu haina jukumu lolote hapa la kuwajibika kwa sababu Halmashauri ndiyo zinasimamia masuala ya elimu, Wakurugenzi ndiyo wanajukumu la kusimamia elimu ya shule ya msingi na sekondari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi haina ofisi, bado ofisi zao ziko chini ya Halmashauri zilezile. Walimu wanalalamika kutolipwa mishahara yao, wanalalamika kutokupandishwa vyeo na wanalalamikia Wakurugenzi wa Halmashauri. Sasa mimi niulize swalii, utawala bora uko wapi? Mtu amekupa fadhila ya chumba chake, leo utamwajibisha vipi anapokulalamikia kwamba Walimu hawapandishwi vyeo, wamekatwa mishahara yao, hawakupewa sababu yoyote na hiki Kitengo kimefadhilliwa pale chini ya Halmashauri kimepewa chumba, huyu mtu wa Idara ya Ukaguzi atamwajibisha vipi Mkurugenzi? Mimi ninaona hapa kwa kweli kuna haja ya kuangalia muundo mpya wa Wizara na majukumu yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wameongea sana, lakini mimi naomba nikazie. TAMISEMI ina majukumu mengi. TAMISEMI ishughulikie masuala ya malambo, masuala ya majosho bado ije tena ishughulikie Walimu, hii inakuja kweli? Hii taasisi imekuwa kubwa, tunasema hii *organization inahitaji restructuring*, tutakuwa tunalaumu watu. Asilimia 60 ya watumishi wa umma ni Walimu, sasa unawapelekaje TAMISEMI? Lazima kuwe na chombo kinachosimamia Walimu na shughuli zake na *hierarchy ijulikane* mpaka tufike kwenye Baraza la Mitihani mpaka kutangaza matokeo lakini tukienda kwa mfumo huu hakuna wa kumwajibisha mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwenye ukubwa wa Wizara. Tangu tulivyopata uhuru na nimepata takwimu kidogo hapa, mwaka 1961 wanafunzi wa shule za msingi walikuwa 486,000, mwaka 2001 walikuwa 4,875, mwaka 2012 ni 8,247, hiyo ni kwa shule za msingi tu. Shule za sekondari

mwaka 1961 walikuwa wanafunzi 11,832, mwaka 2012 wanafunzi wa shule za sekondari ni 1,884,277 yaani hii *organization* imeshakuwa kubwa na majukumu yake ni mengi, tukiacha TAMISEMI waingize mikono, Wizara ya Elimu iingize mikono kidogo, tutashindwa kusimamia majukumu mazima ya elimu. Kwa hiyo, niombe sana Serikali yangu hebu itazame upya mfumo mzima wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye rasimu tuliyopewa hapa ya kuchunguza kushuka kwa matokeo ya elimu, utaona kuna changamoto zingine ni vitu vidogo sana na wala havihitaji hela. Wanasema kushuka kwa elimu ni kwa sababu ya upungufu wa madawati. Mimi najiuliza swali, tuwe wazalendo, tuna misitu, tuna magogo, tuna miti, tunavuna tunauza, hawa watoto watacaa chini mpaka lini? Tuazimie hapa, hili suala hallhitaji pesa nyingi, magogo ni yetu, kama ni utunzaji wa mazingira ni jukumu letu, kwa nini tusivune haya magogo sasa tutengeneze madawati ya kutosha, tuondoe utaratibu wa wanafunzi kukaa chini ili kupandisha kiwango cha elimu. Hili suala halina haja ya kuundiwa Tume. Ni suala ambalo liko wazi, watoto wamekuja pale wanakaa chini, ataandikaje sasa na tunaambiwa ni miaka mitatu sijui miaka kumi na nne mtoto ndiyo anakuwa na upeo wa ku-grasp mambo. Sasa kama amekaa chini miaka kumi na nne yote, atawezaje ku-perform? Naiomba Serikali sasa, hili suala la madawati tumelichoka, tunaomba sasa kila shule kabla haijanza kufanya kazi mwanafunzi na dawati lake, miti ikakatwe, wapewe mafundi selemara watengeneze madawati wanafunzi wakae kwenye madawati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu madai ya Walimu. Mimi najiuliza na TAMISEMI naomba watusaidie maana ndiyo wanashughulika na shule za msingi na sekondari, Walimu wanakaa vijijini wanafundisha kutoka kituo chake cha kazi mpaka anakofuata mshahara, anatumia zaidi ya Sh.20,000/-. Kuna huduma za *M-Pesa* na Tigo Pesa, watu wamesajili namba zao za simu, kwa nini msiwalipe mishahara kutumia *M-Pesa*, kwa nini

mnawalazimisha watu waje mjini kuchukua mishahara yao, kwa nini msikae na taasisi hizi za simu mkaona namna ya kuwasaidia?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Msafiri.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Msafiri, namwita Mheshimiwa Kibona, ajiandae Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye busara wakiwa wanasafiri kwenye gari, basi na chombo chochote, gari lao likikwama hawaanzi kulaumiana kwamba nani kabeba nini, wewe umebeba kilo ngapi, lakini watu wenye busara wanasukuma kile chombo kitoke kwenye matope na safari iweze kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafananisha hapa tulipofika na gari liliokwama. Tumekwama kwa upande wa elimu, kama Taifa tumekwama. Nianze na mfumo wetu wa elimu. Naomba niseme kwa ujumla kwamba hali ni mbaya, tulishasema wakati ule, alikuwepo ndugu yetu mmoja mionganoni mwetu mwaka juzi alisema kwamba jamani ndugu zangu TAMISEMI ina mzigo, lakini naona yule mtu hakusikilizwa. Nami narudia tena kwamba TAMISEMI imeelemewa na mzigo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo yapo kwenye elimu, watu wanakurupuka wanasema fulani ajuzulu, fulani afukuzwe, ndugu zangu sivyo, tutafute njia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mgumu sana kusema kama alivyosema fulani. Kwa mara ya kwanza leo nasema kama alivyosema Mheshimiwa Serukamba mdogo wangu, nami naungana naye kwamba tutafute utaratibu sasa, iundwe Tume safi, sasa sijui nani ataiunda, lakini najua mionganoni mwetu wapo watu. Mungu hajatunyima watu, wapo watu wenye busara, tuunde Tume, waangalie suala zima la elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kule kwangu lleje nilitembelea shule moja Mwalimu anasema leo hatusomi, leo watoto hawasomi kwa sababu hamna chaki, anasema ameuza kuku wake kwa ajili ya kununua chaki amemaliza kuku wake mpaka aongee na mke wake anunue chaki. Chaki hiyo inanunuliwa na Halmashauri, Halmashauri ipo TAMISEMI, watoto hawajasoma shule na hawajahudhuria madarasani, matokeo yamekuja mabaya anashikwa shati Mulugo, anashikwa shati Kawambwa, kwa nini lakini kitendawili kidogo hiki tusikione? Naungana na wenzangu tuliangalie jambo hili, nami kwa kweli nitashangaa iwapo mwakani tutakuja tena hamna mabadiliko katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mitihani. Ni jambo la kusikitisha. Pale Wizarani, mimi nashindwa kuelewa, mimi siyo Mwalimu lakini wote tumeshuhudia watoto wanafanya mitihani kwa kuchagua, wanaenda sekondari. Safari iliopita nilikuwa nasafiri kwenye gari moja nikasikia kuna mahali mtu mwenye upungufu wa akili (taahirah) ameenda shule ya sekondari tena ya vipaji maalum. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hata mimi ukiniliza swali kwa Kichina lakini ukaniambia ni-*tick*, ninaweza kufumba macho nika-*tick* na katika kumi huenda nikapata saba.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mambo haya ninashauri Serikali iangalie upya, Madaktari wetu pale Wizarani wayaangalie upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo usemi unaosema haki huinua Taifa na dhambi ni laana kwa wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhambi ninayoiona katika nchi hii, ni upendeleo. Tumefika mahali pabaya. Ninacho kitabu alichotugawia leo Mheshimiwa Waziri, pesa imepatikana, pesa ya Watanzania igawanywe kwenye shule mbalimbali ili zifanyiwe ukarabati. Kule katika Wilaya ya Ileje tumpata shule Nne, Wilaya zingine shule 25 zinakarabatiwa, hii ni dhambi. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Monduli shule mbili.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaambiwa kwa jirani yangu, Mzee wangu hapa Mheshimiwa Lowassa shule mbili.

**MBUNGE FULANI:** Kilimanjaro?

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Naomba Wabunge tuungane, kuna mdudu mbaya yupo pale Wizarani na inawezekana haya matokeo mabaya ni mkakati maalum.

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaah!

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Haiwezekani Wilaya moja ipewe pesa kukarabati shule 25, shule 22 na Wilaya nyingine ipewe shule mbili na Wilaya ya Ileje ipewe shule tatu, nnne, haiwezekani! Tumeshaliona hilo, tutafuatilia, naomba tuungane kwa pamoja ili haki iweze kutendeka. Waziri na Naibu Waziri wako ninawapeni pole, tunahisi mnahujumiwa kwa hiki ninachokisema, maana huku si kukosea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishasema kipindi kilichopita juu ya matokeo ya mtihani wa kidato cha nne, tuliwapa pole wazazi, kwa yaliyotokea. Safari hii nasimama kuipongeza Serikali kwa sababu safari ile nilisema kwamba tusije na majibu rahisi, Tume iundwe na ituambie tatizo hasa

ni nini. Serikali yetu imekuja na majibu, tunashukuru kwamba walau kilichofanyika ndicho tulichokuwa tunalia, lakini Tume itakayoundwa, hii tunayoshauri sasa, ije na majibu sahihi kuliko haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana Serikali yangu ya CCM kwamba sasa kule lleje naambiwa shule mbili ambazo zinatarajiwa moja kuwa *high school*, shule ya sekondari ya Kafule, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu, wananchi wa kule hawana shule hata moja ya *high school*, macho yapo shule ya sekondari ya Kafule, mtakapokuwa mnateua, mtakapokuwa mnapita kwa shule zingine, naomba msitupite na sisi kule lleje, mtukumbuke shule ya sekondari ya Kafule iweze kuwa kidato cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, niwape nafasi wenzangu waweze kuchangia katika mjadala uliopo mbele yetu, naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu, ahsante sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, Mheshimiwa Selasini na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie katika mjadala unaoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi simfahamu Mama Ndalichako, wala simfahamu Profesa Mkandala lakini ninafuatilia kwa karibu sana kazi zao. Kutohana na jinsi mambo haya yanavyokwenda, nimelazimika kwenda kutafuta ziada ya ninavyowafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa tu ni kwamba Mama Ndalichako alikuwa Mwanafunzi bora Canada wakati akifanya PhD. yake ya mambo ya *standardization*. Kazi anazofanya Profesa Mkandala kila mmoja anazijua. Nimesikia watu wakisema wajiu zulu, mimi nataka niwaambie wasijiuzulu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niwaambie wasijiuzulu kwa sababu Wabunge tumekuwa na mazoea ya kuchanganya utalaam na siasa na kwa kiasi kikubwa tumeharibu nchi hii kwa sababu ya kuchanganya utalaam na siasa. Ndiyo maana mipango mingi ya maendeleo ambayo watalaam wetu wanatushauri inafeli katika nchi yetu lakini ikienda nchi za jirani inafanikiwa na wenzetu wanapata maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1973, Baraza la Mitihani halijawahi kubadilisha mfumo wake wa kupima matokeo ya wanafunzi. Kama mnavyojua mifumo iko miwili, *flexible* na *fixed*. Baraza lilikuwa linatumia *fixed* mpaka mwaka 2010 wanafunzi wa kidato cha nne walipofanya vibaya ikaundwa Tume, Tume ile ikaleta ushauri badala ya kutumia huu mfumo *flexible grade ranges* wakaamua kutumia huu wa *fixed* ambao haubagui *Bible Knowledge* wala *Islamic Knowledge*. Naona tunataka kufanya hoja ya watoto wetu kufanya vibaya katika *Islamic Knowledge* na *Bible Knowledge* kuwa jambo la msingi na muhimu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishangaa Serikali, ninyi Wazee mlio mbele yetu nawashangaa, Katiba ya nchi inasema kwamba suala la dini ni suala binafsi la mtu na Serikali haina dini na wala haipaswi kuingiza dini katika utaratibu wake wa uendeshaji. Nchi hii ina Wakristo, ina Waislamu na ina wapagani. Mimi nashauri, kama *Bible Knowledge* na *Islamic Knowledge* ni matatizo, Serikali mmeshaambiwa na Katiba fanyeni kazi zenu, acheni kujihuisha na mambo ya dini. Anayetaka mtoto wake atahiniwe kwa *Bible Knowledge* ampeleke seminari, hata mimi nilitahiniwa huko Seminari *Bible Knowledge*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayetaka mtoto wake atahiniwe *Islamic Knowledge* ampeleke *Islamic Seminary*. Kwa taarifa yenu hata kama mtoto wangu angefaulu akapata 'A' katika *Bible Knowledge* haimsaidii kwa namna yoyote katika matokeo yake kwenda *form five* au kwenda kokote. Kwa nini tumtese Mama Ndlichako kwa sababu ya

*Bible Knowledge na Islamic Knowledge, kwa nini tumtese Profesa Mkandara kwa sababu ya Bible Knowledge na Islamic Knowledge? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkumbuke kwamba bajeti hii inachangiwa na Watanzania wote hata wapagani wanaichangia, hata Mahindu wanaichangia na wengine wanaichangia, kwa nini sisi Wakristo na Waislamu tung'ang'ane tu na *Bible Knowledge* na *Islamic Knowledge*. Mheshimiwa Waziri na Serikali fanyeni uamuzi masomo haya yashughulikiwe na dini husika basi, biashara imekwisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisema hilo, naomba nzungumzie baadhi ya matatizo ya elimu katika nchi yetu, mengi yamezungumzwa, matatizo ya Walimu yamezungumzwa naunga mkono na lazima yashughulikiwe, matatizo ya Wakaguzi wamezungumzwa yashughulikiwe, lakini ambalo napenda nzungumze leo hii ni mmomonyoko wa maadili katika Taifa letu. Mmomonyoko wa maadili ambao hata unashuhudiwa na kupigwa debe na sisi Viongozi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia mchangiaji mmoja rafiki yangu na Mkwe wangu Kapt., Mstaafu wa Jeshi, akisema CHADEMA wanakisebusebu na kiroho papo kwa sababu ya maandamano, lakini akasahau maandamano ya CCM yanaitwa matembezi ya mshikamano, sasa hilo sitaki kulizungumza na sitaki kuingia kwa undani zaidi. (Makofi/ Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mzungumzaji Mkwe wangu Kapt. Komba anasahau ana wimbo unasema, Wapinzani tuwakamate, tuwachanechane, tuwatupe. Anafundisha Taifa letu na watoto wetu na sisi tunapiga makofi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hilo tu, ana wimbo unaoimbwa ‘Watanzaniaa, Watanzania Mwapendeza’.

*(Mheshimiwa Mbunge aliimba  
wimbo anaouzungumzia)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendeza wakati hatuna elimu, tunapendeza wakati hatuna maji, tunapendeza wakati tuna shida lukuki. Kwa hiyo, tuangalie ni nini tunawafundisha watoto wetu au kwa njia ya nyimbo au kwa njia ya vitabu na vinginevyo. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, lingine ambalo linasababisha matatizo katika elimu yetu ni utawala wa shule zetu. Mimi nina tatizo katika Jimbo langu na namwomba Waziri pamoja na wenzake wanaisaidie katika tatizo hili. Pale Jimboni kwangu kuna Kaimu Afisa Elimu anaitwa Adelina Kwayu. Huyu mama ukweli ni kwamba anawakera sana Walimu na wengi amewakatisha tamaa sana, wakienda kwake kwa ajili ya matatizo yao ni lugha chafu pamoja na kejeli. Wakitaka matatizo yao yashughulikiwe yeye mwenyewe wakati mwengine anapoteza mafaili yao au anapoteza *document* zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu mama alikuwa na matatizo Moshi Vijiji, Waziri Mkuu 2010 akapokea malalamiko yake, sasa malalamiko yale yamehamishwa kutoka Moshi Vijiji yameletwa Rombo. Naomba mnisaidie kushughulikia hilo kwa sababu Walimu wamekata tamaa na Waziri nilikuambia, kila Walimu wapya wanaporipoti Rombo, inachukua miezi mitatu katika mateso bila posho, bila nini, mpaka wanapopata posho zao ni kwa sababu ya Watendaji kama hawa. Kuna Walimu tangu mwaka 2005 hadi sasa hawajapanda madaraja, wanakaa katika mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na suala la nidhamu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini nakushukuru ni kengele ya pili.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nimwita Mheshimiwa Yahya Issa Kassim na Mheshimiwa Rweikiza ajiandae.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja hii lakini pia kuna kila sababu ya kuwapongeza viongozi wetu Waziri wa Elimu na Naibu Waziri wake kutokana na kazi wanazozifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, chungu hakiwezi kuiva ila yapatikane mafya matatu. Katika mafya hayo lazima katika kutoa elimu kwa watoto wetu mzee ni lazima ashiriki, mtoto mwenyewe lakini na Mwalimu. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wenyewe tuangalie ni namna gani watoto wetu tunawaenzi katika kutafuta elimu. Namna gani wazee tunafuatilia watoto wetu kuhakikisha kwamba wanapata elimu bora. Ukiangalia kwa muda huu suala hili limepotea, mzee hamjui mtoto, mzee hajui ni wakati gani mtoto wake anarudi shule, wakati gani anakwenda shule wala hana taarifa naye. Kwa hivyo, hapo tusitegemee kuweza kufanikisha katika suala la elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hili ambalo tunalizungumza kuhusu shughuli zetu za mtihani na mara nydingi tunamlaumu Waziri, Waziri hana matatizo, tumesema kwamba kuna Kamati ya Mitihani, kuna Kamati ya Kutunuku na tunasema kwamba kuna Bodi ya Baraza. Hawa ndiyo kwa

kweli wanaoshughulika na hiki ndiyo chombo cha mwisho cha kutangaza matokeo, Waziri hawezi kuyaingilia kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, siyo suala ambalo leo unashimama hapa unasema sijui Waziri awe hivi, halafu unasema kwamba Waziri hana makosa lakini ajiuzulu, maana yake nini? Wewe huna makosa halafu ukashtakiwe? Kwa hivyo, ninahisi kuna mambo kwa kweli si busara kuweza kuyazungumza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo jingine jamani ni kuwa taaluma ya dini ya aina yoyote, ndiyo kichocheo cha mtoto kuweza kufanikisha mambo yake. Kama huna taaluma ya dini ya aina yoyote mimi nasema wewe siyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taaluma ya dini ya aina yoyote ndiyo inayomfunza maadili mema. Leo ninashangaa mtu anasema kwamba suala hili si lazima, masuala haya tuna wajibu ya kuyaendeleza kwa nguvu zote, ikiwa dini ya Kiislamu ikiwa ya Kikristo, tuna kila njia na utaalam tunauona kwamba watu wanafanya hivi siyo kwamba kwa mambo ya Kiingereza tu au lugha, siyo kwa mambo hayo, mpaka kwa upande wa dini na haya ndiyo yanayofanikisha katika taratibu zetu. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Kweli kabisa.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu anakuja hapa kiongozi anasema labda akasome seminari labda akasomee wapi, kweli tuna akili sisi? Tunasema bado tuna haja ya dini kuendelezwa, tena kwa hali yoyote. Kuendeleza dini tunawafunza watoto wetu maadili mema. Hawezi kuwa mtoto na maadili mema wakati hana taaluma yoyote ya dini, hawezi kabisa. Tena suala hili likemewe kwa nguvu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa kuna haja vilevile kwa upande mwingine suala hili kulikazania zaidi. Muundo uliofanzika si muundo sahihi. Mimi binafsi walikuja watoto kwa habari hii ya dini kusikitika kwamba muundo uliotumika si

muundo barabara, ikiwa tunasema mambo ya lugha basi mambo yao yote yalingane, kama tunazungumza mambo ya dini basi mambo yao yote yalingane. Haiwezi kuwa kwamba sehemu fulani tunaikweza *marks* sehemu nyingine tunaishusha, sio mahala pake. Haiwezi kuwa leo elimu ya dini ya Kiislamu tuseme tunaipa 35 hadi 59 tuipe 'D' lakini 35 mpaka 49, *Bible Knowledge* tuipe 'D' inakuwaje? Marks 10 zaidi? Hii ni dhuluma kubwa sana. Elimu ya dini ya Kiislamu 60 hadi 69 ni 'C', *Bible Knowledge* 50 hadi 64 ni 'C' inakuwaje? Lazima mambo yetu yaende sawia. Hapa tunaweza kusema lolote tunalosema itakuwa ni kweli, kama tunaiangusha dini ya Kiislamu, tunaweza kusema hivyo kwa upande mwingine. Si haja yetu kusema hivyo lakini tutafika kusema hivyo, kwa nini iwe hivyo? Hili ni kosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, Watanzania nataka msikilizze vizuri sana, Watanzania tumejidanganya muda mrefu sana kuhusu elimu. Watoto muda mrefu mitihani wanaipata kabla ya mtihani wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili hii utaona kidogo upungufu wa udanganyifu umepungua lakini huko nyuma kwa kweli watoto wetu mitihani ya wizi mtupu na ndiyo tunaona leo hata watendaji wetu maofisini, angalieni nyie mliokuwa viongozi maofisini, kweli mna watendaji wazuri?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Kwa nini watendaji si wazuri? Kwa sababu muda mrefu walikuwa wanafanya udanganyifu na hili ndilo lillotawala na hamjalisema hili. Nyote mnasimama lakini hili hamsemi na wengine wanajijua hapa katika maendeleo yao yote wamefanya kwa njia hiyo, wanajijua wengine hapa. (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Wataje!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mwalimu, nimesimamia mitihani, Mudhihiri nimemsimamia mtihani wa *form six*, alikuwa Mbunge hapa, muulizeni nilikuwa nafanya

kazi vipi? Uadilifu sasa hivi hakuna na hasa shule za *private* wanafanya biashara. Shule za *private* zinakwenda kibiashara, nasema mimi leo hapa.

**MBUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mmekuja 1995 pale, mambo nayajua vizuri sana, nimesomesha watoto kule wanakuja Dar es Salaam kusoma, nawauliza vipi mambo, wananiambia mambo kule uwe na pesa. Mnatuambia nini nyie? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto kutoka Zanzibar ukimwona ka-pass anakuja chuo kikuu muogope kwa sababu amepata kwa haki yake. Ninyi mnatafuta uchawi, uchawi wakati mnao wenyewe. Mnatafuta uchawi wakati uchawi mmeukalia? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna kila sababu kuwasifu wale, kwani mwaka 2011 baada ya kufutiwa matokeo, mwaka 2012 ndio matokeo yametokea namna hii. Kila mmoja aliogopa akaona itamfika aibu. Nasema *keep it up, keep it up*, kazi izidi kuendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba shule *private* mzifuatilie vizuri sana...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Kassim. Sasa namwita Mheshimiwa Rweikiza, ajiandaye Mheshimiwa Kigola na Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami pia naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja wala siyo pungufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kabisa kwamba nimesikitishwa sana na hotuba ya CHADEMA, ya Kambi ya

Upinzani walivyosema kwamba Serikali ya CCM inahujumu elimu ili ienddelee kutawala. Mimi nasema maneno haya wameyasema kwa sababu ya kutopenda kufikiri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu waliojenga shule za msingi kila Kijiji, ni CCM. Waliojenga shule za sekondari kila Kata au sekondari mbili kila Kata, ni CCM. Vyuo vikuu kama cha Dodoma hiki kikubwa sana, ni CCM.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vikuu binafsi vingi sana vimeruhusiwa vinaendelea vizuri, ni CCM. Sasa mtu anasema CCM inahujumu elimu, ili iendelee kutawala hiyo ni ukosefu wa kufikiri vizuri, hizo ni porojo tu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba tuongeze jitihada, wamesema Wabunge kwamba kuna mkanganyiko Wizara ya Elimu na TAMISEMI kuna mkanganyiko, tuboreshe utendaji katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Idara ya Ukaguzi, ipewe kipaumbele. Narudia kama walivyosema Wabunge wengine na mimi nasisitiza huwezi kupata elimu bora bila ukaguzi mzuri, haiwezekani. Binadamu ni lazima asimamiwe awe na woga fulani ili afanye kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, turudishe *Commission* ile *Tanzania Teacher's Commission* sijui ilifutwaje. Walimu hawajui waombe wapi maslahi yao, ajira ziko mara TAMISEMI, mara Wizara ya Elimu mara Mkurugenzi, mishahara yao hajjulikani inatoka wapi, madai yao hawajui wadai wapi, maslahi hawajui wapate wapi, hawana nyumba. Kwa hiyo, mimi nafikiri ufumbuzi wa hayo yote kwa Walimu ni kurudisha ile *Teacher's Service Commission (TSC)*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie lugha ya kufundishia, wanafunzi wengi wanafeli mitihani yao hasa *form*

four kwa sababu ya lugha. Hawajui Kiingereza, anaanza darasa la kwanza au la awali kwa Kiswahili hadi darasa la saba. Anaanza Kidato cha kwanza kwa lugha Kiingereza, miaka mitatu minne anafanya mitihani yote kwa Kiingereza, hawezu kujibu maswali yale. Tuamue kwamba lugha moja itumike kufundisha na mimi nasema ni Kiingereza kwa sababu tukisema Kiswahili hatukai peke yetu hapa duniani tuko katika dunia ya nchi nydingi na lugha ya kidunia ni Kiingereza, tutumie lugha moja ya kufundishia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo kwenye Baraza la Mitihani. Mimi nasema Baraza la Mitihani limezidiwa, halina pesa za kutosha kufanya kazi yake. Kazi zake inafanya vizuri lakini halipati pesa za kutosha. Bajeti zenyewe ni hizi ndogo ndogo hazitoshi. Tunapanga bajeti hapa lakini haziendi. Mwaka jana darasa la saba walifanya mtihani wa kuchagua huu A, B, C na D, ni mbinu ambayo wameibuni kupunguza gharama kwa sababu hawana pesa. Hawana pesa ya kutosha ili Walimu wakae pale Dar es Salaam au sehemu nydingine kusahihisha mitihani, haitoshi. Kwa hiyo, hata wanafunzi hawakuandaliwa vizuri. Kule kwangu Bukoba walifanya jaribio moja la OMR, kusiliba kule, jaribio moja halitoshi kuwaandaa wale wanafunzi, kwa hiyo walifeli. Baraza halina pesa za kutosha, lina kazi kubwa sana. Lisimamie matokeo ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha nne, kidato cha sita, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na vyuo vingine. Kwa kweli wana kazi kubwa sana lakini hawana fedha ya kutosha. Naomba waongewe mafungu ili kazi yao iweze kuonekana vizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Sera katika kusimamia elimu nafikiri bado ina matatizo. Mwaka jana kama tulivyosikia kwenye Tume ile walibadilisha utaratibu wa zile *grading* tunazosema hapa, *fixed* au *flexible* bila kuhusisha wadau wengine ambao ni shule, Walimu, wazazi na wanafunzi wenyewe. Kwa sababu mwanafunzi anajua kwamba akipata 21 ni 'D' lakini anapewa 'F' kwa sababu hakujua kwamba 21 ni 'F', yeye anahangaika, anajua uwezo wake ni mdogo apate angalau 21 apate 'D' kumbe 21 siyo

'D' ni 'F' kwa sababu hawakuambiwa mapema, ilikuwa ni siri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nasema Sera hii kwa kweli ya kufanya siri namna hii siyo nzuri lazima wadau wote wajulishwe. Sheria inasema kubadili hizi *grades* lazima iwe *gazetted*, haikufanyika hii. Sasa kama ni Wizara ya Elimu, kama ni TAMISEMI ilifanya makosa makubwa sana kuto-*gazette* haya mabadiliko ya *grade ranges*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, unasema kwamba tuseme 'F' ni 0-34, kweli 34 ni 'F', hafai huyu mwenye 34, mwanafunzi ana 34 kwa mia hafai ni 'F', tunam-*condemn* kwamba hana maana, hana anachokijua, si haki hata kidogo. Lazima hivi viwango virekebishwe kama nchi nyiningine zinavyofanya, kuna 'E' kuna 'S' mpaka ufikie 'F' labda 10 au 12 kweli amefeli, 34 haiwezi kuwa 'F'. Lazima hivi viwango tuviangalie upya ili wanafunzi watendewe haki. Wanafunzi wanajiua, wamekufa sijui watano, sijui sita maana kwenye matokeo ya *mock* kwenye Kanda huko kwenye Wilaya, kwenye Mkoa anakuwa *division one*, *division two*, anakuja matokeo ya *mwisho* *division zero*, anajiua. Mzazi anachanganyikiwa, kauza shamba mwanae asome, anashangaa mwanae anapata sifuri, lazima achanganyikiwe. Shule zinafungwa, wazazi wanaona kwa kweli hawatendewi haki, watoto hawatendewi haki, mimi nasema kwamba Sera hii irekebishwe na isimamiwe viziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusimamie elimu ili matunda yake yawe mazuri lakini kwa ujumla wake naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru, sasa namwita Mheshimiwa Kigola, ajiandae Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja na sababu zinazonifanya niunge mkono hoja ni kwamba katika Wizara hii imeweza kuziona zile shule ambazo zina matatizo makubwa. Nilikuwa najaribu kusoma hili jedwali, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba umeweza kujibu hoja zetu za Wabunge ambazo huwa tunaleta hapa. Kwa mfano, shule ile ya Malangali, shule ya Malangali nimeona kwenye Jedwali imeiwekwa na ile shule kweli inahitaji ukarabati mkubwa. Tukiongelea ukarabati unaotakiwa kufanya pale ni kuanzia umeme, shule ile haina umeme. Vilevile nilikuwa nimefanya ziara pale, hakuna majiko kabisa na ile shule ni kubwa sana. Sasa nimeona hapa kwenye bajeti ya Wizara imwekwa, mimi nakushukuru sana kwamba umeliona hilo. Katika Wilaya ya Mufindi, ameweza kutupatia shule kama 11 lakini hizi shule 11 ambazo amesema anaenda kufanya ukarabati tunaomba iende kama illvyopangwa na kama itaenda kama illvyopangwa ni sehemu ya uboreshaji wa elimu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema Ifwagi sekondari, Kasanga, Kiyowela, Kibengu, Itengule, Itandula na Nyololo. Shule hizi ni kweli zina matatizo makubwa na ukienda pale, tukizungumzia kwamba kuna uboreshaji wa elimu, mpaka sasa hivi zile shule zina hali ngumu sana. Namwomba Mheshimiwa Waziri tunapoongelea ukarabati lazima tuguse kwenye umeme. Shule hazina umeme kabisa na ni shule nzuri, zimekaa sehemu nzuri na zina watoto wengi sana lakini hazina miundombinu kamili, sasa watoto watasomaje kama hazina umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine naomba niongelee elimu tunaanza wapi? Tunapozungumzia elimu ni kuanzia elimu ya awali mpaka vyuo vikuu. Sasa hapa mara nyingi Wabunge wengi tunalalamika sana, tunasema elimu imeshuka na tukisema elimu inashuka, inashuka kuanzia wapi? Elimu inayoshuka inaanzia elimu ya awali. Utakuta shule zetu nyingi sana za awali hazina Walimu. Walimu waliopo pale tunasema wa kujitolea. Sasa jamani Mwalimu wa kujitolea kweli atatoa elimu bora na tunahitaji hapa ubora wa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Wizara hii Walimu wanaotakiwa kufundisha shule za awali isiwe wa kujitolea na kila shule ya msingi lazima iwe na shule ya awali. Nimeona hapa tunahangaika mara sijui tuongeze madarasa kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la nane, pale tulikwishaongeza mtoto anaanza shule ya awali anaingia shule ya msingi anasoma miaka saba anaenda sekondari. Sasa shule ya awali utakuta Walimu wale wanajitolea halafu hawalipwi. Mtu anatokea tu kijijini pale anajitolea, unaenda shule yenye haina madawati na darasa lenyewe lina vumbi tupu, sasa unasema tunataka kuboresha elimu, kwa nini tunahangaika? Shule ya awali haina vitabu, sasa uboreshaji wa elimu utakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri azingatie kwenye msingi mkubwa hata unapojenga nyumba ukikosea msingi basi hiyo nyumba haiwezi kusimama vizuri. Sasa sisi tunaangalia juu, huku awali hatujaona vizuri. Watoto wale wanakaa tu, halafu madarasa yenye hata madawati hayapo, ni vumbi tupu, hii haiwezi kuwa sahihi kabisa. Sasa nataka nitoe wito kwamba shule za awali lazima zitengewe bajeti nzuri inayoeleweka katika Halmashauri zetu na tuhakikishe kwamba zinasimama vizuri na watoto wanafundishwa vizuri na kila shule ya msingi lazima iwe na Mwalimu ambaye amesomea Ualimu siyo wa kujitolea. Hili lazima tulizingatie. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye sekondari. Sekondari za Kata, nashukuru Serikali ya Chama cha Mapunduzi kila Kata kuna sekondari, hilo mimi nakubaliana nalo kabisa lakini tuna matatizo makubwa mojawapo ikiwa ni Walimu wa sayansi. Mwanafunzi hawezi akafanya mtihani wa masomo ya sayansi wakati hakufundishwa. Kama shule haina Mwalimu wa sayansi hakuna haja ya kumpatia mwanafunzi mtihani! Unampatia mtihani wa nini wakati hakusoma! Shule nydingi za Kata hazina Walimu wa sayansi. Lazima Serikali iwasomeshe bure Walimu wa sayansi, tusipofanya hivi kila siku tutakuwa tunatoa zero. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshafanya utafiti katika sekondari, tuna watoto yatima wako pale, kuna watoto wanatoka kwenye mazingira magumu, hii michango ya sekondari imezidi na imepita kiwango. Tunasema sekondari ada ni Sh.20,000/= siyo Sh.20,000/= inafika kama laki moja na ngapi ukipiga hesabu. Mimi naiomba Serikali kama kuna uwezekano ada shule za sekondari tufute, tusiwe na ada kabisa ijulikane hakuna ada pale watoto wasome, ada tuweke chuo kikuu. Watoto saa hizi wanahangaika wanaenda shulenii wanafukuzwa ada, wakifukuzwa ada, mtoto anakaa wiki mbili nyumbani hajaenda shulenii, anasema mimi ada haipo, sasa tunasema tufanyaje? Utakuta mchango wa madawati, mchango wa mlinzi, vitu vimewekwa pale vingi sana mpaka wazazi hawaelewi walipe kipi, mtoto anarudishwa nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naishauri Serikali ada ya sekondari ifutwe, watoto wasome, tuweke vyuo vikuu kuwe kuna ada. Tunajua hakuna kitu cha bure lakini sekondari ada ijulikane hakuna mchango wala nini watoto wapate elimu. Sasa hivi wanajitokeza watu wanasesma tunawasadida watoto yatima, utamsaidiaje mtoto yatima peke yake halafu watoto wengine wasisome, wanashindwa kulipa, vijiji kule wanashindwa kulipa. Naomba sana suala hili lizingatiwe. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye elimu ya vyuo vikuu. Elimu ya vyuo vikuu sasa hivi imekuwa shida sana. Hata Walimu wanaosomea Ualimu, hawalipwi ada. Halipwi ada mtu anatoka kwenye mkondo wa Ualimu anafundisha shule ya msingi, anaenda diploma, anaenda chuo kikuu halafu hapati ada bado anahangaika mshahara wake mdogo, hana posho, anajilipia mwenyewe, hivi mwalimu anaweza akajilipia mwenyewe? Kwa nini Serikali isimlipie ada ili aweze kupata digrii yake nzuri na arudi kufundisha. Kuna Walimu wengine wameenda kusoma, wametoka shule ya msingi wameenda kusoma, mshahara wao kule unashuka. Badala ya kupandishwa daraja mtu ana digrii eti daraja linaludi nyuma, mimi sijawahi kuona hiyo. Hiyo ni *system* ya wapi? Haiwezekani, mtu akipata digrii na mshahara

unapanda juu na daraja linapanda juu, ndiyo motisha ya Mwalimu hiyo. Vitu vingine ni vidogo sana, ni vyta kufanya siku moja, mbili, tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu na upandishaji wa madaraja ya Walimu inaonekana kama *issue* ngumu sana, ni haki ya Mwalimu daraja lipande. Utasikia Mwalimu sijui wameandika fomu, wewe katika komputa yako hujui kuna Walimu wangapi wanatakiwa kupanda daraja kila mwaka? Wizara lazima ihakikishe kila mwaka Mwalimu anapanda daraja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu bahati nzuri nimeona utatoa semina kwa wataalam, toa semina kwa Walimu, Walimu ndiyo wanatakiwa wapewe semina siyo wataalam. Walimu ndiyo wanafundisha watoto wetu kule, hizo posho, hizo *allowance*, wape Walimu. Walimu wana mishahara midogo, utampaje semina mtu ambaye keshapata utaalam. Tunataka wale Walimu wa shule za msingi katika Halmashauri zetu lazima wapewe semina za kutosha kufuatana na mabadiliko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu bahati nzuri nimeona mtihani, watoto wetu walifeli na sisi Wabunge tulishituka. Haiwezekani ikafikia 60% watoto wamefeli. Namshukuru Waziri Mkuu kwa kuunda ile Tume, imechunguza meona na mwaka jana nakumbuka kwenye Jimbo langu walifeli watu 361, kuna Walimu walifukuzwa kazi kule, walismamishwa kazi kule, sasa hawa waliosababisha mtihani ukaja vibaya sijui mtawachukulia hatua gani? Tunataka Waziri atuambie wakati wa ku-*finalise* hapa utuambie waliosababisha mpaka Tume ikaundwa na Waziri Mkuu, kuna hatua gani wamechukuliwa, hatuwezi kuwaacha. Mimi kule kwangu kuna Walimu wameteremshwa daraja, alikuwa Mwalimu Mkuu anakuwa Mwalimu wa kawaida, sasa na wale waliosababisha washushwe madaraja, kwa nini wasishushwe, tufuate usawa. Kama ni usawa wale waliosababisha Walimu wakafukuzwa au wakateremshwa madaraja na sisi tunataka waliosababisha mpaka wakafikia 60% aibu kwa Taifa letu, aliyetuaibisha huyo, ashuke daraja, hapo tunatengeneza

usawa. Kama Waziri hautafanya hili, kweli sisi Wabunge hatutaelewa vizuri, tunataka usawa. Hatuwezi kusema elimu inashuka wakati kuna watu wanashusha elimu, elimu inapanda halafu wewe unasema inashuka? (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ya pili?

**MWENYEKITI:** Ni ya pili, nakushukuru sana.

Sasa namwita Mheshimiwa Jenista Mhagama, ajiandae Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Lissu, dakika tano, tano.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kabisa kwanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa sababu, yako maeneo ambayo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya vizuri katika suala la elimu ingawa bado upo upungufu ambao hatuna budi kuutizama na kuufanya kazi kwa nguvu zote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajikita zaidi kwenye hoja za msingi na kubwa nilizonazo, nianze na hili la Taarifa ya Mgawo wa Shule za Ukarabati katika nchi yetu. Naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri, pamoja na kukuunga mkono kwenye hoja hii, kama hutakuja na tamko la kubatilisha mgawo wa ukarabati wa shule hizi, nitasimama na kutoa shilingi na kutokupitisha bajeti yake. Mgawo huu wa ukarabati wa shule hauzitendei haki, hautoi usawa wa kielimu katika Mikoa na elimu ya nchi yetu ya Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa naangalia hiki kitabu, mimi nimeshangaa kwanza, hivi aliyekuwa anaandaa hii taarifa alikuwa anaandaa akiwaje? Hapa kuna shule

inaitwa Namabengo Sekondari, imendikwa shule hii iko Songea Vijiji ni wakati shule hii iko Wilaya ya Namtumbo kwa Mheshimiwa Vita Kawawa.

**WABUNGE FULANI:** Oooh!

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Hapa kuna shule ya Chabruma, imeandikwa iko Songea Vijiji, lakini kumbe shule hii iko Songea Mjini, Jimbo la Mheshimiwa Nchimbi. Hapa kuna shule inaitwa Matogoro imeandikwa iko Songea Vijiji, lakini shule hii kumbe iko Songea Mjini kwenye Jimbo la Mheshimiwa Nchimbi. Ukihesabu idadi ya shule hizi kwenye huu Mkoa wa Ruvuma, eti shule zitakazofanyiwa ukarabati ziko 42 tu, lakini ukienda kwenye Mkoa wa Kilimanjaro ziko shule 102. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kweli huu mgawo ni sahihi? Hapo ukitalia tu ukazihesabu hizi shule, unaona kabisa kwamba, hawa wataalamu wetu hawa, mimi sielewi wamefanya kitu gani katika mgawo wa hizi shule. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hebu arejee, iko Mikoa mingi sana, ukienda Lindi, Mkoa wa Mtwara, hazifiki shule 42, sasa mgawo huu ni kwa manufaa ya watoto gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema Mheshimiwa Waziri, futa mgawo huu, gawanya shule hizi kwa usawa katika nchi nzima. Watoto wa Watanzania wote, wanahitaji majengo bora yenyе kufaa katika kupata elimu. Ukifanya hilo Mheshimiwa Waziri, hii kukuunga kwangu mkono kwa asilimia mia moja nitasimama hapa kifua mbele na kukuunga mkono. Usipobatilisha hili Mheshimiwa Waziri, waambie wataalamu wako kwamba, hizi ni salamu mgawo huu urudiwe upya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kusema hayo, ninaomba sasa nieleze yafuatayo. Mimi nimezaliwa kwa Mwalimu, baba yangu ni Mwalimu, Mwalimu Joachim Ngonyani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule nakumbuka nikiwa motto, mama yangu alikuwa anapata heshima kubwa kweli, mke wa Mwalimu.

**WABUNGE FULANI:** Sawa kabisa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Akipita kila mahali, kila mtu anasema mke wa Mwalimu amepita lakini leo ukiwa Mwalimu, ukiwa mke wa Mwalimu, ukiwa mume wa Mwalimu, hakika hakuna hata anayeshtuka wewe uko Kijiji au upo mahali popote, hamna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliamua kwenda kusomea Ualimu kwanza kwa ajili ya wito wangu, lakini ile hali aliyokuwanayo baba ya heshima pale Kijiji, nilikuwa naona hakuna kazi nzuri yenye heshima kama kazi ya Mwalimu. Leo hebu tujiulize, Waziri tusaidle, hivi haya malalamiko ya Walimu kila siku ambayo hayapatiwi ufumbuzi, tatizo ni nini? Kwa nini hatumalizi kero hizi za Walimu? Matokeo yake tunakuja hapa tunaanza kulumbana, tunamtafuta mchawi, mchawi ni huyu, mchawi ni yule, mchawi ni huyu, tukae. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilishakuwa kwenye Tume ya kufuatilia matatizo ya Walimu mwaka 2004, tulifanya kazi kubwa tulizunguka nchi nzima. Hivi matokeo ya Tume ile yamefanyiwa kazi kiasi gani? Tutaendelea kuunda hizi Tume, lakini bila kukaa na kutafakari, kuwakomboa hawa Walimu, hatutaweza kufanikisha kitu chochote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Walimu hawana nyumba, Walimu wanapata shida kwenye posho zao, Walimu hawana mishahara yao, Walimu wanalamika kupandishwa madaraja, hawapandishwi. Sasa tunafanya nini kama kila siku hadithi ni hiyo? (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Sawasawa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini, tunapata kigugumizi cha kurudisha Tume ya

Huduma kwa Walimu? Tujifunze kwa nchi za jirani, wenzetu wa Kenya. Tume ya Huduma kwa Walimu ndio inayowasajili Walimu. Tume hii ndio inawapandisha madaraja yao. Tume hii ndio inatoa adhabu kwa Walimu watovu wa nidhamu, wanaadhibiwa; inafanya kazi hiyo Tume ya Elimu. Tume hiyo ndio inayoshughulikia mpaka masuala ya mirathi ya Walimu. Tume hii ndio inayoshughulikia mazingira yote ya kazi ya Walimu. Leo hii sisi tunahangaika na mfumo tulionao katika nchi yetu, ifike mahali tuondokane na huu mfumo unaotufanya elimu yetu isiendo mbele iendelee kurudi nyuma. Turudishe Tume ya Huduma kwa Walimu na kama kutakuwa na tatizo lolote tupate mtu wa kumkamata na kumuuliza. Tukiyaweka haya yote kwenye Tume ya Huduma kwa Walimu, tutaiuliza Tume inafanya nini na kiwango cha elimu kinashuka kwenye nchi yetu? Bila kufanya hivyo, tutaendelea kupiga *mark time* na hatutaenda mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 60 ya wafanyakazi wa Tanzania ni Walimu, tukiwachukua hawa Walimu 60%, tunawapeleka TAMISEMI, wanakutana na Manesi ambao ni asilimia kubwa inayofuatia, wanakutana na Watendaji wa Vijiji na wa Kata, hivi kweli, mzigo huu mkubwa tunauweka sehemu moja, tutaweza? (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Hatuwezi.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye maamuzi sahihi kwa wakati sahihi. Naomba sana Tume ya Huduma kwa Walimu irejeshwe iweze kuyashughulikia haya, yapo malalamiko kuna Walimu wengine sasa hivi maadili yameshuka, hakuna Tume ya kuyaangalia hayo, ikiwepo Tume tunaweza tukafanya kazi hiyo vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja ya msingi ya masuala ya kiwango cha ufaulu lakini suala zima la kiwango cha elimu nchini. Nakubali yote waliyosema Wabunge wenzangu lakini tunasahau suala moja la lishe. Tukijenga madarasa, tukitengeneza madawati,

tukatengeneza kila kitu lakini kama utapiamlo na udumazi wa watoto utabakia kuwa 42%, hatutaondoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoto ili aweze kukua na kufanya vizuri, anatakiwa ubongo wake uwe imara, sisi Walimu tunajua, toka akiwa umri wa mwaka 0 - 5. Umri huo unamsaidia sana mtoto kupata akili nzuri, unamsaidia mtoto kujifunza vizuri, watoto wetu hawana lishe, wana utapiamlo, bila kufanya hivyo, hatuwezi. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini kwa kweli, naomba yale niliyoyasema yazingatiwe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, una dakika tano.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa wengi ambaao wamelalamika sana juu ya matatizo ya elimu tangu mjadala huu uanze leo asubuhi, ni wale vilevile ambaao wameunga hoja ya Serikali kwa asilimia mia moja. Kwa hiyo, inawezekana hizi kelele kwamba kuna matatizo ni kelele za kinafiki tu. Haiwezekani wakasema Serikali imekosea kwa kiwango hiki, halafu bado wakaunga hoja ya Serikali hiyohiyo kwa asilimia mia moja. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie muda mfupi nilionao kuzungumza vitu ambavyo viko kwenye maandiko na nyaraka za Serikali hii ya CCM. Kwenye Kitabu cha Takwimu Muhimu za Elimu kilichochapishwa na Wizara na kugawiwa humu Bungeni, kinaonesha jinsi ambavyo tangu Serikali hii ya sasa ya CCM ilipoingia madarakani mwaka 2005 jinsi ambavyo elimu yetu imeporomoka. Hicho kitabu hakikuandikwa na CHADEMA, kimeandikwa na Serikali ya CCM, kimesainiwa na Waziri Jumanne Kawambwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Taarifa ya Awali ya Waziri Mkuu juu ya janga la mwaka huu la watoto kufeli, iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Waziri Lukuvi, ilielekeza kidole cha lawama kwa Baraza la Mitihani lakini nyaraka za Serikali yenyewe zinaonesha kwamba Baraza la Mitihani lilielekezwa na Wizara kutumia utaratibu mpya wa kusahihisha mtihani wa mwaka jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho kikao kilichotoa hayo maelekezo, Mwenyekiti wake alikuwa Mheshimiwa Jumanne Kawambwa, Waziri, alikuwepo vilevile Naibu wake, Mheshimiwa Philipo Mulugo na alikuwepo Profesa Sifuni Mchome, ambaye amepewa kazi ya kuja kutwambia kosa ni nini. Badala ya kusema kosa ni sisi tulioCAA mwaka jana Disemba tukabadilisha utaratibu wa kusahihisha mitihani, sasa tunalaumu Baraza la Mitihani. Hizo zote ni nyaraka za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka wakati wa bajeti kama huu, Wabunge wote huwa tunapewa Kitabu ambacho wengi wetu hatukisomi, tunafanya mambo mengine. Waziri Mkuu anapowasilisha hotuba yake, huwa anagawia kila Mbunge, kitabu kinaitwa Majedwali Yanayoambatana na Hotuba ya Waziri Mkuu, miaka yote kinatolewa. Ukiangalia takwimu zillizoko kwenye kitabu hicho, angalia hata za mwaka huu tu, uangalie mafungu ambayo yanatolewa na Serikali kwa ajili ya shule zetu lakini hayatumiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu za mwaka 2011/2012 peke yake, kulikuwa na zaidi ya shilingi bilioni 24 ambazo takwimu za Waziri Mkuu, zinaonesha zilipelekwa shulenii, lakini hazikutumika. Hayo majedwali hayaajaandaliwa na CHADEMA, yameandaliwa na Serikali hii ya CCM. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni rahisi sana kusema watoto wetu wanafeli kwa sababu hii au ile. Ni rahisi kupiga siasa kama ambavyo Wabunge wa Chama cha Zamani wamekuwa wanafanya lakini nyaraka za Serikali

ambazo nimezitaja na hizo ni baadhi tu, zinaonesha kwamba Serikali hii ya CCM ni janga la elimu la Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa sababu ni dakika tano tu, Bunge hili, wanaowajibika mbele ya Bunge si Maafisa wa Serikali ni Waziri, ajiuzulu. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Lissu, sasa namwita Mheshimiwa Silinde, dakika tano.

## TAARIFA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa *Chief Whip* wa Upinzani, kwamba, CCM sio Chama cha Zamani ni Chama Tawala, hiyo tu basi, inatosha. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, muda wako umekwisha, kaa.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Kaaaa!

**MWENYEKITI:** Kaa tu, muda wako umekwisha, nakuomba ukae Mheshimiwa Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka tu kusema...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lissu, nakuomba ukae. Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku tumekuwa tukirudia maneno. Tulizoea kufundishwa tukiwa wadogo na tumeendelea kufundishwa hivyo, ukiwa baba katika familia, mtoto wako akifanya vibaya aibu inaanzia kwako wewe mzazi. Mtoto akifanya vizuri sifa inakwenda vilevile kwa mzazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunashangaza Taifa. Hakuna mtu asiyejua kwamba elimu ya Tanzania leo hii hamna kitu, ni sawasawa na sifuri. Watoto wanaotoka au zao tunalolizisha, hamna kitu. Miongoni mwa maajabu ya dunia hii yapo Tanzania, mtoto anamaliza darasa la saba hajui kusoma na kuandika, anafaulu sekondari, miongoni mwa maajabu ya Serikali na Chama cha Mapinduzi, nyote mnafahamu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zimeletwa hoja Bungeni kutaka kunyanya ubora wa elimu, sisi Wabunge, kwa macho yetu wote hapa, ndio tumekuwa wa kwanza kuzizua zisiende kusaidia ubora wa elimu, tunamlalamikia nani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayeropa elimu ni sawasawa na yule anayeropa roho ya mwanadamu. Leo Taifa linalalamika kuna watoto 210.000 wamepata daraja sifuri, wanakwenda wapi? Serikali, itupe majibu maana wale watoto wa daraja la sifuri maisha yao yameishia palepale, ni machangudoa wa baadaye, ni vibaka wa baadaye, ni majambazi wa baadaye, ni tegemezi kwa Taifa, halafu kesho unanyanya unawaambia nawaomba muwe wazalendo, watakuwaje wazalendo, wamepata daraja sifuri? Nani wa kulaumiwa? Lazima tuilaumu Serikali, ni lazima tumlaumu Waziri husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mheshimiwa Kawambwa, mtasema tusilaumu, ameshika Wizara ngapi tangu amekuwa Waziri? Wizara tano, utaondoka kwenye Taifa hili Wizara tano umeshika, umeacha *mark* ya namna

gani ambayo Taifa litakutambua? Ni lazima tuzungumze ukweli; mmezowea kupindisha sana ukweli, mnataka kutuachia Taifa la namna gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ndio itakayokuja kuwagharimu, hamwoni ninyi, tunajaribu kuwasaidia kwa kila namna, tumewaonesha njia, lakini mnashindwa kufanya kazi. Mnakwenda kutuwakilisha kwenye Vikao vya Kimataifa, kama Waziri unashindwa kuliwakilisha Taifa, unategemea nini katika hili Taifa leo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anguko la elimu na matokeo haya ni aibu kwa Rais kwa sababu Rais ndio namba moja, ndio Baba wa hili Taifa. Ni aibu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni aibu vilevile kwa Watendaji wa Serikali na sisi wote kwa ujumla. Mimi nawaambia kama hamuwezi kazi, tupeni tupige kwa sababu, tupo watu wenye uwezo ambao tunaweza tukafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakuhakikishia leo ukinipa shilingi bilioni tano katika Jimbo langu la Mombasa, hakuna mwanafunzi hata mmoja atakayekaa chini, hakuna Mwalimu atakayelalamika nyumba, hakuna darasa litakalokosa vitabu na elimu itakuwa juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashangazwa na tunaendelea kushangazwa, miaka ya 1980 Tanzania ilikuwa ya tatu katika ubora wa elimu; katika watoto 10, Mwalimu Nyerere kipindi hicho, watoto 10, tisa walijua kusima na kuandika. Leo 2013, miaka 33 ijayo katika watoto 10 tisa hawajui kusoma na kuandika, *it is a shame on you*, hatuwezi kwenda na mfumo wa namna hii kwa sababu, msiandike takwimu za kwenye makaratasi, twendeni kwenye uhalisia. Uhalisia si ndio unvyoonjesha, haya matakwimu kila mtu anaweza kuyataja, nimejenga madarasa 100, wanafunzi wamefaulu wangapi, lakini twendeni kwenye uhalisia, twendeni Vijiji watoto hawasomi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Serikali, mtueleze. Watoto 210,000 wanarudia madarasa Kidato cha I na cha

VI? Mnawapeleka VETA wakasome upya? Tunataka kuona maisha yao ya baadaye kwa sababu, tukiendelea kuwavumilia kwa mfumo huu, hatutafika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, msije kuwa *marked* kama wauwaji wa elimu Tanzania. Naweza kusema msije kuwa *marked* kama wauwaji wa elimu Tanzania, kipaumbele cha kwanza kwenye Taifa ni elimu, vingine vyote vinakuja. Mwalimu ndio *source* ya kila kitu, mwaka 1980 hapakuwa na madarasa yakutosha, wanafunzi walisomea chini ya miti, lakini elimu ilikuwa iko juu kwa sababu, Walimu walijitoa. Walimu walijua kumtengeneza mtoto wa leo, maana yake unajenga Taifa la baadaye. Sasa hii ndio tunayoitaka, lakini leo Serikali ya Awamu ya IV imeshindwa kutekeleza. (*Makofii*)

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Silinde. Sasa namwita Mheshimiwa Riziki Omar Juma.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie machache katika hoja hii ya Wizara ya Elimu. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uwezo wa kusimama hapa mbele ya hadhara hii ya Bunge nami niweze kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kusema kwamba pamoja na nia njema ambayo inaonekana ipo ndani ya vitabu lakini kiutekelezaji haionekani kwamba kuna nia njema katika kuliendeleza suala hili la elimu katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayotengwa kila mwaka haionekani kwamba ina nia ya kutondoka hapa tulipo au hapa tuliposimama katika suala la elimu. Ukiangalia bajeti ya mwaka unaoishia tarehe 30, Juni ukaangalia na

bajeti iliyopangwa kwa mwaka huu, ni dhahiri kwamba majukumu ya Wizara ya Elimu hayawezi kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nji kwenye Idara ya Ukaguzi. Pamoja na kwamba fedha hatuna, ni jambo kubwa ambalo linachangia kiwango kikubwa cha kufeli wanafunzi wetu katika shule zetu za *primary*, sekondari na hata hiyo mitihani ya Taifa ambayo inafanyika. Jambo lolote wazee wanasema kwamba ikiwa halina msimamizi haliwi. Idara ya ukaguzi inapaswa kupewa fedha ya kutosha ili iweze kusimamia Kitengo hiki cha Ukaguzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu enzi na enzi wazee wanasema tena walikuwa wanasema kipemba kwa kuimba hasa wakibembeleza watoto, jambo haliwa likita msimamizi na majaliwa. Sisi majaliwa tunayo, tuna wanafunzi wa kutosha lakini usimamizi hatuna na hilli tunalibeza makusudi. Mwalimu ye yote na mtu ye yote ambaye utampa kazi afanye bila kumsimamia, hawezu kuifanya kazi ipasavyo, hataifanya kazi kama vile unavyotaka wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, huyo tunayekwenda kumsimamia tumemwezesha kiasi gani, tumemweka katika mazingira gani? Tunakwenda kumsimamia Mwalimu ambaye anaishi katika mazingira magumu, anafundisha katika mazingira magumu, hana kitabu cha ziada wala cha kiada, hana vifaa vya kufundishia, mazingira anayofundishia ni mabaya na ni magumu, anafundisha katika darasa la tope, ikinyesha mvua lazima avae *rain boot* ndiyo aingie darasani, hawezu kufundisha Mwalimu huyo akazalisha zao zuri na mwanafunzi anayefundishwa pale akatoka akiwa ameelimika vya kutosha. Naiomba Serikali tuangalie tunafanyaje ili kujitoa hapa tulipo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wachina katika mapinduzi ya Kichina waliamua kwamba lazima vijana wao wawafundishe utaalami ili watoke pale wakiwa ni wataalam na leo hii Wachina, Thailand na nchi nyingine mbalimbali, wako mbali sana, wamepiga hatua kwa sababu leo sisi inaonekana tunatoa wanafunzi ili waende wakafanye kazi

maofisini. Hatutoi vijana watakaokwenda kuanza maisha katika Taifa lao hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajenga vyuo vya VETA lakini ukiangalia idadi ya vyuo vya VETA yaani vyuo vya ufundi na vyuo vikuu vingi ni vyuo vikuu ambavyo vinazalisha hawa wanafunzi ambao wanaambiwa wanapewa mitihani, wanafanya mitihani ya kutengenezewa kabisa, kwa hiyo pale VETA tungewekeza vyua kutosha katika vyuo vyetu, tukajenga vyuo vya kutosha katika kila Wilaya na tukawekeza vyua kutosha kwa vifaa vinavyohusika kijana wetu akitoka pale anaenda kujitegemea tayari tumeshamwezesha. Tukajenga na viwanda ikiwa kijana pale akitoka kila mmoja na ujuzi wake anakwenda kufanya kwa mujibu wa uwezo alionao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaandaa hapa mazingira ya Idara ya Ulaguzi lakini Mwalimu ambaye tunamtaka aende akakaguliwe hatujamweka vizuri kwa hiyo bado tutazalisha lilelile Taifa ambalo limedumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana madeni ya Walimu, ni jambo zito sana, sijui ni miaka mingapi sasa tunaimba madeni ya Walimu. Hebu tuamue jamani, tuamue kwa ukweli kweli tuseme sasa nini hasa tunataka tufanye kwa sababu suala la elimu ni suala la muhimu sana katika Taifa. Daktari anahitaji Mwalimu, mkulima anamhitaji Mwalimu, mtu ye yeyote katika dunia hii anamhitaji Mwalimu, Mbunge anamhitaji Mwalimu na Waziri anamhitaji mwalimu. Sasa kama hatukuandaa mazingira mazuri tukapata elimu iliyo bora, tukatoa Walimu wazuri, tukazalisha Taifa lilito bora nadhani tutafika mahali pabaya sana Taifa hili, Taifa litaendelea kudumaa. Naiomba sana Serikali tupige hatua ya kusema kwamba sasa tunataka kujielekeza kwenye elimu kwanza, elimu kwanza hatujaifanyia kazi. Tunasema elimu kwanza tunaiacha, tunakwenda kilimo kwanza tunaacha, kesho tutakuja afya kwanza tutaacha, hatupigi hatua. Lazima tuende kwa mpangilio, kama hatukwenda kwa mpangilio hatutafika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu zina matatizo. Shule moja ina wafunzi 400, hiyo naisema kwa uhakika. Tangu mimi sijazaliwa, nina maana kabla ya Mapinduzi ya 1964, shule hiyo ina wafunzi 400, ina matundu mawili ya vyoo, *that means* kila tundu moja linatumwa na wanafunzi 200. Fikiria kwanza tundu hilo bado linafanya kazi, bado liko hai linatumika, wanafunzi hawa wanajisaidia wapi? Mazingira aliyosema Mheshimiwa Jenista Mhagama kwamba afya bora, lishe bora lakini lishe na afya ikiwa vyoo viko katika hali hiyo katika shule zetu tunawapeleka wapi vijana wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Bodi ya Mikopo. Katika bajeti ya Wizara ya Elimu, ukiangalia utakuta ni titi kubwa la fedha ingawaje halitoshi lakini humo ndani yake mna mikopo ya wanafunzi. Ukitazama sehemu kubwa ni fedha za mikopo ya wanafunzi. Nashauri kwamba fedha hizi za mkopo wa wanafunzi zitoke Hazina moja kwa moja zisiingizwe kwenye bajeti ya Wizara, zisiingizwe kabisa katika bajeti ya Wizara, zitoke moja kwa moja Hazina zisiingie katika titi lile la bajeti ya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo napendekeza naomba niseme kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusema naunga mkono hoja kwa sababu hali ya elimu ni mbaya sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, sasa namwita Mheshimiwa Azza Hamad ajiandae Mheshimiwa Zainab Kawawa na tunamalizia na Mheshimiwa Mkosamali.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa afya na hatimaye nimeweza kusimama ndani ya ukumbi huu ili kuweza kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asiyeshukuru kwa kidogo hata kwa kikubwa pia hawezi kushukuru. Kwanza, niseme naunga mkono hoja bajeti ya Wizara hii na sababu za kuunga mkono hoja ninazo. Kwanza, niishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kutupatia Walimu wa kutosha Mkoa wa Shinyanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwa mwaka huu wa fedha, shule ya msingi, tulipangiwa Walimu 198 walioripoti ni 190. Shule za sekondari, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tulipangiwa Walimu 85 walioripoti 66. Kwa hali hii, naishukuru sana Serikali na naipongeza iendelee kwa kazi hiyo nzuri inayofanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, kuna mambo ambayo wanapaswa kurekebisha. Tunaupungufu mkubwa wa nyumba za Walimu, naomba sana, kuna Wilaya ambazo ziko pembezoni, Wilaya ambazo zina mazingira magumu, hata mwaka jana nilivyochangia nilisema, kwa nini Wilaya hizi hatuziangalii au kwa nini Wilaya hizi hatuzipi kipaumbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Jimbo la Solwa kwa ujumla lina Kata ambazo kwa uhakika wakati wa masika pia hazifikiki mfano kata ya Mwakitalyo. Ukitaka kwenda kwenye Kata ile mpaka uzunguke Kahama au uzunguke Mwanza. Walimu wanaoishi Kata ya Mwakitalyo wako kwenye mazingira magumu, wanakaa kule miezi sita mpaka wapelekewe mishahara yao kule. Naomba sana tuwaangalie Walimu hawa katika mazingira wanayoishi kwa kuwajengea nyumba lakini pia tuangalie posho zao kwa sababu Mwalimu kama huyu anatoka kwenye Kata ile anazunguka kupita Mwanza hebu niambie anatumia siku ngapi mpaka arudi kwenye kituo

chake cha kazi. Kwa hiyo, tuangalie pia posho tunazowalipa hawa Walimu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwenye ukarabati wa shule zetu ambao tumeletewa na Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu hiki. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa sababu katika zile shule mbili kila Halmashauri, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tumepata shule ya Kituli Sekondari na Samuye Sekondari na hivi ninavyoongea ukarabati unaendelea kule, ndio maana nimesema usiposhukuru kwa kidogo hata kwa kikubwa pia huwezi kushukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ukarabati huu unaoendelea kule, niombe sana, ukarabati huu kweli tunaufanya lakini tunesahau mabweni ya wasichana. Wasichana hawa wanatembea umbali mrefu kilomita 5-10 kwenda shuleni, hivi tunategemea wanakutana na vishawishi vingapi mpaka wanafika kule shuleni? Mimi niwaombe sana tukiwa tunakarabati shule hizi tukumbuke kujenga mabweni ya wasichana vinginevyo hakuna tunachokifanya kwa wasichana hawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nasikitika sana kwenye kitabu hiki, narudia kusema nasikitika sana, aliyenacho ndio anayeongezewa. Mkoa wa Kilimanjaro unaongoza kwa kila kitu, barabara za lami Kilimanjaro, shule nzuri za maghorofa Kilimanjaro, umeme Kilimanjaro, maji Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 155 - 158 inasikitisha, umewekwa pale Mkoa wa Shinyanga, sasa ninashindwa kuelewa, mimi nadhani kuna namna ambayo inatafutwa katika Wizara hii, kuna mkakati maalum unaotafutwa kwenye Wizara hii. Kuna watu wana jambo wanalifanya kwa sababu sielewi kwa hali ya kawaida uniambie Bariadi ipo Mkoa wa Shinyanga, uniambie Bukombe ipo Mkoa wa Shinyanga, uniambie Meatu ipo Mkoa wa Shinyanga, sielewi. Hivi aliyeandika kitabu hiki ni nani, anaijua nchi hii kweli? Inasikitisha sana ndio maana nasema kuna mkakati mimi nadhani umeandaliwa wa makusudi mazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwamba pamoja na mikakati hiyo, kuna vitu ambavyo vimeandikwa humu mimi sielewi. Mkoa wa Kilimanjaro, shule 102, Mkoa wa Shinyanga shule 31, kweli tutafika tunakokwenda? Mbaya zaidi, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga tuna shule 26 za sekondari, nimesema ukarabati katika shule mbili ndio unaoendelea lakini hapa ni shule nne tu ambazo ziko ndani ya kitabu hiki wakati kuna Wilaya zina shule mpaka 30 zinakarabatiwa, ni haki tunatenda? Tufike mahali hii keki ya Taifa tugawane wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikubaliani na takwimu zilizopo hapa. Manispaa ya Shinyanga ina shule za sekondari 17 lakini kwenye kitabu hiki kuna shule mbili tu. Niliuliza hata wakati nachangia Kilimo, mna mpango gani na Mkoa wa Shinyanga, kwa nini kila kitu mnatuchakachua? Mimi nakuomba Waziri uksimama hapa unipe majibu ya uhakika vinginevyo uifute kabisa orodha ya vijiji vyote na shule zote zilizowekwa kwenye kitabu hiki kwa sababu kitabu hiki kimelenga kutugawa wananchi na Watanzania kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitu vingine yaani unaangalia tu unacheka, hapa imeendikwa Shinyanga vijiji kuna shule ya sekondari inaitwa Kishapu, wakati ni uongo mtupu hatuna shule ya sekondari inaitwa Kishapu. Kwenye kitabu hikihiki kuna shule ya sekondari inaitwa Mazoka, Shinyanga Vijiji hatuna shule hiyo. Sasa mimi najiuliza hizi takwimu zimetoka wapi? (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Azza, hiyo ni kengele ya pili.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Zainab Kawawa, ajiandae Mheshimiwa Felix Mkosamali.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa mara nyingine kutoa pole zangu rasmi kwa wananchi wa Liwale hususan viongozi wa CCM akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo, dada yangu Faith Mitambo, kwa kuchomewa nyumba zao kutokana na mgogoro uliopo wa korosho na ninaendelea kuisisitiza Serikali fanyeni hima ili mgogoro huo uweze kutatuliwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kwanza nianze na kuwasilisha kwenye Meza yako muhtasari wa madai ya Walimu wa sekondari wa nchi nzima. Nimekabidhiwa orodha hii toka kwa baadhi ya Walimu amba wana madai yao ya msingi ikiwa ni pamoja na malimbikizo ya mishahara yao, madai ya malipo ya likizo, madai ya malipo ya uhamisho, wengine wana madai ya malipo ya masomo, wengine wanamadai ya malipo ya matibabu na ya kujikimu na jumla kuu ya kiwango hiki imefikia shillingi bilioni 33 mpaka kufikia mwezi Mei 2013. Naomba nikabidhi kwenye Meza yako Tukufu ili Wizara iweze kufanya kazi madai haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu mambo machache, kwanza, ninaamini wote tunakubaliana na dhamira njema ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ya kukuza elimu kwa kuongeza idadi ya shule katika ngazi tofauti tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini wapo wengine hapa wanasema *historically* elimu yetu ilikuwa imara sana na sasa hivi elimu imeshuka, tulikokwama ni wapi? Nadhani kwamba tulikoanzia kwenye kukwama ni pale tulipoongeza idadi ya shule. Tuliongeza hizi shule kwa nia njema kabisa ya kukuza wigo wa elimu kwa Watanzania bila

kujali itikadi zetu, bila kujali imani zetu, bila kujali chochote kile. Kwa hiyo si jambo la maana sana kwa wengine kuona kama vile tunakoelekea ni kuiua elimu kwa sababu ukishafanya *expansion* ya hizi shule kwa vyovoyote vile mahitaji pia yataongezeka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo mzee wangu mmoja napenda kutumia msemo wake aliniambia kwamba ukishafanya *extension* ya shule hizi maana yake kuna *risk* ambazo huwezi ukazikwepa na hizi *risks* ndiyo hizi ambazo leo hapa tumekuwa tunazijadili kwa mapana na mrefu lakini niwaombe tu na kuwasih i sisi viongozi hapa tuache kuleta siasa kwenye elimu. Tumejadili mambo ya msingi, yaende yakatekelezwe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *trend* ya michango hapa, wengi wamekuwa wakilalamikia huu mgawanyo wa ukarabati wa shule. Mimi napenda niiombe Wizara, ifike wakati sasa ibatilishe hili jedwali na iende ikakae *seriously* kulifanya kazi ili haki iweze kutendeka. Sina haja ya kurudia maneno lakini kimsingi hata mimi niliviyolipitia sioni kama huu mgawanyo umetenda haki, kwa vyovoyote vile ipo Mikoa baadhi ya maeneo ya upande fulani watalalamika tu, hata ungekuwa wewe unatokea Kusini ungelalamika tu. Kwa hiyo, mimi naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kubatilisha jedwali hili na mimi kwa kweli siungi mkono hoja katika Wizara hii mpaka Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya kubadilisha jedwali hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikifanya utafiti kidogo tu, juu ya mfumo wa hizi taasisi zinazohusika na elimu yetu ya Tanzania. Kuna Wizara ya Elimu, kuna Taasisi ya Elimu ambayo inatunga mitaala na kuna Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani lenyewe kazi yake ni kutunga maswali ya mitihani kulingana na mitaala ambayo imepewa bila kujali kwamba wanafunzi wamefundishwa *syllabus* ngapi. Wakati huohuo Wizara ya Elimu nayo inazungumza kwamba hai-*coordinate* na Baraza la Mitihani na wala hai-*coordinate* na Taasisi ya Elimu ambayo inatunga mitaala na ndiyo moja ya vichochoeo

vya *failures* katika hawa wanafunzi wetu wa sasa hivi. Kwa hiyo, ninaomba hilo nalo mlitizame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nydingine ambayo nimeletewa hapa kutokana na utafiti wangu inasema kwamba, mitaala inabadilishwa sana, wote tunafahamu ni kweli, lakini mitaala inapobadilishwa imekuwa haishirikishi wadau mbalimbali. Hatuwashirikishi Walimu, hatuwashirikishi *policy makers*, hatuwashirikishi hata wazazi.

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab tunakushukuru sana.

**MHE. ZAINAB RASHID KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba *document* zangu zikabidhiwe Mezani kwako.

*(Hapa Mheshimiwa Zainab R. Kawawa alikabidhi Mezani  
Nyaraka za Madai ya Walimu alizokuwa akizzungumzia)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru na sasa namwita Mheshimiwa Mkosamali na mzungumzaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Mng'ongo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kuhusu jambo la msingi la Taifa ambalo ni elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nazungumza mara nyangi na wazungumzaji wengine waliopita, Mwenyekiti wa Kamati wakati anaanza kuzungumza, alisema yeye anakumbushia ya mwaka jana. Maana yake ni kwamba haya mambo tunayoyasema, mambo ya Wakaguzi na kadhalika yalishasemwa sana, mwaka jana, mwaka juzi, tumeyazungumza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiona mtu jambo anaambwa kila mwaka hasikii, haelewi, ujue huyo mtu tatizo lake ni uwezo wa kuongoza basi, hakuna tatizo lingine. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayosema siyo kwamba watu wanachangia hutuba, wanakumbushia tu! Wanakumbushia yale ambayo tulikuwa tunayasema, kila siku *we are singing songs in the house*. Tunaimba nyimbo kila siku, tunawaambia, tazameni *Hansard* shida ni viongozi, hawa watu hawana uwezo wa kuongoza hii Wizara, hawawezi, badilisheni, hamjabadilisha watu hawa, mwaka kesho tunakuja kuimba nyimbo nyingine. Mkaandike hotuba, mje tuendelee kuimba nyimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo tunayasema, sisi hatuna chuki na hawa watu, ndiyo maana nayasitiza, wale Mawaziri wanaofanya vizuri tunawasifia na wale wababaishaji tutawaambia tu kwamba hamfai tena bila kuficha, sisi hatukuchaguliwa tuje kubipubipu hapa, tulichaguliwa kuja kuwaambia kwamba hamwezi wale ambaa mmeshindwa. Huu ni uwezo mdogo wa kuendesha mambo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kidato cha nne yalisababisha vifo vyta wanafunzi watatu ambaa walijinyonga. Mmoja anaitwa Atusi Godfrey, yeye anatoka shule ya St. Sosteness, iko Karagwe kwa Mheshimiwa Gosbert Blandes, wa pili anaitwa Fidelis Michael anatoka shule ya Kanyeye Sekondari iko Tabora Mjini, Manispaa, kwa Mheshimiwa Ismail Rage na watatu aliyejinyonga anaitwa Barnaba Venant anatoka *Debrabant Secondary School*, Temeke. Sasa hawa wote walijinyonga wanatoka Majimbo ya CCM na wanaunga mkono hoja. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kwamba sisi tunayasema tu haya, kwamba tunaumia tu sisi, haya mambo hayana chama. Haya mambo watoto wale waliofeli wengine hata hawana vyama. Tuwe *serious!* Watu wanasimama hapa, Wabunge, wanasimama wanaunga mkono wakati

wanaona haya mambo yanaendelea hivihivi kila siku. Nyie ni watu wa namna gani? Kwa nini tusiamue Wizara hii tusiipitishe mpaka watu hawa wabadilike ili mwaka kesho mambo yasitokee kama haya? Mmeshaona watu hawana uwezo wa kufanya kazi mnaendelea kupitisha bajeti, haiwezekani!

### KUHUSU UTARATIBU

**MWENYEKITI:** Kanuni!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Unitazamie muda!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama hapa kwa mujibu wa Kanuni ya 64(b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesisimama hapa kwa heshima zote kwa Mheshimiwa Mkosamali ambaye anajua ninamheshimu sana, ambaye ni Mwanasheria mwenzagu. Amezungumza hapa katika mchango wake kwamba kuna mwanafunzi mmoja ambaye alijinyonga kwa sababu za kufeli mtihani kutoka katika Jimbo langu la Karagwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko makini sana katika Jimbo langu la Karagwe, ninajua kwamba kuna wanafunzi wengi wamefariki Karagwe na siyo huyo peke yake, lakini wanafunzi waliookufa, wamekufa kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu na siyo vinginevyo.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah!

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Pia hakuna taarifa yoyote ya Polisi ambayo inaeleza kwamba mwanafunzi huyo amejinyonga kwa sababu ya kufeli mtihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuomba utaratibu kuhusiana na taarifa hizo za uongo za Mheshimiwa Felix Mkosamali.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Labda hafamu kwa sababu hata *RPC* wa Kagera alisema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, endelea!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Eeh niendelee tu, kwa sababu hata *RPC* wa Kagera alisema na watu wengine. Ngoja niendelee. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii tumekwisha kusema ina Sera za aina mbili za elimu. Kuna watu wanasoma shule za *english medium* ambazo ndiyo Wabunge wengi hapa watoto wenu wanasoma huko, ndiyo maana hamko *serious* kwa sababu watoto wenu wanasoma shule za *english medium*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule nzuri, wanalala kwenye mabweni ...

**WABUNGE FULANI:** Wanaenda nje ya nchi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Wengine wanaenda nje ya nchi. Baba wa Taifa alitengeneza mfumo mzuri sana, watu mlikuwa mnatoka vijijini hapo, mnajifahamu, mnapewa nauli, mnasoma kwenye shule za mabweni. Leo ninyi viongozi wa sasa hivi mmejitenga na wale watu waliowachagua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkichaguliwa mnakwenda mnaweka watoto wenu *english medium* halafu mnakwenda kuwadanganya wao kwenye shule ambazo hazina vitabu, hazina madawati halafu mnawambia hayo ni maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi baba wa Taifa alikuwa hawapeleki watoto wake nje ya nchi alikuwa hana hela? Ndugu zangu tunaomba mbadilike, watu wanajua, watu sasa hivi wanaelewa. Siku watu wakitoka kule Manzese wameshajua kwamba ninyi mnakaa maeneo gani, tunaomba mbadilike, tunawaambia mara ya mwisho, watawafuata, ninyi mmesoma mpaka Baba wa Taifa

akawawezesha kununua nyumba Masaki. Sasa leo na ninyi je, wale watu wa kule kwenu nao mmewatengenezea mfumo na wenyewe waje waishi Masaki kama ninyi! Au kwa sababu mlishagawanya nyumba zile na elimu mmeigawanya mara mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya hayakubaliki hata kidogo, shule hizi zinafundishwa kwa Kiingereza, mitaala tunaambiwa ni ya Kiswahili. Tulikuja hapa na hoja mwezi wa kwanza, Mheshimiwa James Mbatia akawaambia, tuunde Kamati ya kushughulikia masuala haya, ninyi wenyewe mlikataa, ambao leo mmekuja kuzungumza na Mheshimiwa Serukamba na wewe umeomba Kamati iunde, mbona hukukubali siku ile? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende *objectively*, watu wasiwe wanakuja hapa leo wanasema hiki, kesho mtu anabadilika, sisi tuliosoma *logic* kwenye *philosophy* tunakatazwa. Kuna *principle of non contradiction*. Mtu ambaye ni kiongozi, mtu anayejiamini lazima awe *systematic*, muwe mnasema kitu kimoja. Mambo ya kuunga mkono, mnakataa, mnaunga mkono, wakati mnajua mambo yakipitishwa yanaenda kuwa hivyo hivyo, huo ni unafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pongezi kwa Baraza la Mitihani. Baraza la Mitihani linafanya kazi nzuri na wale wanaolishtumu toka hawa viongozi wameingia, akina Mama Ndlichako, watu *wanao-perform* mpaka Canada wanaogopa wamedhibiti wizi wa mitihani kama ulivyokuwa huko nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale wenyewe shule binafsi ambao walikuwa wanataka mitihani iibiwe ndiyo wanataka hawa watu watolewewe, wanatafuta sababu ili hawa watu watoke ili wakaibe mitihani pale. Tumeshafahamu ajenda zenu, acheni wale watu wafanye kazi, yule mama anatoka kule Kigoma sijui Jimbo la mama Buyogera na nani huko! Wamekula mawese ya kutosha na dagaa wa migebuka, vichwa viko vizuri. Wamepata 'A', kama sisi

tulivyokuwa tunapata wakati tunasoma, tulikuwa tunapata 'A' tupu! *Division one za point saba*, ngapi mimi nimepata, kwa hiyo, tunazungumza mambo ambayo tunayafahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lile Baraza linafanya kazi nzuri, tuliache liendelee kusahihisha na kutunga mitihani. Nisisitze kitu kimoja. Baraza la mitihani halina watu wanaofanya kazi pale kwa ajili ya kutunga mitihani au kusahihisha mitihani, Baraza la Mitihani linachukua Walimu waliowafundisha watoto kuja kutunga mitihani. *Then*, linachukua Walimu tena waliowafundisha wale watoto kuja kusahihisha mitihani. Sasa kama Mwalimu aliyemfundisha mtoto wake anaona mtoto amefeli, ninyi mna-standardise vitu gani? Mna- standardise nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri lazima awajibike, lazima mjiuzuru, mmeshindwa kazi, mmeshindwa kuongoza Wizara hii, mmeshindwa *complete* kwa sababu ni miaka yote tunawaambia *trend*, vitabu mnatupa ninyi wenyewe vyा *statistics*, mji-asses wenyewe kama alivyofanya Rais Mwinyi, watu wamekufa akajiuzuru. Siyo kwamba alikuwa amefanya yale yeye na ninyi tumeona mmeshindwa kusimamia, tunaomba mtupishe muiache Wizara hii iongozwe na watu wenye uwezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza mara nydingi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nakushukuru ni kengele ya pili. Mheshimiwa Mng'ong'o, mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kujenga shule nyingi na vyuo vikuu ambavyo wenzetu wamesoma na wameweza kuweza kusimama hapa na kuchambua hayo wanayochambua, kwa sababu ya elimu waliyoipata kutoka kwenye shule na vyuo vilivyojengwa na Serikali ya CCM la sivyo tusingekuwa na uwezo wa kuongea kama tunavyoongea leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, timesoma bure wote hapa, hata wanaosema wamepata *point* saba, wamepata *point* saba kwenye shule zilizojengwa na Serikali ya CCM. Hata vyuo vikuu hivyo anavyoviongolea. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala ambalo wote wamelizungumza la mgao uliomo humu ndani. Mbona huu mgao hatuulalamikii? Naomba hizo takwimu walizozungumza wajumbe wenzangu, turudi tutazame, Waziri tusaidie, chambua wote tupewe keki hii ya ukarabati wa shule kwa usawa. Kila mmoja kama ni shule kumi, kama ni shule ngapi, Mikoa yote Tanzania nzima tupate. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Siyo Kilimanjaro 100.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kweli matokeo yamekuwa mabaya, wenzangu wote wameyajadili, siwezi kuyarudia. Naomba nizungumzie tatizo la watoto kwamba wamejiua, naomba kushangaa. Kuna watoto wasichana na wengine wamekufa kwa sababu ya kupata mamba, mbona hatujadili watoto kujengewa mabweni, watoto wa kike wamejiua, kwa sababu wamepata mimba na hawana uwezo wa kurudi shule ya sekondari, mbona hatuyazungumzii haya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuyazungumze yote kwa ujumla wake. Nafikiri tutakuwa viongozi kama tutajadili vitu

kwa kuiangalia vyote kwa pamoja. Watoto wetu wengi wa kike wamepata mimba na wavulana waliowapa wako mashuleni na wamejua hatuyazungumzi hapa. Naomba yote tuyazungumze, tusichukue kipengele cha watoto kushindwa mitihani. Kila mwaka watoto wamekuwa wengine wanashindwa mitihani kwa bahati mbaya na kwa sababu hawapati ushauri mzuri, wanachukua hatua ambazo ni za mkato. Kwa hiyo, naomba hili tuliangalie kama suala mtambuka kwa ujumla wake kwamba tatizo ni kubwa, lakini tukichukulia kwamba watoto kumi, sijui watoto wangapi walikufa kwa ajili ya kushindwa mtihani, kuna watoto wasichana wengi ndugu zangu kama hamjui takwimu hizi wamejua kwa sababu ya kupata mamba, matumaini yao yalikuwa kuwa viongozi. Naomba hili tuliangalie na tuwajengee *hostel*/na kuwarudisha shulenii kupunguza tatizo hili, hili nalo ni kubwa sana la kulitizama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya CCM, mimi naomba niseme, nimezaliwa Kijiji na wakati nasoma sekondari nilikuwa peke yangu, leo nafurahi kuona watoto wengi wako sekondari wanasoma kwa sababu shule za kata zimejengwa na watoto wote wako shuleni wanasoma, watoto wengi wangekuwa wameolewa, wengine wana mimba na wana watoto zaidi ya watatu na wavulana pia wengine wangekuwa wako mtaaani, shule ziko, wanasoma. Tukubali tusikubali, mtoto ye yote aliye pata elimu ya sekondari, hata kama amepata *division* sifuri, hawezi kufanana na yule ambaye hakwenda sekondari. Hilo tukubali kabisa kama tunataka kutenda haki kwa hawa wananchi tunaowaongoza na pia kama tunataka kuwa wakweli. Wazazi wako vijijini, hawakusoma kwa sababu shule za sekondari hazikiuwepo, sasa hivi wanajitahidi wanapeleka watoto shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachoomba mimi, tuangalie sasa suala la watoto wote kusoma sekondari bure, hii michango tunayoizungumza yote iondoke, watoto wote wapate elimu sawa na kwa umoja wao halitakuwepo tatizo, michango itakuwa imepungua na kila mtoto atapata muda wa kwenda sekondari. Kama tutakuwa tunaangalia, kwa

ujumla wa kuchambua bila kutazama kwamba historia ilikuwa wapi, Mikoa mingine ilikuwa na shule moja tu lakini watoto wako shulen i wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina uhakika watoto hawa tuwajengee mazingira ya kuwa wafanyabiashara, kuwa wakulima wazuri, tuwape mafunzo ya kilimo, mafunzo ujasiriamli ule wanaohitaji, vyuo vya ufundi viwepo mpaka kwenye maeneo ya Tarafa, wapate elimu ya ufundi wakiwa kule, waweze kujitegemea. Nina uhakika kwamba hawawezi kuwa wezi kama wenzangu walivyosema, eti wezi, majambazi, watoto waliosoma shule ya sekondari hawawezi kuwa wezi wala majambazi, eti watakwenda kuangalia sijui watu wako Masaki, sijui wapi, hiyo siyo sera nzuri ya kuongea sisi viongozi ndani ya Bunge hili, hatuwezi kuzungumza kwamba wananchi wanatuona, vijana wanatuoana, watatufuata Masaki, hilo siyo suala la kuzungumza, tuzungumze hawa watoto tutawafanyaje, watoto wetu waliokosa nafasi za kwenda shule na wote tushirikiane kama kitu kimoja bila kutupa lawama kwa yule au kwa yule. Tuna watoto wetu wako huko, tunataka waende shule, tunataka wasome, lakini tuwatafutie vyuo vya ufundi, wasome waweze kujiajiri, tuwape mitaji waweze kufanya biashara. Wale ambaao wanataka kurudia shule, tuwape nafasi ya kurudia shule ili waweze kufaulu mitihani yao. Wale wanaotaka kusoma kwa miaka miwili, tuendeleze huo taratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Walimu limeshazungumzwa kwa undani sana, turudishe ile Tume iliyokuwa inaangalia Walimu na maslahi yao! Wote bila Walimu tusingkuwa hapa, hata wote tunaozungumza hapa, tunazungumza kwa sababu Walimu walitfundisha vizuri na walikuwa na mazingira mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matatizo, mimi nali sema hili, Mheshimiwa Jenista Mhagama namuunga mkono, alizungumzia suala la lishe, tunaliangalia nusu, hebu tufanye utafiti, asilimia 42 ya watoto wana udumavu na huu udumavu unaharibu ufikiri wao. Hebu tuangalie, tufanye *research* inaweza pia kuwa inachangia pamoja na kuwa

tunazungumza kisiasa tu, eti tuangalie sehemu gani sijui sehemu gani tusiangularie, utafiti tufanye, tutagundua kwamba lishe inachangia kwa kiasi kikubwa ufaulu wa watoto wetu shuleni kama una lishe duni huwezi kufikiri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba kabisa, nawaomba Wabunge wenzangu tusilifanyie utani na napongeza kabisa Serikali jukumu ililolichukua la kukipa kipaumbele suala la lishe na uhakika wa chakula majumbani. Turudishe pia chakula shuleni, watoto wale, mbona zamani tulikuwa tunakula hata kwa kwenda na chakula chetu, limeenda wapi? Mtoto ambaye hawesi kuwa na chakula nyumbani na kula milo yote, basi awezekupata mlo mmoja shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaangalie watoto yatima katika mugwanyo wa shule. Tunapoangalia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mng'ong'o nakushukuru, hiyo kengele ya pili!

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu ya wachangiaji kwa siku ya leo imekwisha, nawashukuru wote, naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 5 Juni, 2013 saa 3.00 Asubuhi)*